**2 MEI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 2 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MHE. LUCY J. SABU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa majukumu

ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga.

Na. 198

### Malipo ya kiinua mgongo kwa wazee wasioajiriwa

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE K.n.y. MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italipa kiinua mgongo kwa wazee ambao hawajawahi kuajiriwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kiinua mgongo ni malipo ambayo hulipwa na mwajiri pindi mfanyakazi wake anapostaafu kufanya kazi. Hata hivyo, kutokana na kuwepo

kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambapo mwajiriwa na mwajiri huchangia, mfanyakazi hulipwa pensheni badala ya kiinua mgongo na hupokea mafao ya mkupuo mara anapostaafu na badaye kuendelea kulipwa pensheni ya kila mwezi kwa maisha yake yote. Hivyo, kwa sasa hakuna mfumo wa kulipa kiinua mgongo kwa mzee ambaye hajawahi kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu ya Serikali, tunatambua kwamba nchi hii hujengwa na wafanyakazi ambao wameajiriwa na wafanyakazi ambao hawajaajiriwa kwa mfano wakulima na wafugaji.

Je, sasa Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia hawa watu ambao wameijenga nchi yetu kwa muda mrefu wakiwa hawajaajiriwa kwa kazi za Serikali kwa maana ya wakulima na wafugaji ili kuwasaidia wanapofikia umri ambao hawawezi kufanya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali inapaswa kuzingatia Watanzania wote wanaojenga nchi yao katika kufanya kazi mbalimbali. Moja ya mikakati ya Serikali ambayo iliona suala hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema, ni pamoja na kubadilisha skimu za utoaji wa pensheni katika mifuko ya hifadhi ya jamii na

kuzingatia kwamba yapo makundi ambayo siyo ya wafanyakazi, wanafanya kazi zisizo rasmi, lakini wanafanya kazi kwa mfano kwenye maeneo ya viwanda, kilimo, biashara na wajasiriamali wadogo wadogo. Tayari Mfuko wa *NSSF* ambao unashughulika na sekta isiyo rasmi umeanza kukusanya michango kwa kuwatambua hawa walio kwenye makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bado Serikali pia kwa kutambua kwamba wapo ambao ni wajenzi wa Taifa na wakifikia katika hatua ya uzee wanahitaji msaada. Serikali imekwisha kuandaa vituo vya wazee ambao wanakuwa wanahitaji msaada wa Serikali kwa mfano wa matibabu na maisha, kuna mpango maalum wa *TASAF* ambapo zaidi ya wazee 647,512 ni wanufaika wa mfuko huo. Lakini zaidi ya hapo pia vipo vituo maalum zaidi ya 14 katika mikoa 26 nchini ambavyo Serikali imeviweka kwa ajili ya kuwasaidia wazee, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi yanayohusu huduma mbalimbali za wazee ikiwemo tiba na mengineyo. Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuleta Sera ya Wazee Bungeni ili kwa ujumla wake tuangalie mapungufu na yale ambayo yanaweza kufanyika kuweza kujenga mazingira mazuri ya wazee wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze kwa swali zuri ambalo limeendana kabisa na mpango wa Serikali ambao tunaufanya hivi sasa. Katika vituo hivyo vya wazee, na katika utaratibu uleule wa kuangalia makundi ambayo yanahitaji msaada zaidi, hasa katika masuala ya chakula, malazi, mavazi, matibabu na *welfare* yao kwa ujumla, tayari Sera ya Wazee ipo na iko katika hatua za kwenda kufanyiwa marekebisho ili kuweza kuhakikisha tunawasaidia wazee hawa, ikiwa ni pamoja na kuunda mabaraza ya wazee katika ngazi za halmashauri huko mpaka ngazi ya vitongoji, mitaa na vijiji ambayo tayari imekwisha kuanza kufanya kazi na zinafadhiliwa na halmashauri zetu kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Mheshimiwa Katani.

Na. 199

**Kumalizia sekondari zilizojengwa na wananchi – Tandahimba**

**MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha kumalizia ujenzi wa sekondari zilizojengwa na wananchi Kata za Mnchimbwe, Kwanyama na Litehu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Jimbo la Tandahimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua jitihada zinazofanywa na wananchi katika kuibua miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa shule. Serikali imeendelea kuunga mkono jitihada hizo kwa kumalizia miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kupitia mapato ya ndani ilitoa shilingi milioni 200 kwa ajili ya umaliziaji wa Shule ya Sekondari ya Kwanyama. Mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali illipeleka shilingi milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Litehu kupitia mradi wa *SEQUIP* na Mwaka wa Fedha 2022/2023, shilingi milioni 250 zilitolewa na Serikali kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mndumbwe. Aidha, Shule za Sekondari katika Kata za Mnchimbwe, Kwanyama na Litehu zimekamilika, zimesajiliwa na tayari zinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za umaliziaji wa maboma ya shule katika halmashauri zote nchini kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali: -

Kata za Mahuta na Mkwedu hazina shule ya sekondari kabisa; je, Serikali inaweza ikatupa fedha kwa ajili ya kujenga sekondari hizo kwa sababu tayari wananchi wameshaanza kujenga maeneo yale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kata hizi alizozitaja Mheshimiwa

Katani hapa Serikali tayari iko mbioni kupeleka shilingi milioni 470 kwenye halmashauri 184 nchi nzima kwa ajili ya ujenzi wa shule nyingine za sekondari katika kata zile ambazo bado hazijapata shule hizi za sekondari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni utaratibu kwa wananchi kutumia nguvu zao kujenga shule ama zahanati. Lakini bahati mbaya sana kumekuwa kuna udanganyifu kwenye halmashauri, hawazielezei kwa kina thamani ya kifedha ambazo wametumia nguvu za wananchi. Matokeo yake wanaomba Serikali pesa kwa madhumuni kwamba wanataka kumalizia maboma lakini hawaelezi ile nguvu, matokeo yake ni kwamba…

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni kwamba Serikali inatoa pesa lakini pesa ambayo inatolewa na Serikali haitumiki kwa matumizi yanayotakiwa kwa sababu kuna udanganyifu wa fedha ambayo imetolewa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lini Serikali itafanya uchunguzi wa kina ili kujua kama fedha zinazotolewa kwa ajili ya kumalizia maboma ni za kumalizia maboma na nguvu za wnanachi vilevile zinajulikana ni kiwango gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya tathmini ya mara kwa mara katika halmashauri zetu kuangalia hali ya maboma ambayo yanaripotiwa na wakurugenzi wa halmashauri. Hivi tunavyoongea tayari kuna timu ambayo inafanya tathmini ya kuweza kuona maboma yaliyopo na hizi fedha zinazopelekwa kwenye shule za sekondari na hizi tunazopeleka kwenye shule za msingi kuona wamekwenda kumalizia maboma yaliyokuwepo ama wameanza madarasa mapya. Kwa hiyo Serikali muda wote imekuwa ikifanya tathmini hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama.

Na. 200

**Hoja za Ukaguzi wa Mfuko wa Jimbo**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA** aliuliza: -

Je, kwa nini hoja za ukaguzi hutokea pale fedha za Mfuko wa Jimbo zinapotumika kwa wajasiriamali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa kwa Sheria Na. 16 ya mwaka 2009 na unaelekeza miradi ya kutekelezwa kupitia

Kamati ya Mfuko ambayo Mbunge ni mwenyekiti na afisa mipango wa halmashauri ni katibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo mahususi la kuanzishwa kwa Mfuko huu wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ni kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa katika ngazi ya jamii na kupitishwa kwenye vikao mbalimbali vya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya halmashauri zimekuwa zikitumia fedha za Mfuko wa Jimbo kutoa mitaji kwa wananchi, hususan wanawake, watu wenye ulemavu na vijana, hali inayosababisha ugumu wakati wa kufanya ufuatiliaji na tathmini na kusababisha hoja za ukaguzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kizito.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ipo mifuko ya halmashauri ambayo pia inatoa huduma kwenye vikundi vya wajasiriamali na mfuko huu wa maendeleo wa jimbo umeonesha ugumu wa utekelezaji kutokana na masharti yaliyowekwa, kwa nini sasa Serikali isione haja ya kuleta hii sheria ili iboreshwe ili kukidhi mahitaji ya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu kama ambavyo wananchi wamekusudia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba mfuko huu upo

kisheria na ulianzishwa kisheria. Nachukua maoni ya Mheshimiwa Mhagama na tutaona ni namna gani tunakusanya maoni pia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengine humu ndani kabla Serikali haijaanza mchakato wa kubadili sheria hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Wabunge wote wa Viti Maalum na Wabunge wa Majimbo wako sawa kwa mujibu wa Katiba. Je, Serikali haioni haja ya kuleta sheria ambayo itaruhusu Wabunge wa Viti Maalum waweze kupewa mfuko wa jimbo ili na wao waweze kushiriki katika maendeleo ya halmashauri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, pale tutakapoanza kukusanya maoni ya wadau ambao ni ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kuona namna gani tunaleta katika Bunge lako hili Tukufu Mabadiliko ya Sheria hii ya Mfuko wa Jimbo, tutazingatia pia hili suala la Wabunge wa Viti Maalum.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; Mheshimiwa Esther Midimu.

Na. 201

## Kurudia ujenzi wa barabara ya kutoka Mwigumbi hadi Maswa

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kurudia ujenzi wa Barabara ya Mwigumbi – Maswa ambayo imejengwa chini ya kiwango na imeshaharibika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi alianza kazi za kurudia ujenzi wa maeneo yote ambayo yalionekana hayakidhi viwango vya ujenzi kwa gharama zake mwenyewe mnamo tarehe 10 Juni, 2021. Kazi za marudio ziko katika hatua za mwisho ambapo zimefikia asilimia 98 na zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza: -

Je, ni kwa kiasi gani Serikali imejiridhisha kuwa marekebisho hayo yamekidhi viwango?

Swali la pili; kwa kuwa barabara ya Kolandoto – Meatu mpaka Kateshi iko kwenye ilani, je, ni lini Serikali itaijenga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejiridhisha kwanza kwa kumsimamia zaidi mkandarasi na kuhakikisha kwamba kila hatua anayoifanya mhandisi mshauri pamoja na mkandarasi kupewa majukumu ya kuhakikisha kwamba anakwenda kufanya kazi kwa kiwango kinachotakiwa. Hata hivyo, atakapokuwa amekamilisha kazi hii itahakikiwa na wataalam kuhakikisha kwamba vigezo vyote vya barabara kwa maana ya jinsi ilivyosanifiwa ndivyo ilivyorekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili; barabara aliyoitaja ya kuanzia Kolandoto – Meatu kwenda Katesh ni sehemu ya barabara ndefu ambayo ipo kwenye mpango pia wa *EPC+F*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Cecil.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwezi mmoja sasa tangu nisimame hapa nikiuliza kuhusu Barabara ya Masasi – Nachingwea, na Mheshimiwa Naibu Waziri utakumbuka ulinijibu kwamba iko kwenye hatua za *financing.* Na niliuliza lini mchakato huo utakamilika, hatukuweza kupata majibu wakati ule. Sasa ninauliza tena: -

Ujenzi wa Barabara ya Nachingwea – Masasi ambao ulikuwa kwenye hatua ya *financing;* hatua hiyo itakamilika lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Masasi Nachingwea inakwenda mpaka Liwale. Kama nilivyosema, ni kati ya barabara saba ambazo ziko kwenye *EPS+F;* na taratibu za manunuzi kwa maana ya upande wa *finance* kwa wenzetu wa fedha bado zinaendelea zote kwa pamoja, kwa barabara zote saba. Kwa hiyo zitakapokuwa mchakato huu umekamilika tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Waziri, barabara ya Kibaha – Morogoro -Dodoma kwenda mpaka Mwanza hamuoni kama imelemewa sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sijakusikia hiyo barabara.

**NAIBU SPIKA:** Barabara kutoka Kibaha – Morogoro kwenda Dodoma – Mwanza – Iringa huoni barabara zimelemewa sasa hivi, mna mpango gani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kibaha hadi Morogoro ipo kwenye *PPP* ambapo itajengwa kwa *express way* njia nne; na kutoka Morogoro kuja Dodoma

hadi Mwanza ni kweli magari yameongezeka. Serikali ina mpango wa kuipanua hiyo barabara ili iweze kukidhi haja ikiwa ni pamoja na maeneo yote ya miinuko na maeneo ya ku-*park* kuweza kuipanua ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Gwajima, kwa niaba Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo.

Na. 202

**Serikali kupanua barabara ya Tegeta – Wazo**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO K.n.y. MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapanua barabara ya Tegeta kuelekea kiwanda cha Saruji Wazo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kipande cha barabara ya Tegeta – Wazo Hill kilikarabatiwa Mwaka 2014 kwa kiwango cha lami kwa njia mbili *(Single Carriage Way)* ya upana wa mita 7 na njia za waenda kwa miguu zenye upana wa mita 1.5 kila upande. Upana huo unakidhi viwango vinavyohitajika kwa matumizi ya barabara ya njia mbili. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa wingi wa magari katika sehemu hii ya Tegeta – Wazo Hill, Serikali ina mpango wa

kupanua barabara hii kuwa njia nne na utekelezaji wake utategemea upatikanaji wa fedha.Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua sasa barabara ya kutoka Kokoto mpaka Kongowe ni lini upanuzi wake utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, na swali la pili, Je, ni lini sasa barabara ile ya kutoka Mbande Kisee mpaka Msongora ambayo imekuwa ni adha kwa wapiga kura wa Dar es Salaam ujenzi wake utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na barabara ya pili Mbande kwenda Msongora kilomita hizo tatu ambazo zimebaki tunategemea zitaanza kutekelezwa katika bajeti hii tunayoanza kuikamilisha. Na barabara hii ya Kokoto kwenda Kongowe upanuzi wake, naomba Mheshimiwa Mbunge asubiri tuone kwenye bajeti tumependekeza tufanye nini. Tunajua tayari kuna changamoto kubwa tuweze kuitekeleza hii barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo la Manyoni Mashariki kuna Barabara ya kutoka Sorya kwenda Hika – Makulu – Londoni na Ikungi Singida. Je,

ni lini Serikali itaanza kufanya upembuzi na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga katika kiwango cha lami ? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika,naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo tumeipendekeza ifanyiwe usanifu mwaka wa fedha tunaoanza kama bajeti yetu itapitishwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara yetu ya Kitonga kumekuwa na ajali nyingi sana, na wiki iliyopita tu basi lilitumbukia pale, na ajali ikitokea magari yanakaa takriban siku nzima au siku mbili. Je, lini Serikali itaona sasa umuhimu wa kujenga barabara mbadala ya kutoka Mahenge kwenda Udekwa kupitia Utalisoli mpaka Ilula ?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo : -

Mheshimiwa Naibu Spika,ni kweli lile eneo la Kitonga limekuwa na changamoto kubwa. Tayari Serikali ilishatoa maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Iringa wasaidiane na Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Iringa kuangalia uwezekano wa kufanya *by-pass* ya Mlima Kitonga ili kunapotokea changamoto kuwe na uwezekano wa kuwa na njia mbadala, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave jiandae Mheshimiwa Yahya.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara inayotoka Buza kwenda kuunganisha jimbo la Ukonga pamoja na Temeke ?

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kusaidiana na wenzetu wa TAMISEMI tutahakikisha kwamba hiyo barabara tunaijenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya jiandae Ginzabuke.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika,nashukuru, Mkoa wa Mtwara una unganishwa ni Mkoa wa Lindi hadi Morogoro kwa kuanzia katika Wilaya ya Nanyumbu. Barabara hii iko ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Je, ni lini barbara hii itajengwa kwa kiwango cha lami ?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika,ahsate. Naomba Mheshimiwa Yahya aweze kurudia jina ya zile barabara alizozitaja niweze kumjibu vizuri.

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Yahya zungumza Kiswahili si Kimakonde, barabara haieleweki huku.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ninayoizugumza iko ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Inaanzia Wilaya ya Nanyumbu katika mji wa Mangaka inakwenda Liwale hadi Morogoro. Je, barabara hii

ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama inavyozungumzwa ndani ya ilani ya Chama Cha Mapinduzi ?

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, na kwa kweli tumeongea naye. Hii barabara ni kweli ipo kwenye Ilani. Inapotoka Wilaya ya Nanyumbu kwenda Liwale inapita Selous ambapo inakwenda Ilonga kwenda Mahenge kuunganisha na Mkoa wa Morogoro. Tumeweka kwenye mapendekezo kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuunganisha Mkoa wa Mtwara, Lindi na Mkoa wa Morogoro kupitia eneo la Ilonga – Mahenge, ahsante.

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika,ahsante. Je, ni lini Barabara ya Uvinza – Maragarasi yenye kilometa 51 itamalizika kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Uvinza - Maragarasi ni barabara ambayo ipo kwenye ujenzi kwa msaada wa Abu Dhabi na Kuwat *Fund,* kilometa 51.3 Mkandarasi yuko *site*. Kinachokwamisha sasa hivi kutokwenda kasi ni kwa sababu ya Mvua nyingi inayonyesha; lakini Mkandarasi ameahidi kwamba atakamilisha kwa muda kulingana na jinsi tulivyokubaliana naye, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naoma kujua ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga barabara ya kutoka Chapwa halmashauri ya Mji wa Tunduma kuelekea Chindi mpaka Chitete ili kurahisisha mawasiliano ndani ya Wilaya ya Momba ?

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kwa sasa inahudumiwa na wenzetu wa *TARURA,* ambayo inaunganisha Makoa Makuu ya Wilaya ya Momba Chitete kuja Tunduma. Hata hivyo nitaichukua ili kama Serikali tuone namna tukavyofanya kuijenga kwa kiwango cha lami ili kuiunganisha Tunduma na Makao Makuu ya Wilaya ya Momba Chitete, ahsante.

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia Mheshimiwa Zuwena Athumani Bushiri.

Na. 203

**Kufunga umeme kwenye Mnara wa Halotel Kata ya Ngujini – Mwanga**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza: -

Je, ni lini umeme utafungwa kwenye mnara wa halotel uliopo kata ya Ngujini Wilayani Mwanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Jukumu la kuunganisha umeme kwenye minara ya mawasiliano ya simu nchini, ikiwemo ile iliyojengwa kwa ruzuku ya Serikali, ni jukumu la watoa Huduma, hii ni pamoja na gharama za kuunganisha umeme na kuendesha minara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kusimamia huduma za mawasiliano nchini kwa kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi matakwa ya leseni zinazotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Wilaya ya Mwanga Mkoani Kilimanjaro kuna kata ambazo hazina mawasiliano mpaka wananchi wapande juu ya miti ndio wapate mawasiliano ; na kata hizo zina changamoto ya kuvamiwa na Tembo mara kwa mara.

a) Je, nini kauli ya Serikali ya kuwasaidia wananchi hao kupata mawasiliano ili wanapopata matatizo waweze kutoa taarifa?

b) Je,ni lini Serikali itadhibiti Wizi wa fedha za wananchi kwa kupitia simu kwa kuwa tatizo hili limekuwa ni changamoto kubwa sana katika nchi hii ?

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika,napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuwena Athuman Bushiri, Mbunge Viti Maalumu Kilimanjaro kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Zuwena kwa kazi kubwa ya kuwatetea wana Kilimanjaro katika masuala ya mawasiliano. Mheshimiwa Zuwena alifanya Ziara katika Tarafa ya Jipendae, na akatujulisha Serikali na tukapokea malalamiko hayo ambayo ni changamoto, na Serikali tukayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kata ambazo Mheshimiwa Zuwena amezitaja, Kata ya Kwakoa, Kilya, Tohora pamoja na kata ya Kibisini tayari zimeingizwa kwenye utaratibu wa kupatiwa huduma za mawasiliano. Lakini katika eneo ambalo linaenda katika lango la Hifadhi ya Mkomazi pia nalo Serikali inatarajia kuingia mkataba na *TTCL* ili iweze kufikisha huduma ya mawasiliano katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwas wali la pili, Serikali haiwezi kupuuza malalamiko ya wananchi. Suala la wizi kwenye masuala ya simu na fedha za wananchi katika mitandao ya simu, nipende kusema jambo moja. Huduma ya mawasiliano ina wadau watatu, kuna watoa huduma, kuna watumiaji wa huduma na kuna Serikali. Serikali kazi yake ni kuhakikisha kwamba watoa huduma wanatoa huduma katika mazingira rafiki, lakini na watumiaji wa huduma wanapata huduma ambayo inaendana na haki ambazo wanazitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maelekezo kwa *TCRA* kufanyia kazi malalamiko ya wananchi ili kujiridhisha na changamoto jinsi ambavyo ilivyo na kuhakikisha kwamba tunatoa majibu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ni lini kata ya Mkindi, Kata za Masagaru, Kwekivu na Kimbe vijiji hivi vitapitiwa na minara kwa ajili ya masiliano kwa ajili ya wanachi wa maeneo hayo ?

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika,napenda kujibu swali la Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi huu wa tano Serikali inatarajia kuingia mkataba na watoa huduma ili kuweza kufikisha huduma ya masiliano katika maeneo 763. Vile vile Serikali imeshaanza kufanya tathmini katika vijiji 2116 vitakavyokamilika. Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano vikiwemo vijiji na kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amevitaja, ahsante sana.

Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Ngasa.

Na. 204

**Kupatiwa gari Ofisi ya Zimamoto – Igunga**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaipatia gari Ofisi ya Zimamoto ya Wilaya ya Igunga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa Mbunge wa Igunga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya magari kwa Jeshi la Zimamoto na uokoaji Nchini. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga bajeti ya jumla ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ununuzi wa magari matano ya kuzima moto ambayo yatasambazwa katika mikoa na wilaya zenye upungufu wa magari ya zimamoto na uokoaji nchini ikiwemo Wilaya ya Igunga. Kwa sasa Wilaya ya Igunga inahudumiwa na gari la zimamoto lililopo Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuliongezea wataalam na vitendea kazi ikiwemo magari ya kuzimia moto na uokoaji kwa ajili ya kuzifikia wilaya zote nchini kutegemea upatikanaji wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngasa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Igunga ni moja ya miji inayokua kwa kasi kubwa sana kutokana na kuongezeka

kwa shughuli za kiuchumi na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watu.

a) Je, Serikali, kwa kutowapatia mpaka sasa gari la zimamoto haioni ni kuhatarisha maisha ya raia na mali zao endapo itatokea janga la moto ?

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta ni moja ya kimiminika hatarishi sana duniani, na sisi Igunga tunashughuli za bomba la mafuta zinaendelea pale na kuna *camp* kubwa sana ambapo tunaona itakuwa hatari sana endapo shughuli hizi zitaendelea na hatutakuwa na gari la Zimamoto endapo kutatokea na changamoto yoyote ya mlipuko au maafa.

b) Je, Serikali inachukua hatua gani au mkakati gani kwa ajili ya kukabiliana na jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika,napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika,kwanza tunatambua kwamba kuna uhaba wa magari ya zimamoto, tumekiri hapa ; na kwamba tumeanza utekelezaji wa bajeti kwa kupunguza tatizo hili kwenye maeneo ambayo hayana, lakini yote yanategemea upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, tumesema kwenye jibu la Msingi. Igunga kutokana na hizo shughuli nyingi za kiuchumi pamoja na hilo bomba la mafuta linalopita kwenye eneo lake, tunalipatia kipaumbele kwa mwaka ujao ili wapate gari la kuzimia moto, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali langu, Mkoa wa Njombe na halmashauri

mbalimbali nchini ikiwemo Makete wanalipa ushuru wa *fire* lakini maeneo haya hayana gari za *fire*. Ni ipi kauli ya Serikali kwa halmashauri zote nchini ambazo haziona gari za *fire* na wanalipa ushuru wa *fire* iktu ambacho kwa wnanchi kimekuwa ni kero na wamekuwa wakituuliza maswali mengi?

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika,ushuru unaolipwa si kwamba ndio unaokwenda kununua gari za zimamoto kwa sababu ni ushuru kidogo sana ukilinganisha na gharama za gari hizi; gharama za gari hizi hutegemea bajeti ya Serikali. Hata hivyo fedha zile zinalipwa kuwezesha Jeshi la Zimamoto na Ukoaji kutoa elimu ya namna ya kujikinga na majanga ya moto na majanga mengine ya kibinadamu kwenye maeneo hayo. Nikuahidi Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote, kwamba kipaumbele cha Serikali kuanzia mwaka ujao ni kupata fedha ili kuweza kuzipatia wilaya zote gari za zimamoto kwa kadri fedha zitapopatikana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mwanyika, jiandae Mheshimiwa Mariki.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Mkoa wa Njombe una majanga makubwa sana upande wa misitu, na misitu ndio uchumi. Anaweza kutoa kauli ya Serikali kuhusiana na kutoa kipaumbele kwa mkoa huu muhimu na Mji wa Njombe ? (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimuahidi kwamba itaendelea kutoa kipaumbele kama ambavyo sasa hivi ina gari mbili, moja iko Njombe Mjini nyingine liko Makambako.

Tutaendelea kuimarisha utoaji wa gari hizi ili hatimaye kua-*address* matatizo ya majanga yakijitokeza katika mkoa huo, nashukuru.

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Zaidi ya miaka kumi Mkoa wa Katavi umekuwa hatuna gari la Zimamoto.

Je ni lini Serikali italeta gari la Zimamoto katika Mkoa wa Katavi?

**NAIBU SPIKA :** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika,Mkoa wa Katavi unalo gari moja la zimamoto lakini tunatambua kwamba ni bovu na liko kwenye matengenezo. Tutakachofanya ni kuharakisha matengenezo ya gari hili, ili angalau liweze kurejeshwa Katavi liweze kutoa huduma stahiki, nashukuru.

**NAIBU SPIKA :** Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Njelu Kasaka.

Na. 205

**Ujenzi wa Gereza Chunya**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kumalizia ujenzi wa Gereza Chunya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Gereza Chunya ulianza mwaka 2016 kama kambi kwa kujenga na kukamilisha bweni moja la kulala wafungwa, jiko la wafungwa na nyumba mbili za kuishi askari. Vilevile ujenzi uliendelea kwa jengo la utawala na nyumba mbili za kuishi askari ambapo upo kwenye hatua ya msingi. Aidha, katika mpango wa bajeti 2023/2024 Serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi milioni 50 ili kugharamia uendelezaji wa ujenzi wa Gereza Chunya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kiasi cha fedha ambacho kimetengwa takribani Milioni 50 tunashukuru, isipokuwa kiasi hiki ni kidogo sana kuweza kumaliza gereza hili. Swali la kwanza; kwa kuwa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani bado haijasomwa, je, hatuwezi tukaongeza hizi fedha ili gereza hili liishe kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa gereza hili linakwenda kuisha, sasa ni muda muafaka kuweza kupata vitendea kazi vya ofisi pamoja na gari. Je, Serikali inatuahidi nini ili tuweze kupata vitendea kazi hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunatambua ni kiasi kidogo Mheshimiwa Mbunge, lakini tulisema pamoja na ufinyu wa bajeti angalau gereza lile uendelezaji wake usisimame. Hata hivyo, nimuahidi tu kwamba kipaumbele baada ya mwaka huu 2023/2024 mwaka unaofuata 2024/2025, tutaongeza fedha za kutosha ili angalau ujenzi wake uwe wa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umuhimu wa kuwepo vitendea kazi, ofisi tumesema inaendelea kujengwa na gari tutapeleka kutokana na bajeti yetu itakavyoruhusu, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Gereza la Karanga lililopo Mkoani Kilimanjaro ni katika yale magereza ya awali sana Tanzania. Miundombinu yake ni chakavu na hasa nyumba za wafanyakazi. Je, ni lini Serikali itatupa kipaumbele kukarabati gereza hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ajiandae Mheshimiwa Kuchauka.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Karanga tunatambua ni chakavu na ni la muda mrefu, lakini ni gereza ambalo angalau lina miradi ya maana ikiwemo hiki Kiwanda cha Viatu. Jambo moja ambalo namuahidi Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba kupitia mapato yao ya ndani ikiwemo ya uuzaji wa viatu, waanze ukarabati lakini ngazi ya Serikali Kuu wataenda kutenga fedha kwa ajili ya kukrabati magereza makongwe ikiwemo Gereza la Karanga kadri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Gereza la Liwale pamoja na kwamba lina uzio wa miti, Mkuu wa Gereza amejenga nyumba tano *za two in One* na bado nyumba zile zimeishia kwenye linta. Je, Serikali haioni umuhimu wa kumwongezea fedha Askari yule ili wamalizie nyumba zile za maaskari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge, kwa wale wanaofanya juhudi kama Mkuu wa Gereza wa Liwale pamoja na juhudi za Mbunge ambaye anatoa fedha kwenye fungu lake kwa ajili ya kuliwezesha gereza hili, tutaendelea kuwa-*support* kwa kuwapa bajeti ili miradi kama hiyo iweze kukamilishwa ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta wawekezaji wengi nchini. Mwaka 2021 *GDP* ya Serikali ya Tanzania ilikuwa ni Bilioni 61 *USD Dollars,* leo Tanzania ni 85 *Bilion USD Dollars,* wawekezaji na wananchi wanataka kuona *CCTV* ndani ya mitaa yetu na haya madaraja yanayojengwa wakati wa usanifu wekeni *component* ya *camera* kwenye madaraja.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Shekilindi.

Na. 206

**Mpango wa pembejeo kwa wakulima wa mbogamboga**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa pembejeo wakulima wa mbogamboga nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika,, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa utoaji wa ruzuku za viuatilifu, mbegu na mbolea kwa mazao yote yanayozalishwa nchini. Kwa kipekee utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea ni kwa mazao yote ya nafaka, mbogamboga, mikunde na mazao mengine yote yaliyozalishwa na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wakulima ndio wananufaika na pembejeo za ruzuku, wanapaswa kujisajili kwa kuainisha mashamba na mazao anayozalisha na hivyo kuweza kununua pembejeo za ruzuku kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Serikali. Lengo la Serikali kutoa ruzuku za pembejeo kwa mazao yote, ni kupunguza gharama kwa wakulima, kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Masoko ya Wilaya ya Lushoto hupoteza zaidi ya tani 400 za mbogamboga na matunda kwa kila mwezi. Je, Serikali haioni sasa kuna haja

ya kujenga soko kubwa lenye *cold room* kwa ajili ya kuhifadhi mazao yale au mbogamboga zile ili wananchi wasiendelee kupata hasara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha kwa kuwapelekea wawezeshaji wakulima wa mbogamboga ili kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao yetu haya ya mbogamboga na matunda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekilindi, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Lushoto na Wilaya za Mkoa wa Tanga, Serikali sasa hivi inafanya tathmini ya kuangalia maeneo ya kujenga masoko, kwa sababu hatutaki kufanya makosa ambayo yamewahi kutokea huko nyuma katika baadhi ya miradi ambapo hata katika wilaya ya Lushoto, kuna jengo lililojengwa la Ubaridi *(cold room facility)* ambayo mpaka leo haitumiki. Kwa hiyo, nataka nitumie nafasi hii kumwambia Mheshimiwa Mbunge, hivi sasa tunavyoongea wataalam wa Wizara wako Mkoa wa Tanga wakiangalia wapi tuweke masoko ili tuweze kutatua tatizo la mazao ya mbogamboga na matunda hasa machungwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha:

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Jimbo la Hai kuna wakulima wengi wa mbogamboga wanaolima kwenye mashamba yao binafsi na kwenye vyama vya ushirika, lakini wakulima hao wanaathirika na migogoro iliyopo kwenye vyama vya ushirika. Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro kwenye Vyama vya Ushirika Makoa, Mrososangi, Mkundoo, Nkusinde,

Byamungo, Narumu na pale *Silver Bay* ili wakulima hawa waendelee na kazi yao ya kulima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwenye Chama cha Ushirika cha Kikafu chini, Mrososangi, Mkuu, Chama cha Makoa na baadhi ya vyama vingine na hata Chama Kikuu cha *KNCU* katika Mkoa wa Kilimanjaro kuna migogoro ambayo inaendelea. Nataka nimhakikishie tu kwamba Mrajisi wa Vyama Vikuu vya Ushirika, hivi sasa tumempa *ultimatum* kwamba kufikia tarehe 30, Mei awe amemaliza migogoro yote iliyopo na wawekezaji ambao wamekuwa chanzo cha migogoro hii katika vyama hivi. Serikali inaendelea kuchukua hatua za kisheria ili tuweze kuwachukulia hatua za kisheria kwa sababu wao kuwa wawekezaji hatuwezi kuwaruhusu waweze kutumia nafasi hiyo kuweza kuathiri vyama vya ushirika na kuruhusu ubadhirifu unaoendelea katika vyama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu kwamba Mrajisi wa Vyama Vikuu vya Ushirika anafahamu, kapewa *ultimatum* na asipochukua hatua za kinidhamu kwa viongozi wa vyama hivi, Serikali itamchukulia yeye hatua na tutamshauri Mheshimiwa Rais amwondoe katika nafasi hii kwa sababu nafasi aliyonayo ni ya uteuzi wa Mheshimiwa Rais.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na changamoto sana kwenye suala la masoko hasa katika kilimo cha zao la

parachichi na wakulima wamekuwa wakihangaika wenyewe. Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuna soko la uhakika katika zao hili la parachichi ambalo litaleta Tanzania pesa nyingi za kigeni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester, Mbunge wa Viti Maalum na mkulima wa parachichi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba parachichi ni moja zao ambalo linakuwa kwa kiwango kikubwa na hivi sasa kama Serikali tuko katika hatua za mwisho tukishirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kufungua Soko la China ambalo ni soko la uhakika. Vile vile, Waheshimiwa wataona kwamba Serikali imefanya kazi kubwa ya kufungua masoko mengi katika zao la parachichi. Mwaka huu 2023 zao la parachichi *export* imeongezeka kutoka katika tani 8,000 mpaka tani 29,000. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaendelea kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo inawakabili wakulima wa parachichi sio soko tu, ni miundombinu ya uhifadhi na miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo hayo. Nataka tu niwahakikishie kwenye bajeti mwaka kesho 2024/2025, mtaona mwaka huu 2023/2024 tunaanza kujenga *common use facility,* lakini mwaka 2024/2025, katika bajeti ya Wizara ya Kilimo kutakuwa na *program* mpya ya kuwasaidia wakulima 10,000, kuwachimbia visima na kuwapa *irrigation kit* za Hekta moja kwa kila mtu ili aweze kuweka katika shamba lake. Kwa hiyo Serikali inaendelea kufanya kazi hizo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea muda wetu unakwenda, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu lijibiwe...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee nimekupa nafasi huna haja ya kutazama nani anakujibu swali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba swali langu namba….

**NAIBU SPIKA:** *No, no, no*, sio kazi yako kuuliza Serikali nani anaYejibu, uliza swali lako hata mimi nitakujibu. Uliza swali usiseme Waziri wa Fedha hayupo pale.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** tatizo unaongea sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba swali langu namba 208, lijibiwe.

Na. 208

**Bajeti kwa jicho la jinsia**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutengeneza Bajeti kwa jicho la jinsia?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/2024 umetoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli kuzingatia masuala ya jinsia, wakati wa

uandaaji, uwasilishaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelekezo hayo, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo ikiwemo Shirika la Umoja wa Mataifa la Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake - *UN Women* inaendelea kushirikiana na Serikali kujenga uwezo katika maandalizi ya nyaraka za sera kwa kuzingatia masuala ya kijinsia. Aidha, katika mwaka 2022/2023, Wizara ya Fedha na Mipango imeunda kikosi kazi kwa ajili ya kuboresha Mwongozo wa maandalizi ya mipango na bajeti ya Serikali kwa jicho la kijinsia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hili suala sio jipya, limeanza toka mwaka 1997 kupitia *TGNP*, mwaka 2000 Serikali ikafanya mradi wa majaribio, mwaka 2010 kikaundwa hicho kikosi kazi anachokisema. Sasa kwa maelezo ya Waziri leo mwaka 2023 anasema kikosi kazi, maana yake anatuambia kwamba Serikali haiko *serious,* haijawa tayari bado kutimiza *commitment* zake za Mikataba ya Kimataifa iliyosaini? Kwa sababu sio jipya. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa hili jambo ni la muda mrefu hamwoni sasa kwa mwaka ujao wa fedha 2024/2025 ni wakati muafaka kwa Serikali kupitia Wizara hii kuelekeza kila Wizara kuja na tamko la kijinsia katika upangaji na utekelezaji wa bajeti yake? Dhamira ni Serikali ama wananchi wajue kila shilingi iliyopangwa mwanababa amefaidika vipi, mwana mama amefaidika vipi, kijana amefaidika vipi, mlemavu amefaidika vipi? Ndio *spirit* ya hii *concept.* Sasa hamdhani kama Wizara ya Fedha …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee, uliza swali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hawaoni sasa kwa mwaka ujao wa fedha 2024/2025, mwelekeze kila Wizara ije na tamko la bajeti la kijinsia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima James Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza Serikali haiko *serious?* Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko *serious* na tuko tayari kufanyia kazi masuala yote na maoni ambayo yanatolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, maoni yake tumeyachukua na tutakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Malleko.

Na. 207

**Kupeleka umeme katika vijiji na vitongoji vya Mkoa wa Kilimanjaro**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji na Vitongoji vya Mkoa wa Kilimanjaro ambavyo havina huduma ya umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Naibu Spika, Mkoa wa Kilimanjaro una jumla ya vijiji 519 ambapo mpaka sasa vijiji 11 tu havina umeme. Vijiji hivi vimepangwa kupatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA,* awamu ya tatu, mzunguko wa pili, ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kilimanjaro una vitongoji 2,260 na kati ya hivyo, vitongoji 286 tu ndiyo havina umeme. Vitongoji hivyo vitaendelea kupatiwa umeme kupitia Miradi ya Ujazilizi kwa kadri fedha zitakavyopatikana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza.; je, ni vigezo gani vinatumika kupanga ugawaji wa umeme kwa *urban peri -urban* pamoja na *REA?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni upi mpango wa Wizara katika kushughulikia malalamiko ya wananchi juu ya *tariff* kwa bei za umeme kuwa kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Malleko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la kwanza, *TANESCO* imekuwa ikipanga Mradi wa *REA* uende wapi na *Peri-Urban* uende wapi kulingana na taarifa zinazotolewa na TAMISEMI. Pia wenzetu wa TAMISEMI ndio wenye dhamana ya kusema hapa ni mjini na hapa ni kijijini, hapa ni Halmashauri ya Mji, hapa ni Jiji na hapa ni Manispaa. Kwa hiyo, sisi *TANESCO* tumekuwa tukipata taarifa za TAMISEMI na tunatumia hizo kupeleka Miradi ya *Peri-Urban* kwenye maeneo ya mijini na Miradi ya *REA* kwenye maeneo ya vijijini. Pia tumeendelea kushirikiana nao kubaini maeneo jinsi yanavyobadilika ili tuweze kufikisha huduma sahihi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili, katika hizi nchi za jirani na Tanzania, watu wenye bei za chini kabisa za umeme ambazo kimsingi kabisa zimewekewa ruzuku na Serikali ni Tanzania. Gharama za uzalishaji na usambazaji wa umeme Tanzania haziko na usawa na uwiano sahihi na gharama zinazolipwa na wananchi katika kupata ile huduma ya umeme na kuunganishwa. Kwa hiyo, gharama zetu ziko chini na sisi tunadhani kuna haja ya kuzitazama vizuri ili shirika liweze kuendelea kujiendesha na kuweza kutoa huduma sahihi kwa wananchi na kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, jiandae Mheshimiwa Leah. Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINE C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali iliahidi kuvipatia umeme vijiji vilivyopo katika Kata ya Mwamalili, Kolandoto, Chibe, Mwawaza na *Old* Shinyanga; je, ni lini Serikali itavipatia umeme vijiji hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu

swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, Shinyanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote ambavyo havikuwa na umeme na havina umeme hadi sasa viko katika Mradi Mkubwa wa Umeme wa *REA*, awamu ya tatu, mzunguko wa pili. Kufikia Desemba, 2023 tuna uhakika vijiji hivyo vitakuwa vimepata umeme kupitia mikataba ambayo tuko nayo na inayoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huo ndio tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza kilomita mbili katika ile kilomita moja tuliyokuwa nayo awali. Kwa hiyo wigo wa mradi utakuwa ni mpana zaidi kuweza kuwafikia wananchi wengi katika vitongoji kwa ajili ya kupata maendeleo kwenye maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuwasha umeme kwa wakati katika vijiji vya Jimbo la Meatu hususani kwenye kata ambazo zilikuwa hazijaguswa. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kusambaza umeme wa ujazilizi katika vitongoji vyote vya Jimbo la Meatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunashukuru kwa pongezi angalau kuna maeneo ambapo Mradi wetu wa *REA III, round II* umekamilika ikiwemo Mkoa wa Simiyu na tunaendelea kuhakikisha kwamba na maeneo mengine

mradi unakamilika. Katika vitongoji kama nilivyotangulia kusema tayari tumepata fedha kwa ajili ya kuongeza wigo kutoka kilomita moja hadi kilomita tatu ambazo zitafika katika vitongoji vingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali inatafuta fedha nyingi zaidi za kuweza kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote takribani 36,000 ambavyo vimebaki Tanzania visivyokuwa na umeme takribani shilingi 6,500,000,000,000 na tunaamini zitapatikana na umeme katika miaka minne, mitano au sita ijayo, vitongoji vyote Tanzania vitafikiwa na huduma ya umeme.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Manyanya.

Na. 209

**Uhaba wa maji katika Vijiji vya Mwambao wa Ziwa Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia maji Vijiji vilivyopo mwambao wa Ziwa Nyasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika; naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Ziwa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwambao wa Ziwa Nyasa una vijiji 39 na kati ya hivyo vijiji 18 vinapata huduma ya maji na vijiji 21 havina. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali inatekeleza Miradi ya Maji ya Lituhi, Liuli, Ngumbo, Puulu,

Songambele na Nangombo-Kilosa, inayotarajia kukamilika katika mwaka wa fedha 2023/2024 na kunufaisha vijiji 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali ipo katika hatua za mwisho kukamilisha usanifu wa Mradi wa Maji Ndengele-Mbuyula utakaohudumia vijiji vitatu na itaendelea na usanifu katika Kijiji cha Ndonga. Ujenzi wa miradi hii utafanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza ninashukuru sana Serikali kwa jitihada ambazo zimeshaanza kufanyika katika ukanda wa Ziwa Nyasa. Kwa kuwa, Jimbo hili lina pande kuu mbili za Umatengo na Ziwa Nyasa, katika eneo hili la Umatengo kuna Kata ya Lumeme Kijiji cha Luhindo, Uhuru na Mipotopoto lakini pia Kata ya Luhangalasi zina tatizo kubwa sana la maji.

Je, Wizara ina mpango gani wa kupeleka fedha za dharura kwa ajili ya kuvisaidia vijiji hivi angalau hata kama ni Shilingi Milioni Moja.

Swali la pili, katika ukanda wa mwambao uliozungumzia kuna Kijiji cha Mtupale na Chiwimbi hivi havijazungumzwa, Je, mpango wa Serikali ni nini ili kuhakikisha na wenyewe wanapata maji?*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya, Wizara ya Maji pamoja na mpango mkakati wa kuhakikisha tunatumia rasilimali toshelevu, kwa maana ya mito na maziwa Wizara ya Maji imejipanga sasa hivi tuna mitambo katika kila Mkoa, moja ya maelekezo ambayo niyatoe na tunashirikiana na Mheshimiwa Mbunge eneo hilo

ambapo kama kuna tuwezekano wa kupata maji ya kisima basi tutachimba kwa haraka kuhakikisha wananchi wake wanaanza kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tarehe 10 Mei, bajeti yetu ya Wizara ya Maji tunawasilisha kwa hiyo moja ya mikakati mizuri ambavyo tumejipanga ni kuhakikisha tunakamilisha changamoto ya maji kwa kiwango kikubwa sana. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fedha ya dharura iliyotoka Wizarani kwako Mheshimiwa Waziri, bado haijamaliza changamoto ya maji Jimbo la Nkasi Kaskazini. Tunapenda kufahamu mchakato wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kusambaza kwenye Mkoa wa Rukwa umefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu Mwenyezi Mungu ameijalia tuna rasilimali za maji juu ya ardhi na chini ya ardhi mita za ujazo bilioni 126, maji yaliyokuwa juu ya ardhi ni zaidi ya mita za ujazo bilioni 105. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha tunatumia rasilimali hizi toshelevu kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mpango mkakati wa Wizara yetu ya Maji na tutawasilisha katika bajeti yetu ya Terehe Kumi Mwezi wa Tano ni kuhakikisha tunatumia Ziwa

Tanganyika kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji Kigoma, Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Katavi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Nyamoga kwa niaba ya Mheshimiwa Amandus.

Na. 210

**Mradi wa maji kutoka Kihesa Mgagao hadi Masalali – Kilolo**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE K.n.y. MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji wa Kihesa Mgagao, Masege hadi Masalali - Kilolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi wa maji katika vijiji vya Kihesa Mgagao, Masege hadi Masalali upo kwenye hatua za mwisho za kumwajiri Mkandarasi. Utekelezaji wa mradi utaanza Mwezi Mei, 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Mei, 2024. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa matenki matatu (3) yenye jumla ya ujazo wa lita 250,000, ujenzi wa mtandao wa mabomba ya maji yenye urefu wa kilometa 25.4 na ujenzi wa vituo 25 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wananchi wapatao 9,006 waishio kwenye vijiji hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kuna baadhi ya vitongoji katika vijiji hivyo havijawekwa kwenye orodha ya mpango wa kuwekewa vitu kwa ajili ya kuchotea maji. Je, Serikali inaweza kupokea maombi mapya sasa maalum kwa ajili ya kuongeza vituo vya kuchotea maji kwenye vijiji ambavyo vimepitiwa na mradi huu?

Swali la pili, miradi mingi kwenye Halmashauri zetu imekwama kwa sababu ya upatikanaji wa mabomba ambayo yananunuliwa kwa pamoja kupitia *RUWASA* Makao Makuu. Je, Serikali sasa inatuhakikishiaje kwamba mabomba sasa yanakwenda kupatikana kwa wakati ili kutokukwamisha miradi mingi kwenye Halmashauri zetu?

**NAUBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jukumu mahsusi na Wizara ya Maji ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama, tunao huu mradi mkubwa ambao unajengwa na kuna baadhi ya vitongoji ameviainisha ambavyo vinahitaji maji, nataka nimhakikishie kukamilika kwa mradi huu na hivyo vitongoji navyo vitapokea kuhakikisha nao wanapata huduma ya maji safi na salama.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji Vijijini ni kuhakikisha tunatatua changamoto

ya maji katika maeneo ya vijijini. Tulikuwa na changamoto ya manunuzi na tumepewa ombi na maelekezo ya Bunge ni kuhakikisha manunuzi haya yanafanyika katika maeneo ya Mikoa, tulishakaa na wenzetu wa manunuzi kwa maana ya *RUWASA* maelekezo ya Wizara ni kwamba manunuzi yote yanatakiwa kufanyika katika Mikoa husika ili kuharakisha utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mnamo mwaka 2021 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliweka Jiwe la Msingi wa ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji cha Kifura ambao wakati huo ulikuwa asilimia 43, mpaka leo mradi huo umetelekezwa na uko asilimia 43 hiyohiyo. Je, ni nini mpango wa Serikali kutenga fedha ili kukwamua mradi huu wa maji ili wananchi wa Kifura waweze kupata maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, kubwa mradi huu wa Kifura ni mradi ambao ulikuwa unatekelezwa na kampuni ya Nangai pamoja na taasisi ambayo inaitwa *ENABEL,* tulikuwa na changamoto baina ya huyu Mkandarasi na hii taasisi, tumekwisha kaa nao na moja ya maelekezo ambayo tumempatia yule Mkandarasi, Tarehe 31 Agosti, akabidhi mradi huo ili wananchi wa Kifura waendelee kupata huduma ya maji safi na salama.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar jiandae Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kuipongeza Serikali ya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kusambaza maji vijijini. Je, wizara iko tayari kushusha bei ya maji Wilaya ya Nyang'hwale kutoka 1,700 kwa *unit* na kufanya iwe 1,500 ili kuhamasisha wananchi wengi kuweza kujiunga na mtandao huo wa maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni haki ya mwananchi kupata huduma ya maji lakini mwananchi naye asisahau anao wajibu wa kulipia *bill* za maji. Kwa hiyo, ameonesha hiyo changamoto na nimuombe basi Saa Saba tuweze kukaa na timu yetu tuone namna nzuri ya kuhakikisha wana Nyang'hwale tunatatua changamoto hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu ajiandae Mheshimiwa Oliver

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naishukuru sana Serikali kwa kutusaidia kuweka miradi ya maji kwenye vijiji takribani Vinne kikiwemo Kijiji cha Matare pale katika Jimbo la Singida Mashariki. Hoja yangu na swali langu Mheshimiwa Waziri, mradi umekamilika na Mkandarasi amemaliza kazi changamoto iko kwenye umeme na tumeshalipia watu wa *TANESCO* mpaka leo umeme haujawekwa.

Je, ni lini Serikali itahakikisha umeme unawekwa ili wananchi wa Matare waanze kutumia maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Wizara ya Maji inafanya

kazi kwa ukaribu sana na Wizara ya Nishati na wamekuwa msaada mkubwa kwetu, hili jambo tutalifuatilia kwa haraka kuhakikisha ujenzi wa eneo hilo linakamilika kwa haraka. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Mradi wa Maji Kyerwa, Nyaruzumbula mpaka Kamuli ni lini utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyoeleza Tarehe 10 mwezi Mei, tunawasilisha bajeti yetu, nataka nimhakikishie kama Mheshimiwa Rais alivyosema mambo ni moto, mambo ni *fire* tutakwenda vizuri katika kuhakikisha jambo hili linaenda vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

Na. 211

**Hitaji la maji Kata za Msalala**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Kata za Ikunda, Mwakata, Menga, Shilela na Lunguya - Msalala?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa upanuzi wa miradi ya maji ya Mhangu - Ilogi na Nduku - Busangi itakayohudumia Kata za Ikunda, Mwakata, Menga, Shilela na Lunguya zilizopo Wilayani Msalala. Kwa sasa taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea na ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri mradi wa Nduku - Msangi – Ntobo ni mradi ambao umechukua muda mrefu sana, kwa hatua iliyofikiwa sasa wameweza kukosa kiasi cha Shilingi Milioni 50 tu kwa ajili ya Mkandarasi kuchimba mtaro, kuchelewa kwa mradi huu kumesababisha sasa Hospitalli ya Wilaya ya Ntobo kukosa maji na hivyo kupelekea mlipuko wa magonjwa mbalimbali kwenye hospitali ile ya Wilaya.

Je, ni lini sasa Wizara itatoa kiasi hiki kwa dharura ili ipeleke fedha hizo hospitali ya Wilaya iweze kupatiwa maji?

Swali langu la pili, Kata niliyoitaja hapa kwa maana ya Mwakata imepitiwa na bomba kuu linalotoka Kagongo kwenda Isaka na Kata hii haina maji. Je, ni nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Kata hii na yenyewe inanufaika na maji hayo kwa sababu bomba hilo limepita maeneo hayo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Kaka yangu wa Msalala kwamba Wizara ya Maji mwezi huu tumepokea Bilioni 67 kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi. Kwa hiyo, moja ya maeneo ambayo tutayapa kipaumbele cha haraka ni eneo la Msalala kuhakikisha mradi huu unakamilika na wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni juu ya mradi ambapo bomba kuu linapita. Sera inasema bomba kuu linapopita vijiji ambavyo vipo karibu na kilomita 12 kulia na kushoto mwa bomba kuu, vinahakikishiwa kwamba vinapata huduma. Nataka nimhakikishie hili tumelipokea na tunaenda kulifanya kazi kuhakikisha kwamba Kata hiyo nayo inapata huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, Mheshimiwa Gwajima na Mheshimiwa Hawa wajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri ulituahidi mwaka jana kwenye Bunge la Bajeti ungetuchimbia visima katika shule za Kata ndani ya Manispaa ya Iringa, ulipokuja kwenye Wizara Rais mwezi wa Agosti uliahidi kuleta gari katika Mkoa wa Iringa ili tuweze kupata huduma hiyo ya visima, sasa hatijachimbiwa visima mpaka leo.

Swali langu ni kwanza huogopi kwenda motoni? Namba Mbili mnatuchimbia lini visima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, tuliomba kuwa na magari kwa ajili ya uchimbaji visima katika kila Mkoa, magari yale tumekwishayapata na katika kila Mkoa tumekwishayapeleka. Ninamuomba Mheshimiwa

Mbunge katika yale maeneo ambayo anaona tunahitaji uchimbaji visima, kwa sababu vitendea kazi tunavyo, hatuna kisingizio chochote. Kwa hiyo, jukumu letu ni kuhakikisha maeneo ambapo panatakiwa kuchimbiwa visima tunakwenda kuchimba visima. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gwajima ajiandae Mheshimiwa Hawa.

**MHE. ASK. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mradi mkubwa wa maji unaotokea Ruvu Chini kukamilika lakini baadhi ya Kata za Jimbo la Kawe kama Mbezi Juu hazina maji kabisa. Nini kauli ya Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kubwa mradi ule mkubwa tumeshaukamilisha na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika wiki ya maji alikuja kuuzindua, kazi iliyobaki ni suala zima tu la usambazaji. Kwa hiyo, kikubwa tutaongeza kasi juu ya usambazaji maeneo haya ya Mbezi Juu na maeneo mengine kuhakikisha kwamba wanapata huduma ya majisafi na salama

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo imenufaika na mradi wa maji ya Ziwa Victoria. Jimbo la Tabora Mjini ni moja kati ya Majimbo hayo ambayo yamepata maji hayo lakini Kata zilizoko pembezoni mpaka sasa hazijanufaika na maji hayo.

Je, Serikali mna mpango gani wa kupeleka fedha ili iwasaidie kusambaza maji na wananchi wetu waweze kunufaika na mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuthamini kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali, kulikuwa na mradi mkubwa zaidi ya Bilioni 600 kuyatoa maji Ziwa Victoria kuyapeleka Tabora, Nzega hadi Igunga. Nataka nimhakikishie maeneo hayo yote ya pembezoni ambayo yanahitaji maji tutayafikia kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama na tutatoa fedha Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; tunao wageni waliopo Jukwaa la Spika ni wageni wawili wa Mheshimiwa Spika ambao ni Ndugu Mary Mwenisongole, Katibu wa CCM Wilaya ya Mbinga, karibu na Ndugu Enock Joseph, Afisa Makao Makuu ya CCM, karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni viongozi wa Soko la Kimataifa la Samaki Ferry kutoka Magogoni Jijini Dar es Salaam ambao ni Ndugu Benetson Lutenta - Mwenyekiti, Ndugu Mbaraka Kilima – Mjumbe na Ndugu Christina Kalekezi – Mjumbe, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni viongozi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe - Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Daniel Mushi - Naibu Katibu Mkuu (Mifugo), Ndugu Agnes Meena - Naibu Katibu Mkuu

(Uvuvi), pia wameambatana na Watendaji Waandamizi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ni Mheshimiwa Suleman Masoud Makame - Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Ndugu Mariam Abdallah Ibrahim - Mke wa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega. Sasa Mama Ulega siku nyingine ukija uvae rangi tofauti hicho kitambaa *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wengine ni Sheikh Mustafa Rajab - Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; Sheikh Khamis Mtupa - Sheikh wa Mkoa wa Pwani; Sheikh Khammas Abdurahmani Mzee - Sheikh wa Wilaya ya Mkuranga; Ndugu Salimin Buda - Katibu Baraza la Masheikh Mkoa wa Pwani; Father Ayubu Mwang'onda - Baba Paroko Kanisa Katoliki Mkuranga; na Mchungaji Adamu Kitungulu Ngunda - Kiongozi KKKT Mkuranga. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Mwinshehe Shabani Mlao - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani; Dkt. Blandina Lugendo - Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi *(FETA);* Profesa Yunus Mgaya - Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi *(TAFICO);* Ndugu Yahaya Mgawe - Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi *(TAFIRI);* Profesa Zacharia Massanyiwa - Mwenyekiti wa Bodi ya Maziwa Tanzania; Ndugu Clement Tesha - Mwenyekiti wa Bodi ya Nyama Tanzania; Prof. Sebastian Chenyambuga - Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi *(TALIRI);* Ndugu Selina Lyimo - Mwenyekiti wa Bodi ya Maabara ya *Veterinary* Tanzania; Ndugu Fuad Jaffer - Mkurugenzi Mtendaji *ASAS;* Ndugu Mark Tsoxo - *Country Director* wa *Heifer International;* Ndugu Said Meck Sadick - Mkurugenzi wa *SAMEKI Ltd.* na Mkuu wa Mkoa Mstaafu; Ndugu Shehai Amdani - *DPPR* Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni saba wa Mheshimiwa Mohamed Monni ambao ni Wenyeviti wa UVCCM wa Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mhandisi Jalali Mkunji - Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Chemba. *(Makofi)*

Wapo wageni nane wa Mheshimiwa Boniphace Getere ambao ni Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 47 wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari Ayalagaya ya Babati Vijijini wakiongozwa na Mkuu wa Shule hiyo Mwalimu Stephen Naman. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni watumishi 134 na walimu 26 kutoka Shule ya Msingi Mtube ya Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nyongeza ya wageni waliopo Jukwaa la Spika ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni Ndugu Lucas Mhavile, Mchekeshaji na Balozi wa Maziwa ya *ASAS,* kwa jina lake maarufu ni Joti. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nina mgeni mahsusi ambaye ni mtoto wangu, Ndugu Haji Manara. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, haya makofi hakuyajia hapa, hapa kaja na lingine, hapa ni Balozi wa Maziwa ya *ASAS*. Naona makofi yamekuwa madogo.

Tunaye Ndugu Salama Jabir, Mtangazaji na Balozi wa Maziwa ya *ASAS*; Ndugu Steven Magombeka, *Brand Manager* wa *ASAS;* Ndugu Frank Njabudenge, Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB);* na Ndugu Jackline Mocho, Mkurugenzi wa *IFAD*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo aliniletea ombi kwenye hotuba yake anataka kutoa pongezi kwa baadhi ya vilabu. Nimempa masharti, timu moja tu. Sasa nitatizama kama atafuata masharti ya kiti au laa! *(Makofi)*

Katibu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Cecil.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil sio jina lako hilo!

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo nimesimama.

**NAIBU SPIKA:** Sasa mbona husemi, unaanza ku… *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tupo wawili.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Naitwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mbunge.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. Kuna suala linaloendea sasa hivi, baada ya Jeshi la Polisi kutangaza kuhusu suala la ukaguzi wa leseni za madereva Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba ajali nyingi zinazotokea zina sababu nyingi, ikiwemo uzembe wa madereva, pamoja na barabara zetu, baadhi ya maeneo zinasababisha ajali, lakini tangazo limetoka kutoka kwa *IGP* anawataka madereva wote wafanyiwe ukaguzi wa leseni zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Wabunge wengi hapa ndani tunaendesha magari na ni madereva, lakini wengi hatujapita kwenye vyuo vya udereva; na wasiokuwa na sifa wanaenda kufutiwa leseni zao. Tafsiri yake ni kwamba tutaenda kupoteza ajira za watu wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nifahamu na utupe mwongozo wako kuona kama jambo hili ni sahihi kufanyika sasa hivi, kama vipi basi, Jeshi la Polisi liongeze muda ili waweze kukagua hivyo vyeti vya madereva pamoja na kupitia upya hizo leseni zao.

**NAIBU SPIKA:** Umesoma vizuri hiyo kanuni? Hili jambo limetokea leo Bungeni humu? Serikali imesikia hoja yako, baadaye utaonana na Waziri wa Mambo ya Ndani umweleze hoja yako.

Mheshimiwa Lemburis.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, …

**NAIBU SPIKA:** Kanuni gani?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 76 lakini naomba kujikita kwenye Kanuni ya 55 (2) (a) na (c) na cha (3) (a), (b) na (c) na kifungu kidogo cha (4).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limetokea hivi karibuni kwa maana ya kuzimika kwa taa kwenye Uwanja wa Taifa wakati *Taifa Stars* wakicheza na Uganda. Ilikuwa ni taharuki ya mechi kutulia kwa muda mrefu bila kuchezwa, lakini juzi tena tarehe 30 wakati Yanga na *Rivers* ya Nigeria wakicheza, taa zilizimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haina maana kwamba Taifa halipati aibu nje ya nchi, ukizingatia kwamba wanaocheza ni nchi nyingine na Tanzania, huko nje tunatizamwa katika jicho ambalo siyo la kulijengea heshima Taifa letu. Ni kwa nini jambo hili linajirudia mara kwa mara? Naomba mwongozo wako, Serikali haiona kwamba inatutia aibu katika jambo hili bila kuchukua hatua za makusudi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, Mheshimiwa Lemburis ameomba mwongozo wake, sina haja ya kuurudia. Kwa vile jambo halijatokea hapa, lakini amekwenda kwenye Kanuni ya 55, amezungumza hoja yake. Ni hoja ya msingi, lakini Serikali imeshachukua hatua ya watu ambao wamehusika na hilo jambo, na hatua zinaendelea kuchukuliwa na uchungzi unaendelea kufanywa.

Sisi ambao ni watu wa karibu sana na masuala ya mpira tunajua kinachoendelea, na Serikali ipo makini. Kuna ukarabati mkubwa unaendelea sasa hivi, ambao *tender* nafikiria inafunguliwa leo ambapo imekaribisha wazabuni kutoka nchi za nje kuweza kufanya *full* ukarabati kwenye uwanja wetu wa Taifa ili mambo kama hayo yasitokee tena.

Nakushukuru sana. Tunaendelea. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu 99 – Mifugo, na Fungu 64 – Uvuvi, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/2023 na makadirio ya mapato ya matumizi ya fedha ya mwaka 2023/2024 kwa Fungu 99 – Mifugo, na Fungu 64 - Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma na mwingi wa ukarimu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha hotuba yangu ya kwanza siku ya leo.

Aidha, kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi na kumteua Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge kuwa Naibu Waziri. Tunaahidi kutumia uwezo wetu wote kutekeleza wajibu wetu kwa ufanisi na uadilifu na kuhakikisha rasilimali za mifugo na uvuvi zinasimamiwa na kutumika kikamilifu, kulichangia mapinduzi ya uchumi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wake mkubwa anaouonesha katika kuiongoza nchi yetu na kuifanya iendelee kupiga hatua kubwa za maendeleo za kiuchumi, kijamii kisiasa na kuaminika Kimataifa. Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoshirikiana na Mheshimiwa Rais kuwaletea maendeleo Watanzania. Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunaahidi kuendelea kuwaunga mkono na kutekeleza dira, miongozo na maelekezo wanayoyatoa katika kuwatumikia wananchi hususan wafugaji, wavuvi, wachakataji, wasindikaji na wafanyabiashara ya mifugo na Samaki, na mazao yake kwa maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi kuwaombea viongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu wawe na afya, na Mwenyezi Mungu awape hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu. Vile vile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea na usimamizi mahiri wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kazi nzuri ya uratibu na usimamizi wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru na kumpongeza kwa hotuba yake nzuri ambayo imebainisha malengo na kazi zinazotekelezwa na Serikali kwa mwaka 2023/2024. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo tayari kutekeleza

malengo hayo ili kuwaletea maendeleo wananchi na kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, na Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni wazi kuwa chini ya uongozi wenu, Bunge letu la Kumi na Mbili limeendelea kuwa mahiri katika kuisimamia na kuishauri Serikali na hivyo kuongeza ufanisi katika kusimamia rasilimali za umma na kuwatumikia wananchi. Aidha, napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Bunge kwa kuteuliwa kuongoza Kamati hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo; Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri kuwa Makamu Mwenyekiti; na Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuwa Wajumbe wa Kamati. Tunaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao na usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati kwa maelekezo na ushauri wao mzuri walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango bajeti ya Wizara ya mwaka 2022/2023 na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri, mapendekezo na maoni ya Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara Profesa Riziki Silas Shemdoe na Naibu Makatibu Wakuu; Dkt. Daniel Elius Mushi upande wa Mifugo; na Bi.

Agnes Kisaka Meena, upande wa Uvuvi, kwa kuwa viungo muhimu kati yangu na watumishi na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naiu Spika, kipekee nawashukuru kwa dhati na kuwapongeza Watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuiendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mkuranga, Mkoani Pwani kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuhakikisha nawawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu pamoja na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuishukuru familia yangu, hususan mke wangu kipenzi, Bi. Mariam Abdallah Ibrahim, na watoto wangu kwa kunivumilia na kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kuwapa pole, wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa na mashabiki mbalimbali wa Klabu ya Simba kwa matokeo yaliyopatikana kule Morocco. Hata hivyo, naomba pia niipongeze Timu ya Simba kwa kiwango kizuri walichoonyesha kwenye pambano lile. Nitumie nafasi hii pia kuipongeza sana Klabu ya Wananchi, Klabu ya *Yanga Africa* kwa kufanikiwa kuingia hatua ya nusu fainali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, muda wako ni mdogo sana, hebu endelea na hotuba. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza Klabu ya Yanga

kwa kufanikiwa kuingia hatua ya nusu fainali ya Kombe la *CAF*. Tunaitakia heri klabu yetu hii iweze kufika fainali na hatimaye ichukue Kombe hili la *CAF* na kuipa nafasi Tanzania. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia uniruhusu niseme ya kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Mifugo na Uvuvi ni utajiri. Kwa sababu hiyo, maono ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika muda wake huu wa miaka miwili aliyokaa madarakani, tumeshuhudia ya kwamba mifugo yetu na uvuvi ina uwezo wa kutuingizia fedha nyingi kuliko tulivyofikiri pale awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 kwa mara ya kwanza Taifa letu limeshuhudia, tumeuza nyama nje ya Taifa letu kutoka tani 1,700 mpaka tani 12,000. Hii yote ni kutokana na diplomasia nzuri ya kiuchumi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2023/2024 kwa Fungu 99 - Mifugo, na Fungu 64 – Uvuvi ambayo pia inapatikana katika vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge na tovuti ya Wizara www.mifugouvuvi.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, maeneo ya kipaumbele katika mwaka 2022/2023. Katika mwaka 2022/2023 Wizara ilianza kutekeleza mpango wa mabadiliko ya Sekta ya Mifugo ili kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na pato la Taifana kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa ni kuimarisha huduma za maji, huduma za malisho na vyakula vya mifugo; kuwezesha

upatikanaji wa mbegu bora za mifugo; kuimarisha afya ya mifugo; kuboresha huduma za ugani; kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo; kuimarisha masoko na kuwezesha uongezaji thamani mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Fungu 99 ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 40. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, kiasi cha shilingi 19.9 tumeweza kuzikusanya. Katika mwaka 2022/2023, bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kupitia Fungu 99 ilikuwa ni Shilingi bilioni 92, ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 21.3 zilikuwa ni mishahara, shilingi bilioni 24, matumizi mengineyo na shilingi bilioni 46 kwa ajili ya kuteleza miradi ya maendeleo, ikijumuisha shilingi milioni138. 9 fedha za nje kwa ajili ya miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Machi 31, 2023, shilingi bilioni 29.6 zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 65.4 ya shilingi bilioni 45.3 zilizotengwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.4 zimetumika kulipa mishahara na shilingi bilioni 14.2 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 27.2 sawa na asilimia 58.4 ya shilingi bilioni 46.7 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, zimepokelewa na kutumika hadi Machi 31, 2023. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 27 ni fedha za ndani na shilingi milioni 106 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya sekta ya mifugo; katika mwaka 2022/2023 idadi ya mifugo nchini imeongezeka kutoka ng'ombe milioni 35.3 hadi ng'ombe milioni 36.6 na mbuzi kutoka milioni 25.6 hadi mbuzi milioni 26.6 na kondoo kutoka milioni 8.5 mpaka milioni 9.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuku wameongezeka kutoka milioni 92.8 hadi milioni 97.9 ambapo kuku wa asili

wameongezeka kutoka milioni 42.7 hadi milioni 45.1 na kuku wa kisasa kutoka milioni 50.1 hadi milioni 52.8 na nguruwe kutoka milioni 3.4 hadi milioni 3.7. Aidha ukuaji wa Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2021 umefikia 5.0% na kuchangia 7% kwenye Pato la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022 ng'ombe 2,218,293 pamoja na kondoo 2,121,187 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.7 waliuzwa katika minada mbalimbali ya hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe milioni 2.19 pamoja na mbuzi na kondoo milioni 1.7 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 waliouzwa katika mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa 4.3% kutoka tani 769,966 mwaka 2021 hadi tani 803,264.3 mwaka 2022/2023. Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 3.4 mwaka 2021 hadi lita bilioni 3.6 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la 5%. Vipande vya ngozi milioni 14 vimezalishwa mwaka 2022 ikilinganishwa na vipande vya ngozi milioni 13.6 zilizozalishwa mwaka 2021/2022. Uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai bilioni 4.9 mwaka 2021/2022 hadi bilioni 5.5 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la 13%.

Mheshimiwa Naibu Spika, 35% ya kaya zilizopo nchini zinajishughulisha na ufugaji. Kati ya hizo, 39.3% wanafuga ng'ombe, 36.2% wanafuga mbuzi, 13.5% wanafuga kondoo na 10.9% wanafuga nguruwe. Aidha 55.4% ya kaya hizo pia hujishughulisha na ufugaji wa kuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Mifugo, Sera, Sheria na Kanuni; katika mwaka 2022/2023 Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na kuandaa rasimu. Aidha sheria tisa za Sekta ya Mifugo zimefanyiwa urekebu kwa maana ya *revision* ambapo zinasubiri kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Vilevile marekebisho yamefanyika kwa kanuni mbili

zilizo chini ya Sheria ya Magonjwa ya Nyama sura 156 pamoja na Sheria ya Tasnia ya Nyama sura 421 tafsiri na kanuni kwa Lugha ya Kiswahili. Aidha kutoka katika Lugha ya Kiingereza kwenda katika Lugha ya Kiswahili. Aidha Wizara imetangaza notisi ya wakaguzi wa ngozi 101 yenye *GN* namba 285 ya mwaka 2023 kupitia Sheria ya Biashara ya Ngozi sura namba 120.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji, malisho na vyakula vya mifugo. Katika mwaka 2022/2023 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetambua na kuyasajili maeneo 77 ya malisho yenye jumla ya hekta 994,827 kutoka kwenye halmashauri nane za wilaya ambapo maeneo hayo yametangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa *GN* namba 597 ya tarehe 7 Oktoba, 2022. Pia Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi imetenga jumla ya hekta 195,028 za maeneo ya malisho katika halmashauri za wilaya 14 na hivyo kufanya maeneo ya malisho yaliyotengwa kufikia hekta 3,384,485 kutoka hekta 3,189,456 mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la 6.1%

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 kilo 22,691 za mbegu bora za malisho zilizalishwa ikilinganishwa na kilo 4,481 zilizozalishwa mwaka 2021/2022. Pia marobota 248,209 ya *hay* yamevunwa katika mashamba ya Serikali na ya watu binafsi. Aidha taarifa kuhusu ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo inapatikana katika Ibara ya 64 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeanzisha mashamba darasa 100 ya malisho yenye ukubwa wa ekari 520 katika halmashauri 44 na kusambaza mbegu tani 8.56 kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa na wafugaji binafsi kuendeleza ufugaji kwenye Kijiji cha Msomera.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza eneo la wafugaji la Msomera, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kupima na kutenga vitalu vya ufugaji 112 vyenye ukubwa wa hekta 100 kila kimoja kwa ajili ya malisho;

(ii) Kujenga, bwawa la maji;

(iii) Kujenga majosho sita na kukarabati moja;

(iv) Wizara pia imehimilisha ng'ombe 1,252;

(v) Tumeanzisha mashamba darasa manne yenye ukubwa wa ekari 10 kila moja na kuyapatia mbegu za malisho kilo 280;

(vi) Kusambaza mbegu za malisho kilo 110 kwa wafugaji binafsi; na

(vii) Kusaidia uhamishaji wa mifugo 13,937 kutoka Pori Tengefu la Loliondo kwenda Msomera.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kwa kushirikiana na *Heifer International* wananchi wamehamasishwa kuunda ushirika wa wafugaji wamefundishwa usindikaji mdogo na biashara ya maziwa, pia tumefanikiwa kujenga kituo cha kisasa cha ukusanyaji wa maziwa katika eneo hili la Msomera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzalishaji mbegu bora na masoko, katika mwaka 2022/2023 Wizara imezalisha dozi 116,558 za mbegu bora za ng'ombe katika Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji *(NAIC)* pale Arusha pia ng'ombe 60,697 wamehimilishwa nchini ikilinganishwa na ng'ombe 64,463 waliohimilishwa mwaka 2021/2022. Aidha madume bora 366

ya ng'ombe yamenunuliwa na kusambazwa kwa vikundi vya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara imejenga minada 19, kukarabati minada minne ili kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo. Pia tumenunua minada 82 na tunaendelea kusambaza kwenye minada.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya ya mifugo, hadi Oktoba 30 mwaka 2022 jumla ya mifugo 5,292,738 wametambuliwa na kusajiliwa kwenye Mfumo wa Utambuzi. Katika mwaka 2022/2023 lita 52,560 za dawa za kuogesha mifugo zenye thamani ya shilingi bilioni 2.39 zimenunuliwa na kusambazwa. Aidha ujenzi wa majosho 257,000 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 83 unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 jumla ya dozi 243,365,631 za chanjo zimetolewa kwa mifugo mbalimbali dhidi ya magonjwa mbalimbali ikilinganishwa na dozi 223,592,415 zilizotolewa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ugani wa mifugo. Katika mwaka 2022/2023 Wizara imenunua pikipiki 1,200 kwa ajili ya maafisa ugani na magari 13 kwa ajili ya kuratibu huduma za ugani katika *Secretariat* za Mikoa. Pia yametolewa mafunzo rejea kwa maafisa ugani 515, aidha maafisa ugani 3,018 kati ya 3,201 wamesajiliwa katika mfumo wa M-Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Wizara imeanzisha vituo atamizi vinane vyenye uwezo wa kuwa na vijana 240 kwa wakati mmoja. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya vijana 238 wakiwemo vijana wa kike 71 na vijana wa kiume 167 wamesajiliwa. Vijana hao wamewezeshwa kununua ng'ombe 2,222 ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa ajili ya utekelezaji wa mpango ambapo kila mnufaika atapatiwa ng'ombe 10 wa kunenepesha na

kuwauza kila baada ya miezi mitatu kwa awamu nne kwa mwaka hadi anapohitimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe taarifa ya kwamba ng'ombe hawa 10 kama mbegu, kijana yule anapomaliza mafunzo yale ndiyo mtaji na tumemuandalia eneo katika maeneo ya ardhi ya Serikali aweze kwenda kunenepesha waweze kuzalisha nyama nzuri, tuingize viwandani na hatimaye tuweze ku-*export* nyama ya kutosha kwenda katika mataifa yanayohitaji, na hii itatoa ajira na itakuwa ni fursa kwa vijana wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya Ranchi ya Taifa ya *NARCO,* ili kuimarisha utendaji wa *NARCO* Wizara imeanza kutekeleza mpango wa mabadiliko wa miaka mitatu 2022/2023 hadi 2024/2025 wenye vipengele vitano ambavyo ni uboreshaji wa mbari za mifugo, uendelezaji wa malisho na vyakula vya mifugo, unenepeshaji wa mifugo, skimu za unenepeshaji kupitia vijana na wanawake na uendelezaji wa masoko. Aidha utekelezaji wa maeneo hayo umehusisha uwekezaji wa shilingi bilioni 4.6 zilizotengwa kutoka Serikalini zilizowezesha kununua ng'ombe wazazi 1,000, matrekta mapya manne, Matela manne, Beila za kukusanyia majani tatu, reki moja na kuchimba visima virefu saba katika Ranchi za Kongwa, Mnzeri na Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jambo hili kwa mara ya kwanza toka *NARCO* imeanzishwa na baada ya kuonekana kuwa imepotea na sasa kwa haya tunayoyafanya, naomba nichukue fursa hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya wenzangu wote Wizarani kumshukuru sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uthubutu na utayari wake wa kutuelekeza maono yake na hatimaye tunaanza kwa vishindo na kwa maelekezo yake kufufua shirika letu hili pendwa la *NARCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji huu utaiwezesha *NARCO* kutumia maeneo yake kikamilifu na kuongeza tija. Aidha katika mwaka 2022/2023 marobota 38,200 ya malisho yamezalishwa na nyama kwa maana ya *Kongwa Beef* tani 159.2 zimezalishwa na kuuzwa. Naomba nichukue fursa hii pia kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge hapo nje kuna maonesho na nyama yetu ya *Kongwa Beef* ipo, nzuri sana inapatikana karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Bodi ya Nyama imeendelea kusimamia biashara ya nyama kwenda nje ya nchi ambapo hadi tarehe 30, 2023 tani 12,243.79 zenye thamani ya dola za Marekani 51,894,622 zimeuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 8,877 zenye thamani ya dola za Marekani 36,264,786 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la 43.1%. Biashara imekua kutokana na jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji pamoja na uwepo wa machinjio sita zenye ithibati ya kusafirisha nyama nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Machi, 31, 2023 wakala wa maabara ya *veterinary* Tanzania yaani *TVLA* imezalisha dozi 51,340,610 za aina saba za chanjo za magonjwa ya kipaumbele na kuzisamabaza nchini ikilinganishwa na dozi 50,640,250 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa mafunzo ya mifugo kwa maana ya *LITA,* katika mwaka 2022 *LITA* imeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga kumbi nne za mihadhara na *hostel* mbili katika kampasi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa maduhuri, katika mwaka 2023/2024 Wizara kwa upande wa Sekta ya Mifugo inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 42,105,000,000 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele katika Sekta ya Mifugo, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Uvuvi kwa mwaka 2023/2024 umeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo yetu;
(ii) Kuongeza ajira kwa vijana na wanawake ili kuimarisha upatikanaji wa malighafi za viwanda vya mazao ya mifugo;
(iii) Kuboresha mbari za mifugo kwa maana ya koo za mifugo;
(iv) Kuimarisha afya ya mifugo;
(v) Kuboresha huduma za ugani, mafunzo na utafiti wa mifugo;
(vi) Kusudio la kuanzisha mamlaka ya kusimamia miundombinu ya mifugo; na
(vii) Kuimarisha biashara na kuongeza thamani ya mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivyo baadhi ya kazi zitakazofanyika katika mwaka 2023/2024 ni pamoja na kuanzisha skimu za umwagiliaji katika mashamba ya malisho ya Vikuge na Langwira. Vikugwe pale Kibaha na Langwira kule Ruvuma pamoja na Ranchi za *NARCO* za Kongwa na Mzeri na kujenga mabwawa na visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo na kuanzisha mashamba darasa 150 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka kulihakikishia Bunge ya kwamba tumekubaliana na tumedhamiria katika

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, maeneo yote ya mifugo yanayomilikiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni lazima yatumike kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuzalisha nyasi ambazo zitatumika kwa matumizi ya ndani ya Taifa letu ambayo itaondoa migogoro ya wakulima na wafugaji, migogoro ya wafugaji na hifadhi lakini pia vile vile kwa diplomasia kali kabisa ya uchumi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, soko la majani kwa maana ya malisho limefunguka. Waheshimiwa Wabunge karibuni sana tuwekeze kwa pamoja tuhakikishe kwamba tunailisha dunia siyo nyama tu na samaki, bali pia na majani. Tunataka tuone majani yakisafirishwa kutoka ndani ya Taifa letu yakienda nchi za Asia na kwingine wanakohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha vituo vipya vya uwekezaji vya vijana na kuendeleza vituo vingine vilivyoanzishwa. Tatu kuhimilisha ng'ombe 100,000 kuendelea kununua madume bora na kuyagawa kwenye vikundi vya wafugaji, kununua ng'ombe wazazi 1,200 kwa ajili ya mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba na kuzalisha dozi milioni 1.5 na mbegu bora za mifugo katika kituo cha *NAIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuendesha kampeni ya udhibiti magonjwa kwa kujenga majosho 246, kununua dawa za kuogesha mifugo lita 56,000 na kusambaza chanjo dozi milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba jambo la *vaccination* kwa maana ya kupiga chanjo mifugo yetu ni jambo ambalo litafanywa katika utaratibu tukisimamia sisi sote kwa pamoja kuhakikisha kila mfugo katika Taifa uweze kuchanjwa, hii nayo ni katika mkakati wa kuongeza mauzo ya *export* tupate *forex* na kuboresha mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kununua pikipiki 1200 na magari 3, zana za huduma za veterinari na zana za uhimilishaji *(AI Kit)* 184. Kwa mara ya kwanza Wizara hatutaishia kuwapa pikipiki tu wagani wetu lakini mtawaona wagani vijijini kule tukiwa tumewakabidhi na *kits* za kufanyia kazi ya utoaji wa huduma za mifugo katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha kampasi mpya ya *LITA* Songwe; kukamilisha taratibu za upatikanaji wa ithibati kwa mbegu za malisho ili ziuzwe madukani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu za mazao mengine yote mpunga, mahindi ma nyinginezo zinauzwa madukani lakini mbegu za majani ya malisho kwa ajili ya mifugo haziuzwi madukani. Kwa mara ya kwanza Serikali tunakwenda kuhakikisha kwamba mbegu hizi za malisho zitauzwa madukani pia ili wafugaji wetu waweze kuzipata kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha skimu za unenepeshaji katika Mashamba ya *NARCO;* narudia hapa; kuanzisha skimu za unenepeshaji katika Mashamba ya *NARCO* na vituo vya kupumzishia mifugo, kujenga na kukarabati minada na kufunga mizani kwenye minada ya awali na kujenga vituo 10 vya kukusanya maziwa. Hili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumefungua milango kwa vijana wetu na akina mama katika maeneo yetu ya *NARCO,* tunataka twende tukafanye skimu za kunenepeshea mifugo na tuwaunganishe na masoko. Pia naomba Bunge lituunge mkono, tunataka tuendeshe zoezi la kupeleka mizani kuanzia katika minada yetu ya awali. Hii biashara ya kuuza ng'ombe kwa makisio iwe ni mwisho ng'ombe wote wauzwe kwa kilo kama vile ambavyo nyama inauzwa buchani kwa kilo ianzie kule chini na si kumnunua ng'ombe kwa kumkisia. Jambo hili litawaheshimisha wafugaji wetu wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukusanya maoni ya wadau na kufanya tathmini ya uanzishaji wa Mamlaka ya Kusimamia na Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo. Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu tumekuwa tukielekezwa na kamati yetu ya Bunge. Kamati ya Bunge imetoa maelekezo mahususi ambao natumaini itakuja yenyewe kujieleza hapa ya kwamba tunataka tuwape heshima wafugaji wetu; na ndiyo maana tunakusudia tukusanye maoni haya ili tuone malambo, majosho, visima vya maji, hivi ambavyo vipo katika maeneo yetu viwe na msimamizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo tunajenga josho, tunajenga lambo lakini matokeo yake halina msimamizi ambaye anaweza kusema jambo hili liko sawa, jambo hili haliko sawa, huyu achangie, huyu asichangie. Lakini kwa maelekezo ya Bunge tunakwenda kukusanya maoni, tutapanua uwanja ili wadau wote waunganike waweze kutupa maoni yaliyo thabiti na hatimaye tufike katika hatua itakayokuwa imetufikisha mahala hapa ili wafugaji wetu waweze kupata huduma hii kwa ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuvutia wawekezaji kwenye mbegu bora za kuku, vyakula vya mifugo, madawa na chanjo, pamoja na uzalishaji wa mbari za mifugo na mbegu za malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutambua na kusajili kwenye mfumo wa kielektroniki takriban mifugo 40,603,262, ili kuwa na taarifa sahihi kwa ajili ya kuboresha mifugo na kukidhi hitaji la masoko ya ndani na nje ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uvuvi Fungu 64; hali halisi ya sekta ya uvuvi. Katika mwaka 2022, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia 1.8 kwenye Pato la Taifa na kukua kwa asilimia 2.5. Aidha, sekta ya uvuvi inatarajia kutoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi 197,763 na wakuzaji viumbe maji kwa maana ya wafugaji samaki, wakulima wa mwani,

wanenepeshaji kaa na wengineo 34,057 na takriban Watanzania milioni 4.5 wanaojishughulisha na shughuli mbalimbali zinazohusiana na uvuvi. Katika mwaka 2022 biashara ya mazao ya uvuvi imeendelea kuimarika katika soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, jumla ya tani 29,466.98 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 453.8 na idadi ya samaki hai wa mapambo 150,308 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.82 waliuzwa nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, idadi ya miundombinu ya ukuzaji viumbe maji imefikia mabwawa 32,878 na vizimba 993, vitotoleshi *(hatcheries)* vya kuzalisha vifaranga vya samaki na viwanda nane vya kutengeneza chakula cha samaki. Aidha, uzalishaji wa mazao mbalimbali ya ukuzaji viumbe maji ulifikia tani 33,525 na vifaranga vya samaki 35,967,180 ambapo kati ya hivyo, vifaranga 31,000 vimepandikizwa katika malambo mbalimbali nchini ili kuongeza upatikanaji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato na matumizi, makusanyo na maduhuli ya mwaka 2022/2023. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 40 kupitia Fungu 64. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 17.4 zimekusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 176.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 40 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 135 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Fungu 64 lilitengewa jumla ya shilingi bilioni 40. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 12.7 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na shilingi bilioni 27.8 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi Machi, 2023, jumla ya shilingi bilioni 16

zimetolewa, sawa na asilimia 41.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida; ambapo shilingi bilioni 9.3 ni fedha za mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 7.5 ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 135.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Hadi Aprili, 2023, jumla ya maombi ya shilingi bilioni 41.2 yamewasilishwa ambapo kiasi cha shilingi bilioni 6.6 zimelipwa na shilingi bilioni 34.6 zipo kwenye hatua mbalimbali za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, hadi kufikia Aprili, 2023, jumla ya siku kazi 4,743 za doria zimefanyika, ambazo ni sawa na asilimia 60.8 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Wizara imefanya kaguzi 8,649 kati ya kaguzi 9,472 zilizopangwa ili kuhakiki ubora, usalama wa mazao ya uvuvi na uimara wa mfumo wa uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2023 watalii 35,562 walitembelea hifadhi za bahari na maeneo tengefu ambapo shilingi bilioni 1.68 zilikusanywa ikilinganishwa na watalii 22,562 ambapo shilingi bilioni 1.18 zilizokusanywa katika mwaka 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 42.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili la watalii limetokana na jitihada mahususi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuutangaza utalii wa nchi yetu kupitia filamu ya *The Royal Tour,* tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, jumla ya vifaranga vya samaki milioni 35.9 vimezalishwa

nchini ikilinganishwa na vifaranga milioni 30.3 vya mwaka 2021/2022, sawa naongezeko la asilimia 18.6 la uzalishaji. Vilevile jumla ya wananchi 8,788 walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa ikilinganishwa na wananchi 7,884 wa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu inaendesha programu maalum ya uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji, kwa maana ya ufugaji wa samaki, unenepeshaji kaa na kilimo cha mwani kwa vijana 500; ambapo awamu ya kwanza imenufaisha vijana 200. Vile vile, Wizara inaendelea na utaratibu wa kuwapata vijana wengine 300 wanaotarajiwa kupewa mafunzo katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuvutia uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi, *TAFICO* imeandaa mpango wa biashara *(business plan)* ambao umeainisha miradi ya kimkakati kwa ajili ya kuongeza tija katika uvuvi wa bahari kuu na mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi. Pia, katika mpango huo *TAFICO* itashirikisha sekta binafsi katika kuibua na kutekeleza baadhi ya miradi kwa utaratibu wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, imetoa leseni za uvuvi wa bahari kuu kwa meli 48, ambapo meli tatu ni za ndani na meli 45 ni za nje ikilinganishwa na leseni 25 zilizotolewa mwaka 2021/2022. Kuongezeka kwa leseni hizi kumeongeza makusanyo kutoka shilingi bilioni 3.3 mpaka bilioni 6.2 katika mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limechangiwa na juhudi za makusudi za kufungua mipaka na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji zinazofanywa na Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili tunataka tuhakikishe kwamba *TAFICO* ifunguke, ialike uwekezaji kwa kushirikiana nayo, iwe na meli za kutosha na yenyewe ichukue leseni kutoka Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu iende ikavue, kusudi tusitegemee mapato ya kutokana na leseni zile za makampuni ya nje peke yake, bali tuzalishe wenyewe, tuchakate, tuuze katika soko letu la ndani na vilevile kiasi tuweze kuuza katika masoko yetu ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, kampuni ya Albacora Group ya Uhispania imeshusha hapa nchini tani 100 za samaki wasiolengwa *(by-catch)* pamoja na kufundisha mabaharia wa Kitanzania 10; watano kutoka Tanzania bara na watano kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie fursa hii kumshukuru sana pacha wangu Mheshimiwa Makame Waziri wa Uchumi wa Bluu ambaye yuko pale juu kwa ushirikiano mzuri anaonipa wakati wote tunapoyaendea majambo haya yanayohusu uvuvi haswa uvuvi wa bahari kuu na hata ule mwingine. Na tunazo programu za pamoja za kuhakikisha kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar Daktari Hussein Ally Mwinyi hawa wanakwenda kuwa ndio machampioni wa uchumi wa bluu katika Taifa hili na barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko, ambapo usanifu wa kina *(Detail Design)* umefanyika, na kazi ya uchimbaji imeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Masharti Nafuu *(Extended Credit Facility – ECF)*. Katika mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kuwezesha mikopo nafuu ya uvuvi kwa kuwakopesha boti za uvuvi 158 kwa wanufaika 2,753 na mradi wa vizimba 613 vya

kufugia samaki vyenye wanufaika 3,154 na mkopo wa pembejeo za ukulima wa mwani kwa wanufaika 2,030.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika eneo hili uniruhusu niseme yafuatayo; miaka miwili iliyopita mimi Abdallah Ulega Waziri wa Mifugo na Uvuvi nilifanya utafiti wa kisanyansi. Utafiti ule ulionesha kwamba moja ya kikwazo kikubwa kinachopelekea wavuvi wetu washindwe kufanya vizuri ni dhana duni. Jambo ambalo limekuwa likisemwa na Waheshimiwa Wabunge mara kadha hapa.

Mheshimiwa Spika, utafiti ule umedhibitisha ni kweli, na kwa kushirikiana na manguli wa sayansi ya Samaki Profesa Yunus Daud Mgaya, Makamu Mkuu wa Chuo Mstaafu ambaye yupo pale, mwalimu wangu namshukuru sana na Profesa Razaki Lokina ambaye ni mchumi wa samaki, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha *UDOM*, tuliandika andiko ambalo limetangazwa katika *Journal of Geographical Association of Tanzania* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam linalodhibitisha ni kweli kwamba wavuvi hawa wanahitaji zana bora. Ndiyo maana Serikali ya Rais Dkt.i Samia Suluhu Hassan imetekeleza jambo hili kwa vitendo kwa kuanzia na boti 158. Katika mwaka huu tutaendelea na jambo hili kwa mapana na marefu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, sehemu ya fedha hizi zilielekezwa katika kuanzisha mashamba darasa 13 ya ufugaji wa samaki katika halmashauri za wilaya 13 kama zilivyoainishwa katika Ibara ya 202. Wizara inaendelea na taratibu za ununuzi wa meli mbili za uvuvi wa bahari kuu zenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)*. Katika mwezi huu wa Juni/Julai tangazo la mkandarasi wa kuweza kutengeneza meli hizi litatangazwa rasmi na hatimaye shirika letu lianze kuwa na meli zenye mita 24. Meli hizi zitaliwezesha shirika hili kuvua katika maji ya ndani ya bahari vilevile na kwenda katika maji makubwa, kwa maana ya maji ya *EEZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 17.5 kwenye sekta za mifugo na uvuvi. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 13 zilitolewa kwa wazalishaji katika sekta ya mifugo na shilingi bilioni 3.35 zilitolewa kwenye sekta ya uvuvi. Naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mkurugenzi, kaka yangu, Ndugu Nyabundege ambaye yuko pale jukwaani aendelee kuongoza jambo hili ili tuweze kuweka heshima kwa wafugaji na wavuvi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo iliyotolewa ilielekezwa kwenye maeneo yafuatayo; Ufugaji wa kuku, unenepeshaji wa ng'ombe *(fattening)* kwenye miradi 13 iliyopo katika mikoa ya Tabora, Pwani, na Manyara. Hili naomba niwasisitize na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wadau wetu wengine wa mifugo katika mikoa yetu wachangamkie huduma hii ya mikopo kutoka *TADB* na benki nyingine za biashara za NMB, *NBC*, *CRDB*, *Equity Bank;* wote wako tayari. Hivi sasa wanatoa pesa nyingi sana kwa *program* za unenepeshaji wa ng'ombe *(fattening)*. Fursa imefunguka Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan amefungua fursa tuichangamkie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa nguruwe pia ulipata fedha katika miradi saba iliyopo katika mikoa ya Pwani na Mara. Uzalishaji wa chanjo za mifugo, ufugaji wa samaki katika mabwawa, mradi mmoja uliopo mkoani Pwani ambao unafanywa na Kampuni ya *Tanlapia,* naomba mkipata nafasi mkaone maajabu ya kazi nzuri inayofanywa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi na uuzaji wa samaki kutoka Ziwa Victoria zilitolewa kwenye miradi miwili iliyopo Ukerewe. Kipo kikundi kinatwa Bukasiga kinachoongozwa na Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Michael Mkundi, ambapo kinafanya vizuri sana. Wameweza kuzalisha

barafu vilevile wameweza kupata pesa kutoka Benki ya Kilimo ya kununua mashine ya ukaushaji wa dagaa. Naomba nitumie fursa hii kuwapongeza sana wana ukerewe wale kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa samaki kwenye vizimba, miradi mwili ya uvuvi katika Mkoa wa Mara. Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatekeleza mradi wa *Blue Economy for Growth* wenye lengo la kuinua uzalishaji wa mazao ya mwani na uvuvi wa samaki kwa kutoa mikopo ya gharama nafuu kwa ajili ya ununuzi wa boti za kisasa, ujenzi wa vizimba vya kufugia samaki na utoaji wa ushauri wa kitaalamu. Hadi sasa maombi 400 yamepokelewa na yanafanyiwa uchambuzi. Mradi huu unatekelezwa katika mikoa yote iliyozungukwa na maziwa makuu, ambayo ni Ziwa Victoria, Tanganyika, Rukwa na Nyasa na mikoa inayopakana na Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele katika mwaka wa fedha 2023/2024; katika mwaka 2023/2024 Sekta ya Mifugo na Uvuvi imepanga kutekeleza vipaumbele vinavyoendana na kufungamanisha uchumi wa bluu hususani matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi ikiwemo uvuvi wa asili na ukuzaji wa viumbe maji. Vipaumbele hivyo ni pamoja na kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari kuu, kuimarisha taasisi za uvuvi ili kuongeza ushiriki katika uchumi wa bluu, kusudio la kuanzisha mamlaka ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi nchini Tanzania, lakini pia kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji, kuimarisha udhibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi na masoko, kuimarisha huduma za ugani wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivyo baadhi ya kazi zitakazofanywa katika mwaka 2023/2024 ni pamoja na:

(i) Kuendelea na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko;

(ii) Ununuzi wa meli tatu za uvuvi wa bahari kuu;

(iii) Kufanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika bahari kuu; na

(iv) Kutoa leseni kwa meli za uvuvi wa bahari kuu kupitia Mamlaka yetu ya Uvuvi ya Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili kuimarisha Taasisi za Uvuvi kwa kujenga miundombinu muhimu, kununua boti zenye vioo chini ili kuongeza utalii kwenye hifadhi za bahari na maeneo tengefu kwa maana ya *eco – tourism,* kufanya tafiti za kujua wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika Maziwa na Bahari ya Hindi; kujenga vyumba vya mihadhara na vifaa vya kufundishia katika kampasi tano za Vyuo vyetu vya *FETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na sekta binafsi *TAFICO* itajenga viwanda vya kutengeneza chakula cha samaki na kuchakata mazao ya uvuvi, itakarabati gati la kuegesha meli na kununua magari ya ubaridi, kutoa mafunzo kwa mabaharia kuhusu uvuvi wa bahari kuu na kujenga ghala la ubaridi jengo la mtambo wa kuzalisha barafu na jengo la uhandisi wa mitambo ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakusudia kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi mahususi kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi. Mamlaka hii itawezesha kupunguza au kuondoa changamoto zinazoikabili Sekta ya Uvuvi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na uvuvi haramu, hivyo kuongeza wingi wa samaki, usalama wa chakula, ongezeko la ajira,

kipato cha mtu mmoja mmoja na pato la Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 na maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ibara ya 43(f) lakini na maelekezo mahususi ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nenda kwenye hitimisho, nenda kwenye maombi ya pesa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliyochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika Mwaka 2022/2023 yametokana na uongozi bora na mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuwatambua na kuwashukuru Washirika wa Maendeleo waliochangia mafanikio ya Sekta za Mifugo na Uvuvi. Naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mkuranga ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya Jimbo na ya Taifa kwa ujumla.  Nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, katika Mwaka 2023/2024 Wizara inaomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa jumla ya shilingi 295,920,933,000. Kati ya fedha hizi shilingi 112,460,777,000 ni kwa ajili ya Sekta ya Mifugo - Fungu 99 na shilingi 183,874,156,000 ni kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi - Fungu 64. Mchanganuo wa Fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia jumla ya shilingi 112,460,777,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo shilingi 50,122,677,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 61,924,107,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi bilioni 50.1, Mishahara ni bilioni 23.9, Matumizi Mengineyo ni bilioni 26.1. Fedha za Matumizi ya Maendeleo bilioni 61.9, fedha za ndani ni Shilingi Bilioni 56.5 na fedha za nje ni Shilingi Bilioni 5.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi, Wizara inaomba jumla ya shilingi bilioni 183.8 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 49.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 134.4 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mishahara ni shilingi bilioni 15.3 na Matumizi Mengineyo ni shilingi bilioni 34. Fedha za ndani ni shilingi bilioni 110.6 na fedha za nje ni shilingi bilioni 23.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**2 MEI, 2023**

## HOTUBA YA MHESHIMIWA ABDALLAH HAMIS ULEGA (MB) WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2023/2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi); Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya mwaka 2023/2024 kwa Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu ya kwanza siku ya leo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi na kumteua **Mhe. David Ernest Silinde** (Mb) kuwa Naibu Waziri, tunaahidi kutumia uwezo wetu wote kutekeleza wajibu wetu kwa ufanisi na uadilifu na kuhakikisha rasilimali za mifugo na uvuvi zinasimamiwa na kutumika kikamilifu ili kuchangia mapinduzi ya uchumi wa nchi yetu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wake mkubwa anaouonesha katika kuiongoza nchi yetu na kuifanya iendelee kupiga hatua kubwa za maendeleo ya

kiuchumi, kijamii, kisiasa na kuaminika Kimataifa. Pia nimpongeze **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoshirikiana na Mheshimiwa Rais kuwaletea maendeleo watanzania. Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunaahidi kuendelea kuwaunga mkono na kutekeleza dira, miongozo na maelekezo wanayoyatoa katika kuwatumikia wananchi hususan wafugaji, wavuvi, wachakataji, wasindikaji na wafanyabiashara wa mifugo na samaki na mazao yake kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Nitumie nafasi hii kuwaombea viongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu, wawe na afya njema, na aendelee kuwapa hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea na usimamizi mahiri wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

4. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kazi nzuri ya uratibu na usimamizi wa shughuli za Serikali. Pia, namshukuru na kumpongeza, kwa hotuba yake nzuri ambayo imebainisha malengo na kazi zitakazotekelezwa na Serikali kwa mwaka 2023/2024. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo tayari kutekeleza malengo hayo ili kuwaletea maendeleo wananchi na kukuza uchumi wa Taifa letu.

5. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kukupongeza wewe binafsi na ***Mheshimiwa*** Naibu Spika, kwa kuendelea kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni wazi kuwa chini ya uongozi wenu Bunge letu la 12 limeendelea kuwa mahiri zaidi katika kuisimamia na kuishauri Serikali na hivyo kuongeza ufanisi katika kusimamia rasilimali za umma na kuwatumikia wananchi. Aidha,

napenda kuwapongeza wenyeviti wa kamati mbalimbali za Bunge kwa kuteuliwa kuongoza kamati hizo.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mhe**. David Mwakiposa Kihenzile (Mb)** kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, **Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri (Mb)** kuwa Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati, tunaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao ya usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia, natoa shukran za dhati kwa Kamati kwa maelekezo na ushauri wao mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2023/2024. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri, mapendekezo na maoni ya Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu.

7. ***Mheshimiwa Spika*****,** namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara **Prof. Riziki Silas Shemdoe** na Naibu Makatibu Wakuu **Dkt. Daniel Elius Mushi** (Mifugo) na **Bi. Agnes Kisaka Meena** (Uvuvi) kwa kuwa viungo muhimu kati yangu na watumishi na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Kipekee, ninawashukuru kwa dhati na kuwapongeza watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini.

8. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mkuranga, kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu pamoja na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo.

9. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya kipekee napenda kuishukuru familia yangu hususan Mke wangu kipenzi Bi. Mariam Abdallah Ibrahim na watoto wangu kwa kunivumilia na kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na Mpango wa Bajeti ya Wizara Mwaka 2023/2024 kwa fungu 99 - Mifugo na Fungu 64 - Uvuvi.

## B. SEKTA YA MIFUGO (FUNGU 99) UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023

### Maeneo ya Kipaumbele katika Mwaka 2022/2023

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 Wizara ilianza kutekeleza Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo ili kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa, na kupunguza umaskini. Maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa: **kuimarisha huduma za maji, malisho na vyakula vya mifugo; kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo; kuimarisha afya ya mifugo; kuboresha huduma za ugani; kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo; kuimarisha masoko; na kuwezesha uongezaji thamani mazao ya mifugo**.

### Makusanyo ya Maduhuli

12. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Fungu **99** ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **40,100,000,000**. Hadi kufikia tarehe Aprili 30, 2023 kiasi cha shilingi **19,932,373,759.75** kimekusanywa sawa na **asilimia 49.71** ya lengo la makusanyo kwa mwaka (Kiambatisho Na. 28). Upungufu huu umechangiwa na ukame ulioathiri mifugo, pamoja na kuondolewa kwa baadhi ya tozo katika Kanuni za Magonjwa ya Wanyama (Udhibiti wa Usafirishaji wa Mifugo na Mazao yake) za mwaka *2022* iliyorekebisha

tozo ya minada, na Kanuni za Tasnia ya Nyama za mwaka 2011; ili kuhamasisha biashara ya mifugo nchini.

**Fedha zilizoidhinishwa kwa Ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo 2022/2023**

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kupitia Fungu 99 ilikuwa jumla ya Shilingi **92,050,824,000.** Kati ya fedha hizo Shilingi **21,336,097,000** zilikuwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi **23,983,679,000** matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi **46,731,048,000** sawa na **asilimia 51** zilikuwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi **46,592,173,000** zilikuwa fedha za ndani na Shilingi **138,875,000** fedha za nje.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida na Maendeleo**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika bajeti ya Shilingi **45,319,776,000** zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kiasi cha Shilingi **29,621,661,107.24** sawa na **asilimia 65.36** kimepokelewa na kutumika hadi kufikia mwezi Machi, 2023. Kati ya fedha hizo, Shilingi **15,418,770,053.26** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na Shilingi **14,202,891,053.98** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika bajeti ya Shilingi **46,731,048,000** zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo jumla ya Shilingi **27,190,813,815.35** sawa na asilimia **58.36** zimepokelewa na kutumika hadi kufikia mwezi Machi, 2023. Kati ya fedha hizo Shilingi **27,083,938,815.35** ni fedha za ndani na Shilingi **106,875,000** ni fedha za nje.

**Hali Halisi ya Sekta ya Mifugo**


16.***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, idadi ya mifugo nchini imeongezeka kutoka ng'ombe **milioni 35.3**

hadi ng'ombe **milioni 36.6**, mbuzi kutoka **milioni 25.6** hadi **milioni 26.6** na kondoo kutoka **milioni 8.5** hadi **milioni 9.1.** Pia, kuku wameongezeka kutoka **milioni 92.8** hadi **milioni 97.9** ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 42.7** hadi **milioni 45.1,** kuku wa kisasa kutoka **milioni 50.1** hadi **milioni 52.8** na nguruwe kutoka **milioni 3.4** hadi **milioni 3.7** (**Kiambatisho Na. 1**) **.** Aidha, ukuaji wa Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2021 umefikia **asilimia 5.0** na kuchangia **asilimia 7.0** kwenye Pato la Taifa.

17.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 ng'ombe **2,218,293** na mbuzi/kondoo **2,121,187** wenye thamani ya Shilingi trilioni **1.7** waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **2,194,937**; mbuzi/kondoo **1,782,010** wenye thamani ya Shilingi trilioni **1.5** waliouzwa katika mwaka 2021/2022.

18.***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa asilimia **4.3** kutoka tani **769,966.7** mwaka 2021/2022 hadi tani **803,264.3** mwaka 2022/2023 (**Kiambatisho Na. 2**). Kati ya hizo, tani **544,983.8** ni za nyama ya ng'ombe; tani **113,781.8** za nyama ya mbuzi na kondoo; tani **96,915.6 za** nyama ya kuku na tani **47,583.1** za nyama ya nguruwe. Ongezeko hilo limechangiwa na wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao na kukua kwa soko la nyama la ndani na nje ya nchi. Aidha, uzalishaji wa nyama ya ng'ombe uliongoza, ukifuatiwa na nyama ya mbuzi na kondoo, kuku na nguruwe kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.1**.

**Kielelezo Na. 1: Uzalishaji Wa Nyama Nchini, 2022/2023**




***Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi.***

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika asilimia ***35*** ya kaya za watanzania wanaojishughulisha na kilimo, kati yao asilimia **39.3** wanafuga ng'ombe, asilimia **36.2** wanafuga mbuzi, asilimia **13.5** wanafuga kondoo na asilimia **10.9** wanafuga nguruwe. Aidha, asilimia **55.4** ya kaya hizo pia hujishughulisha na ufugaji wa kuku (2019/2020 NSCA).

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **bilioni 3.4** mwaka 2021/2022 hadi kufikia lita **bilioni 3.6** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia **5**. Vipande vya ngozi milioni **14.1** vimezalishwa mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na vipande milioni **13.6** vilivyozalishwa mwaka 2021/2022. Uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 4.9** mwaka 2021/2022 hadi **bilioni 5.5** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia **12.2.**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 4.9** mwaka 2021/2022 hadi mayai **bilioni 5.5** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia **12.2** (**Kiambatisho Na. 2**). Ongezeko hilo limesababishwa na kuimarika kwa vituo **28** vya kutotolesha vifaranga vya kuku vilivyopo nchini, mashamba **25** ya kuku

wazazi, kuongezeka kwa ufugaji wa kuku wa mayai na hatua mbalimabli ambazo zimeendelea kuchukuliwa za kudhibiti uingizaji holela wa vifaranga kutoka nje ya nchi.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni **3.4** mwaka 2021/2022 hadi lita bilioni **3.6** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia **5**, ambapo kati ya hizo, lita bilioni **2.4** zilitoka kwa ng'ombe wa asili na lita bilioni **1.2** zilitoka kwa ng'ombe wa maziwa (**Kiambatisho Na. 2**). Aidha, kati ya ng'ombe milioni **36.6** waliopo nchini, ng'ombe wa maziwa ni milioni **1.3**.

23. **Mheshimiwa Spika**, vituo vya kukusanyia maziwa vimeongezeka kutoka **238** mwaka 2021/2022 vilivyokuwa vikikusanya lita milioni **64.8** kwa mwaka hadi kufikia vituo **246** mwaka 2022/2023 ambavyo vinakusanya takriban lita milioni **68.7** kwa mwaka. Aidha, viwanda vya kusindika maziwa vimeongezeka kutoka **105** mwaka 2021/2022 vilivyokuwa vinasindika lita milioni **77.6** kwa mwaka hadi kufikia **152** mwaka 2022/2023 vinavyosindika lita milioni **77.3** kwa mwaka. Viwanda **47** vilivyoongezeka vina uwezo wa kusindika maziwa kati ya lita **100** hadi **1,000** kwa siku **(Kiambatisho Na. 3).** Pia, katika kukidhi mahitaji ya soko la maziwa, vibali **605** vya kuingiza maziwa kutoka nje ya nchi vyenye jumla ya lita milioni **11.6** zenye thamani ya shilingi **22,765,482,217.50** vilitolewa. Aidha, TDB (TDB) imeendelea kusimamia, kuratibu na kuendeleza tasnia ya maziwa nchini ambapo jumla ya wafanyabiashara **374** walikaguliwa katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Songwe, Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 jumla ya vipande vya ngozi milioni **14.1** (ng'ombe milioni **4.4**, mbuzi milioni **7.2** na kondoo milioni **2.5**) vyenye thamani ya Shilingi **bilioni 31.1** vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni **13.6** (ng'ombe milioni **4.2,** mbuzi milioni **6.9** na kondoo milioni **2.5**) vyenye thamani ya Shilingi **bilioni 28.5**

vilivyozalishwa mwaka 2021/2022. Ongezeko hilo la uzalishaji wa vipande vya ngozi limechangiwa na wafugaji kuongeza uelewa kuhusu ufugaji wa kisasa na kibiashara wenye kuhamasisha uvunaji wa mifugo kwa wakati kwa ajili ya soko la ndani na nje pamoja na mafunzo yanayoendelea kutolewa kwa wachunaji na wapanga madaraja ya ngozi.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2022/2023, Mashamba ya kuku wazazi nchini yameongezeka kutoka **24** hadi **25** (**Kiambatisho Na.4**) yakiwa na uwezo wa kutunza zaidi ya kuku wazazi **1,400,000**. Aidha, kwa sasa kuna jumla ya vituo **28** vikubwa vya kutotolesha vifaranga nchini katika mikoa ya Dar es Salaam (**9**), Iringa (**2**), Njombe (**1**), Pwani (**11**), Kilimanjaro (**2**), Arusha (**1**), Mbeya (**1**) na Mwanza (**1**) (**Kiambatisho Na.5**).

**Marekebisho ya Sera, Sheria na Kanuni Katika Sekta ya Mifugo**

**Marekebisho ya Sera**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni, mikakati na programu mbalimbali za kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini. Mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 yamekamilika, ambapo rasimu ya Sera ya Mifugo iliyorekebishwa ipo katika hatua za maamuzi ya Serikali. Maboresho hayo yamefanyika ili kuwezesha Sekta ya Mifugo kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Awamu ya Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) kwa kipindi cha 2021/2022 - 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals* - SDGs); Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo; Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo (2022/23-2026/27) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020.

***Sheria na Kanuni***

27. **Mheshimiwa *Spika,*** Wizara imeendelea kupitia na kufanya marekebisho ya sheria za Sekta ya Mifugo ili kuboresha mazingira ya biashara na kuwezesha ukuaji wa Sekta ya Mifugo ambapo katika mwaka 2022/2023 sheria tisa (**9**) za Sekta ya Mifugo zimefanyiwa urekebu (revision*)* kwa ushirikiano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sheria hizi zinasubiri kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

28. **Mheshimiwa *Spika*,** katika kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji wa biashara ya mifugo na mazao yake, Wizara imefanya marekebisho ya kanuni mbili (2) zilizo chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama SURA 156 pamoja na Sheria ya Tasnia ya Nyama SURA 421 ambazo ni; *The Animal Diseases (Animal and Animal Products Movement Control) Regulations, GN.No.478C/2022* na *The Meat Industry (Location, Design, Construction and Operation of Livestock Markets) (Amendment) Regulations, GN No.516/2022*. Pia, Wizara imetangaza maeneo ya malisho kupitia notisi ya Serikali ya *Grazing Land and Animal Feed Resources (Delineation of Grazing Lands) Notice GN No. 597/2022* iliyotengenezwa chini ya Sheria ya "Grazing Land and Animal Feed Resources" SURA 180. Aidha, Wizara imetangaza notisi ya wakaguzi wa Ngozi **101** yenye GN No.285/2023 kupitia Sheria ya Biashara ya Ngozi SURA 120.

29. **Mheshimiwa *Spika,*** Wizara imefanya tafsiri ya kanuni mbili (2) kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili kwa lengo la kurahisisha uelewa wa Kanuni hizi kwa watumiaji. Kanuni hizo ni *The Veterinary Act (Code of Conduct for Veterinary Paraprofessional Assistants) Regulation, GN.No.386/2005* na *The Veterinary Act (Code of Professional Conduct and Ethics for Veterinarians and Veterinary Specialist), GN.No.384/2005*.

## Uzalishaji wa Mifugo na Masoko

### *Huduma ya Uhimilishaji*

30. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mbari za mifugo hapa nchini Wizara imeendelea kukiimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kukipatia vitendea kazi ikiwemo mashine za kupima mimba (**1**), kupima joto wakati wa kuhimilisha (**3**), kujaza na kuziba mirija ya mbegu (**1**), kuweka taarifa kwenye mirija (**1**), *Semen extender* chupa **140** na mirija ya mbegu ya kupaki mbegu pakiti **250** kwa ajili ya kuzalisha mbegu. Aidha, Wizara imenunua madume bora manne (**4)** ya mbegu aina ya Brahman moja **(1),** Ayrshire mawili **(2)** na Boran moja **(1)** kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu. Wizara kupitia kituo cha NAIC imezalisha mbegu dozi **116,558.**

31. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji ambapo katika mwaka 2022/23 hadi Aprili 30, 2023, ng'ombe **60,697** wamehimilishwa hapa nchini kupitia kambi za uhimilishaji ikilinganishwa na ng'ombe **64,463** waliohimilishwa mwaka 2021/2022 (**Kiambatisho Na.6**). Uhimilishaji umepungua kutokana na uhaba wa malisho kutokana na ukame ulioathiri maeneo mengi ya ufugaji.

### *Ugawaji wa Madume ya Mbegu*

32. ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuboresha mbari za ng'ombe ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa na nyama, madume bora **366** ya ng'ombe yamenunuliwa na kusambazwa kwa wafugaji kupitia vikundi vya Wafugaji. Madume hayo yamesambazwa katika Halmashauri saba (**7**) za Chamwino (**50**), Msalala (**50**), Maswa (**50**), Chato (**50**), Mvomero (**40**), Mkuranga (**50**), Buchosa (**36**) na Mkalama (**40**).

***Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba***

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba kwa kununua ng'ombe wazazi **1,160.** Kati ya hao, ng'ombe **1,000** ni aina ya Borani kwa ajili ya Mashamba ya Mabuki **(500)** na Sao Hill **(500**). Pia, ng'ombe **160** aina ya Friesian wamenunuliwa kwa ajili ya shamba la Kitulo ili kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mitamba bora kwa ajili ya wafugaji na kuongeza uzalishaji wa maziwa na nyama. Aidha, katika jitihada za kuongeza ng'ombe wazazi, jumla ya mitamba **606** imezalishwa na kuongezwa kwenye kundi la ng'ombe wazazi. Vilevile, Wizara imenunua matrekta matatu (**3**) na mashine za kuvuna malisho **15** (Bailer **5**, Hay rakes **5** na Mower **5**) kwa ajili ya kuzalisha na kuvuna malisho.

***Uzalishaji wa Kuku wa Nyama na Mayai***

34. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imewezesha uwekezaji wa shamba la kuzalisha kuku wazazi halisi (*Grandparent Stock*) lenye uwezo wa kufuga kuku **60,000** na kuzalisha mayai ya kuku wazazi halisi **40,000** kwa siku. Aidha, uwekezaji huu utapunguza uagizaji wa vifaranga wazazi kutoka nje ya nchi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya vifaranga **83,845,967** wamezalishwa na kusambazwa nchini. Kati ya hao, vifaranga **64,457,555** ni wa kuku wa nyama, vifaranga **12,424,064** ni wa kuku chotara ambapo kati ya hao Sasso ni **8,286,244** wanaozalishwa na kampuni ya *Silverlands Tanzania Ltd*, Kuroiler **2,643,043** wanaozalishwa na kampuni ya *AKM Glitters*, Tanbro **1,494,777** wanaozalishwa na kampuni ya *Interchick* na vifaranga **6,964,348** ni wa kuku wa mayai.

***Uzalishaji wa Nguruwe***

36. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Wafugaji wa Nguruwe Tanzania (TAPIFA) imeratibu zoezi la uhimilishaji ili kuondoa changamoto ya koo za nguruwe kuzaliana ndani ya mbari (*inbreeding*). Hadi kufikia Machi 31, 2023 jumla ya mirija **670** ya mbegu za nguruwe zimehimilishwa na jumla ya nguruwe wa mbegu **196** wameingizwa nchini. Aidha, Wizara imeondoa tozo katika mbegu za nguruwe na nguruwe wa mbegu wanaoingizwa nchini kutoka nje ya nchi.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, jumla ya tani **47,583.1** za nyama ya nguruwe zimezalishwa ikilinganishwa na tani **44,420.33** zilizozalishwa mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la **asilimia 7.12.** Aidha, Wizara inahamasisha wafugaji wa nguruwe kutumia mbegu bora kwa teknolojia ya uhimilishaji.

**Biashara ya Mifugo na Mazao Yake**

***Biashara ya Mifugo***

38. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 31, 2023, jumla ya ng'ombe **2,218,293** na mbuzi/kondoo **2,121,187** wenye thamani ya Shilingi trilioni **1.74** waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **2,194,937**; mbuzi/kondoo **1,782,010** wenye thamani ya Shilingi trilioni **1.5** waliouzwa katika mwaka 2021/2022. Ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa minadani limetokana na mahitaji mbalimbali ikiwemo nyama katika soko la ndani na nje ya nchi pamoja na hamasa ya uvunaji wa mifugo.

***Tasnia ya Ngozi***

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya Ngozi imeendelea kusimamia biashara na ubora wa ngozi kwa kusajili na kutoa leseni kwa maghala **17** ya ngozi kwa kampuni za wafanyabiashara wanaosafirisha ngozi kwenda nje ya nchi.

40. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza jukumu la kusimamia uzalishaji na ubora wa ngozi na biashara yake kwa kuzingatia Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008, kila Mkoa na Halmashauri zake wameelekezwa kuwa na wataalam wa kusimamia uzalishaji, uhifadhi na biashara ya ngozi, ambao wameteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Biashara ya Ngozi. Katika mwaka 2022/2023, Wizara imeteua wakaguzi wa ngozi **101** kutoka mikoa **13** na kukamilisha idadi ya wakaguzi **214** kwa mikoa yote **26** kwa ajili ya kusimamia uzalishaji, ubora wa ngozi na biashara ya ngozi zinazozalishwa hapa nchini.

41. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 30, 2023, jumla ya vipande vya ngozi **748,009** vyenye uzito wa kilo **3,591,396** (ng'ombe vipande **748,009**) vyenye thamani ya shilingi bilioni **5.50** viliuzwa nje ya nchi katika nchi za Nigeria, Ghana, Togo na Pakistan ikilinganishwa na vipande vya ngozi **1,630,740** (ng'ombe vipande **1,367,405,** mbuzi **236,683** na punda **26,652**) vyenye uzito wa kilo **7,370,533** vyenye thamani ya shilingi bilioni **10.1** vilivyouzwa nje ya nchi katika nchi za Ghana, Nigeria, Uganda, Togo, China, Italy, Afrika Kusini na Pakistan mwaka 2021/2022. Aidha, mauzo ya ngozi kwenda nje ya nchi yameshuka kwa sababu asilimia **96** ya ngozi huuzwa katika nchi ya Nigeria ambayo ilikuwa na uchaguzi. Hivyo, wafanyabiashara walisimama kusafirisha ngozi kwenda Nigeria.

42. ***Mheshimiwa Spika***, Viwanda vya ngozi vya *ACE Leather* na *Himo Tanneries* vinaendelea na usindikaji wa ngozi ambapo kiwanda cha *Himo Tanneries* kinasindika wastani wa vipande vya ngozi ya ng'ombe **73,000** na mbuzi **182,500** kwa mwaka na *ACE Leather* kinasindika wastani wa vipande vya ngozi **3,600** za mbuzi na **27,000** za ng'ombe kwa mwaka. Aidha ngozi zilizosindikwa hadi hatua ya mwisho zinauzwa kwenye kiwanda cha *Kilimanjaro International Leather* na wajasiliamali wadogo wanaotengeneza bidhaa za ngozi.

43. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 jumla ya jozi za viatu **2,927,500** zimezalishwa ikilinganishwa na jozi **2,855,600** zilizozalishwa mwaka 2021/2022. Ongezeko hilo limetokana na kuanza kwa uzalishaji wa kiwanda cha *Open Sanit* kilichopo Dar es Salaam na viwanda **150** vya wajasiriamali wadogo na wa kati (*SMEs*) vinavyotengeneza bidhaa za ngozi pamoja na ongezeko la upatikanaji wa ngozi bora **(Kiambatisho Na.7).**

**Ujenzi wa Minada na Udhibiti wa Biashara ya Mifugo na Mazao yake**

44. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imejenga minada **19** na kukarabati minada minne (**4)** ili kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, ukarabati na ujenzi upo katika hatua mbalimbali. Ili kuwezesha wafugaji kupata bei inayoendana na thamani halisi ya mifugo, Wizara imenunua na kusambaza mizani **82** kwenye minada ya awali. Hatua hii itahamasisha wafugaji kunenepesha mifugo yao ili kupata uzito mkubwa na hatimaye bei nzuri.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kusimamia vituo sita (**6**) vya utoaji huduma kwa wafanyabiashara wa mifugo na kudhibiti utoroshaji wa mifugo katika maeneo ya Handeni (Ndelema), Monduli

(Makuyuni), Busega (Lamadi), Buhigwe (Mnanila), Misenyi (Kyaka), na Momba (Tunduma). Pia, vituo hivyo vimepatiwa vitendea kazi zikiwemo mashine za POS kwa ajili ya kuhakiki taarifa za usafirishaji wa mifugo na bidhaa zake.

## Rasilimali za Malisho, Vyakula na Maji kwa Mifugo

### *Malisho, Vyakula na Maji kwa Ajili ya Mifugo*

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) imeendelea kuimarisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo ambapo bwawa la Kimambi (Liwale) lenye ujazo wa lita milioni **95** na Matekwe (Nachingwea) lenye ujazo wa lita millioni **102** yamejengwa, na bwawa moja (**1)** la Mhanga (Itigi) lenye ujazo wa lita milioni **54** limekarabatiwa. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa kisima kirefu cha Lwami katika Wilaya ya Mwanga na kuendelea na ujenzi wa mabwawa **11** na visima virefu vitatu **(3)** katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini.

47. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na ORTAMISEMI imetambua na kuyasajili maeneo **77** ya malisho yenye jumla ya hekta **994,827.29** kutoka kwenye Halmashauri **8** za Wilaya za Mwanga, Tanganyika, Mvomero, Kiteto, Mbulu, Simanjiro, Longido na Karatu. Aidha, maeneo hayo yametangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa G.N **597** ya tarehe 7/10/2022. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya hekta **195,028.29** za maeneo ya malisho katika Halmashauri za Wilaya **14** na hivyo kufanya maeneo ya malisho yaliyotengwa kufikia hekta **3,384,485.54** kutoka hekta **3,189,456.94** mwaka 2021/2022 (**Kiambatisho Na.8 na 9**).

48. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza upatikanaji wa malisho na mbegu za malisho, katika mwaka 2022/2023 mashamba mawili (**2**) ya kuzalisha mbegu za malisho na malisho yameimarishwa kwa kuyapatia vitendea kazi vikiwemo *hay bailer* mbili (**2),** *hay rake* mbili **(2)** na *mower* tatu **(3).** Aidha, katika mwaka 2022/2023 mashamba ya Wizara na taasisi zake yamezalisha mbegu bora za malisho kilo **22,691.65** ikilinganishwa na mwaka 2021/2022 ambapo uzalishaji ulikuwa jumla ya kilo **4,481.90**. Pia, jumla ya marobota **248,209** ya hei yamevunwa kutoka katika mashamba ya Serikali na binafsi ambapo mashamba ya Serikali yamezalisha jumla ya marobota **130,132** na mashamba binafsi yamezalisha marobota **118,077.** Ongezeko la uzalishaji wa mbegu na malisho katika mashamba ya Serikali na taasisi limetokana na ongezeko la uwekezaji wa mashine, zana na vifaa shamba.

49. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) imeanzisha mashamba darasa **100** ya malisho yenye ukubwa wa ekari **520** katika Halmashauri **44**. Katika utekelezaji wa mpango huo, Serikali imenunua mbegu tani **8.56** ambazo zimesambazwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) na wafugaji binafsi. Lengo la mpango huu ni kuwafundisha kwa vitendo wafugaji namna ya kulima, kupanda, kutunza, kuvuna na kuhifadhi malisho na mbegu.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka kutoka tani **1,380,000** mwaka 2021/2022 hadi tani **1,580,000** mwaka 2022/2023. Ongezeko la uzalishaji huu limetokana na Serikali kuendelea kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa Sekta Binafsi ili kukabili ongezeko la mahitaji ya vyakula vya mifugo. Aidha, viwanda vipya **22** vya kuzalisha vyakula vya mifugo vimesajiliwa katika mikoa **8** ya Arusha (**4**), Kilimanjaro (**3**), Dar es Salaam (**4**), Morogoro (**2**), Iringa (**3**), Mbeya (**1**), Pwani (**3**) na Shinyanga (**2**) na kufanya viwanda

vya kuzalisha vyakula vya mifugo kuongezeka kutoka **199** mwaka 2021/2022 hadi **221** mwaka 2022/2023. (**Kiambatisho Na. 10**).

51. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuboresha ubora na usalama wa vyakula vya mifugo, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imetoa mafunzo kuhusu mfumo wa Utoaji wa Vibali vya Kielektroniki (MIMIS) kwa wakaguzi **212** wa rasilimali za vyakula vya Mifugo katika mikoa **26** nchini; na kuwezesha kukagua maeneo **221** ya kuzalisha, **364** ya kuuza na **73** ya kuhifadhi rasilimali za vyakula vya mifugo. Vilevile, maeneo mapya **22** ya kuzalisha Vyakula vya mifugo yamesajiliwa katika mikoa **8** ya Arusha (**4**), Kilimanjaro (**3**), Dar es Salaam (**4**), Morogoro (**2**), Iringa (**3**), Mbeya(**1**), Pwani (**3**) na Shinyanga (**2**) **(Kiambatisho Na. 11)** .

**Ushirikishwaji wa wadau katika uendelezaji wa maeneo ya malisho**

52. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha maeneo ya malisho yaliyotengwa kwenye vijiji yanaendelezwa, Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali kama vile UCRT, WWF na TPWF ilitoa mafunzo kwa viongozi **65** na wafugaji **1,603** wa vijiji **42** katika Halmashauri za Mbulu na Longido ambapo walipewa elimu kuhusu upatikanaji, uendelezaji na usimamizi wa maeneo ya malisho na kupatiwa nakala **102** za Mwongozo wa Malisho kwa rejea.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Tanzania People and Wildlife* (TPW) imetoa mafunzo kwa Kamati **50** za usimamizi wa maeneo ya malisho katika vijiji **61** na kufanya tathmini, usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malisho kwa kushirikiana na vijiji vilivyopo katika Wilaya za Simanjro (**3**), Babati Vijijini (**5**), Monduli (**22**), Ngorongoro (**2**), Longido (**25**), Same (**2**) na Mwanga (**2**); ambapo jumla ya hekta **2,136.33** (Ekari **5,279**)

zimeondolewa vichaka na kazi ya kuzuia mmomonyoko wa udongo kwenye makorongo **383** imefanyika.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Mradi wa *AgriResult Tanzania* imewaunganisha wazalishaji wa malisho ya mifugo kwenye mpango wa ruzuku (Dola za Kimarekani **21** kwa kilo **470** za malisho zitakazozalishwa na kuuzwa) ambapo jumla ya dola za Marekani **223,000** zimepatikana kwa ajili ya kutoa ruzuku hiyo. Mpango huu unatekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Tanga, Arusha na Singida kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari **1,795**. Aidha, kupitia mpango huu kilo **5,000** za mbegu ya malisho aina ya mtama lishe (*Sugar graze*) zimeingizwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya uzalishaji wa malisho.

**Jitihada za Kuendeleza Eneo la Msomera**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuendeleza eneo la wafugaji la Msomera, Wizara imetekeleza yafuatayo:- kupima na kutenga vitalu vya ufugaji **112** vyenye ukubwa wa hekta **100** kila kimoja kutoka kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta **22,746.94** lililotengwa kwa ajili ya malisho; kujenga bwawa la maji, kujenga majosho sita (**6**) na kukarabati moja (**1**); kuhimilisha ng'ombe **1,252**; kuanzisha mashamba darasa manne (**4**) yenye ukubwa wa ekari **10** kila moja na kuyapatia mbegu za malisho kilo **280**; kusambaza mbegu za malisho kilo **110** kwa wafugaji binafsi; kusaidia uhamishaji wa mifugo **13,937** kutoka Pori Tengefu la Loliondo kwenda Msomera; kuunda ushirika wa wafugaji; kufundisha usindikaji mdogo na biashara ya maziwa ili biashara ianze; kusaidia ushirika kuweka mifumo ya usimamizi wa maeneo ya malisho yaliyopimwa, majosho na mabwawa; na kuweka duka la pembejeo.

**Utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi**

56. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ambapo, katika mwaka 2022/2023 jumla ya migogoro **55** inayohusu wafugaji na maeneo ya hifadhi, wakulima, vyanzo vya maji, uvamizi wa maeneo ya Serikali na taasisi na ranchi za NARCO imepokelewa. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imefanikiwa kutatua jumla ya migogoro **13** katika mikoa **10** ya Arusha, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Morogoro, Rukwa, Singida, Tabora na Tanga **(Kiambatisho Na.12).**

**Ustawi wa Wanyama**

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Wizara imetoa elimu ya ustawi wa wanyama kwa wadau **3,200** hususan kuzingatia Sheria ya Ustawi wa Wanyama SURA 154 na kanuni zake kupitia mikutano ya hadhara. Aidha, elimu imetolewa kupitia vipindi **52** vya runinga na **65** vya radio mtawalia. Aidha, Wizara iliratibu mikutano minne ya wadau wa ustawi wa wanyama, ilikuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa ustawi na maendeleo ya punda kwa nchi **17** za Afrika na kuendeleza ustawi wa punda kwa kushirikiana na Taasisi za *ASPA, Brooke East Africa, BEA* na *NFA*.

***Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo***

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi imeendelea kutekeleza Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 19 ya mwaka 2008 kwa kutumia hereni za kielektroniki. Hadi kufikia Oktoba 30, 2022, jumla ya mifugo **5,292,738** ambao ni ng'ombe **4,460,354**, punda **66,863**, mbuzi **513,729** na kondoo **251,792** wametambuliwa na kusajiliwa kwenye mfumo wa utambuzi. Aidha, tarehe 3

Novemba, 2022 Serikali ilisitisha zoezi la Utambuzi wa mifugo kwa muda ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza hapo awali.

**Huduma ya Afya ya Mifugo**

***Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo***

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kudhibiti magonjwa **13** ya kipaumbele ambayo ni kikwazo katika uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake (**Kiambatisho Na.13**). Magonjwa hayo yanaathiri wanyama na baadhi ya magonjwa hayo huambukiza binadamu kutokea kwa wanyama. Katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo yaenezwayo na wadudu ambapo masuala mbalimbali yametekelezwa kama ifuatavyo: -

(i) Jumla ya Halmashauri **172** zimegawiwa dawa za kuogesha mifugo lita **52,560** kwa ajili ya majosho **2,644** na mashamba ya kuzalisha mitamba na Taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuogesha mifugo;

(ii) Jumla ya majosho **257** yenye thamani ya Shilingi **5,903,441,000** yanajengwa katika Mamlaka **83** za Serikali za Mitaa (**Kiambatisho Na.14**);

(iii) Hadi kufikia Aprili 30, 2023, jumla ya michovyo **1,040,762,493** (ng'ombe ni **500,572,121** mbuzi **223,982,134,** kondoo **250,774,038** na Punda **65,434,200**) ya kuogesha mifugo imefanyika ikilinganishwa na michovyo **446,997,857** iliyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea na udhibiti wa magonjwa ya mifugo ya mlipuko kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa chanjo za mifugo dozi **679,827,610** za magojwa mbalimbali ya kipaumbele zikiwemo dozi **160,584,610** zilizozalishwa nchini (dozi **51,034,610** kutoka TVI, dozi **46,300,000** kutoka NOVABI, na dozi **63,250,000** Hester Biosciences Africa Limited). Aidha, jumla ya dozi **519,243,000** ziliingizwa kutoka nje ya nchi kufikia Aprili 22, 2023;

(ii) Jumla ya dozi **243,365,631** za chanjo zimetumika kuchanja jumla ya mbuzi na kondoo **3,613,061** dhidi ya Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR); ng'ombe **5,673,213** dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) na ng'ombe **332,795** dhidi ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) ikilinganishwa na dozi **223,592,415** za chanjo zilizotolewa mwaka 2021/2022; na

(iii) Jumla ya dozi **229,051,500** zimetumika kuchanja kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo/kideri, kati ya hizo dozi **70,217,433** ni za matone na dozi **158,834,067** za kuchanganya na maji (Lasota) ikilinganishwa na dozi **201,497,319** zilizotumika kuchanja kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo mwaka 2021/2022, ambapo kati ya hizo dozi **68,481,856** zilikuwa ni za matone na dozi **133,015,463** za kuchanganya na maji (Lasota).

61. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO), Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine imeendelea kutumia Dhana ya Afya Moja katika kukabiliana na magonjwa ya wanyama yanayoathiri binadamu kwa kutekeleza yafuatayo:- Ng'ombe **1,914,372,** mbuzi **891,338** na kondoo **316,021** walichanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta katika mikoa minne (4) ya Arusha, Songwe, Manyara na Kilimanjaro; Mitamba **34,200** imechanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba katika

Wilaya za Arusha, Karatu, Babati na Dodoma; Matukio **107** ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa yalifuatiliwa katika Mikoa ya Tabora, Iringa, Singida, Dodoma, Rukwa, Arusha, Lindi, Morogoro, Kigoma, Shinyanga na Pwani. Aidha, jumla ya mbwa **1,424,513** na paka **114,618** walichanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa kupitia kampeni mbalimbali ikiwemo Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani inayoadhimishwa tarehe 28 Septemba kila mwaka.

***Kuimarisha Uchunguzi na Upatikanaji wa Taarifa za Magonjwa ya Mifugo***

62. ***Mheshimiwa Spika,*** matukio ya magonjwa ya mifugo ya mlipuko yamepungua kutoka **376** katika mwaka 2021/2022 hadi **247** mwaka 2022/2023 sawa na punguzo la asilimia **34**. Aidha, katika mwaka 2022/2023 jumla ya mifugo **357,234** iliripotiwa kuugua ikiwemo ngómbe **268,756,** mbuzi **63,745,** kondoo **24,733** na nguruwe **391** ambapo mifugo **23,503** ilikufa kutokana na magonjwa ikiwemo ngómbe **9,838**, mbuzi **10,511** kondoo **2,579** na nguruwe **300.** Matukio ya magonjwa yamepungua ikilinganishwa na mifugo **501,301** iliyougua katika mwaka 2021/2022 ikiwemo ng’ombe **458,112** mbuzi **26,121,** kondoo **16,241** na nguruwe **575** ambapo mifugo **243,112** ilikufa kutokana na magonjwa **(Kiambatisho 15).**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na FAO imetoa mafunzo ya ufualitiaji wa magonjwa ya wanyama (*In Service Applied Veterinary Epidemiology Training–ISAVET*) kwa maafisa mifugo **25**. Vilevile, mafunzo ya matumizi ya simu katika kukusanya na kutoa taarifa za matukio ya magonjwa ya mifugo (EMA-i) kwa watalaam **180** kutoka katika wilaya **6** yalitolewa.

***Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yake na Kulinda Afya ya Jamii***

64. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara yanayotokana na magonjwa yanayoambukiza kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, katika mwaka 2022/2023 Wizara imefanya ukaguzi wa mifugo **7,234,601** (ng'ombe **722,319** mbuzi **416,945**, kondoo **161,448,** nguruwe **185,656** na kuku **5,748,233)**. Aidha, jumla ya ng'ombe **9,294**, pamoja na mbuzi na kondoo **20,478** walikaguliwa na kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, mifugo **6,837** wakiwemo ng'ombe **3,211** na mbuzi na kondoo **3,626** walikaguliwa na kuingizwa nchini kwa ajili ya mbegu bora.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, mayai ya kutotolesha kuku wazazi trei **61,074** zilisafirishwa nje ya nchi na trei **6,480** ziliingizwa nchini; mirija **14,330** ya mbegu za ng'ombe na *bags* **10** za nguruwe ziliingizwa ndani ya nchi. Pia, tani **702.4** za mazao mengine ya mifugo ikiwemo pembe za ng'ombe na kwato zilisafirishwa nje ya nchi.

**Baraza la Veterinari Tanzania**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania, imefanya ukaguzi wa vituo **2,110** vya kutolea huduma za afya ya wanyama katika Halmashauri **121**. Aidha, vyuo sita **(6)** vya mafunzo ya afya na uzalishaji wa wanyama vya CANRE (Dar es Salaam), Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA) (Morogoro), COPE Mahinya (Ruvuma), Kaole (Pwani) Hagafilo (Njombe) na Boligaram (Dar es Salaam) vimekaguliwa. Ukaguzi huo umebainisha umuhimu wa kuimarisha mafunzo ya vitendo kwa wanavyuo ili wawe na weledi wa kutosha.

67. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 wapo Madaktari **1,079** wa Mifugo waliosajiliwa na Baraza la Veterinari Tanzania. Kati ya hao, wanaume ni **974** na

wanawake ni **105**. Pia, wataalam wasaidizi wa afya ya wanyama **193** wameandikishwa na kuorodheshwa na kufanya idadi yao kufikia **5,041** ambapo kati yao wanaume ni **3,419** na wanawake ni **1,622**. Aidha, leseni **7** zimetolewa kwa wakaguzi wa nyama, tatu (**3**) kwa wahimilishaji na tatu (**3**) kwa wataalam wa maabara na kufanya wakaguzi wa nyama kufikia **911**, wahimilishaji **81** na wataalam wa maabara **73**. Pia, vituo **96** vya kutolea huduma za afya ya wanyama vilisajiliwa na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia **2,345**.

68. ***Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Baraza la Veterinari linaendelea kusimamia mafunzo ya uanagenzi kwa wahitimu wa shahada ya udaktari wa Wanyama. Aidha, jumla ya madaktari wa Wanyama wahitimu **109** wanaendelea na mafunzo hayo katika vituo **68** vilivyopo katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya Nchi **(Kiambatisho Na 16**). Pia, mitihani ya kuandikishwa imefanyika kwa wahitimu **1,272** wa stashahada ya afya na uzalishaji wa Wanyama kwa ajili ya kupata sifa ya kuandikishwa na kuweza kutoa huduma za afya ya mifugo.

**Ugani, Utafiti na Mafunzo**

***Huduma za Ugani wa Mifugo***

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kujenga mazingira wezeshi kwa Maafisa Ugani ambapo katika mwaka 2022/2023 imenunua jumla ya Pikipiki **1,200** kwa ajili ya Maafisa Ugani wa ngazi ya Kata, Vijiji na Mitaa. Pia, Wizara imenunua magari **13** yakiwemo *Toyota Hard Top* (**2**) na *Toyota Double Cabin* (**11**) yatakayosambazwa katika ngazi ya Wizara na Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za ugani.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2022/2023 Wizara ilipanga kutoa Mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani **800** ambapo hadi kufikia Aprili 30, 2023, jumla ya maafisa ugani **515** walipatiwa mafunzo wakiwemo **28** wawakilishi kutoka Sekta Binafsi na **487** kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mafunzo hayo yalifanyika katika kanda zote nane (**8**) za Kati; Nyanda za Juu Kusini; Ziwa Magharibi; Ziwa Mashariki; Magharibi; Kaskazini; Mashariki; na Kusini ambapo jumla ya Mikoa **26** na Halmashauri **119** zimefikiwa.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na upungufu wa huduma za ugani katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara inaendelea kuimarisha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha wafugaji wengi kupata huduma kwa wakati. Hadi kufikia Aprili 30, 2023 jumla ya maafisa ugani **3,018** kati ya **3,201** wamesajiliwa katika mfumo wa TEHAMA wa utoaji wa huduma za Ugani wa M- Kilimo.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mfumo huo, Maafisa Ugani na Wafugaji wamewezeshwa kuwasiliana kwa njia ya ujumbe mfupi wa maneno kupitia rejista ya mtandaoni iitwayo *call sheet.* Aidha, Mafunzo maalum ya Matumizi ya mfumo wa M-Kilimo na Ugani Kiganjani (*Digital Agricultural Service Portifolio*) yametolewa kwa maafisa Mifugo **36** wa Sekterariet za Mikoa. Lengo la mafunzo hayo ni kuendelea kutoa elimu na kusajili Maafisa ugani na Wafugaji katika Mfumo wa M-Kilimo waliopo katika Mikoa yao.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wafugaji kupitia uanzishwaji wa mashamba darasa ya mifugo. Jumla ya Vikundi **25** vimebainishwa na kufanyiwa tathmini ya kuanzisha Mashamba Darasa ya Ufugaji kuku kutoka katika mikoa ya Kilimanjaro (**7**), Ruvuma (**7**), Simiyu (**4**) na Shinyanga (**7**). Pia, Wizara inaendelea na utekelezaji wa uanzishwaji wa mashamba darasa ya kuku katika Halmashauri za Songea

(**3**) na Maswa (**3**) ambapo taratibu za ununuzi wa vifaranga **18,000** kwa ajili ya vikundi (**6**) katika Halmashauri hizo umekamilika.

74. ***Mheshimiwa Spika**,* Wizara kwa kushirikia na wadau wa sekta imeendelea kusambaza teknolojia za ufugaji bora, uzalishaji, usindikaji wa mazao yatokanayo na mifugo, hifadhi ya malisho pamoja na upatikanaji wa masoko kupitia maonesho na maadhimisho mbalimbali. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi 31, 2023 jumla ya wadau **60,504** wamefikiwa wakiwemo **23,471** kupitia maonesho ya Kimataifa ya Biashara Saba Saba, **34,195** Nane Nane na **2,838** Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani. Pia, jumla ya vipeperushi **8,685** na vitabu **429** vya ufugaji bora vimechapishwa na kusambazwa kwa wadau.

**Uratibu wa Utafiti na Mafunzo ya Mifugo**

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za Utafiti wa Mifugo nchini ambapo imefanya tathmini katika vituo vya Utafiti vya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kutembelea vituo hivyo **(7)** na Taasisi binafsi **(11)** zinazofanya utafiti unaohusiana na Mifugo nchini. Lengo la tathmini hiyo lilikuwa kubaini tafiti mbalimbali zinazofanyika pamoja na uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na utekelezaji wa Agenda ya Utafiti wa Mifugo nchini ya mwaka 2020-2025.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imefanya tathmini katika vyuo nane (**8**) vya Mafunzo ya Mifugo vya Wakala ya Mafunzo ya Mifugo LITA na vyuo tisa (**9**) vya binafsi iliyolenga kubaini uzingatiaji wa mitaala ya Wizara, uwiano wa wakufunzi na wanafunzi na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Tathmini hiyo ilibaini kuwa vyuo hivyo vinazingatia mitaala na miongozo. Pia, tathimini imefanyika katika chuo kipya cha *Borigarum*

*Agriculture Technical College* kilichopo Kigamboni Jijini Dar es Salaam kinachotoa mafunzo ya fani za mifugo iliyopelekea Chuo hicho kupatiwa idhini ya kutumia mitaala ya Wizara.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu upatikanaji wa wanafunzi **13** kutoka Vyuo vya Serikali na wanafunzi **54** kutoka vyuo binafsi vya mifugo kwenda nchini Israel kwa ajili ya mafunzo ya utarajali wa mifugo (*Internship programme*). Mafunzo hayo yamekuwa chachu kwa vijana kupata nafasi nzuri ya kujifunza zaidi kwa vitendo, teknolojia na bidii ya kazi.

78. ***Mheshimiwa Spika**,* Serikali kupitia Wizara imeanzisha vituo nane (**8**) vya uwekezaji vya vijana vyenye uwezo wa kuchukua jumla ya vijana **240** kwa mwaka. Lengo ni kuwawezesha vijana kupata uzoefu katika kuanzisha na kuendesha miradi ya ufugaji kibiashara, kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa mazao bora ya mifugo, malighafi kwa ajili ya viwanda nchini na kuongeza fursa ya kujiajiri. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya vijana **238** wakiwemo wa Kike **71** na wa kiume **167** wamesajiliwa katika vituo Atamizi vya LITA (**6**) na TALIRI (**2**). Vilevile, jumla ya ng'ombe **2,222** wamenunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo ambapo kila mnufaika amepatiwa ng'ombe kumi (**10**) wa kuwanenepesha na kuwauza kila baada ya miezi mitatu kwa awamu tatu kwa mwaka hadi kuhitimu.

**Taasisi Zilizo Chini ya Sekta ya Mifugo**

***Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)***

79. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha utendaji wa NARCO, Wizara imeanza kutekeleza Mpango wa mabadiliko wa miaka mitatu (2022/2023 hadi 2024/2025) wenye vipengele vitano ambavyo ni:- uboreshaji wa Mbari

za Mifugo; uendelezaji wa malisho na vyakula vya mifugo; unenepeshaji wa mifugo; Skimu za unenepeshaji kupitia vijana na wanawake; na uendelezaji wa masoko. Aidha, utekelezaji wa maeneo hayo umehusisha uwekezaji wa Shilingi **bilioni 4.6** zilizotengwa kutoka serikalini kwa ajili ya ununuzi wa ng'ombe wazazi **1,000**, matrekta manne (**4**), Tela nne (**4**), Beila tatu (**3**), Reki moja (**1**) na kuchimba visima virefu **7** katika ranchi za Kongwa, Mzeri na Ruvu. Uwekezaji huu utaiwezesha NARCO kutumia maeneo yake kikamilifu na kuongeza tija.
Aidha, katika mwaka 2022/2023 marobota **38,200** ya malisho yamezalishwa na nyama (*Kongwa beef*) tani **159.2** zimezalishwa na kuuzwa.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na NARCO ni pamoja na kuzalisha ndama **1,958;** kusambaza ng'ombe aina ya borani **100** kwa ajili ya kuboresha kosaafu za mifugo; kununua ng'ombe **214;** kuzalisha na kuuza nyama ''Kongwa beef''' tani **159.2;** kunenepesha na kuchinja ng'ombe **1,592**; kufyeka na kuondoa vichaka ekari **1,000** katika Ranchi za Kongwa (ekari 700), Ruvu (ekari 100) na West Kilimanjaro (ekari 200) kwa ajili ya kuruhusu ukuaji wa malisho; kuzalisha jumla ya robota **38,200** za malisho ikilinganishwa na robota **2,386** zilizozalishwa katika kipindi cha mwaka 2021/2022; kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji **272** katika vijiji vinavyozunguka Ranchi za NARCO; na jumla ya wanafunzi **304** kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo wamepatiwa mafunzo kwa vitendo.


***Bodi ya Nyama Tanzania***

81. ***Mheshimiwa Spika***, *katika* 2022/23 Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) imeendelea kusimamia na kuendeleza tasnia ya nyama nchini kwa kufanya kaguzi, kusajili, kutoa elimu na ushauri kwa wadau **9,251** katika mnyororo wa thamani kwa lengo la kuhakikisha nyama

inayoingia sokoni inakidhi vigezo vya ubora na usalama. Pia, jumla ya wadau **6,234** (maduka ya nyama, machinjio, viwanda vya kuchakata na kusindika nyama na minada) walikaguliwa na kukidhi vigezo vya kufanya biashara katika mikoa **14** ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma, Simiyu, Shinyanga na Tabora.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Bodi ya Nyama, imeendelea kusimamia biashara ya nyama kwenda nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili 30, 2023 jumla ya tani **12,243.79** (zikiwemo tani **457.59** za nyama ya ngómbe, tani **8,689.80** za nyama ya mbuzi, tani **2,969.20** za nyama ya kondoo, tani **2.10** za nyama ya kuku, tani **2.40** za nyama ya nguruwe na tani **122.70** za nyama nyingine) zenye thamani ya Dola za Kimarekani **51,894,622.44** zimeuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani **8,877.80** za nyama zenye thamani ya Dola za Kimarekani **36,264,786.13** sawa na ongezeko la asilimia **43.1** hadi kufikia mwezi Aprili, 2022. Mwenendo wa mauzo ya nyama nje ya nchi umeendelea kuonesha ongezeko kama **Kielelezo Na.2** kinavyoonesha.

**Kielelezo Na. 2: Uagizaji Na Mauzo Ya Nyama Nje Ya Nchi**



**Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

83. ***Mheshimiwa Spika***, Jitihada kubwa za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji mpya imewezesha kupatikana masoko ya nyama katika nchi za Hong Kong, Vietnam, Kuwait, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai), Oman, Jordan, Bahrain, Kenya na Comoro. Aidha, mafanikio hayo yamechangiwa pia na uwepo wa machinjio sita (**6**) za kisasa zenye ithibati ya kusafirisha nyama nje ya nchi, ambazo ni Alpha Choice, Chobo Investment, Tanchoice Limited, Elia Food Oversea Limited, Machinjio ya Dodoma na Nguru Hill Limited.

***Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB)***

84. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kujenga vituo **10** vya kukusanyia maziwa vyenye uwezo wa kukusanya lita za maziwa **44,000** kwa siku kwenye Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Simiyu, Kagera na Njombe. Aidha, vituo hivi vitaongeza kiasi cha maziwa kinachokusanywa kupitia mfumo rasmi kwa lita **milioni 84.7** kwa mwaka hivyo kuendeleza juhudi za Serikali kuboresha ubora wa maziwa na kuimarisha upatikanaji wa maziwa kwa viwanda vya ndani.

85. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TDB imeendelea na uratibu wa biashara ya maziwa na bidhaa za maziwa ndani na nje ya nchi. Hadi Aprili 30, 2023 jumla ya lita (LME) milioni **11.6** zenye thamani ya Shilingi **22,765,482,217.50** ziliingizwa ndani ya nchi kutoka nchi za Uganda, Afrika Kusini, Uingereza, Ireland, Kenya, Oman, Dubai, Denmark, Netherland, Ufaransa, Uturuki, Falme za Kiarabu na Burundi. Aidha, jumla ya lita **278,549.80** zenye thamani ya Shilingi **944,348.371.96** ziliuzwa nje ya nchi hususani nchini Yemen.

86. **Mheshimiwa Spika**, TDB kwa kushirikiana na wadau wa Tasnia ya Maziwa inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni kwenye mikoa ya Kilimanjaro, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Arusha, Dodoma, Morogoro na Mwanza. Kupitia Mpango huo, idadi ya shule za msingi zinazoshiriki ziliongezeka kutoka **39** mwaka 2021/2022 hadi shule **130** mwaka 2022/2023 sawa na asilimia **233**. Aidha, idadi ya wanafunzi wa shule za msingi wanaoshiriki katika mpango huo waliongezeka kutoka **13,701** mwaka 2021/2022 hadi wanafunzi **97,554** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia **612.** Shule hizo ni kutoka mikoa ya Kilimanjaro (shule **24** wanafunzi **8,276**), Iringa (shule **8** wanafunzi **930**), Ruvuma (shule **1** wanafunzi **745**), Mbeya (shule **4** wanafunzi **2,975**), Arusha (shule **2** wanafunzi **1000**), Dodoma (shule **27** wanafunzi **34,050**), Morogoro (shule **40** wanafunzi **36,722**) na Mwanza (shule **24** wanafunzi **12,856**). Pia, idadi ya shule za sekondari **4** zenye wanafunzi **2,133** (Ruvuma shule **1** wanafunzi **1088**, Arusha shule **1** wanafunzi **520**, na Dodoma shule **2** wanafunzi **525**) zimejiunga na mpango huo hivyo kufanya jumla ya shule zote nchini zinazoshiriki mpango huo kufikia **134 (Kiambatisho Na. 17)**. Wizara inaendelea kuhamasisha shule nyingine zaidi kujiunga na mpango huo na wadau wengi zaidi wanahamasishwa kuchangia kufanikisha mpango huo, lengo likiwa kuzifikia shule zote nchini.

87. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/2023, TDB imeendelea na mpango wa kuongeza vituo vya kuuzia maziwa katika Ofisi za Serikali ambapo vituo vimeongezeka kutoka **10** na kufikia vituo **18** katika Mikoa ya Dodoma tisa (**9**), Mbeya vinne (**4**), Katavi kimoja (**1**), Tanga kimoja (**1**), na Dar es salaam vitatu (**3**). Aidha, natoa wito kwa viongozi wote wa Serikali, watumishi na wananchi kwa ujumla kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kutumia maziwa yanayozalishwa na kusindikwa na viwanda vya ndani ya nchi ili kukuza soko la ndani la maziwa.

88. **Mheshimiwa Spika**, TDB imeendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa kupitia maonyesho ya Sabasaba, Nanenane, maadhimisho ya Wiki ya Maziwa, Siku ya Unywaji Maziwa Duniani (World Milk Day), Siku ya Unywaji Maziwa Shuleni, na Siku ya Chakula Duniani. Kupitia matukio haya jumla ya lita **8,089** za maziwa zilitumiwa na washiriki mbalimbali. Aidha, idadi ya watoto na wanafunzi waliogawiwa maziwa katika matukio hayo ilikuwa **6,312** waliotumia lita **3,314**.

89. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2022/2023, TDB ilisajili jumla ya wadau **247** ambapo kati ya hao wamo wazalishaji **36**, wasindikaji **48**, wafanyabiashara **82**, waingizaji wa maziwa nchini (Importers) **34**, wauzaji wa maziwa nje ya nchi (*Exporters* watano (**5**), wasambazaji (*Distributors*) **19**, wakusanyaji (*milk collectors*) **20** na wauzaji wa pembejeo za uzalishaji wa maziwa watatu (**3**). Aidha, katika kipindi hicho jumla ya maghala **87** ya kuhifadhia maziwa yalisajiliwa. Halikadhalika, TDB ilitoa elimu kuhusu Sheria ya Tasnia ya Maziwa Sura 262 na Kanuni zake kwa Wadau **640** wa Tasnia ya Maziwa wakiwemo wafugaji wa ng'ombe wa maziwa **400**, wasafirishaji 30, wasindikaji **30**, wauza maziwa **124** na wasimamizi wa vituo vya kukusanyia maziwa **56** katika Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha na Tanga.

***Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania***

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) ina majukumu mbalimbali nchini ambayo ni pamoja na kuzalisha chanjo za magonjwa ya mifugo, kufanya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo, kuhakiki ubora wa vyakula vya mifugo, kufanya usajili na kuhakiki ubora wa viuatilifu vya mifugo nchini, na kufanya tafiti za magonjwa ya mifugo. Katika mwaka 2022/2023 TVLA imetekeleza yafuatayo: -

(i) Uzalishaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo umeongezeka kutoka dozi **50,640,250** mwaka 2021/2022 hadi dozi **51,034,610** za aina saba (**7**) za chanjo za magonjwa ya kipaumbele na kuzisambaza nchini kupitia vituo vyake vya kanda ambapo chanjo hizo zinajumuisha dozi **48,720,860** za chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Mdondo (TEMEVAC I-2); dozi **216,800** Ugonjwa wa Kimeta; dozi **278,700** za Ugonjwa wa Chambavu; dozi **1,330,400** Ugonjwa wa Mapafu ya Ng'ombe; dozi **2,950** Kutupa Mimba; dozi **366,000** za muunganiko wa Kimeta na Chambavu (TECOBLAX) na dozi **118,900** za Ugonjwa wa Mapafu ya Mbuzi.

(ii) Kuboresha miundombinu ya Taasisi ya Uzalishaji Chanjo Tanzania (TVI) ikiwa ni pamoja na kuweka intaneti ya mkongo wa Taifa na kufunga vifaa vya kisasa vya maabara.

(iii) Kuanza ujenzi wa jengo la maabara kwa ajili ya uzalishaji wa chanjo za magonjwa ya virusi.

(iv) Kufanya utafiti wa chanjo mbili za Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo ambao hadi sasa upo katika hatua mbalimbali za utengenezaji wake.

(v) Kufanya uchunguzi wa magonjwa katika sampuli **14,467** za wanyama ambapo magonjwa mbalimbali ya Wanyama yalitambuliwa yakiwemo Mdondo na Ndui kwa kuku, Homa ya Nguruwe, Kimeta, Ugonjwa wa Kutupa Mimba, Nagana, Ndigana Kali, Ndigana Baridi na Homa ya Mapafu ya Ng'ombe.

(vi) Kufanya uchunguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo, ambapo jumla ya sampuli **1,846** za vyakula vya mifugo kutoka kwa wazalishaji na waagizaji umefanyika na ushauri wa kitaalamu umetolewa.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania katika mwaka 2022/2023 imeanza kutekeleza jukumu la kudhibiti viuatilifu vya Wanyama nchini, jukumu ambalo awali lilikuwa chini ya Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (*Tanzania Plant Health and Pesticides Authority* - TPHPA) ambapo hadi Machi 31, 2023 imetoa vibali **37** vya kuingiza viuatilifu nchini. Aidha, kampuni **13** zilizosajiliwa zimeingiza viuatilifu vya wanyama jumla ya lita **376,437** za viuatilifu vya kimiminika, kilo **16,048** za viuatilifu vya unga na kilo **2,600** za viambata vya kuzalishia viuatilifu nchini.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 TALIRI imeendelea kufanya tafiti za mifugo ambapo jumla ya tafiti **87** zinaendelea kufanyika. Tafiti hizo zinahusu uboreshaji wa mbari za ng'ombe, mbuzi, kuku, nguruwe, uendelezaji wa malisho, uzalishaji wa mbegu bora za malisho na ushiriki wa wanawake na vijana katika shughuli za Ufugaji. Kupitia tafiti hizo jumla ya ng'ombe chotara wa nyama na maziwa (*Dual purpose*) **109**, mbuzi chotara **221** walizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji katika Halmashauri **13** nchini; malisho aina ya nyasi *(Cenchrus ciliaris)*, mikundekunde (*Clitoria ternatea)* na mitimalisho (*Leucaena pallida)* ambapo marobota **5,173** ya nyasi kavu (*hay*) na kilo **4,000.1** za mbegu za malisho zilizalishwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha, aina **10** za mbegu za malisho zimefanyiwa tathmini ambapo kati ya mbegu hizo aina tano (**5**) zipo katika hatua mbalimbali za kupata ithibati. Ithibati ikitolewa itawezesha mbegu hizo kuzalishwa na kuuzwa kibiashara na wadau wote.

93. ***Mheshimiwa Spika***, TALIRI kwa kushirikiana na Kampuni ya AKM Gilitters na Silverland kupitia mradi wa *Women Business* imetoa mafunzo kwa wanawake **200** kuhusu ufugaji wa kuku chotara kibiashara katika maeneo ya Mtama, Ruangwa, Hai na Siha kwa lengo la kuimarisha

shughuli za uzalishaji katika mnyororo wa thamani ya kuku na bidhaa zake.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, jumla ya mbuzi wa asili **1,800** (Pare White **225,** Gogo White **900**, Galla **225** na Sukuma **450)** na mbuzi wa kigeni *Boer* **65** wamenunuliwa kwa ajili ya vituo vya utafiti. Aidha, ununuzi huo umelenga kuzalisha mbuzi chotara **(F1)** kwa kutumia madume **133** ya Malya yaliyopo katika vituo vya Taasisi na majike ya asili yaliyonunuliwa. Pia, madume aina ya *Boer* walionunuliwa watatumika kuzalisha aina nyingine ya chotara (F1) kwa kutumia majike ya asili yaliyonunuliwa ili kuongeza upatikanaji wa mbuzi bora nchini.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uzalishaji wa mbegu za malisho, Serikali imenunua Matrekta **(4)**, *disc plough* **(3**), *harrow* **(2)**, *bailer* **(1)** na *forage chopper* **(1)** kwa ajili ya kuwezesha utafiti wa malisho, uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho. Vifaa hivyo, vimesambazwa katika Vituo vya Utafiti vya TALIRI Tanga, Kongwa, Mabuki, Uyole na Mpwapwa.

***Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)***

96. ***Mheshimiwa Spika***, LITA imeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga kumbi nne (**4**) za Mihadhara katika kampasi za Morogoro (**1**), Mpwapwa (**1**) na Mabuki (**2**) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **250** kila moja kwa wakati mmoja. Pia, hosteli mbili (**2**) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **216** kila moja zimejengwa katika kampasi za Morogoro na Mpwapwa (**Kielelezo Na.3**). Vile vile, samani zimefungwa katika kumbi mbili (**2**) za mihadhara katika Kampasi ya Tengeru.

**Kielelezo Na. 3: Hosteli Za Lita Mpwapwa Na Morogoro**



*Hosteli -Mpwapwa (Mbele)*



*Hostel -Mpwapwa (Nyuma)*





*Hosteli- Morogoro (Mbele)* Hosteli- Morogoro (Nyuma).

97. ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuongeza idadi ya wataalam na wawekezaji watakaochangia kuleta maendeleo katika Sekta ya Mifugo nchini katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) imedahili jumla ya wanafunzi **4,136** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ikilinganishwa na wanafunzi **3,972** waliodahiliwa katika mwaka 2021/2022.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia LITA imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji **18,293** kupitia mafunzo kwa vitendo ya huduma za ushauri kupitia utekelezaji wa mpango wa *outreach na excursions* katika jamii zinazoishi jirani na kampasi za Wakala. Mafunzo hayo yalihusu ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, usindikaji wa maziwa na uzalishaji wa malisho na mbegu.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kutatua changamoto ya uhaba wa vyumba vya mihadhara, Wizara kupitia LITA imekamilisha ujenzi wa kumbi mbili za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **250** kila mmoja katika Kampasi ya Mabuki. Pia, LITA imekamilisha taratibu za kupata na kumiliki eneo lenye ukubwa wa hekta (Ha) **70** katika Wilaya ya Mbozi mkoa wa Songwe kwa ajili ya kuanzisha kampasi mpya na kufanya LITA kuwa na jumla ya kampasi tisa (**9**).

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia LITA imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji **18,293** kupitia mafunzo kwa vitendo ya huduma za ushauri kupitia utekelezaji wa mpango wa *outreach* na *excursions* katika jamii zinazoishi jirani na kampasi za Wakala. Mafunzo hayo yalihusu ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, usindikaji wa maziwa na uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho.

## MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024

### Maeneo ya kipaumbele katika Sekta ya Mifugo

101. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bjeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) kwa mwaka 2023/2024 umeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:- Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo ili kuboresha mbari za mifugo; Kuimarisha upatikanaji wa malisho, vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo; Kuimarisha Afya ya Mifugo; Kuboresha Huduma za Ugani; Kuanzisha na Kuendeleza Vituo Atamizi vya Uwekezaji vya Vijana; Kuimarisha Huduma za Utafiti na Mafunzo ya Taaluma za Mifugo; Kuwezesha uongezaji thamani na biashara ya mifugo na mazao yake; Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO); kuanzisha mamlaka ya kusimamia

miundombinu ya mifugo; na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli katika Sekta.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza vipaumbele hivyo, baadhi ya kazi zitakazofanyika katika mwaka 2023/2024 ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha skimu za umwagiliaji katika mashamba ya malisho ya Vikuge na Langwira, pamoja na ranchi za NARCO za Kongwa na Mzeri; Kujenga mabwawa na visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo; na kuanzisha mashamba darasa **150** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Wizara;

(ii) Kuanzisha vituo vipya vya uwekezaji vya vijana na kuendeleza vituo vingine vilivyoanzishwa;

(iii) Kuhimilisha ng'ombe **100,000**; kuendelea kununua madume bora na kuyagawa kwenye vikundi vya wafugaji; kununua ng'ombe wazazi **1,200** kwa ajili ya mashamba ya Serikali ya kuzalisha Mitamba; na kuzalisha dozi **1,500,000** za mbegu bora za mifugo katika kituo cha NAIC;

(iv) Kuendesha kampeni ya udhibiti magonjwa kwa kujenga majosho **246**, kununua dawa za kuogesha mifugo lita **56,000** na kusambaza chanjo dozi **500,000,000;**

(v) Kununua pikipiki **1,200** na magari **3**, zana za huduma za veterinari (vet kit) **1,100** na zana za uhimilishaji (AI Kit) **184**; kuanzisha kampasi mpya ya LITA Songwe; kukamilisha taratibu za upatikanaji wa ithibati kwa mbegu za malisho ili ziuzwe madukani; na kuanzisha kituo cha utafiti wa mifugo cha Kanda ya Magharibi Wilayani Nsimbo mkoa wa Katavi;

(vi) Kuanzisha skimu za unenepeshaji katika Mashamba ya NARCO na Vituo vya kupumzishia mifugo; Kujenga na kukarabati minada; na kufunga mizani kwenye minada **70** ya awali; na kujenga vituo **10** vya kukusanya maziwa;

(vii) Kuiwezesha NARCO kuzalisha ndama **5,479** kutokana na majike wazazi **6,849** na kunenepesha ng'ombe **12,696** kupitia programu ya kujenga uwezo wa uwekezaji kwa vijana itakayofanyika katika ranchi ya NARCO Kongwa na kuzalisha marobota ya hei **55,000** katika ranchi ya Kongwa na Mzeri kwenye eneo la Ha.**11,000**;

(viii) Kukusanya maoni ya wadau na kufanya tathmini ya uanzishaji wa Mamlaka ya Kusimamia na Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo;

(ix) Kuvutia wawekezaji kwenye mbegu bora za kuku, vyakula vya mifugo, madawa na chanjo, pamoja na uzalishaji wa mbari za mifugo na mbegu za malisho; na

(x) Kutambua na kusajili kwenye mfumo wa kielektroniki takriban mifugo **40,603,262**, ili kuwa na taarifa sahihi kwa ajili ya kuboresha mifugo na kukidhi hitaji la masoko.

**Sera, Sheria na Kanuni Katika Sekta ya Mifugo**

103. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006, itaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agriculture Sector Development Programme – ASDP II);* na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Wizara pamoja na miradi ya mifugo, Wakala, Bodi na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kuratibu na kuboresha utekelezaji wa Sheria zinazosimamia Sekta ya Mifugo ikiwemo kuendelea na zoezi la marekebisho, tafsiri ya Kanuni mbalimbali ili kuleta uelewa kwa watumiaji, kutoa elimu ya sheria kwa wafugaji, wadau wa sekta ya mifugo pamoja na watumiaji wote wa Sheria na Kanuni.

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

105. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2023/24 Wizara kwa upande wa sekta ya mifugo (fungu 99) linatarajia kukusanya **shilingi 42,105,000,000** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

**Huduma ya Uhimilishaji**

106. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/2024 Wizara imepanga kuendelea kuboresha mbari za mifugo kwa kuhimilisha ng'ombe **100,000** katika mikoa **26;** kununua madume bora ya mbegu **200** ya ng'ombe aina ya Borani na kuyasambaza kwa wafugaji pamoja na kusanifu na kuendeleza mfumo wa kitaifa wa uhimilishaji kwa lengo la upatikanaji na ufuatiliaji wa taarifa za ng'ombe wanaohimilishwa. Aidha, dozi **1,500,000** za mbegu bora za mifugo zitazalishwa katika kituo cha NAIC.

107. ***Mheshimiwa Spika*****,** ili kuendelea kuhifadhi mbari za asili ambazo zipo hatarini kutoweka, Wizara imepanga kujenga maabara ya kuhifadhi rasilimali za kijenetiki za mifugo ya asili katika Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC).

**Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba**

108. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/2024 Wizara imepanga kuimarisha Mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba kwa kuyapatia vitendea kazi; kuongeza mitamba **1,200** katika mashamba ya Nangaramo na Ngerengere; kuondoa vichaka hekta **1,000;** na kulima malisho hekta **2,000**. Pia, Wizara imepanga kukarabati nyumba **20** za watumishi katika mashamba na Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji.

**Uzalishaji wa Nguruwe**

109. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Wafugaji Nguruwe Tanzania (TAFIPA) itaendelea kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mbegu bora za nguruwe ikiwemo huduma za uhimilishaji wa nguruwe.

**Udhibiti wa Biashara ya Mifugo na Mazao Yake**

110. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo nchini, Wizara imepanga kujenga minada mitano (**5**) ya awali na kukarabati minada minne (**4**) ya upili na miwili (**2**) ya mipakani mwaka 2023/2024. Aidha, Wizara imepanga kununua mizani **70** kwa ajili ya kuwezesha wafugaji wauze kwa bei nzuri na kuhamasisha wafugaji kunenepesha mifugo yao.

111. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Wizara imepanga kujenga miundombinu ya kunenepesha mifugo katika vituo vitatu (**3**) vya kupumzishia mifugo (*Holding Ground*) vya Kitaraka, Kizota na Makuyuni ili kuweka mazingira wezeshi na kutoa fursa ya unenepeshaji mifugo.

**Tasnia ya Ngozi**

112. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ubora wa ngozi zinazozalishwa hapa nchini, katika mwaka 2023/2024 Wizara imepanga kuwawezesha wakaguzi **10** wa ngozi kwa kuwapatia vitendea kazi zikiwemo pikipiki **10**. Pia, Wizara imepanga kununua mashine **10** na visu **1,000** kwa ajili ya kuchunia ngozi.

**Rasilimali za Malisho, Vyakula na Maji kwa Ajili ya Mifugo**

113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kujenga mabwawa matano (**5),** kuchimba visima virefu sita (**6**), kuanzisha Mashamba Darasa **150** ya Malisho yenye ukubwa wa ekari tano (**5**) kila moja katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali; Kutoa mafunzo kwa wakaguzi **100** wa maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo ili kuhakikisha ubora wa vyakula vya mifugo na malisho unazingatiwa. Serikali itaendelea kuwahamasisha wawekezaji katika Sekta Binafsi kuongeza uzalishaji kufikia tani **2,000,000** za vyakula vya mifugo; Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Mamlaka za Serikali za Mitaa imepanga kutenga takriban hekta **500,000** za maeneo ya malisho nchini.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kuimarisha mashamba ya Vikuge (Kibaha) na Langwira (Mbarali) yanayozalisha mbegu na malisho kwa kuyapatia vitendea kazi vikiwemo matrekta manne (**4**); *mower* mbili (**2**); hei *bailer* mbili (**2**); *hay rake* mbili (**2**); *forage hervester* mbili (**2**) na *forage bailer* mbili (**2**). Wizara itachimba visima virefu vya maji vitatu (**3**) na kuweka mfumo wa umwagiliaji kwenye mashamba hayo ili kuongeza uzalishaji wa malisho kufikia marobota ya hei **200,198** na mbegu za malisho tani **32.08**. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho ili kuongeza uzalishaji kufikia kilo **10,000** za mbegu za malisho na marobota **150,000** ya hei. Pia, Wizara itawezesha uzalishaji wa malisho aina ya *Napier (Juncao)* katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Pwani. Vilevile, Wizara itajenga maghala **15** ya kuhifadhia rasilimali za malisho na vyakula vya mifugo katika maeneo mbalimbali nchini ili kuwa na hifadhi ya vyakula vya mifugo.

## Huduma ya Afya ya Mifugo

115. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara itawezesha uzalishaji, uagizaji nje ya nchi na usambazaji wa dozi **500,000,000** za chanjo za magonjwa **13** ya kipaumbele; kuchanja mifugo **108,000,000** dhidi ya magonjwa mbalimbali; kununua dawa za kuogeshea mifugo lita **56,000;** kujenga majosho **246;** na kuhamasisha uogeshaji wa mifugo kufikia michovyo **bilioni 1.2** kwa mwaka.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za magonjwa **13** ya mifugo ya kipaumbele na kutoa taarifa kwa wakati ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa hayo.

## Ukaguzi wa Mifugo na Mazao Yake

117. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa afya ya jamii inalindwa dhidi ya magonjwa yanayotoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, Wizara itaendelea na ukaguzi wa mifugo na mazao yake kwenye minada, machinjio, vituo vya ukaguzi vya ndani ya nchi na mipakani (*Zoo-sanitary Inspection Border Posts*). Pia, Wizara itaratibu uchinjaji na ukaguzi wa ng'ombe wapatao **1,850,000**, mbuzi **1,100,000**, kondoo **320,000**, nguruwe **380,000** na kuku **6,000,000** katika mwaka 2023/2024.

118. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaratibu ukaguzi wa mifugo na mazao mbalimbali ya wanyama ambapo ng'ombe wapatao **20,000**, mbuzi na kondoo **40,000** wanatarajiwa kukaguliwa wanaposafirishwa nje ya nchi na ng'ombe wapatao **2,500**, mbuzi na kondoo **300** wanatarajiwa kukaguliwa wanapoingizwa nchini. Pia, Wizara inatarajia kukagua na kuidhinisha nyama ya ng'ombe tani **2,000** pamoja na nyama ya mbuzi na kondoo tani **12,000** kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

## Ustawi wa Wanyama

119. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kutoa elimu ya ustawi wa wanyama kwa wadau **4,300** hususan katika kuzingatia Sheria ya Ustawi wa Wanyama SURA 154 na Kanuni zake. Aidha, Wizara itateua wakaguzi wa ustawi wa wanyama **184** katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa na **81** katika vituo vya ukaguzi vya ndani na mipakani.

## Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo

120. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kutambua na kusajili kwenye mfumo wa kielektroniki takriban mifugo **40,603,262**, (ng'ombe **18,639,646**, mbuzi **16,262,271**, kondoo **5,348,208** na punda **353,779**), ili kuwa na taarifa sahihi kwa ajili ya kuboresha mifugo na kukidhi hitaji la masoko.

## *Ugani, Mafunzo na Utafiti*

### *Huduma za Ugani wa Mifugo*

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa Maafisa Ugani wa ngazi zote, Wizara katika mwaka 2023/2024, itanunua pikipiki **1,200,** vifaa tiba (*Veterinary Kit*) **1,100** na vifaa vya uhimilishaji (*Artificial Insemination Kit*) **184** kwa ajili ya Maafisa Ugani katika Halmashauri **184**. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani (ToT) **1,000** katika Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu teknolojia za mifugo, pamoja na kutoa mafunzo ya ufugaji bora wa kibiashara kwa wafugaji **100,000**.

### Utafiti na Mafunzo

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha vijana na wanawake kwenye ufugaji wa kibiashara na kuongeza

malighafi kwenye viwanda vya nyama nchini, Wizara itaendelea kuimarisha Vituo Atamizi nane **(8)** vilivyoanzishwa na kuongeza vingine nane **(8)** katika mwaka 2023/2024. Pia, Wizara itahuisha Mitaala inayotumika katika vyuo vya mifugo ili kuendana na matakwa ya kuhuisha mitaala kila baada ya miaka mitano (**5**) yaliyoelekezwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET). Aidha, Wizara itaendelea kuratibu Kampasi **8** za LITA na vyuo **12** vya binafsi vinavyotoa Mafunzo ya Mifugo, pamoja na kuratibu Vituo saba (**7**) vya Utafiti wa Mifugo Nchini (TALIRI) na Taasisi kumi na moja (**11**) zinazofanya tafiti za mifugo ili kuhakikisha mafunzo na tafiti zinazofanyika zinakidhi vigezo.

***Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mifugo***
***Baraza la Veterinari Tanzania***

123. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania itafanya ukaguzi wa vituo **2,195** vya huduma ya afya ya wanyama; kukagua vyuo **21** vinavyotoa na vinavyotarajia kutoa mafunzo ya afya na uzalishaji wa mifugo; kusajili Madaktari **70** wa Wanyama; kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi **2,500**; kutoa leseni **300** kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara za veterinari; na kusajili vituo **300** vya kutolea huduma ya afya ya wanyama katika Mamlaka **184** za Serikali za Mitaa. Pia, Baraza litaendesha mitihani ya kuandikishwa kwa wahitimu **2,000** wa stashahada ya afya na uzalishaji wa mifugo.
***Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania***

124. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Taasisi ya Chanjo Tanzania (*TVI*) inatarajia kuzalisha jumla ya dozi milioni **97.4** za chanjo za magonjwa saba (**7)**; kukamilisha utengenezaji na uzalishaji wa chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR); kuendelea na utafiti ili kutengeneza chanjo ya Kichaa cha Mbwa; kununua vifaa vya maabara;

kufanya ukarabati mkubwa wa Maabara za Kanda ya Kusini – Mtwara na Kanda ya Ziwa – Mwanza; kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la kisasa kwa ajili ya uzalishaji wa chanjo za magonjwa yatokanayo na virusi; kuboresha miundombinu ya maabara kwa ajili ya usajili na uhakiki ubora wa viuatilifu vya wanyama;

***Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)***

125. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo :-

(i) Kuzalisha ndama **5,479** kutokana na majike wazazi **6,849**;
(ii) Kuweka uzio wa fensi katika eneo la nyanda za malisho lenye ukubwa wa ekari **2,450** katika ranchi za Kongwa, Mkata, Mzeri, Ruvu na Missenyi;
(iii) Kutekeleza mradi wa unenepeshaji wa ng'ombe **12,696** katika ranchi za Kongwa, Ruvu na Mzeri;
(iv) Kujenga *'feedlots unit''* (**3**) 'kwa ajili ya shughuli za unenepeshaji katika ranchi ya Mzeri, Kongwa na Ruvu;
(v) Kuuza nyama bora ya ''Kongwa beef'' tani **346.8** kupitia maduka ya Kampuni;
(vi) Kuzalisha marobota ya hei **55,000** katika ranchi ya Kongwa na Mzeri kwenye eneo la Ha.**11,000**;
(vii) Kuuza madume bora ya ng'ombe aina ya Boran **1,075** kwa wafugaji wa asili kwa ajili ya kuboresha kosaafu ya mifugo yao;
(viii) Kununua madume bora **33** ya ng'ombe aina ya borani kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji katika ranchi ya Kalambo; na
(ix) Kutoa mafunzo ya ufugaji bora kwa wafugaji **362** na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi **500** kutoka katika vyuo mbalimbali nchini**.**

***Bodi ya Nyama Tanzania***

126. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Bodi imepanga kutoa mafunzo kwa wadau **1,209** wa tasnia ya nyama katika Mikoa **18** ya Tanzania Bara, na kufanya Ukaguzi na Usajili wa Wadau **4,500** wa Tasnia ya Nyama ili watambulike rasmi. Aidha, Bodi itaendelea kutekeleza programu ya kuwajengea uwezo wafugaji ili kuleta uzalishaji wenye tija na kuzalisha nyama bora kwa watumiaji.

127. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Bodi imepanga kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Bodi ya Nyama Tanzania ili kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa wadau.

128. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha tunapata nyama bora na salama ambayo inakidhi viwango vya biashara na ulaji katika mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kujenga machinjio moja (1) ya kisasa ya nguruwe Mkoani Dar es Salaam pamoja na machinjio (1) ya kisasa ya kuku Mkoani Dodoma. Pia, Wizara itaendelea kuzihimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na machinjio na makaro ya kuchinjia nguruwe katika maeneo yenye uhitaji.

***Bodi ya Maziwa Tanzania***

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 TDB itavipatia vyama vya Ushirika **10** mitungi **100** ya kubebea maziwa ili kuwezesha usafirishaji wa maziwa kutoka kwa wafugaji kwenda kwenye vituo vya kukusanyia maziwa na kuwezesha upatikanaji wa maziwa bora na salama kwa walaji. Vilevile, TDB itawezesha upatikanaji wa vifungashio **15,000** kwa vikundi **10** vya ushirika wa maziwa. Aidha, TDB itaendelea kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa maziwa katika Ofisi **10** zaidi za Umma ili ziweze kujiunga na Mpango wa Unywaji Maziwa Ofisini na kuwezesha shule **100**

zaidi kujiunga na Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni katika Halmashauri mbalimbali nchini.

130. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/2024, TDB imepanga kuwajengea uwezo wadau wa maziwa **2,000** na wakaguzi wa maziwa **164** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Aidha, mafunzo kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa yatatolewa kwa vikundi **30** vya wafugaji sanjari na kufanya ukaguzi wa wadau **1,200**, kuwezesha usajili wa wadau **400**, na kukuza uelewa wa Sheria ya Maziwa kwa wadau **800** ili kuboresha mnyororo wa thamani wa maziwa.

131. **Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha upatikanaji wa maziwa kwenye viwanda vya kusindika maziwa na kupunguza upotevu wa maziwa, katika mwaka 2023/2024 TDB imepanga kujenga vituo 10 vya kukusanyia maziwa katika mikoa ya Pwani, Iringa, Mbeya, Songwe, Tabora, Mara, na Katavi.

***Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)***

132. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kusogeza huduma za utafiti kwa wafugaji na wadau waliopo katika Kanda ya Magharibi na sehemu ya Nyanda za Juu Kusini inayojumuisha mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi, na Rukwa; Wizara kupitia TALIRI itajenga jengo moja (**1**) la ofisi katika kituo kipya cha TALIRI kitakachofunguliwa katika Halmashauri ya Nsimbo Mkoa wa Katavi. Aidha, katika mwaka 2023/2024 TALIRI itaendelea na ujenzi wa maabara tatu (**3**) za kupima ubora wa nyama na maziwa katika vituo vya TALIRI Uyole, Tanga na Mpwapwa. Pia, TALIRI itaendelea kufanya tafiti katika maeneo ya kipaumbele ambayo ni: uzalishaji na uendelezaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo; kuku na nguruwe na uchambuzi na uhifadhi wa kosaafu za mifugo mbalimbali ya asili. Tafiti nyingine zitahusu uendelezaji wa malisho na uzalishaji wa mbegu za malisho, lishe na ubora wa vyakula vya mifugo.

### *Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)*

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, LITA inatarajia kudahili wanafunzi **4,508** na kuendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi zake nane **(8).** Aidha, LITA itajenga kampasi mpya mkoani Songwe, Wilaya ya Mbozi kwenye eneo la hekta **70** na kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na huduma za ushauri kwa wafugaji na wadau wengine kupitia programu za mafunzo ya ujirani mwema na ziara za mafunzo *(outreach programme and excursions*). Pia, LITA inatarajia kuongeza uzalishaji na utunzaji wa mifugo na malisho bora kwa ajili ya mafunzo na kama mashamba darasa kwa wadau mbalimbali.

## C. SEKTA YA UVUVI (FUNGU 64)

### Hali ya Sekta ya Uvuvi

134. ***Mheshimiwa Spika,*** uvuvi umeendelea kuwa Sekta muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu. Katika mwaka 2022, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia **1.8** kwenye Pato la Taifa na kukua kwa asilimia **2.5.** Aidha, Sekta ya Uvuvi inatoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi **197,763** na wakuzaji viumbe maji **34,057** na takriban watanzania **Milioni 4.5** wanajishughulisha na shughuli mbalimbali zinazohusiana na uvuvi katika mnyororo wa thamani. Pia, Sekta ya Uvuvi inachangia katika kipato cha familia pamoja na kuongeza usalama wa chakula na lishe ambapo samaki huchangia asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za uvuvi zinafanywa zaidi na wavuvi wadogo kwenye maji ya asili ambapo huchangia takriban asilimia **95** ya samaki wote wanaovuliwa nchini. Hadi Aprili, 2023, jumla ya wavuvi wapatao **197,763** walishiriki moja kwa moja katika shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi vipatavyo **58,448**

na kuwezesha kuvuna tani **426,555.46** za samaki zenye thamani ya Shilingi **trilioni 2.86** (**Kiambatisho Na. 18**). Kati ya hizo, tani **381,113.22,** sawa na asilimia **89** ni kutoka maji baridi na tani **45,442.24,** sawa na asilimia **10.7** ni kutoka maji chumvi.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji katika uvuvi wa kibiashara ambao hufanyika katika maji ya kitaifa kwa kuhusisha uvuvi wa kambamiti na Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Mazingira hayo yamewezesha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari kuu kutoa leseni kwa meli **48** kwa ajili ya kuvua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ). Kati ya hizo, meli **45** ni za kigeni na meli tatu (**3**) ni za ndani. Aidha, uvuvi wa kambamiti hufanyika kwa msimu kuanzia mwezi Machi hadi Septemba, katika kanda ya Kaskazini maeneo ya Bagamoyo, Saadani na Pangani na mwezi Aprili hadi Agosti katika Kanda ya Kusini maeneo ya Mkuranga, Kibiti na Kilwa kila mwaka. Katika msimu wa mwaka 2023, jumla ya meli tisa (**9**) ziliomba vibali vya kuvua kambamiti kati ya hizo, meli nne (**4**) zimekidhi vigezo na kupewa leseni. Katika msimu wa uvuvi – mwaka, 2022 jumla ya meli sita (**6**) zilizopewa leseni zilivua tani **57.59** za kambamiti zenye thamani ya shilingi **milioni 835.04**.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, biashara ya mazao ya uvuvi imeendelea kuimarika katika soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, jumla ya tani **29,466.98** za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi **bilioni 453.8** na idadi ya samaki hai wa mapambo **150,308** wenye thamani ya shilingi **bilioni 1.82** waliuzwa nje ya nchi. Katika kipindi hiki, jumla ya tani **6.24** za samaki zenye thamani ya **shilingi bilioni 0.22** zimeingizwa nchini.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeimarisha vituo **36** vya Usimamizi na Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na vituo **8** vya Uthibiti Ubora wa Mazao ya Uvuvi na Masoko katika

maeneo yote ya maji kwa kuvipatia vitendea kazi na vifaa vikijumuisha *printer* **29**, kompyuta mpakato **28**, kompyuta za mezani **34**, *scanner* **24** ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi na ukusanyaji wa maduhuli.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, idadi ya miundombinu ya ukuzaji viumbe maji imefikia mabwawa **32,878**, vizimba **993,** vitotoleshi **39** vya kuzalisha vifaranga na viwanda nane (**8**) vya kutengeneza chakula cha samaki. Aidha, uzalishaji wa mazao mbalimbali ya ukuzaji viumbe maji ulifikia tani **33,525.46** na vifaranga vya samaki **35,967,180 (Kiambatisho Na. 19)** ambapo kati ya hivyo, vifaranga **31,000** vimepandikizwa katika malambo mbalimbali nchini ili kuongeza upatikanaji wa samaki. Vilevile, hadi kufikia Aprili 2023 tani **4,337.9** za chakula cha samaki zilitumika nchini **(Kiambatisho Na. 20)**.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kuwawezesha wavuvi kukopeshwa boti za uvuvi za kisasa na zana zake, ufugaji samaki kwenye vizimba na uzalishaji wa zao la mwani kwa kupatiwa mkopo wa masharti nafuu utakaosimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

141. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kuendelea na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko – Lindi, ujenzi wa masoko saba (**7**) ya mazao ya uvuvi na Mialo mitatu (3. Aidha, miundombinu hii itaimarishwa kwa kujenga mitambo ya kuhifadhia mazao kama vile vyumba vya ubaridi na mitambo ya kuzalisha barafu. Vilevile, Serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya ukuzaji viumbe maji na mashamba darasa.


**MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023**
**Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka**

**2022/2023**

142. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 40,000,000,000** kupitia Fungu 64. Hadi Aprili, 2023 **Shilingi 17,392,394,050.74** sawa na asilimia **43.48** ya lengo la mwaka zilikusanywa kutoka Sekta ya Uvuvi sawa na asilimia **51.61** ya lengo la kukusanya **Shilingi 33,333,333,333.33** hadi Aprili, 2023. (**Kiambatisho Na. 21**).

143. ***Mheshimiwa Spika***, fedha hizi zimekusanywa kutoka vyanzo vifuatavyo: leseni za usafirishaji samaki na mazao yake nje ya nchi (*Export Licences*); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi ndani ya nchi (*Import Licences*); ushuru wa mrabaha (*Export Royalty*); Mapato mengineyo (*Miscellaneous receipts*); mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (*Import Royalty*), leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari, tozo ya maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti, kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi ndani ya nchi (*Movement Permit*), mauzo ya vifaranga vya samaki na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi (**Kielelezo Na. 4**).

**Kielelezo Na. 4: Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi Aprili, 2023**




***Chazo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi.***

144. ***Mheshimiwa Spika***, miongoni mwa sababu za kushuka kwa makusanyo ni pamoja na upungufu wa watumishi wa Sekta ya Uvuvi kwenye vituo vya Ulinzi na Usimamizi wa rasilimali za Uvuvi na Uthibiti Ubora wa Viwango na Masoko; kuwepo kwa mianya ya utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenye maeneo ya maji na mipakani; kuwepo kwa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi; kupungua kwa uzalishaji wa samaki na hivyo kupungua malighafi kwenye viwanda vya kuchakata samaki; kupungua kwa sampuli za mazao ya uvuvi yanayopimwa kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi; na ufinyu wa bajeti pamoja na uhaba wa vitendea kazi kwenye baadhi ya vituo kama magari, pikipiki na boti.

**Fedha zilizoidhinishwa kwa Mwaka 2022/2023**

145. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya **Shilingi**

**176,201,183,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 40,522,421,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 135,678,762,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida.**

146. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2022/2023 Fungu 64 lilitengewa jumla ya **Shilingi 40,522,421,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 12,719,235,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na **Shilingi 27,803,186,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi Machi, 2023, jumla ya **Shilingi 16,804,782,829.97** zimetolewa, sawa na asilimia **41.47** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 9,318,749,750.93** ni fedha za mishahara ya watumishi (PE) na **Shilingi 7,486,033,079.04** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC).

**Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

147. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha **Shilingi 135,678,762,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo **Shilingi 98,682,025,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 36,996,737,000** ni fedha za nje. katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha Shilingi bilioni 135.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Hadi Aprili, 2023, jumla ya maombi ya **shilingi bilioni 41,251,987,361.19** yamewasilishwa ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 6,625,345,688.98** zimelipwa na **shilingi bilioni 34,626,641,672.21** zipo kwenye hatua mbalimbali za malipo.

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2022/2023**

**Usimamizi wa Sera na Sheria**

148. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imefanya maboresho ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2022 (GN 478B na 478E) kwa kupunguza gharama za ada za leseni na tozo mbalimbali kwa lengo la kuwapunguzia gharama za uendeshaji wavuvi na wafanyabiashara wa

mazao ya uvuvi nchini. Katika maboresho hayo, baadhi ya ada za leseni zilizounganishwa kuwa moja ni pamoja na Kambakoche hai na Kaa hai, Pweza na Ngisi waliogandishwa na Kambamiti wenye vichwa na wasio na vichwa (*head on and headless*). Kabla ya marekebisho hayo, kila zao lilikuwa linalipiwa kiasi cha Dola za Marekani **500** ikiwa ni ada ya leseni ambapo kwa sasa ada ya leseni ni Dola za Marekani **500** kwa mazao yote yaliyounganishwa kwa wafanyabiashara wadogo.

149. ***Mheshimiwa Spika***, maboresho hayo, pia, yamepunguza ada ya leseni ya uvuvi wa uduvi kutoka Dola za Marekani **300** hadi **200** kwa mwaka. Aidha, tozo za kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi zimepunguzwa ikiwemo tozo za kusafirisha minofu ya Sangara kutoka Dola za Marekani **0.2** hadi **0.1**, leseni ya dagaa wakavu kutoka Ziwa Victoria, Nyasa na Bahari ya Hindi kutoka Dola za Marekani **0.16** hadi **0.1**, na dagaa wa Ziwa Tanganyika kutoka Dola za Marekani ***0.5*** hadi kufikia **0.3** kwa kilo. Maboresho ya Kanuni hii yamefanyika ili kuhamasisha biashara ya uvuvi na kuongeza usalama wa chakula.

150. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imefanya maboresho ya ushuru wa kusafirisha nje ya nchi mabondo mabichi na makavu ambapo kwa sasa mabondo mabichi/yaliyogandishwa yanatozwa ushuru wa Dola za Marekani **2.7** kwa kilo na kwa Mabondo makavu Dola za Marekani **3.3** kwa kilo ikilinganishwa na awali ambapo mabondo hayo yalikuwa yanatozwa asilimia nne (**4**) kwa kuzingatia bei ya soko.


**Usimamizi wa Takwimu za Uvuvi**

151. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuimarisha ukusanyaji, uchakataji na usimamizi wa taarifa na takwimu za uvuvi kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu**.** Katika mwaka 2022/2023, wavuvi **197,763** na vyombo vya uvuvi **58,448** vilitumika katika

shughuli za uvuvi ikilinganishwa na wavuvi **194,804** na vyombo vya uvuvi **57,991** kwa mwaka 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia **1.5** la wavuvi.

152. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Aprili 2023, jumla ya tani **426,555.46** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 2.9** zilivunwa ikilinganishwa na tani **415,880.6** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 2.8** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2021/2022, ambapo kuna ongezeko la asilimia **3** (**Kielelezo Na. 5**). Aidha, ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa nguvu ya uvuvi.

**Kielelezo Na. 5: Ulinganifu wa Uzalishaji wa Samaki kwa Kipindi cha Julai hadi Aprili 2021/2022 na 2022/2023**




***Chazo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi.***

153. ***Mheshimiwa Spika***, kati ya tani **426,555.5**, zilizozalishwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 tani **300,251.57** sawa na asilimia **70.4** ni kutoka Ziwa Victoria, tani **62,771.68** sawa na asilimia **14.7** ni kutoka Ziwa Tanganyika, tani **5,238.51** sawa na asilimia **1.2** ni kutoka Ziwa Nyasa, tani **12,851.45** sawa na asilimia **3.0** ni kutoka maji madogo na tani **45,442.24** sawa na asilimia **10.7** ni kutoka Ukanda wa Bahari ya Hindi.

154. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *The Nature Conservancy* kupitia Programu ya Tuungane imefanya sensa ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika. Matokeo ya sensa yanaonesha kuongezeka kwa idadi ya vyombo kutoka vyombo **11,506** mwaka 2011 hadi vyombo **11,963** mwaka 2022. Aidha, idadi ya wavuvi imeongezeka kutoka wavuvi **26,612** mwaka 2011 hadi kufikia wavuvi **29,388** mwaka 2022.

155. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (LVFO) imekamilisha tathmini ya uwingi wa samaki katika Ziwa Victoria na matokeo yanaonesha kiasi cha samaki kilichopo ni tani **2,235,822** na kati ya hizo samaki aina ya sangara ni tani **334,341**, dagaa tani **1,060,589**, furu tani **331,709** na uduvi tani **509,183**.

**Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi**

156. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi shirikishi, ulinzi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi nchini kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu na wenye tija kwa wananchi na Taifa.

157. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, hadi kufikia Aprili, 2023, jumla ya siku kazi **4,743** za operesheni maalum na doria ambazo ni sawa na asilimia **60.8** ya lengo la mwaka la siku kazi **7,800** zilifanyika katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi. Matokeo ya operesheni na doria yalikuwa ni kukamatwa kwa zana haramu za uvuvi, samaki wachanga na watuhumiwa ambapo kesi saba (**7**) zilifunguliwa mahakamani. (**Kiambatisho Na 22**).

158. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO)

imeendelea kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kwa kuvijengea uwezo Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) kwa lengo la kuleta ufanisi na kuongeza tija. Aidha, wavuvi **320** kutoka Vikundi **15** vya BMUs katika Halmashauri ya Mkinga walipatiwa mafunzo kuhusu dhana ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira. Pia, wajumbe **210** wa BMUs kutoka vijiji saba (**7**) vya Halmashauri ya Mkinga vinavyojihusisha na uvuvi wa pweza walihamasishwa kuanza ufungaji wa hiari wa uvuvi wa pweza (Mwamba Darasa) kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu wa rasilimali hiyo. Pia, Wizara kwa kushirikiana na WWF imeandaa Mwongozo wa Ufungaji wa Hiari wa Uvuvi wa Pweza kwa Muda wa mwaka 2023.

159. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mwambao *Coastal Network Tanzania* imeendelea kuhamasisha ufungaji wa hiari wa uvuvi wa pweza (Mwamba Darasa) katika vijiji vya Boma Subutini, Boma Kichakamiba (Mkinga) na Ushongo (Pangani) kwa kipindi cha miezi mitatu ambapo tani **27.6** za pweza zenye thamani ya shilingi **Milioni 29.58** zilivunwa. Vilvile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mwambao na vijiji vya Boma Subutini (Mkinga) na Ushongo (Pangani) imeweka baharini miamba ya bandia **90** katika maeneo ya yaliyopo karibu na mwamba darasa kwenye Kijiji cha Bomasubutini (Mkinga) na **99** katika Kijiji cha Ushongo (Pangani) kwa lengo la kuongeza mazalia ya samaki na pweza uzalishaji ambapo wamefikia makubaliano kutovua kabisa kwenye eneo husika.

160. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *The Nature Conservancy,* kupitia Programu ya Tuungane, imetoa mafunzo kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi, athari za uvuvi haramu na uvuvi endelevu kwa wanachama **78** wa BMUs za Kalunga, Mandakerenge na Mtakuja katika Wilaya ya Nkasi.

161. ***Mheshimiwa Spika***, Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Programu ya Tuungane imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha kuchakata mazao ya uvuvi (Migebuka na Dagaa) katika Kijiji cha Buhingu Wilaya ya Uvinza Kigoma unaojumuisha ujenzi wa vyumba vitano **(5)** vya kuchakata, eneo la kupokelea samaki na nyumba ya walinzi. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Programu ya Tuungane imejenga Ofisi ya Maeneo ya Pamoja ya Usimamizi wa Uvuvi (CFMA) katika Kijiji cha Karema, Wilaya ya Tanganyika (Katavi) na kupatiwa samani.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

162. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kuimarisha uthibiti wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kufanya kaguzi **8,649** kati ya kaguzi **9,472** zilizopangwa ili kuhakiki ubora, usalama wa mazao ya uvuvi na uimara wa mfumo wa uzalishaji. Kaguzi hizo zilifanyika katika viwanda **23** vya kuchakata samaki, vituo **37** vya kuhifadhia samaki hai wa mapambo, mialo **10** ya kupokelea samaki**,** masoko **8**, maghala **70** ya kuhifadhia mazao yaliyokaushwa, vituo **17** vya kugandisha samaki**,** viwanda **16** vya mabondo, meli nne (**4**) za uvuvi na vyombo **1,453** vya kusafirisha mazao ya uvuvi.

163. ***Mheshimiwa Spika***, kaguzi **569** zimefanyika viwandani ambapo kati ya hizo kaguzi **415** ni za kawaida na kaguzi za kina **154**; kaguzi **587** zimefanyika kwenye maghala ya kuhifadhia samaki, vituo vya kugandisha samaki, magari ya kusafirisha samaki, mialo ya kupokelea samaki pamoja na masoko. Vilevile, kaguzi **6,924** za uhakiki wa ubora na usalama wa mazao ili kutoa vyeti vya afya kabla ya kusafirishwa nje ya nchi zilifanyika.

164. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kuimarisha mazingira ya uzalishaji, uchakataji, uhifadhi wa mazao ya uvuvi pamoja na miundombinu ya uvuvi ikiwemo mialo ya

kupokelea samaki na masoko kwa lengo la kuthibiti viwango vya ubora na usalama. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, tani **29,466.98** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **150,308** zenye thamani ya shilingi **bilioni 453.80** waliuzwa nje ya nchi na kuingizia Serikali mrabaha wa shilingi **bilioni 12.56** (**Kiambatisho Na. 23**) ikilinganishwa na tani **34,841.72** na samaki hai wa mapambo **169,089** wenye thamani ya shilingi **bilioni 475.01** waliouzwa nje ya nchi na kuingizia Serikali mrabaha wa shilingi **bilioni 13.84** mwezi Aprili 2022. Aidha, Serikali imeendelea kusimamia uingizaji wa samaki ndani ya nchi kutoka nchi mbalimbali ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili, 2023 jumla ya tani **6.92** za samaki zenye thamani ya shilingi **milioni 236.74** zimeingizwa nchini (**Kiambatisho Na. 24)** ikilinganishwa na tani **4.75** zenye thamani ya shilingi milioni **154.23** zilizoingizwa nchini mwaka 2021/2022.

**Maabara ya Taifa ya Uvuvi**

165. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvi imeendelea kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao yake ili kukidhi viwango vinavyokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa. Aidha, Maabara imeendelea kuhuisha hadhi ya Ithibati kupitia kaguzi za kina za Taasisi ya Ithibati ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADCAS) na kukidhi kiwango cha kimataifa cha ISO17025:2017. Pia, Maabara imepokea sampuli **2,216** na kufanya uchunguzi wa vimelea na kemikali ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ikilinganishwa na sampuli **2,027** zilizopokelewa mwaka 2021/2022.

166. ***Mheshimiwa Spika***, Maabara imeongeza wigo wa utoaji wa huduma zake nchini, ambapo imeingia mkataba na Shirika la Viwango la Tanzania (TBS) ili kupokea na kufanya uchunguzi wa sampuli za vyakula vinavyozalishwa katika Kanda ya Ziwa Victoria, jukumu ambalo hapo awali lilikuwa likitekelezwa na TBS. Vilevile, Maabara imeongeza

wigo na njia mpya za uchunguzi wa samaki na mazao yake baada ya Serikali kuingia makubaliano na Jamhuri ya Watu wa China yaliyolenga kuimarisha biashara ya mazao ya uvuvi.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

167. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imeendelea kusimamia maeneo tengefu (**15)** na hifadhi za bahari tatu (**3**). Lengo ni kuhifadhi uoto wa asili, nyasi za bahari,matumbawe, mazalia na makuzia ya samaki pamoja na kulinda na kuhifadhi samaki aina ya papa potwe (*whale shark*), samaki wa mapambo, silikanti na viumbe waliohatarini kutoweka kama kasa na kaa wanao kwea minazi waitwao tuyuyu (*coconut crab*). Vilevile, uhifadhi unalenga kulinda ndege na nyangumi wanaohama kutoka bara moja na kwenda bara lingine, viboko wanaoitika kwa miluzi, magofu yenye historia za kusisimua na karakana za utengenezaji wa boti za asili. Aidha, maeneo hayo yana vivutio mbalimbali vya utalii vikiwemo fukwe nzuri zenye mchanga laini na mweupe zinazopatikana maeneo machache duniani na hivyo kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache zenye vivutio vya asili katika pwani na bahari.

168. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imebarikiwa kuwa na aina **(10)** ya nyasi bahari kati ya aina **(12)** zilizotambuliwa duniani. Nyasi hizi ni bioanuwai muhimu katika uzalishaji wa viumbe maji wa bahari na kukabilina na mabadiliko ya tabianchi. Tathmini imeonesha kuwa katika maeneo ya Hifadhi ya hapa nchini kuna aina **10** za nyasi bahari katika Ghuba ya Mnazi na Maingiliano ya Mto Ruvuma, aina tano **(5)** katika Hifadhi ya Tanga Silikanti na aina nne **(4)** katika Maeneo Tengefu ya Dar es Salaam.

169. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia matumizi endelevu ya bioanuwai na mifumo ikolojia ya bahari, jumla

ya doria zenye siku kazi **541** zilifanyika hadi kufikia Aprili, 2023. Matokeo ya doria hizo ni kukamatwa kwa zana haramu za uvuvi na kiasi cha shilingi **milioni 28.0** kilikusanywa kutokana na faini. Aidha, elimu kuhusu sheria na matumizi ya zana sahihi na uvuvi endelevu imetolewa kwa wadau **755** ili kuhifadhi rasilimali za bahari kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

170. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2023 watalii **35,562** walitembelea Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ambapo kiasi cha shilingi **bilioni 1.68** kilikusanywa ikilinganishwa na watalii **22,562** na shilingi **bilioni 1.18** zilizokusanywa mwaka 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia **42.4** la mapato yatokanayo na utalii.

171. ***Mheshimiwa Spika***, ongezeko hili la watalii limetokana na jitihada za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuutangaza utalii kupitia filamu ya *The Royal Tour*, pamoja na jitihada za MPRU kuendelea kujitangaza kupitia maonesho ya kitaifa, kikanda na kimataifa yakiwemo maonesho ya **46** ya Kimataifa ya Biashara - Sabasaba, Nanenane, *Italy Tanzania Economic Forum*, Siku ya Utalii Duniani (*World Tourism Day*), *Swahili International Tourism Expo* na Karibu Kusini Expo pamoja na kujitangaza kupitia Utalii Popote, Safari Channel na Channel Ten.

**Ukuzaji Viumbe Maji**

172. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, jumla ya vifaranga **35,967,180** vimezalishwa nchini ikilinganishwa na vifaranga **30,332,528** vya mwaka 2021/2022, sawa na ongezeko la asilimia **18.6** la uzalishaji. Kati ya hivyo, Wizara na Taasisi za Serikali zilizalisha jumla ya vifaranga **4,069,172** ikilinganishwa na vifaranga **3,389,240** vilivyozalishwa mwaka 2021/2022 na vituo vya sekta binafsi vimezalisha vifaranga **31,898,008** ikilinganishwa na vifaranga **26,943,288** vilivyozalishwa mwaka 2021/2022. Vilevile, jumla ya wananchi **8,788** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora

za ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa ikilinganishwa na wananchi **7,884** wa mwaka 2021/2022.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika mnyororo wa thamani wa ukuzaji viumbe maji kwa kuwezesha kampuni **15** za ukuzaji viumbe maji kupata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT)* na ushuru wa forodha kutokana na uagizaji wa pembejeo mbalimbali za ukuzaji viumbe maji ambazo hazipatikani nchini. Jitihada hizi zimepelekea kuongezeka kwa uwekezaji katika vitotoleshi vya sekta binafsi kutoka **35** vya mwaka 2021/2022 kufikia **39** vya 2022/2023. Pia, jumla ya tani **4,337.9** za chakula cha samaki zilitumika nchini ikilinganishwa na tani **2,156.7** zilizotumika mwaka 2021/2022. Kati ya hizo, tani **1,325.2** zilizalishwa nchini na tani **3,012.7** ziliingizwa kutoka nje ya nchi

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa mazao ya ukuzaji viumbe maji yanakidhi vigezo vya soko, Wizara imefanya kaguzi zenye siku kazi **160** katika mashamba ya ufugaji samaki (**44**), vitotoleshi vya samaki (**13**) katika mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Simiyu na Tanga ikilinganishwa na kaguzi zenye siku kazi **69** zilizofanyika mwaka 2021/2022. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imetoa mafunzo kwa wanawake **1,019** ambao ni wakulima wa mwani katika mikoa ya Lindi (**459**), Tanga (**347**) na Mtwara (**213**) kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa zao la mwani ili liweze kukidhi viwango vya ubora.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, idadi ya wakuzaji viumbe maji imefikia **34,057** kutoka **31,998** wa mwaka 2021/2022. Idadi ya mabwawa ya watu binafsi imeongezeka kufikia **32,878** kutoka **31,407** ya mwaka 2021/2022**.** Aidha, idadi ya vizimba imefikia **993** (Ziwa Victoria – **911**, Tanganyika – **3** na Malambo mbalimbali – **79**) kutoka vizimba **780** vya mwaka 2021/2022. Ongezeko hili la

uwekezaji limepelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbe maji kufikia tani **33,525.46** kutoka tani **28,856.87** za mwaka 2021/2022. Uzalishaji huu unajumuisha tani **29,106.6** za samaki wa maji baridi (sato na kambale), tani **8.3** za samaki wa maji bahari (mwatiko), tani **4,379.1** za mwani, tani **30** za kambakoche walionenepeshwa, tani **0.6** za kaa, tani **0.86** za majongoo bahari na vipande **550** vya lulu.

176. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza upatikanaji wa mazao yatokanayo na ufugaji samaki kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula na lishe kwa wananchi, Wizara imepandikiza vifaranga **31,000** vya samaki katika malambo mawili (**2**) ya Amani Makolo – Mbinga (**15,000**) na Kidatu - Kilosa (**16,000**).

**Huduma za Ugani wa Uvuvi**

177. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, ili kuhakikisha kasi ya kutoa huduma za ugani kwa wadau wa Sekta ya uvuvi inaongezeka, Wizara imeendelea kuimarisha huduma hizo kwa kutoa mafunzo kwa wadau nchini kwa kutumia teknolojia ya simu za kiganjani kupitia mfumo wa M-kilimo ambapo maafisa ugani **298** kati ya **677** waliopo wamesajiliwa na kuweza kutoa ushauri wa kitaalam kwa wadau **2,208** wa uvuvi.

178. ***Mheshimiwa spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu inaendesha programu ya atamizi maalum ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa vijana **500,** ambapo awamu ya kwanza imenufaisha vijana **200**. Aidha, Wizara itaendelea kuwawezesha vijana waliopata mafunzo kupata mikopo ya pembejeo za ufugaji samaki na kilimo cha mwani kupitia programu ya ECF. Vile vile, Wizara inaendelea na mchakato wa kuwapata vijana wengine **300** wanaotarajiwa kupewa mafunzo katika awamu ya pili.

Programu hiyo inaendeshwa katika vituo **14** ambapo vituo vitatu (**3**) ni vya umma na **11** ni vya sekta binafsi.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kutoa mafunzo rejea kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji nchini ambapo jumla ya wadau **7,819** kutoka katika mikoa ya Geita, Mwanza, Kagera, Mara, Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, pwani na Simiyu wamepatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji wa samaki kibiashara (**418**), utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji (**475**), ufugaji wa majongoo bahari (**121**), uanzishwaji wa vyama vya ushirika na maandiko ya kibiashara (**6,805**). Aidha, wadau **60,504** walipatiwa elimu ya uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya wavuvi, ukuzaji wa viumbe maji na uvuvi endelevu. Kati ya hao, wadau **23,471** wamepatiwa elimu katika maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), wadau **2,838** katika maonesho ya siku ya chakula dunia na wadau **34,195** katika maonesho ya Nanenane.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa vijarida sera viwili (**2**) kuhusu hitaji la kuongeza kiwango cha upatikanaji wa sangara kwenye Ziwa Victoria na matumizi ya satelaiti kwa shughuli za uvuvi kiuchumi vitakavyosaidia Serikali kufanya maamuzi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Aidha, Jumla ya vipindi **26** vya redio na **13** luninga viliandaliwa na kurushwa hewani kuhusu umuhimu wa ulaji wa samaki na utafiti wa uvuvi nchini. Vilevile, vijarida **18,108** vinavyohusu ufugaji bora wa samaki, athari za uvuvi haramu na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi vilisambazwa kwa wadau wa uvuvi kwa lengo la kutoa elimu.

**Taasisi Zilizo chini ya Sekta ya Uvuvi Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania – TAFIRI Utafiti Bahari ya Hindi**

181. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia TAFIRI imefanya tafiti mbalimbali kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe maji ambazo hutumika kuishauri Serikali kuweka mikakati ya uendelezaji na usimamizi wa Sekta ya Uvuvi nchini.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia TAFIRI imefanya utafiti wa kufuatilia ongezeko la tindikali baharini (*ocean acidification*) na aina za kaboni (*sea water carbonate species*) katika maji ya Pwani ya Tanzania ambao ni utelekezaji wa matakwa ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG). Matokeo ya utafiti huu yanatumika kutoa taarifa ya utelekezaji wa lengo **14.3.1** la SDG kuhusu Maisha Chini ya Maji na kushauri mamlaka ipasavyo juu ya athari za ongezeko hili kwenye usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI inaendelea kufanya utafiti wa ukulima mseto wa mwani na samaki katika pwani ya Bahari ya Hindi kama njia ya kuongeza uzalishaji na chanzo cha chakula na kipato kwa jamii za Pwani. Matokeo ya awali ya utafiti huu yanaonesha kuwa mwani unaolimwa kwenye kina cha mita moja na nusu unakua vizuri zaidi ya ule unaolimwa kwenye maji ya mita moja ambapo katika kipindi cha miezi mitatu, mbegu ya kilo moja na nusu imezalisha kilo **16**.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI imeendelea kufanya utafiti wa teknolojia ya kutumia vyungu vinavyowekwa kwenye matumbawe katika uvuvi wa pweza. Aidha, wadau **84** wamejengewa uwezo wa kutumia teknolojia hiyo ambayo itaongeza ufanisi kulinganisha na zana duni ya mchokoo inayotumika sasa.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TAFIRI inatekeleza mradi wa matumizi ya vifaa vya kuvutia Samaki (*Fish*

*Aggregating Devices-FADs*) ambavyo vitasaidia kuvutia samaki katika maeneo ya karibu na mavuvi ya wavuvi wadogo na kuongeza kiwango cha samaki kinachovuliwa na kuimarisha usalama wa chakula, uchumi, na kuongeza malighafi kwa ajili ya viwanda vya kusindika samaki.

**Utafiti Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria**

186. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TAFIRI inatekeleza mradi wa FISH4ACP ambao unalenga kuendeleza mnyororo wa thamani kwa dagaa na migebuka wa Ziwa Tanganyika. Kwa sasa mradi upo kwenye uendelezaji wa mnyororo wa thamani kwa kujenga uwezo wa wachakataji, kujenga miundombinu ya uchakataji, mifumo ya ubaridi na ugandishaji, na kuongeza ushiriki wa wanawake na vijana.

187. ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia TAFIRI imefanya utafiti wa ufuatiliaji wa aina ya samaki wanaofugwa wenye tija katika mabwawa na atamizi (*hatcheries*) kwa kutumia teknolojia ya vinasaba-mazingira (eDNA) kwa nia ya kuboresha ufugaji samaki nchini. Aidha, utafiti huu umewezesha kutambua aina za samaki za asili na ngeni zinazofugwa kwenye maeneo mbalimbali ya Bonde la Ziwa Victoria. Wafugaji wa samaki wapatao **60** wamefundishwa namna ya kutambua aina ya samaki anayefaa kufugwa ili kuondokana na changamoto ya kufuga samaki wasio na tija kwa kushindwa kuwatambua. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuwekwa mikakati ya kuepukana na ufugaji wa aina ya samaki wasio na tija na pia kufuga samaki mchanganyiko hivyo kusababisha uchafuzi wa vinasaba za spishi za samaki.

**Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi – FETA**

188. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, FETA imedahili jumla ya wanafunzi **1,227** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Kampasi za Mbegani (Bagamoyo, Pwani), Nyegezi (Mwanza) na Kibirizi (Kigoma)

katika Tasnia za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji. Mafunzo haya yanalenga kuwapatia elimu ya umahiri kwa vitendo *(Competence Based Education)* ili kupata wataalam waliobobea katika fani husika ambao watakuwa chachu ya kuleta Maendeleo.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** FETA pia imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uelewa na ujuzi wavuvi, wafanyakazi wa viwanda vya samaki na wananchi ili kuzifikia fursa mbalimbali kupitia Uchumi wa Buluu. Jumla ya washiriki **2,655** wamejengewa uwezo katika tasnia za: mbinu bora za kuongeza mnyororo wa thamani kwenye uvuvi na mazao yake (**150**); usalama wa chakula (**286**) na mbinu bora za ufugaji wa samaki wa kibiashara (**1,632**). Aidha, elimu imetolewa kuhusu ufugaji wa Majongoo Bahari (**189);** ufundi stadi wa matengenezo ya majokofu na vipoza hewa (**32**); na mafunzo stadi yenye Ithibati ya TASAC ya uendeshaji na usalama wa vyombo vidogo katika maziwa na bahari (**366**).

190. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala kupitia mradi wa TRUEFISH umeandaa Mpango wa Biashara (*Business Plan*) wa kuendeleza ukuzaji wa viumbe maji. Mpango huo utaimarisha uwezo na weledi wa wakufunzi **25** kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi katika masuala ya ukuzaji viumbe maji. Mafunzo hayo yatafanyika katika nchi za China, Kenya na hapa nchini. Aidha, mpango utaboresha mitaala ya kozi za muda mrefu na kuandaa mitaala tisa (**9**) ya kozi fupi. Vilevile, Mpango utaiwezesha Wakala kupata vifaa na ujuzi wa kutengeneza vizimba vya kufugia samaki, vifaa vya maabara, vifaa vya kuangalia ubora wa maji, vitotoleshi viwili (**2**) vya vifaranga vya sato na kambale, mtambo wa kuzalisha chakula cha samaki, vifaa kwa ajili ya matengenezo ya mifumo ya baridi (*refrigeration and cold rooms*), kompyuta **30** na vitabu vya kufundishia.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

191. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuvutia uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi, TAFICO imeandaa Mpango wa Biashara (*Business Plan*) ambao umeainisha miradi ya kimkakati kwa ajili ya kuongeza tija katika uvuvi wa bahari kuu na mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi. Pia, katika mpango huo TAFICO itashirikisha sekta Binafsi katika kuibua na kutekeleza baadhi ya miradi kwa utaratibu wa ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public - Private Partnership* -PPP).

192. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuboresha utendaji kazi wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) ili kunufaika na uvuvi wa bahari kuu kwa Wizara kuzindua rasmi Menejimenti ya shirika, kukamilisha ukarabati wa awali wa miundombinu zikiwemo ofisi za Makao Makuu yaliyopo Ras Mkwavi – Kigamboni, ufungaji wa mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (*Government Network*) katika Ofisi za Makao Makuu ya Shirika pamoja na, kukamilisha msawazo (*specifications*) wa meli ya uvuvi ya kutumia mishipi (*long line*) ya kuvua bahari kuu, kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa awali na kuendelea na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) kwenye uvuvi wa bahari kuu. Aidha, Shirika limeendelea na hatua za ununuzi wa mtambo mmoja wa kuzalisha barafu utakaofungwa Kigamboni ambapo hadi sasa mzabuni amepatikana na mkataba wa ujenzi umesainiwa.

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu**

193. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imetoa leseni za uvuvi wa bahari kuu kwa meli **48** ambapo meli tatu (**3**) ni za ndani na **45** ni za nje na kukusanya jumla ya shilingi **bilioni 6.2** ikilinganishwa na leseni **25** zilizotolewa mwaka 2021/2022 na kuwezesha kukusanya shilingi **bilioni 3.3** sawa na ongezeko la asilimia **87.9**. Kuongezeka kwa makusanyo kunatokana

na juhudi za makusudi za kufungua mipaka na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji zinazofanywa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, kampuni ya *Albacora Group* ya Uhispania imeshusha hapa nchini tani **100** za samaki wasiolengwa (*by-catch*) pamoja na kufundisha mabaharia wa Kitanzania **10** (**5** kutoka Tanzania bara na **5** kutoka Zanzibar).

195. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 Mamlaka imewawezesha watumishi **10** wa umma kupata mafunzo ya Waangalizi wa Uvuvi (*Fishery Observers*) wa bahari kuu yaliyotolewa na taasisi ya *CapMarine* ya Afrika Kusini na kufanya idadi ya Waangalizi kufikia **17**. Ongezeko hilo la Waangalizi limeongeza ufanisi wa Mamlaka katika kusimamia kikamilifu shughuli za uvuvi wa bahari kuu.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliridhia Mkataba wa Kimataifa wa FAO wa kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi wanachama. Ili kutekeleza mkataba huo na katika kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi kwenye bahari kuu, Mamlaka imeingia makubaliano ya mashirikiano na taasisi nyingine ambazo ni Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA).

197. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imefanikiwa kuandaa Muundo ambao tayari umeridhiwa na Mamlaka husika ambapo utaiwezesha Mamlaka kuajiri watumishi tofauti na ilivyo sasa ambapo watumishi waliopo wameazimwa kutoka katika Wizara na Taasisi za Serikali Tanzania Bara na Zanzibar na hivyo kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

**MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA UVUVI**

**I. Miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Programu ya ASDP II**

198. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko, ambapo Mkandarasi amekamilisha usanifu wa kina (*Detail Design*) umefanyika, na kazi ya uchimbaji imeanza.

199. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji ikiwemo mialo ya Igabilo (Bukoba) na Chifunfu (Sengerema); kufanya usanifu wa ujenzi wa soko la Tunduma (Momba); ujenzi na ukarabati wa vituo vya ukuzaji viumbe maji vya Ruhila (Songea), Nyengedi (Mtama), Rubambagwe (Chato) na Ruvula (Mtwara). Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa mashamba darasa mawili (**2**) kwa lengo la kutoa huduma za ugani katika Halmashauri za Moshi na Mwanga.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imenunua pikipiki **53** kwa ajili ya maafisa ugani wa uvuvi walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha utoaji wa huduma za ugani.

II. **Mradi wa Mkopo wa Masharti Nafuu (*Extended Credit Facility– ECF*)**

201. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2022/2023, Serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani ambapo Sekta ya Uvuvi ilitengewa jumla ya **shilingi bilioni 60**. Fedha hizi zilielekezwa katika kuwawezesha wavuvi kwa kuwakopesha boti za uvuvi **158** zenye vifaa vya kisasa vya uvuvi kwa wanufaika **2,753** **(*Kiambatisho Na.25*)** pamoja na mradi wa vizimba **613** vya kufugia samaki vyenye wanufaika **3,154** na mkopo wa pembejeo za ukulima wa mwani kwa wanufaika **2,030**. Maeneo mengine ni kuwezesha ujenzi wa mialo mitatu (**3**)

ya Ng'ombo (Nyasa), Karungu (Nkasi) na Chato Beach (Chato); ujenzi wa masoko saba (**7**) ya mazao ya uvuvi ya Tunduma (Tunduma TC), Kyamkwikwi (Muleba), Masuche (Momba), Nyamikoma (Busega), Kasanga (Kalambo), Zingibari (Mkinga) na Manda (Ludewa); kununua na kusanikisha mitambo ya kuhifadhia mazao ya uvuvi (*Cold storage);* na mtambo wa kuzalisha barafu (*Ice making plant*) na vichanja vya kukausha dagaa.

202. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, sehemu ya fedha hizi zilielekezwa katika kuanzisha mashamba darasa **13** ya ufugaji wa samaki katika Halmashauri za Wilaya za Njombe, Iringa, Songea, Ruangwa, Kongwa, Tandahimba, Iramba, Maswa, Mkuranga, Uyui, Bariadi, Rombo na Jiji la Dodoma.
Maeneo mengine ni kufanya tathmini ya kimkakati ya athari kwa mazingira (*Strategic Environmental Assessment* - SEA) kwa lengo la kuainisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki kwenye vizimba katika Ziwa Victoria katika Mikoa ya Mara, Geita, Simiyu, Mwanza na Kagera.

**III. Mradi wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Project – SWIOFish*)**

203. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Mradi wa SWIOFish imeendelea na ujenzi wa ofisi ya utawala ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu - Mafia; ujenzi wa awamu ya kwanza ya Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari – Kunduchi, Dar es Salaam na ununuzi wa samani za ofisi za maabara ya TAFIRI – Dar es Salaam.

**IV. Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi**

204. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development Programme – AFDP*), kwa ufadhili wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), inaendelea

na taratibu za ununuzi wa meli mbili (**2**) za uvuvi wa bahari kuu zenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO). Hadi sasa, Msawazo (*Specifications*) kwa ajili ya ununuzi wa Meli hizo, Upembuzi Yakinifu wa Awali (*Pre-feasibility Study*) na andiko dhana umekamilika na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika.

205. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii kwa ajili ya kusanikisha mtambo wa barafu katika eneo la Ras-Mkwavi (Dar es Salaam), ujenzi wa soko la samaki Kipumbwi (Tanga) na ukarabati wa kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Kingolwira (Morogoro). Vilevile, Wizara imepokea vifaa vya maabara na mitambo miwili (**2**) ya kutengeneza chakula cha samaki kwa ajili ya vituo vya Kingolwira na Rubambagwe (Geita). Pia, Wizara imekamilisha utambuzi wa maeneo kwa ajili kusanikisha vifaa vya kuvutia samaki-FADs katika Bahari ya Hindi. Aidha, mafunzo rejea kwa wafugaji samaki **30** yamefanyika na kuanzisha kongani moja itakayojumuisha wafugaji wa samaki katika Mkoa wa Morogoro.

V. **Miradi chini ya Ufadhili wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO)**

206. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na FAO imekamilisha Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi wa mwaka 2021/2022-2036/2037 ambao ulizinduliwa na **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb**) Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Septemba, 2022. Dira ya Mpango huu ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2036 rasilimali za uvuvi zinasimamiwa kwa kushirikisha sekta binafsi ili kuongeza uzalishaji, uboreshaji wa maisha, usalama wa chakula na lishe kwa ukuaji wa uchumi wa buluu.

207. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya tathmini ya awali ya hali ya shughuli na maisha ya wavuvi wadogo na mahusiano ya jinsia, kutoa mafunzo kuhusiana na dhana ya

usimamizi wa uvuvi unaohusisha Ikolojia na Mazingira (*Ecosystem Approach to Fisheries*) na kuhamasisha ufungaji wa hiari wa uvuvi wa pweza kwenye miamba katika vijiji vya Kizingani, Zingibari, Moa, Ndumbani, Kichalikani na Mwandusi katika Halmashauri ya Mkinga ili kuimarisha usimamizi shirikishi na uvuvi endelevu.

**CHANGAMOTO ZA SEKTA YA UVUVI**

208. ***Mheshimiwa Spika***, Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Sekta ya Uvuvi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Baadhi ya Halmashauri zinazoomba kujengewa miundombinu ya uvuvi kutokuwa na ardhi iliyotengwa kwa ajili ya miradi hiyo;

(ii) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa unaokadiriwa kufikia kati ya asilimia **30** na **40** hususan katika maeneo ya vijijini;

(iii) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa bahari kuu na usindikaji wa mazao ya uvuvi;

(iv) Idadi ndogo ya watumishi katika Sekta ya Uvuvi ikilinganishwa na mahitaji yaliyopo; na

(v) Upatikanaji wa vifaranga na vyakula vya samaki vyenye ubora.

209. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizi Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kuhamasisha Halmashauri zote nchini kuainisha maeneo yanayofaa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya uvuvi na kupata hati za umiliki wa ardhi kabla ya kuomba mradi;

(ii) Katika kukabiliana na upotevu wa mazao ya uvuvi Wizara imeshirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta binafsi kuimarisha na kujenga miundombinu muhimu ya uvuvi ikiwemo masoko na mialo; imehamasisha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi; Imehamasisha sekta binafsi kusanikisha mitambo ya kuhifadhia mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa; na imeendelea kutoa elimu ya namna ya kulinda ubora wa mazao ya uvuvi;

(iii) Kupitia Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu sura 388 ya mwaka 2020 na Kanuni zake za mwaka 2021 ambayo imetoa vivutio kwa wawekezaji ikiwemo kuondoa tozo ya Dola za Marekani **0.4** kwa kilo ya samaki lengwa waliovuliwa na meli za kigeni zinazovua katika EEZ ya Tanzania;

(iv) Kuendelea kuimarisha Wakala ya Mafunzo ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi ili kuongeza udahili pamoja na kuendelea kuomba nyongeza ya bajeti ya ikama;

(v) Wizara inaendelea kuimarisha vituo vyake vya kuzalisha vifaranga kwa kuboresha mifumo ya kutotolesha vifaranga na mbari za samaki wazazi; na

(vi) Wizara kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika kuzalisha vifaranga vyenye ubora na viwanda vya kuzalisha vyakula bora vya samaki.

**MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 MAENEO YA VIPAUMBELE KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2023/2024**

210. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi imepanga kutekeleza vipaumbele vinavyoendana na kufungamanisha Uchumi wa Buluu hususan matumizi

endelevu ya rasilimali za uvuvi ikiwemo uvuvi wa asili na ukuzaji viumbe maji. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari kuu;
(ii) Kuimarisha taasisi za Uvuvi ili kuongeza ushiriki katika Uchumi wa Buluu;
(iii) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi;
(iv) Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji;
(v) Kuimarisha uthibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi na masoko.
(vi) Kuimarisha huduma za Ugani wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe maji.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele hivyo, baadhi ya kazi zitakazofanyika katika mwaka 2023/2024 ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko - Lindi; Ununuzi wa meli tatu (**3**) za uvuvi wa Bahari Kuu; Kufanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika bahari kuu; na kutoa leseni **55** kwa meli za uvuvi wa Bahari Kuu kupitia DSFA.

(ii) Kuimarisha Taasisi za Uvuvi kwa kujenga miundombinu muhimu; kununua boti mbili (**2**) zenye vioo chini (*glass bottom boat*) ili kuongeza utalii kwenye Hifadhi za Bahari na maeneo Tengefu (*eco-tourism)*; Kufanya tafiti za kujua wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika Maziwa (Victoria, Tanganyika Natron na Eyasi), Bahari ya Hindi na Bwawa la Nyumba ya Mungu; kujenga vyumba vitano vya mihadhara na vifaa vya kufundishia katika Kampasi tano (**5**) za FETA.

Aidha, TAFICO itajenga viwanda viwili (**2**) vya kutengeneza chakula cha samaki na kuchakata mazao ya uvuvi, itakarabati gati la kuegeshea meli (*Floating*

*Jetty*); na kununua magari mawili ya ubaridi, kutoa mafunzo kwa Mabaharia kuhusu uvuvi wa Bahari Kuu na kujenga ghala la ubaridi, jengo la mtambo wa kuzalisha barafu na jengo la uhandisi wa mitambo ya uvuvi.

(iii) Kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi; Kuendelea na ulinzi shirikishi kwa kufanya doria zenye siku kazi **8,400**, Kuimarisha Vikundi **50** vya Usimamizi shirikishi wa Rasilimali za uvuvi na kutoa elimu kwa wavuvi **360,** Kuimairisha vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kwa kununua boti **10**, mizani tano **(5)** na pikipiki **30**;

(iv) Kuwawezesha wavuvi na wakuzaji viumbe maji kupata pembejeo na zana za kisasa za uvuvi ikiwemo boti **160** na vizimba **893** kupitia programu ya mkopo nafuu (ECF); kwa kujenga mialo saba (**7**), masoko saba (**7**), kujenga vituo **11** vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi, kufanya Upembuzi Yakinifu na kujenga soko la samaki Kigamboni, mashamba darasa **20** ya ukuzaji viumbe maji; Kuanzisha vituo atamizi **14** kwa ajili ya kuwawezesha vijana **750** kushiriki katika programu maalum ya Atamizi kwa miezi mitatu (**3**). Baada ya mafunzo vijana hao watawezeshwa kupata pembejeo za ufugaji samaki na kilimo cha mwani kupitia Programu ya ECF; na kuainisha maeneo ya ufugaji samaki kwa vizimba katika maeneo matano (**5**) yanayozunguka Ziwa Tanganyika na Nyasa

(v) Kuimarisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi kwa kuiwezesha vifaa vya maabara na kufanya uchunguzi wa sampuli **6,000**; Kufanya kaguzi **9,200** za kuhakiki ubora wa mazao ya uvuvi na kujenga vichanja **40** vya kukaushia dagaa ili kupunguza upotevu wa dagaa baada ya kuvuliwa;

(vi) Kuimarisha vituo saba (**7**) vya ukuzaji viumbe maji kwa kukarabati na kuongeza miundombinu ili kuzalisha

vifaranga **milioni 5**, Kupandikiza vifaranga vya samaki katika mabwawa **10** ya asili; Kutoa mafunzo kwa wakulima **2,000** wa mwani;.

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2023/2024**

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa upande wa Idara ya Uvuvi (Fungu 64) inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi **41,000,000,000**. Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na Leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (*Export Licences*); Leseni ya uingizaji mazao ya uvuvi nchini (*Import Royalty*); Ushuru wa mrabaha wa mauzo nje ya nchi (*Export Royalty*); Tozo za Maabara; Faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

**Usimamizi wa Sera na Sheria**

213. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara inatarajia kufanya mambo yafuatayo ili kuiwezesha nchi kunufaika na Uchumi wa Buluu:- (i) Kufanya maboresho ya Sheria ya Uvuvi, Sura 279 katika maeneo mbalimbali na kanuni zinazosimamia Sekta ya Uvuvi ili kuakisi mabadiliko katika Sekta ya Uvuvi (ii) Kutoa elimu ya Sheria za Sekta ya Uvuvi kwa wadau wa uvuvi wa kanda za Ziwa Victoria, Pwani, Ziwa Tanganyika na Nyanda za Juu Kusini.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaimarisha huduma za ugani, mafunzo rejea, elimu kwa umma (vipindi vya televisheni na redio) na maonesho ya Kitaifa ili kusimamia kikamilifu Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya Uvuvi kwa maendeleo ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji nchini.

**Usimamizi wa Takwimu za Uvuvi**

215. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi za

Uvuvi kwa kufanya sensa za uvuvi katika maeneo mawili **(2)** ya maji baridi (Ziwa Nyasa na Rukwa) na maji madogo (Nyumba ya Mungu, ziwa Babati, Eyasi, Natron na Tlawi) ili kujua nguvu ya uvuvi na kiasi cha samaki kilichovuliwa. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha na kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za uvuvi ikiwemo e-CAS na FiRCIS. Pia, Wizara itaendelea kushirikiana na mashirika ya kikanda na kimataifa kufanya Tathmini ya Wingi na Mtawanyiko wa samaki katika maziwa makuu na bahari.

**Usimamizi na Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi**

216. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi mahususi kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi. Mamlaka hii itawezesha kupunguza au kuondoa changamoto zinazoikabili Sekta ya Uvuvi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi. Vilevile, mamlaka hii itakuwa na wajibu wa kusimamia hifadhi za bahari, maeneo tengefu na maji baridi. Pia,ikiwa ni utekelezaji wa sera ya taifa ya uvuvi ya mwaka 2015 ambayo imebainisha "Serikali itaanzisha Mamlaka itakayohusika na uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi na mazingira katika maeneo ya
bahari na maji baridi."

217. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kusimamia na kulinda rasilimali za Uvuvi kwa kushirikisha jamii zinazonufaika na rasilimali za uvuvi, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi pamoja na taasisi nyingine katika kuimarisha usimamizi shirikishi na kuwawezesha wavuvi na wadau wa uvuvi. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Kikosi Kazi cha kudhibiti Uvuvi Haramu na Uharibifu wa Kimazingira *(National Mult Agency Task Team*-NMAT) katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi kwenye

maeneo ya mabwawa, maziwa madogo, maziwa makuu, Bahari ya Hindi na mipakani kupitia doria zenye siku kazi **8,400** ya mazao ya uvuvi. Vilevile, itaimarisha Vikundi **50** vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za uvuvi (BMUs) na kuelimisha wavuvi wadogo **360** kuhusu usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika maziwa makuu na Bahari ya Hindi.

**Uthibiti wa Ubora na usalama wa mazao ya uvuvi**

218. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaviwezesha vituo **11** vya Uthibiti Ubora, Viwango na Masoko ya mazao ya uvuvi kwa kufanya kaguzi **9,200** na kutoa vyeti vya afya **12,000** kwa ajili ya usafirishaji wa samaki na mazao yake nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendelea kudhibiti ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ili kuendelea kukidhi viwango vya masoko ya samaki na mazao yake nje ya nchi.

**Maabara ya Taifa ya Uvuvi Tanzania**

219. ***Mheshimiwa Spika,*** *katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea* kuimarisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi kwa kuiwezesha vifaa vya maabara ili kutekeleza majukumu yake. Aidha, Maabara itaongeza wigo wa kufanya upimaji wa kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kutoka kwa wakuzaji viumbe maji, wachakataji wa dagaa pamoja na mazingira yake ili kulinda afya za walaji wa ndani ya nchi, kikanda na kimataifa. Vilevile, Maabara itaongeza wigo wa sampuli na vipimo vya virutubisho kwenye vyakula vya samaki na vimelea wa sumu kuvu. Maabara itaongezà idadi ya uchunguzi wa sampuli hadi kufikia **6,000.**

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

220. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia MPRU itaendelea kutangaza maeneo yaliyohifadhiwa na vivutio vya utalii vilivyomo pamoja na

kuboresha miundombinu ya utalii wa kiikolojia (*eco-tourism*) ikiwemo kuongeza maboti yenye vioo chini (*glass bottom boat*) ili kuongeza idadi ya watalii kutoka ndani na nje ya nchi na kuongeza mapato yatokanayo na utalii bahari na kwenye maji baridi. Aidha, MPRU itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa hoteli za kiikolojia za kitalii katika maeneo yaliyohifadhiwa ili kuongeza idadi ya watalii na mapato ya Serikali.

221. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia MPRU itatekeleza mradi wa uhifadhi wa pamoja wa usimamizi wa maeneo ya hifadhi yaliyopo katika mpaka wa Tanzania katika Wilaya ya Mkinga na Diani-Chale - Kenya (*Transboundary Marine Conservation Area* - TBCA) ili kuweza kusimamia kwa pamoja rasilimali hizo. Aidha, MPRU kupitia ufadhili mfuko wa GEF (*Global Environmental Facility*) itatekeleza mradi wa usimamizi na ulinzi wa rasilimali za matumbawe katika maeneo ya Kilwa, Mafia na Tanga.

**Ukuzaji viumbe maji**

222. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na uzalishaji wa vifaranga kwa kusimamia na kuendesha vituo saba (**7**) vya ukuzaji viumbe maji (Ruhila – Ruvuma, Kingolwira – Morogoro, Mwamapuli – Tabora, Machui – Tanga, Nyengedi – Lindi, Rubambagwe – Chato na Ruvula - Mtwara) ili viweze kuzalisha vifaranga **milioni 5**.

Aidha, wizara itawezesha upandikizaji wa vifaranga vya samaki katika mabwawa **10** ya asili pamoja na kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora za uzalishaji na ongezeko la thamani katika zao la mwani kwa wakulima **2,000** katika mikoa ya ukanda wa pwani.

223. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara itahamasisha matumizi ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji na udhibiti wa magonjwa ya samaki katika vitotoleshi **15**, viwanda **7** vya vyakula vya samaki na wakuzaji viumbe maji **4,000**

pamoja na matumizi ya Kanuni za Ukuzaji Viumbe Maji kwa maafisa ugani **50** wa Wilaya kwa lengo la kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula cha samaki. Aidha, Wizara itafanya kaguzi katika Mikoa sita (**6**) ili kutathmini uzingatiaji wa Sheria katika uanzishwaji na uendeshaji wa mashamba ya samaki, vitotoleshi na viwanda vya chakula cha samaki.

**Huduma za ugani wa Uvuvi na Ukuzaji viumbe maji**

224. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu itaendelea kukuza ujuzi wa vijana katika kubuni na kuendesha miradi katika tasnia ya ukuzaji viumbe maji kwa kutoa mafunzo kwa vitendo kwa vijana **750**, kupitia programu maalum ya Atamizi kwa vijana. Mafunzo haya yanatolewa kwa muda wa miezi mitatu (**3**) katika vituo vitakavyochaguliwa na wizara vilivyopo maeneo mbalimbali nchini. Lengo la mafunzo haya, licha ya kuwaongezea vijana ujuzi, yatatumika kuhamasisha vijana kufanya uwekezaji kibiashara katika sekta ya uvuvi, kuanzisha kampuni ili kujiajiri pamoja na kuongeza utoaji wa huduma za ugani kwa jamii. Hivyo, kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana kwa kuwawezesha kupata mikopo ya pembejeo za ufugaji samaki na kilimo cha mwani kupitia Programu ya IMF – ECF.

225. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, kwa kutambua uwepo wa maendeleo ya matumizi ya teknolojia za kisasa katika kutoa huduma za ugani ili kuwafikia wadau wengi zaidi, Wizara itaimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa huduma za Ugani Kiganjani (*Digital Services Portifolio* – DSP) na M-Kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu kanda **6** za utoaji wa huduma za ugani, kampasi **5** za FETA na Vituo **5** vya Utafiti. Vilevile, Wizara itaandaa Vijarida vinne (**4**), Makala tatu (**3**) na kurusha hewani vipindi **10** vya luninga na **30** vya redio kuhusu elimu ya Uvuvi na ukuzaji viumbe maji. Pia, Wizara

itahuisha miongozo ya ugani na mafunzo rejea kwa Wagani **500** wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji na kuhamasisha vikundi **50** vya kijamii vya kukopeshana vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji kuunda ushirika.

**TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UVUVI Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, TAFIRI itaendelea kufanya tafiti za kujua wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika Maziwa (Victoria, Tanganyika Natron na Eyasi), Bahari ya Hindi na Bwawa la Nyumba ya Mungu. Tafiti hizi zitasaidia kuweka misingi bora ya usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi.

**Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)**

227. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi itaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi juu ya uelewa na ujuzi wa jinsi ya kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo katika Sekta ya Uvuvi. Mafunzo hayo yatajikita katika mnyororo wa thamani katika uvuvi na ukuzaji viumbe maji. Lengo la Wakala ni kutoa wahitimu wenye weledi, ubunifu na watakaoweza kuleta mchango katika maendeleo ya Sekta. Ili kutimiza azma hii, Serikali itaendelea kuboresha na kuongeza miundombinu na vifaa vya kufundishia katika Kampasi tano (**5**) za Mbegani, Nyegezi, Kibirizi, Gabimori na Mikindani.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, TAFICO itatekeleza kazi zifuatazo; kujenga viwanda vya kutengeneza chakula cha samaki na kuchakata mazao ya uvuvi, kukarabati gati la kuegeshea meli (*Floating Jetty*) la Ras Mkwavi; ununuzi wa magari mawili ya ubaridi na gari moja kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya maendeleo pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa kuvua eneo la bahari kuu. Pia, TAFICO itakarabati miundombinu ikiwemo

ghala la ubaridi, jengo la mtambo wa kuzalisha barafu na jengo la uhandisi wa mitambo ya uvuvi.

229. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TAFICO itawezesha upatikanaji wa meli mbili (**2**) za uvuvi na kuanza kuvua bahari kuu; kuanza uzalishaji wa barafu za chengachenga na za tofali (*block ice*) ili kuwezesha uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi; kuwa na maghala ya ubaridi ya kuhifadhia mazao ya uvuvi kwa ajili ya kuboresha huduma za uhifadhi, kujenga kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi pamoja na kiwanda cha chakula cha samaki.

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)**

230. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu inatarajia kutoa leseni **55** kwa meli za uvuvi wa bahari kuu kutoka ndani na nje ya nchi ambapo kiasi cha Shilingi **bilioni 6.8** zitakusanywa kutokana na leseni na vibali vya uvuvi, na kuuza samaki wasiolengwa (*bycatch*).

231. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Mamlaka itaweka mazingira wezeshi kwa kampuni ya *Albacora Group* kujenga kiwanda cha kuchakata samaki katika Manispaa ya Tanga. Kiwanda hicho, katika awamu ya kwanza kitakuwa na: uwezo wa kuchakata tani **20** za samaki kwa siku, kuhifadhi tani **2,400** za samaki na kuajiri wafanyakazi **100**. Kiwanda hicho kitachakata samaki watakaovuliwa bahari kuu, katika Maji ya Kitaifa (*Teritorial Waters*) kutoka kwa wavuvi wadogo. Aidha, ili kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvuliwa (*post harvest losses*), kampuni itasanikisha mitambo miwili (**2**) ya kuzalisha barafu (Dar es Salaam na Unguja).

232. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, DSFA itaendelea kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa utafiti na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kuhusu maeneo

yenye samaki wengi (*Potential Fishing Zones* - PFZ) baharini kwa kutumia simu janja. Aidha, mfumo huo utaboreshwa kwa kuongezewa moduli ya masoko ya mazao ya uvuvi. Utafiti una lenga kupunguza gharama na muda wa kuvua, kuongeza mavuno na kipato cha wavuvi, kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvuliwa na kuboresha usalama wa wavuvi baharini.

**MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA UVUVI Miradi ya Maendeleo chini ya Programu ya ASDP II**

233. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Sekta ya uvuvi itaendelea na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko Mkoani Lindi kama Ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2021/2022 – 2025/2026).

234. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itakamilisha ujenzi wa mialo minne (**4**) ya Igabiro (Bukoba), Chifunfu
(Sengerema), Igombe (Ilemela) na Kayenze (Ilemela) pamoja na vituo vitatu (**3**) vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vya Sota (Rorya), Simiyu (Busega) na Nyakaliro (Sengerema). Aidha, serikali itafanya Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa soko la samaki Kigamboni na maeneo nane (**8**) ya ujenzi wa miundombinu ya Ofisi za Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi (Kigoma, Tanga, Mtwara, Muleba, Kagera, Mtera, Ikola, na Singida).

235. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa vituo vya ukuzaji viumbe maji vya Ruhila, Nyengedi, Rubambagwe na Ruvula na kufanya upembuzi yakinifu wa vituo vinne (**4**) vya ukuzaji viumbe maji vya Mwamapuli, Katavi, Ludewa na Mkinga.

236. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka

2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha Vituo vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi kwa kuvinunulia boti kumi (**10**) zenye injini, Mizani (**5**) za kupima uzito wa samaki, magari nane (**8**) na pikipiki **30**. Aidha, Serikali itaimarisha uendeshaji wa vituo vitano (**5**) vya ukuzaji viumbe maji (Ruvula, Machui, Kunduchi, Ruhila na Nyengedi) kwa kuvipatia vitendea kazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi na kuainisha maeneo ya ufugaji samaki kwa vizimba katika maeneo matano (**5**) yanayozunguka Ziwa Tanganyika na Nyasa.

237. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itawezesha kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) katika miradi inayotekelezwa chini ya Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi. Vilevile, serikali itaendelea na ujenzi wa kituo cha kuhaulisha teknolojia za uvuvi na ukuzaji viumbe maji Nyakabindi. Pia, Serikali itawezesha ujenzi wa jengo la maonesho ya maadhimisho ya siku ya wakulima (Nanenane) la John Mwakangale Mbeya.

238. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali kupitia TAFIRI itafanya utafiti wa uwingi, bioanuwai na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika na pia itaiwezesha FETA kukamilisha ujenzi wa madarasa na maabara katika Kampasi za FETA-Nyegezi, Mikindani na Gabimori

**Mradi wa Mkopo wa Masharti Nafuu (*Extended Credit Facility– ECF*)**

239. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kutekeleza Miradi ya Maendeleo kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF). Miradi hiyo ni pamoja na: kuendelea kuwezesha ufugaji samaki kwenye vizimba **893**, wakulima **2,100** kupata pembejeo na zana za kuzalisha zao la mwani pamoja na kuwezesha upatikanaji wa boti **160** za kisasa na zana bora za uvuvi kwa njia ya mkopo wa masharti nafuu kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Fedha hizi pia zinalenga

kukamilisha ujenzi wa mialo mitatu (**3**) ya Chato Beach (Chato), Karungu (Nkasi) na Ng'ombo (Nyasa); kukamilisha ujenzi wa masoko saba (**7**) ya Tunduma (Tunduma), Kyamkwikwi (Muleba), Masuche (Momba), Manda (Ludewa), Nyamikoma (Busega), Zingibari (Mkinga) na Kasanga (Kalambo) na kununua na kusanikisha mashine za kusindika na kuchakata dagaa; na kuwezesha ujenzi wa mashamba darasa ya ufugaji samaki katika Halmashauri **20**.

**Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP)**

240. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali kupitia Programu AFDP itaendelea na ununuzi wa meli mbili (**2**) za uvuvi; kujenga na kuendesha mitambo miwili (**2**) ya kuzalisha barafu katika Wilaya za Pangani na Bagamoyo; kujenga na kuendesha chumba cha ubaridi - Pangani; kujenga vichanja **40** vya kukausha dagaa; kujenga mahema sita (**6**) ya kukausha dagaa/samaki kwa kutumia jua; kununua na kusanikisha mitambo miwili (**2**) ya kukausha samaki; kujenga soko la samaki Kipumbwi – Pangani; kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) ya kiwanda cha kuchakata samaki; na kusanikisha vivutia samaki (FADs) **10**.

241. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, ili kuimarisha utendaji kazi wa vituo vya ukuzaji viumbe maji, Wizara inaendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya ukuzaji viumbe maji kama ifuatavyo: ujenzi na ukarabati wa mabwawa na kitotoleshi katika kituo cha Kingolwira. Aidha, vituo vitatu (**3**) vya Kingolwira, Mwamapuli na Rubambagwe vitafungiwa mfumo wa maji katika mabwawa na kupatiwa vitendea kazi kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa vituo. Vilevile, itawezesha vikundi **16** vya vijana katika ukanda wa pwani wanaojishughulisha na unenepeshaji wa kaa na ufugaji wa majongo bahari na kuwezesha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa kongani tatu (**3**) za wafugaji samaki zilizoundwa kwa mikoa ya Morogoro, Tabora na Geita.

**Uwekezaji Sekta ya Uvuvi**

242. ***Mheshimiwa Spika***, ustawi wa shughuli za viwanda vya uchakataji wa samaki na mazao yake unahitaji ushirikiano na sekta binafsi na jitihada za Serikali katika kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na maghala ya kuhifadhia na kugandisha mazao ya uvuvi ambapo hadi sasa kuna viwanda vikubwa vya kuchakata mazao ya uvuvi **21**. Viwanda hivyo vimewekezwa maeneo mbalimbali nchini ambapo ukanda wa Pwani una viwanda (**10**); ukanda wa Ziwa Victoria (**10**) kati ya hivyo tisa (**9**) vinafanya kazi na Kimoja (**1**) kipo kwenye majaribio; na ukanda wa Ziwa Tanganyika (**1**). Vilevile, kuna viwanda **11** vya kuchakata zao la mabondo linalotokana na samaki aina ya Sangara na viwanda vitano (**5**) vya kutengeneza zana za uvuvi. (**Kiambatisho Na. 26**).

243. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi. Uhamasishaji huu umewezesha kuanzishwa kwa kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi cha *Aqua Perch Limited* kilichopo mkoani Mwanza kilichofunguliwa mwezi Januari, 2023 na kuanza uzalishaji wa majaribio mwezi Februari, 2023. Aidha, kiwanda cha *Tanperch Ltd* kilichosimama uzalishaji mwaka 2017 kimefufuliwa Januari, 2023 chini ya umiliki mpya na kubadilisha jina kuwa *Lake Star Limite*d kinatarajia kuanza uzalishaji hivi karibuni.

244. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuboresha mazingira ya kibiashara na kuendelea kuvutia wawekezaji katika Sekta ya Uvuvi, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika ufugaji wa samaki kwenye vizimba ambapo hadi Machi, 2023 uwekezaji umefikia thamani ya shilingi **bilioni 17**.

245. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuweka mazingira

wezeshi ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje wenye nia ya kuwekeza Tanzania ili kukuza uchumi wa Taifa katika shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

**D. MASUALA MTAMBUKA KATIKA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI**

**Utekelezaji kwa mwaka 2022/2023**
**Dawati la Sekta Binafsi la Wizara**

246. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilitoa mikopo ya shilingi **bilioni 17.05** kwenye Sekta za Mifugo na Uvuvi. Kati ya fedha hizo shilingi **bilioni 13.70** zilitolewa kwa wazalishaji katika sekta ya mifugo na shilingi **bilioni 3.35** zilitolewa kwenye sekta ya uvuvi.

247. ***Mheshimiwa Spika,*** Mikopo iliyotolewa ilielekezwa kwenye maeneo yafuatayo;

i. Ufugaji wa kuku shilingi **bilioni 9.96**;

ii. Unenepeshaji wa ng'ombe (*fattening*) shilingi **milioni 996.5** ilitolewa kwenye miradi **13** iliyopo katika mikoa ya Tabora, Pwani, na Manyara; iii. Ununuzi wa mitamba **243** na ujenzi wa mabanda ya kisasa ya ng'ombe shilingi **bilioni 1.31**;

iii. Ufugaji wa Nguruwe: miradi **7** iliyopo katika mikoa ya Pwani na Mara shilingi **milioni 397.70**;

iv. Uzalishaji wa chanjo za mifugo shilingi **milioni 469.89**;

v. Ufugaji wa samaki katika mabwawa: mradi **1** uliopo mkoani Pwani shilingi **milioni 195.70**;

vi. Ununuzi na uuzaji wa samaki kutoka ziwa Victoria shilingi **milioni 55** zilitolewa kwenye miradi miwili iliyopo Ukerewe; na

vii. Ufugaji wa samaki kwenye vizimba: miradi **2** na uvuvi katika mkoa wa Mara shilingi **bilioni 2.80**.

248. ***Mheshimiwa Spika***, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza sekta ya maziwa kupitia mikopo kwa wasindikaji wa maziwa nchini. Katika mwaka 2022/23 Benki ilitoa mikopo kwa viwanda viwili vya maziwa vilivyopo Tanga na Kagera vyenye uwezo wa kusindika lita **120,000** na lita **10,000** za maziwa mtawalia. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo itaendelea kutoa mikopo kwa wasindikaji wa maziwa nchini ili kupunguza changamoto ya usambazwaji wa maziwa kupitia mifumo isiyo rasmi inayohatarisha afya za walaji na pia kuikosesha Serikali mapato.

249. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatekeleza mradi wa *Blue Economy for Growth* (*BE4G25*) wenye lengo la kuinua uzalishaji wa mazao ya mwani na uvuvi wa samaki kwa kutoa mikopo ya gharama nafuu kwa ajili ya ununuzi wa boti za kisasa, ujenzi wa vizimba vya kufugia samaki (*cages*) na utoaji wa ushauri wa kitaalamu. Hadi sasa maombi **400** kutoka vyama vya msingi (AMCOS), makampuni na watu binafsi tayari yamepokelewa na yanafanyiwa uchambuzi. Mradi huu unatekelezwa katika mikoa yote iliyozungukwa na maziwa makuu (Victoria, Tanganyika, Rukwa na Nyasa) na mikoa inayopakana na Bahari ya Hindi.

250. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi iliwezesha kampuni **4** zinazohitaji huduma ya mikopo kwenye utayarishaji wa maandiko ya biashara (*Bankable Business Plans*) ambapo makampuni **3** (Sekta ya Uvuvi) na kampuni **1** (Sekta ya Mifugo) zimenufaika kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Pia, TADB imewezesha upatikanaji wa mikopo ya Shilingi **bilioni 1.7** iliyotolewa katika miradi **29** ya mnyororo wa thamani wa

maziwa, unenepeshaji mifugo na ufugaji nguruwe; miradi **20** ya ufugaji kuku, pamoja na miradi **6** ya uvuvi kwa mwaka 2022/2023.

251. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Dawati limetoa elimu na uhamasishaji kuhusu fursa za uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi kwa vyama vitatu (**3**) vya Kanda ya Ziwa Victoria vya Kikumbaitale, Bwai na Nyang'ombe na kuviwezesha kuandaa maandiko ya biashara ya miradi ya kukausha dagaa, vizimba na ufugaji samaki na kuwasilishwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Aidha, Wizara imefanya tathmini ya uendeshaji wa miradi kwa vyama vya ushirika **22** vya wavuvi (Pwani- **3**, Lindi - **4**, Dar es Salaam – **3**, Mbeya -**1**, Ruvuma – **1**, Geita – **1**, Mara -**3**, Mwanza – **1**, Iringa -**1**, Njombe – **1** na Tanga-**3**). Pia, hadi kufikia Machi, 2023 vyama vya Ushirika vya Uvuvi vimefikia **174** ukilinganisha na vyama 170 vilivyokuwepo mwaka 2021/2022.

252. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi kwa kushirikiana na Wakala wa Bima nchini (TIRA) imeratibu uanzishwaji wa Bima za Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya wafugaji, wavuvi na wafugaji viumbe-maji na kurahisisha upatikanaji wa mikopo. Hadi kufikia Machi **31**, **2023**, wanufaika wote wa mikopo iliyotolewa na Benki ya Kilimo kwenye Sekta za Mifugo na Uvuvi wamenufaika na bima hizo. Aidha, Dawati kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali ya bima nchini linaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kujiunga na mfumo huo wa bima ili kuongeza tija katika ufugaji na uvuvi. Pia, wadau **182** wametembelewa na kupewa ushauri wa kitalaam katika mikoa ya Mbeya, Iringa Tanga, Songwe, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Kigoma, Dar es Salaam, Pwani na Lindi.

253. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi itaendelea

kuhamasisha uwekezaji kwenye Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kuibua maeneo mapya ya uwekezaji; kuwajengea uwezo wafugaji na wavuvi kupitia vikundi na vyama vyao vya ushirika ili wafanye shughuli zao kibiashara; kufanya tafiti ya minyororo ya thamani na masoko; kuwaunganisha wawekezaji na taasisi za kifedha; kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini na kuendelea kutoa elimu kuhusu mwelekeo mpya wa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, Dawati la Sekta Binafsi litatembelea vituo atamizi vya Mifugo na Uvuvi ili kutoa elimu ya biashara, utunzaji kumbukumbu na upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa wafugaji na wavuvi kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

254. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Dawati la Sekta Binafsi itaendelea kuwajengea uwezo (*Capacity Building*) wavuvi na wakulima wa Mwani kuhusu madhara ya vifaa vya plastiki (*Micro-plastics*) kwenye shughuli za uvuvi na kilimo cha mwani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo ASPIRES, Dalberg, Heifer International, SAGCOT na PSSA (*Private Sector Strengthening Activities*).

**Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI**

255. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, jumla ya watumishi **854** wa Wizara wakiwemo **475** wa Sekta ya Mifugo na **379** wa Sekta ya Uvuvi wameendelea kuhamasishwa kupima afya zao kupitia vikao viwili **(2)** na semina mbili **(2)** ambapo watumishi **35** wamepima afya zao kwa ridhaa na kupatiwa ushauri nasaha wa namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU.

256. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 jumla ya vikao vitatu **(3)** vya Kamati ya Ajira vimefanyika, ambapo watumishi **15** wamethibitishwa kazini, watumishi **137**

wamepandishwa vyeo, na watumishi **18** wamebadilishwa kada. Aidha, watumishi **22** wameajiriwa. Vilevile, watumishi **23** wamehama, **21** wamehamia Wizarani na watumishi sita (**6**) wameteuliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi. Aidha, taarifa za watumishi wote **854** zimehakikiwa katika mfumo wa HCMIS. Pia, watumishi **27** waliostaafu wameondolewa kwenye Mfumo wa Taarifa za Utumishi na Mishahara.

257. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi Wizara imewawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Hadi kufikia Machi 31, 2023 jumla ya watumishi **39** wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika Shahada za Uzamivu na Uzamili, Shahada, Stashahada ya Juu, Stashahada na Astashahada**.** Aidha, watumishi **40** wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi kuhusu fani mbalimbali zikiwemo Dhana ya Afya Moja, uendeshaji wa ofisi, utunzaji kumbukumbu, usimamizi wa fedha na masuala ya jinsia.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kutekeleza Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS) ambapo watumishi wote **854** wamejaza fomu na kufanyiwa mapitio ya nusu mwaka. Aidha, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) umeendelea kutumika kuingiza na kutunza taarifa za watumishi na kuhakiki mishahara ya watumishi kabla ya kulipa.

259. ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kujikinga dhidi ya maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI na kupima afya zao kupitia vikao na semina mbalimbali; kuwezesha vikao vinne **(4)** vya Kamati ya Maadili; na kuwezesha utekelezaji wa Mifumo ya Taarifa za Kiutumishi na Mshahara (HCMIS), *Government Salary Payment Portal* (GSPP), Mikataba ya Utendaji Kazi (OPRAS) na Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

260. ***Mheshimiwa* Spika**, katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa kwa kuelimisha watumishi **133** katika vituo vitatu vya kanda ya vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya Mwanza, Tabora na Arusha; na Vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Mtwara, Mwanza, Kagera na Kigoma, kuhusu miongozo, kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma.

261. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa kwa kuelimisha watumishi wote **854** kuhusu masuala ya rushwa.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeomba kupatiwa nafasi **229** katika Ikama ya Watumishi zikiwemo ajira mpya **126**, uhamisho **105** na tano **(5)** za uteuzi. Aidha, jumla ya vikao vinne **(4)** vikiwemo viwili (**2**) vya Kamati ya Ajira na viwili (**2)** vya Baraza la Wafanyakazi vitawezeshwa. Pia, majukumu ya Vyama vya Wafanyakazi, SHIMIWI, mabonanza, Siku ya Wanawake Duniani na masuala ya jinsia yatawezeshwa. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa kwa kuelimisha watumishi kuhusu Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma.

**Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

263. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Trade Mark East Africa (TMEA) imeboresha mfumo wa *Mifugo Integrated Management Information System* (MIMIS) kwa kuongeza *Mobile Application* ambayo imewekwa kwenye mashine za POS kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa vibali vya kielekroniki vya kusafirisha mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. POS **150** tayari zimewekewa mfumo huu na

kusambazwa kwenye vituo vya kukusanya maduhuli. Pia, Wizara imeboresha mfumo wa ukusanyaji maduhuli ya uvuvi (FiRCIS) na kujumuisha vyanzo vyote vya maduhuli vilivyopo katika Sekta ya Uvuvi. Vilevile, mafunzo ya kutumia mfumo huu yametolewa kwa watumishi **206** wanaohusika na ukusanyaji wa maduhuli. Mfumo huu umewezesha upatikanaji wa taarifa za makusanyo kwa wakati, kuokoa muda wa utoaji wa leseni za uvuvi na kuwezesha kutolewa hati ya madai maeneo ambayo hayana mtandao.

264. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara imeendelea kutoa taarifa mbalimbali kwa wadau wa mifugo na uvuvi kupitia vipindi maalum vya redio na televisheni kwa kutayarisha na kurusha hewani jumla ya vipindi **47** vya televisheni na vipindi **84** vya redio (TBC 1, Channel Ten, TBC Taifa na Redio ya Kijamii ya Nyemo FM). Pia, Wizara imeandaa na kutoa taarifa kwenye magazeti mara **150**, majarida **15** ya mtandaoni, tovuti na mitandao ya kijamii mara **1,250**. Vilevile, Wizara imepokea na kushughulikia malalamiko na maoni **26** kati ya malalamiko **26** yaliyopokelewa kutoka kwa wananchi na wadau kwa njia ya simu na mitandao ya kijamii ya Wizara.

Aidha, Wizara imeanza kutumia mfumo wa **eMrejesho** unaotoa fursa kwa wananchi au watumishi kuwasilisha mapendekezo, maoni, malalamiko, maswali na pongezi juu ya utendaji kazi wa Wizara ambapo kupitia mfumo huo, maswali **15** yamepokelewa kutoka kwa wananchi na kushughulikiwa ipasavyo.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Uratibu na Majanga na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kupitia mradi wa *Southern African Center for Infectious Diseases Surveillance* (SACIDS) *Foundation for One Health* itaanzisha Jukwaa Shirikishi la Kidigitali la Utambuzi na Uratibu wa Mlipuko wa Magonjwa ya Mifugo ambapo magonjwa

yatatambuliwa mapema na kushughulikiwa kabla ya kuwa majanga. Aidha, mfumo huo shirikishi utahusisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, watoa huduma za afya ya mifugo na wananchi.

266. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kusimamia ukusanyaji wa maduhuli kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, kutoa msaada wa kiufundi, kusimamia na kuboresha mifumo ya kutoa vibali vya kielektroniki vya kusafirisha mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Vilevile, Wizara itaimarisha mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na kuboresha Jukwaa la Kidigitali la Usajili na Uratibu wa Huduma za Ugani (M-KILIMO) na mfumo wa ukusanyaji maduhuli ya uvuvi (FiRCIS).

267. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kutoa taarifa na maarifa kwa wananchi kuhusu shughuli mbalimbali za sekta ya mifugo na uvuvi kupitia vipindi maalum **52** vya redio, **52** vya televisheni, majarida **20** ya mtandaoni na magazeti. Pia, Wizara itapokea na kushughulikia malalamiko na maoni kupitia mfumo uliohuishwa wa e-Mrejesho (www.emrejesho.gov.go.tz), simu na mitandao ya kijamii ya Wizara.

**Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

268. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kusimamia hifadhi ya Mazingira ikiwa ni pamoja na kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Sekta ya Mifugo, katika mwaka 2022/2023 Wizara imefanya tathmini ya athari za Kimazingira na Kijamii (*Environmental and Social Impacts Assessment* - ESIA) katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua katika vijiji vya Msomera (Handeni), Kwekikwembe (Kilindi), Kaiwang (Kiteto) na ujenzi wa Mnada wa Mifugo wa Msomera uliolenga Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Mazingira (*Environmental Management Plan*). Pia, jumla ya

wafugaji **184** walipatiwa Mafunzo kuhusu ufugaji endelevu unaozingatia hifadhi ya mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

269. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza matakwa ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 ambapo imefanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) kwa miradi yenye takwa hilo inayotekelezwa na Wizara. Vilevile, elimu imetolewa kwa wavuvi **204** kuhusu kupunguza athari za uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinamu ikiwemo uvuvi na ufugaji samaki usiokuwa endelevu kutoka katika Bwawa la Nyumba ya Mungu (**87**) na Bwawa la Mtera (**117**).

270. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaandaa mafunzo kwa wafugaji **350** na wavuvi **200** kuhusu ufugaji na uvuvi endelevu unaohimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Halmashauri **12** nchini; kuendelea kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii katika miradi ya ufugaji na uvuvi; na kufanya ukaguzi wa kimazingira (*Environmental Audit - EA*) katika miradi mitano (**5)** na miundombinu mitano (**5)** ya Wizara.

271. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia kitengo cha Mazingira imepanga kutoa elimu kwa wafugaji wa samaki **80** na wamiliki **15** wa viwanda vya kuchakata samaki katika maeneo ya mwambao wa ziwa victoria kuhusu Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004; Kuwajengea uwezo maafisa **20** kutambua viumbe vamizi (*invasive species*) vinavyoweza kupitishwa mipakani, bandarini na viwanja vya ndege; kutoa elimu kwa wadau **500** juu ya athari za uchafuzi wa maji unaotokana na shughuli za kibinadamu kwa jamii ya wavuvi katika wilaya ya Pangani (**50**) na Bagamoyo (**50**) na katika ziwa Babati (**250**) na Manyara (**150**); Kusimamia Tathmini ya athari kwa

Mazingira na Jamii zinazotakiwa katika miradi inayotekelezwa na Sekta ya Uvuvi.

**Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

272. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuendeleza sekta za Mifugo na Uvuvi. Katika mwaka 2022/2023, Wizara imeshiriki kwenye mikutano na vikao mbalimbali vya Kikanda kama ifuatavyo:-

(i) Kikao cha kuandaa rasimu ya ushirikiano baina ya Tanzania na Uganda katika kukabiliana na magonjwa yanayovuka mipaka na yenye kuambukiza binadamu kwenye maeneo ya mipaka ya Tanzania na Uganda.

(ii) Kikao cha Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa programu ya kutokomeza Sotoka ya Mbuzi na Kondoo kwa nchi za SADC ifikapo 2030 kilichofanyika Gaborone Botswana chini ya ufadhili wa Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH) na FAO.

(iii) Kikao kazi cha kuunda Jukwaa la Afya Moja katika ukusanyaji na utoaji wa taarifa zinazohusu magonjwa yanayoenezwa kati ya binadamu na wanyama chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na *Southern African Center for Infectious Disease Surveillance* (SACIDS).

(iv) Mafunzo kuhusu Mafua Makali ya Ndege kwa nchi za SADC na Afrika Kaskazini yaliyofanyika nchini Rwanda.

(v) Kongamano la kujenga uwezo kwa nguvu kazi iliyopo ili iwe na weledi katika kuhakikisha huduma za veterinari zinatolewa kwa kiwango cha kuridhisha, lililofadhiliwa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(World Organization of Animal Health* -WOAH) – Ofisi ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

(vi) Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Madhara ya Magonjwa yanayovuka mipaka katika biashara.

(vii) Vikao vya Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association* - IORA), ambavyo vilifanya tathmini ya utekelezaji wa programu za IORA zikiwemo Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika Bahari ya Hindi;

(viii) Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Bahari (2022 UN Ocean Conference) ambao ulijadili kuongeza matumizi ya sayansi na ubunifu katika utekelezaji wa lengo la 14 la Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustainable Develiopment Goals-SDG);

(ix) Mikutano ya FAO kuhusu uvuvi mdogo na ukuzaji viumbe maji (*International Year of Artisanal Fisheries and Aquaculture* - IYAFA) ambapo masuala mbalimbali kuhusu IYAFA yalijadiliwa; na

(x) Mkutano wa SADC wa kuandaa Mpango wa Maendeleo wa miaka 15 (*Regional Indicative Strategic Plan*-RISP).

273. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza Sekta ya Uvuvi, Wizara inashirikiana na taasisi za kikanda na kimataifa zikiwemo:- Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC), Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (*Lake Victoria Fisheries Organization* - LVFO), Taasisi ya Sayansi za Bahari Mangaribi mwa Bahari ya Hindi (*Western Indian Ocean Marine Science Association* - WIOMSA), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*South West Indian Ocean Fisheries Commision* - SWIOFC), Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority* - LTA), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Tuna Commission* - IOTC),

Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association* - IORA), Kamisheni ya Usimamizi wa Nyangumi (*International Whaling Commission* - IWC), Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission* - IOC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (*African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness* - AWARFA), Shirika la Afya Duniani (*World Health Organization* - WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama (*World Organization for Animal Health* - WOAH).

274. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) imeendelea kufuatilia viashiria vya Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege unaoambukiza binadamu kutokana na kugusana na ndege wenye virusi vya ugonjwa huo. Ili kufanikisha ufuatiliaji huo, jumla ya sampuli **1,002** zilichukuliwa kwenye maeneo hatarishi (kwenye mikoa ya Kagera na Rukwa) wanakotua ndege kutoka Bara la Ulaya na matokeo ya kimaabara yanaonesha mpaka sasa hakuna virusi vya ugonjwa huo hapa nchini. Aidha, Wizara imeshiriki katika mkutano wa kuandaa Andiko la Mradi wa Maziwa kwa ushirikiano na IFAD (*IFAD Dairy Project Design*).

275. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za Kikanda na Kimataifa ili kuimarisha mahusiano katika uwekezaji, masoko na tafiti zinazohusu Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**Gawio la Serikali katika Sekta za Mifugo na Uvuvi**

276. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara ambazo ni TVLA, TALIRI, LITA, Bodi ya Nyama Tanzania, Bodi ya Maziwa Tanzania, TAFIRI, FETA na MPRU zimetoa gawio kwa Serikali

lenye jumla ya Shilingi **153,203,000**, kati ya fedha hizo, Shilingi **117,203,000** ni za Taasisi za Sekta ya Mifugo na Shilingi **36,720,000** ni za taasisi za sekta ya uvuvi (**Kiambatisho Na. 27**) ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi **152,203,000** kilichotolewa mwaka 2021/2022. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha uwepo wa tija katika taasisi hizo ili kuweza kuchangia zaidi mapato katika Mfuko wa Serikali.

**Michango katika Shughuli za Kijamii**

277. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara zimetoa mchango wa Shilingi **212,105,097.00** ikilinganishwa na Shilingi **202,468,500.00** zilizotolewa mwaka 2021/2022. Michango hiyo ni kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii ikiwemo uchanjaji mifugo, kutoa elimu kwa wafugaji, kuendesha elimu ya uhifadhi katika vijiji nje ya eneo la hifadhi za bahari na maeneo tengefu, pamoja na kutoa misaada ya vifaa vya kielimu kwa shule za msingi katika Wilaya ya Mafia.

**E: HITIMISHO**

278. ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2022/2023 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za Kitaifa na Kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

279. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuzitambua na kuzishukuru nchi za Japan, Korea Kusini, Uingereza, Uholanzi, Ireland, Saudi Arabia, United Arab Emirates (UAE), Oman, Norway, Jumuiya ya Ulaya, Jamhuri

ya Watu wa China, Japan, Ethiopia, Comoro na Misri; kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Naomba pia kutambua na kuzishukuru jumuiya za kikanda ambazo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Shirika la Maendeleo la Kiserikali la Nchi za Afrika Mashariki (IGAD), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU).

280. ***Mheshimiwa Spika***, Aidha, nazishukuru taasisi zinazoendelea kutuunga mkono kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:- Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (*Lake Victoria Fisheries Organization-LVFO*), Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority-LTA*), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Tuna CommissionIOTC),* Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*South West Indian Ocean Fisheries Commision- SWIOFC*), Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association*-IORA), *Western Indian Ocean Marine Science Association* (WIOMSA), Kamisheni ya Kimataifa ya Usimamizi wa Nyangumi (*International Whaling Commission-IWC*), Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission-IOC*), na Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (*African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness-AWARFA*).

281. ***Mheshimiwa Spika,*** nitambue pia mchango wa mashirika mengine tunayoshirikiana nayo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ambayo ni: Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Kiatomiki (*International Atomic Energy*), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Misaada la Poland (Polish Aid), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Taasisi ya Rasilimali

za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU-IBAR), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ireland (TEAGASC), Serikali ya Uholanzi na Serikali ya Japan kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (*Economic and Social Development Programme – ESDP*), na *Overseas Fishery Cooperation Foundation (OFCF) of Japan*.

282. ***Mheshimiwa Spika***, nazishukuru pia taasisi za Kifedha na Wadau wa Maendeleo kwa ushirikiano wao hasa, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GIZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA); na mashirika ya IAEA, UNIDO, ILRI, CIAT, ASARECA, CCARDESA na GEF kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

283. ***Mheshimiwa Spika***, Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation, World Wide Fund for Nature (WWF), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFARM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Social Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC),* pamoja na Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

284. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** kwa namna anavyoliongoza Taifa letu na anavyotusimamia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nina imani kuwa ndani ya uongozi wake tutahakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 inatekelezwa kikamilifu hususan katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

285. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua nafasi hii tena kuwashukuru na kuwapongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa maoni yao na ushauri unaolenga kuboresha na kuimarisha Sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia niwashukuru wadau mbalimbali katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, wafugaji na wavuvi hususan wanaozingatia Sheria katika utendaji wa kazi zao kote nchini kwa kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Napenda kuwaahidi kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuunga mkono juhudi za wafugaji, wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa bidhaa za mifugo na uvuvi.

286. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kurejea tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa David Ernest Silinde (Mb),** Mbunge wa Jimbo la Tunduma, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ushauri na ushirikiano wake katika kusimamia majukumu ya Wizara. Aidha, natoa pia shukrani zangu kwa **Prof. Riziki Silas Shemdoe,** Katibu Mkuu, **Dkt. Daniel Elius Mushi** Naibu Katibu Mkuu (Mifugo) na **Bi. Agnes Kisaka Meena** Naibu Katibu Mkuu (Uvuvi), Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri wanazozifanya.

287. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mkuranga ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na ya Taifa letu, nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo ili niweze kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi.

## F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

288. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya Shilingi **295,920,933,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **112,046,777,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mifugo (Fungu 99) na Shilingi **183,874,156,000.00** kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi (Fungu 64). Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

### Fungu 99: Sekta ya Mifugo

288. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaomba kutumia jumla ya Shilingi **112,046,777,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **50,122,670,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **61,924,107,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

(i) **Fedha za Matumizi ya Kawaida: Shilingi 50,122,670,000**
- Mishahara Shilingi **23,939,807,000**
- Matumizi Mengineyo (OC) Shilingi **26,182,863,000**

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo:**

**Shilingi 61,924,107,000**

- Fedha za Ndani, Shilingi **56,592,173,000**
- Fedha za Nje, Shilingi **5,331,934,000**

**Fungu 64: Sekta ya Uvuvi**

290. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/2024, Wizara inaomba jumla ya Shilingi **183,874,156,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, Shilingi Shilingi **49,462,296,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **134,411,860,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo: -

(i) **Fedha za Matumizi ya Kawaida: Shilingi 49,462,296,000.**

- Mishahara ni Shilingi **15,368,951,000**
- Matumizi Mengineyo **(OC)** ni Shilingi **34,093,345,000.**

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo: Shilingi 134,411,860,000**

- Fedha za Ndani: Shilingi **110,682,025,000**
- Fedha za Nje: Shilingi **23,729,835,000**

291. ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz

292. ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono na nikupongeze kwa kusoma vizuri. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO):** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka Fedha 2022/2023, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni masharti ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 6(1)(c) ikisomwa kwa pamoja na kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, inatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni taarifa hii. Taarifa ya Kamati inahusu

utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na maoni ya Kamati ya Fedha kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu mawili yaani: -

(a) Fungu 99 - Sekta ya Mifugo; na

(b) Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya Uchambuzi na Tathimini; Ufafanuzi wa Jumla; sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja za Wizara wa Mifugo na Uvuvi. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli; katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 80.1. Kati ya fedha hizo Sekta ya Mifugo – Fungu 99 ililenga kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 40.1 hadi kufikia Mwezi, Februari Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi

Bilioni 16.7 sawa na asilimia 41.6 ya lengo la makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Sekta ya Uvuvi – Fungu 64, ililenga kukusanya shilingi bilioni 40 kutoka vyanzo mbalimbali kama vilivyobainishwa kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri. Hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 13.3 sawa na asilimia 33.3 ya lengo la makusanyo. Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu unaoneshwa katika kielelezo namba moja kilichoambatanishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa: -

(a) Jumla ya makusanyo ya maduhuli umefikia asilimia 37.5 tu ya lengo hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 ambayo ni ndani ya robo tatu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

(b) Mwenendo huu wa makusanyo ya maduhuli hauridhishi kwani ni chini ya lengo la makusanyo kulingana na muda uliotumika ambao ni karibu asilimia 75 ya muda wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza Serikali kuona umuhimu wa kupanga malengo ya makusanyo yenye uhalisia. Aidha, Serikali ihakikishe inasimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato na kuziba mianya ya upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitekeleza

Miradi ya Maendeleo iliyotengewa jumla ya Shilingi Bilioni 182.4 kwa mchanganuo ufuatao:-

(a) Sekta ya Mifugo - Fungu 99 ilitengewa shilingi bilioni 46.7 na

(b) Sekta ya Uvuvi - Fungu 64 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 135.7.

Mheshimwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, tarehe 15 – 16 Machi, 2023, Kamati ilifanya Ziara katika Mkoa wa Lindi na kukagua miradi ifuatayo: -

(a) Ujenzi wa Bwawa la Kuvuna Maji kwa ajili ya Mifugo – Kijiji cha Matekwe, Wilaya ya Nachingwea; na

(b) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi – Kilwa Masoko, Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Matekwe; Mradi huu wenye thamani ya shilingi 405.8 unalenga kuhudumia wafugaji wa Vijiji vinne vya Matekwe, Majengo, Kilimarondo na Namatunu kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji kwa ajili ya kunywesha mifugo na bwawa hilo lilitarajia kuhudumia jumla ya mifugo 13,192 ambao ni ng'ombe 9,992, mbuzi 2,711 na kondoo 4,89.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unalenga kutatua migogoro ya muda mrefu baina ya wafugaji na wakulima ambayo imekuwepo na hususani wakati wa kiangazi. Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na kwa sasa mradi huo upo katika kipindi cha uangalizi wa muda wa mwaka mmoja ambacho kitakamilika ifikapo Novemba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko; Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi unalenga kuimarisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi, hususani uvuvi katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari Kuu. Utekelezaji wa mradi huu utagharimu jumla ya Shilingi Bilioni 282 na utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 24 kuanzia Septemba, 2022. Aidha, hadi Kamati inatembelea mradi huo ulikuwa umefikia asilimia saba tu ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi; kutokana na Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati imebaini kwamba:-

(a)Kwenye Ujenzi wa Bwawa la Matekwe:-

(i) Hakuna utaratibu rasmi uliowekwa wa namna bora ya ushirikishwaji jamii katika miradi inayojengwa na wakandarasi na hivyo kupelekea changamoto katika utekelezaji wa baadhi ya miradi;

(ii) Kukosekana kwa chombo maalum cha usimamizi wa utekelezaji wa miradi kunapelekea utekelezaji wa miradi hiyo kufanyika chini ya kiwango;

(iii) Mpaka kipindi Kamati inatembelea mradi huo, birika moja tu ndio lililokuwa limejengwa badala ya mabirika mawili kama ilivyokuwa imepangwa kutekelezwa; na

(iv) Kazi iliyofanyika haifanani na thamani ya fedha iliyotolewa kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo. Aidha, bwawa lililojengwa ni dogo ukilinganisha na mahitaji ya idadi ya mifugo iliyokusudiwa. Vilevile kingo za bwawa zinaonekana kutokuwa imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi. Kamati haijaridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huu kwani hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 7.5 tu ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Ukaguzi wa mradi huu, Kamati inashauri haya yafuatayo:-

(i) Serikali isimamie kwa karibu utekelezaji wa mradi huu ili miradi inayotekelezwa iweze kukamilika kwa wakati;

(ii) Serikali ifanye tathmini ya kuwalipa fidia wananchi wote ambao maeneo yao yamechukuliwa kwa ajili ya mradi huu wa bandari ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima;

(iii) Serikali iweke mazingira mazuri ili kuwezesha wawekezaji kuja nchini kuwekeza kwa kujenga viwanda vya kuchakata samaki katika eneo la mradi; na

(iv) Wakati wa Ujenzi wa Bandari hii Mkandarasi awatumie vijana wanaotoka katika eneo la mradi kwa ajili ya kazi ambazo hazihitaji utaalam (vibarua).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba mradi huu ulichelewa kuanza kwa sababu ya mlipuko wa UVIKO – 19 bado Kamati inaona kuna haja ya kuongeza kasi katika utekelezaji na usimamizi na inaona kuwa tija kwani mradi ukikamilika utaendeshwa kibiashara na utaleta manufaa ya kufungua uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, Kamati inashauri miradi kutekelezwa kwa wakati kwani

ucheleweshwaji wa miradi unasababisha kuongezeka muda na gharama zaidi ikiwemo ulipaji wa riba.

Mheshiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Kamati inapongeza jitihada za Serikali za kuendelea kuwafikishia wananchi miradi mbalimbali ambayo ina lengo la kutatua changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo; kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Sekta ya Mifugo ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni 92.1 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyofafanuliwa kwenye Kielelezo Namba mbili. Aidha, jedwali hili pia linaonesha hali ya upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2023 katika utekelezaji wa bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Februari, 2023 ni asilimia 49.4 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha hauoneshi ni kwa namna gani utekelezaji wa majukumu ya Sekta hii utafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu hizo, Kamati inashauri fedha zilizoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili utekelezaji wa majukumu ya sekta hii ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa. Hali ya upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2023, katika utekelezaji wa bajeti kwa sekta ya Uvuvi inaoneshwa katika kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Februari, 2023 ni asilimia 11.2 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Hadi kufikia Februari 2023, fedha

za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni asilimia 32 tu ya fedha zilizotengwa. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo kwenye Sekta hii ya Uvuvi zilizopokelewa ni asilimia 4.8 tu ya fedha zilizolengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla siyo wa kuridhisha na haioni ni kwa namna gani utekelezaji wa miradi ya maendeleo utafanikiwa. Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza shughuli zilizopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati; wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja imeonesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri. Mfano wa Ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu kuondoa tozo kwenye uzalishaji wa maziwa yanayozalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za utekelezaji zilionesha Serikali imeondoa tozo nane katika tasnia ya maziwa ambazo ni kuondoa *VAT* katika maziwa yanayozalishwa nchini, kuondoa *VAT* katika mitungi ya kusafirishia maziwa, kusamehe ushuru wa forodha katika mitamba na matenki ya kusafirishia na kuhifadhia maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Kamati ilishauri pia Serikali kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji kwa ajili ya mifugo ambapo taarifa ya utekelezaji inaonesha kwamba, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na imekamilisha ujenzi wa visima

viwili vya Matansi (Mkuranga) na Lwami (Mwanga). Mabwawa mawili ya Kimambi (Liwale) na Matekwe (Nachingwea) yamejengwa na bwawa mmoja la Muhango (Itigi) limekarabatiwa. Aidha, ujenzi wa visima vitatu vya Kitaraka (Manyoni), Kapele-Kasinde (Momba), Kinamwigulu (Maswa) na mabwawa 11 unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha biashara ya samaki nje ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zingine ikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imefanya jitihada za kujenga miundombinu ya vyumba vya ubaridi katika baadhi ya viwanja vya ndege. Kwa sasa tayari uwanja wa ndege wa Mwanza umewekewa miundombinu *(cold storage facility)* na zoezi hili linaendelea kwenye viwanja vingine vya ndege kwa kadri ya mahitaji na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ushauri wa Kamati kuzingatiwa kwa sehemu, kuna maeneo ambayo Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wake. Mfano, ujenzi wa bwawa la Matekwe na kwa sababu limetolewa taarifa kwamba limekamilika bado lina mapungufu ambayo yasiporekebishwa tija iliyokusudiwa itakosekana. Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kuzingatia ushauri unaotolewa katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya maduhuli na matumizi ya mwaka wa fedha 2023/2024. Mtoa hoja alieleza kuwa jumla ya shilingi bilioni 42 zinakadiriwa kukusanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kiasi hicho ni ongezeko la asilimia tano ikilinganishwa na lengo la maduhuli la mwaka 2022/2023. Mchanganuo wa makadirio hayo umeoneshwa katika kielelezo Namba Nne (4).

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umeonesha kwamba makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya sekta ya mifugo na uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia tano ikilinganishwa na lengo la makusanyo ya mwaka wa fedha uliopita. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa sekta ya uvuvi yapo sawa sawa na makadirio ya makusanyo ya mwaka uliopita. Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli wa mwaka wa fedha 2022/2023 ambao ulifikia asilimia 37 tu ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji, haitakuwa rahisi kufikia lengo la ukusanyaji kwa mwaka 2023/2024 ikiwa mikakati ya ukusanyaji na vyanzo ni vilevile vilivyotumika kwa mwaka ulioisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maumizi ya kawaida. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakadiriwa kutumia Bilioni 98.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Uchambuzi umeonesha kuwa, katika Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuna ongezeko la Bajeti kwa asilimia 14.4 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliopita. Ulinganifu wa makadirio hayo unaoneshwa kwenye Kielelezo Namba Tano (5).

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi zinadhihirisha kuwa uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zimeongezewa msukumo katika bajeti hii ili kuimarisha sekta ya mifugo na uvuvi na kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zote zilizoombwa zinatumika kulingana na malengo yaliyowekwa vilevile Serikali ihakikishe inaipatia Wizara hii fedha zilizotengwa kwa wakati ili iweze kutekeleza shughuli hizo ilizojipangia kwa mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2023/2024,

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaomba kuidhinishiwa jumla ya bilioni 194.3 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Katika fedha hizo, bilioni 165.3 ni fedha za ndani na Bilioni 29.1 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa Bilioni 11.9 sawa na asilimia 6.5 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yamefafanuliwa katika Kielelezo Namba Sita (6).

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezeka kwa asilimia 6.5. Ongezeko hili linaweza kumaanisha kuwa thamani au idadi ya miradi itakayotekelezwa imeongezeka ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa mwaka wa 2022/2023. Bajeti ya maendeleo ya sekta ya mifugo imeongezeka kwa bilioni 15.193 sawa na asilimia 32.3 na bajeti ya maendeleo ya sekta ya uvuvi imepungua kwa shilingi 3,266,902,000 sawa na asilimia 2.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa jumla, kwa kuwa sehemu kubwa ya ongezeko la bajeti limetokana na fedha za ndani na mikopo kutoka nje, Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo: -

(a) Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

(b) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati fedha za maendeleo na matumizi mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, Taasisi na Idara zilizopo chini yake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(c) Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuongeza tija katika uzalishaji, ni muhimu kwa Watumishi wa Serikali kuzingatia nidhamu kwenye matumizi ya fedha kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kujielekeza kwenye mipango inayotekelezeka ili kuleta maendeleo kwa wafugaji na wavuvi.

(d) Serikali iweke utaratibu mzuri wa ufuatiliaji na usimamizi wa wakandarasi katika hatua za utekelezaji wa miradi. Aidha, Serikali iongeze umakini katika usimamizi wa miradi kwa kushirikisha Halmashauri ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ubora uliokusudiwa na kukamilika ndani ya muda uliopangwa ili kuleta tija.

(e) Kamati inashauri Serikali ianzishe Mamlaka mpya za usimamizi wa miradi nchini, chini ya Wizara hii ambapo kwa upande wa sekta ya mifugo pamoja na mambo mengine, wahusike na kusimamia mabwawa, mifugo, majosho, minada, malambo, visima na kadhalika na upande wa sekta ya uvuvi ianzishwe Mamlaka itakayoratibu shughuli zote za uvuvi baharini, kwenye maziwa na mabwawa.

(f) Utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara uzingatie umuhimu wa kutatua changamoto zinazoikabili nchi yetu na Dunia kwa ujumla ikiwemo tatizo la uhaba wa chakula, matatizo ya mabadiliko ya tabianchi na ukosefu wa ajira kwa vijana.

(g) Serikali iendelee kuwekeza na kuimarisha taasisi za utafiti katika sekta za mifugo na uvuvi nchini ili kuongeza tija katika sekta hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Mifugo Kamati inashauri haya yafuatayo:-

(a) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya maeneo ya malisho na mbegu za malisho ili kusaidia upatikanaji wa uhakika wa chakula cha mifugo na hivyo kuongeza thamani ya mifugo yetu kwenye ushindani katika soko;

(b) Kutokana na umuhimu wa vitalu katika kuzalisha mifugo bora, Wizara ifanye jitihada za ziada kujiridhisha na kuhakikisha kwamba wananchi wanaogaiwa vitalu ni wafugaji kwa kuwa lengo lilikuwa kuwasaidia kupata maeneo ya malisho;

(c) Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi iendelee na utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na watumiaji wengine ili kupunguza migogoro inayoweza kutokea baina yao;

(d) Serikali ifanye sensa ya mifugo ili kupata takwimu sahihi kujua idadi ya mifugo, aina ya mifugo, historia ya mifugo hiyo, ikiwemo magonjwa ili kuweza kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya mifugo ikiwemo upatikanaji wa maeneo ya wafugaji pamoja na kupata soko la kimataifa;

(e) Katika kuanzisha na kuendesha vituo atamizi, Serikali izingatie ufugaji bora wa kisasa ambao utahakikisha bidhaa zetu za mifugo zinakuwa na ubora wa hali ya juu na unaweza kushindana katika soko la ndani na soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya uvuvi. Katika sekta ya uvuvi Kamati inashauri haya yafuatayo: -

a) Serikali iweke mpango mkakati wa kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya samaki ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara;

b) Kutokana na kasi ya ukuaji wa kilimo cha mwani nchini na mwamko mdogo wa wananchi kuhusu zao hili, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: Moja; kuandaa mpango wa kutoa elimu kwa wakulima na wananchi kwa ujumla juu ya kilimo hicho kwa lengo la kuhamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga na kilimo hiki. Mbili; kuhakikisha pembejeo na mbegu bora za kilimo cha mwani zinapatikana kwa wakati. Tatu; kuhakikisha soko la uhakika ndani na nje ya nchi linapatikana;

c) Serikali iandae mpango mkakati wa kuhakikisha upatikanaji wa boti pamoja na zana nyingine za uwezeshaji wa uvuvi bora ili kutumia fursa zilizopo katika vyanzo mbalimbali vya maji vilivyopo nchini, kama vile maziwa, mito na mabwawa. Vyanzo hivi vikitumika vizuri vitaongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, Serikali iweke mkakati wa kuwawezesha wavuvi kupata mikopo nafuu itakayowawezesha wavuvi kununua zana bora za uvuvi;

d) Serikali iandae mpango mkakati wa kuongeza mazalia ya samaki na kuhakikisha kwamba viwanda vya kuchakata mazao ya samaki vinavyojengwa nchini vinapata malighafi ya kutosha;

e) Serikali iweke mkakati wa kudhibiti uharibifu wa mazingira unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na kuua mazalia ya samaki kutokana na ukataji wa mikoko, uhabirifu wa matumbawe na uchimbaji mkubwa wa maji.

f) Ili kukabiliana na changamoto ya uvuvi haramu, Kamati inaishauri haya yafuatayo: Moja; kuwawajibisha wafanyabiashara wanaoingiza nyavu zinazotumika katika uvuvi haramu ili kuepusha uharibifu wa mazingira ya bahari na kuathiri viumbe. Mbili; iwekeze katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza nyavu nchini ili kupata nyavu zinazostahili kwenye uvuvi na kupunguza hasara zinazotokana na uvuvi haramu. Tatu; iongeze ulinzi kwenye suala la uvuvi;

g) Serikali ifanye mapitio ya sera, sheria na kanuni za sekta hii ambazo zimepitwa na wakati ili ziweze kuendana na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Ukuaji wa sekta hizi una umuhimu mkubwa katika kuimarisha biashara za mazao haya ndani na nje ya nchi na kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa - 2025 na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo inachangia asilimia Saba ya Pato la Taifa. Pato hilo linatokana na uzalishaji wa nyama ya ng’ombe, tasnia ya maziwa na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku. Vilevile, sekta ya uvuvi inachangia takribani asilimia 1.8 ya Pato la Taifa. Zaidi ya Watanzania Milioni 4.5 wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku kutokana na shughuli mbalimbali zikiwemo kuunda na

kutengeneza boti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na Baba na Mama Lishe. Aidha, sekta ya uvuvi huchangia asilimia 30 ya protini inayotokana na mazao ya wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, endapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi itapewa fedha kwa ajili ya kufanya uwekezaji kikamilifu na kutumia vizuri rasilimali nyingi zilizopo nchini, Wizara hii inao uwezo wa kufanikisha mipango mbalimbali ya Serikali na kutengeneza faida ikilinganishwa na gharama zitakazowekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao natamani kuwatambua Wajumbe wote kwa majina na kuwataja majina yao hapa, hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega - Mbunge na Naibu wake Mheshimiwa David Silinde - Mbunge kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati. Shukrani za Kamati ziwaendee pia Watendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mipango madhubuti ya kuhakikisha

sekta za mifugo na uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija, kuchangia uchumi wa viwanda, kuinua kipato cha wafugaji na wavuvi pamoja na kuchangia kikamilifu katika malighafi ya viwanda na hivyo kuinua Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndugu Nenelwa Mwihambi - *ndc,* Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge - Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati - Ndugu Elieka Saanya, Ndugu Thuwaiba Jumbe na Ndugu Asia Msangi na Msaidizi wa Kamati - Ndugu Mwimbe John kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio na mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa bajeti na Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 6 (1)(c) ikisomwa kwa pamoja na kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, inatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo.

Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa Fedha

2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu mawili yaani: -

(a) **Fungu 99** -Sekta ya Mifugo; na
(b) **Fungu 64** - Sekta ya Uvuvi

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliyochambuliwa, inagusa maeneo makuu yafuatayo: -

i. Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;
ii. Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi hadi kufikia mwezi Februari, 2023;
iii. Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na
iv. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, maswala yaliyobainishwa hapo juu yanajitokeza katika Taarifa hii. Kwa muktadha huo, naliomba Bunge lako Tukufu lifuatilie kwa kina mtiririko wa Taarifa hii ili kupata msingi wa ushauri unaotolewa na Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo.
Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na ukusanyaji wa Maduhuli, upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida na upatikanaji wa Fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

#### *2.2.1 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli*

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 80,100,000,000**. Kati ya fedha hizo **Sekta ya Mifugo – Fungu 99** ililenga kukusanya jumla ya **Shilingi 40,100,000,000**. Hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 16,691,910,229.75** sawa na

**asilimia 41.6** ya lengo la makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Aidha**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 **Sekta ya Uvuvi - Fungu 64** ililenga kukusanya jumla ya **Shilingi 40,000,000,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali kama vilivyobainishwa kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri. Hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 13,327,540,324**, ambayo ni sawa na **asilimia 33.3** ya lengo la makusanyo. Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika

**Kielelezo Na. 1**.

**KIELELEZO NA 1: Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023**

| **Fungu** | **Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023** | **Makusanyo ya Maduhuli hadi Kufikia Februari, 2023** | **Asilimia ya Makusanyo** |
|---|---|---|---|
| **Fungu 99** – Sekta ya Mifugo | 40,100,000,000 | 16,691,910,229.75 | 41.6 |
| **Fungu 64**- Sekta ya Uvuvi | 40,000,000,000 | 13,327,540,324.00 | 33.3 |
| **JUMLA KUU** | **80,100,000,000** | **30,019,450,553.75** | **37.5** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu 99 na Fungu 64*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

(a) Jumla ya makusanyo ya maduhuli umefikia **asilimia 37.5** tu ya lengo hadi kufikia Februari 2023 ambayo ni ndani ya robo tatu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara;

(b) Mwenendo huu wa makusanyo ya maduhuli hauridhishi kwani ni chini ya lengo la makusanyo kulingana na muda uliotumika ambao ni karibu asilimia 75 ya muda wa utekelezaji;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza Serikali kuona umuhimu wa kupanga malengo ya makusanyo yenye uhalisia. Aidha, Serikali ihakikishe inasimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato na kuziba mianya ya upotevu wa mapato.

***2.2.2 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitekeleza Miradi ya Maendeleo iliyotengewa jumla ya **Shilingi 182,409,810,000.00** kwa mchanganuo ufuatao**: -**

(a) Sekta ya Mifugo (Fungu 99) ilitengewa **Shilingi 46,731,048,000.00**; na
(b) Sekta ya Uvuvi (Fungu 64) ilitengewa **Shilingi 135,678,762,000.00.**

**Mheshimwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, tarehe 15- 16 Machi, 2023 Kamati ilifanya ziara katika mkoa wa Lindi na kukagua miradi miwili ifuatayo:-

i) Ujenzi wa Bwawa la kuvuna maji kwa ajili ya Mifugo – Kijiji cha Matekwe, Wilaya ya Nachingwea; na

ii) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi - Kilwa Masoko, Wilaya ya Kilwa.

### *2.2.2.1 Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Matekwe*

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ujenzi wa bwawa la Matekwe wenye thamani ya Shilingi 405,757,160.00 unalenga kuhudumia wafugaji wa vijiji vinne vya Matekwe, Majengo, Kilimarondo na Namatunu kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji kwa ajili ya kunywesha mifugo. Bwawa hilo linatarajiwa kuhudumia jumla ya mifugo 13,192 ambao ni ng'ombe 9,992, mbuzi 2,711 na kondoo 489.

Aidha, mradi huu unalenga pia kutatua migogoro ya muda mrefu baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi hususan wakati wa kiangazi. Taarifa ya Wizara ilionesha utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa asilimia 100 na kwa sasa mradi huo upo katika kipindi cha uangalizi kwa muda wa mwaka mmoja ambacho kitakamilika ifikapo tarehe Novemba, 2023.

### *2.2.2.2 Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi*

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi unalenga kuimarisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi, hususan uvuvi katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari Kuu. Mkakati wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi umelenga kukuza na kuchochea uwekezaji katika uchumi wa bluu na kuiwezesha Sekta ya Uvuvi kuchangia kikamilifu katika pato la Taifa. Bandari hiyo inategemewa kuwa na ukubwa wa gati lenye urefu wa mita 315 na uwezo wa kuingiza meli 3 hadi 10 kwa wakati mmoja kulingana na ukubwa wa meli. Aidha, inatarajia kuhudumia tani 60,000 za samaki kwa mwaka na boti za wavuvi wadogo 300 kwa wakati mmoja.

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa mradi huu utagharimu **Shilingi 282,006,891,775.81** na utakuwa kwa kipindi cha miezi 24 kuanzia Septemba 2022. Aidha, hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umefikia **asilimia 7.5** ya utekelezaji wake.

### 2.3 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kwamba: -

#### a) Ujenzi wa Bwawa la Matekwe

i. Hakuna utaratibu rasmi uliowekwa wa namna bora ya ushirikishwaji jamii katika miradi inayojengwa na wakandarasi na hivyo kupelekea changamoto katika utekelezaji wa baadhi ya miradi;

ii. Kukosekana kwa chombo maalum cha usimamizi wa utekelezaji wa miradi kunapelekea utekelezaji wa miradi hiyo kufanyika chini ya kiwango;

iii. Mpaka kipindi Kamati inatembelea mradi huu, birika moja tu ndio lililokuwa limejengwa badala ya mawili kama ilivyopangwa kutekelezwa;

iv. Kazi iliyofanyika haifanani na thamani halisi ya fedha iliyotolewa kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo. Aidha, bwawa lililojengwa ni dogo ukilinganisha na mahitaji ya idadi ya mifugo iliyokusudiwa. Vilevile Kingo za bwawa zinaonekana kutokuwa na uimara;

v. Birika lililopo limejengwa chini ya kiwango kwani halikidhi mahitaji ya aina zote za mifugo tajwa, mfano Ng'ombe wenye pembe ndefu hawawezi kunywa maji katika

mabirika hayo. Kamati ina maoni kwamba mabirika mawili hayawezi kufikia lengo la kuhudumia idadi ya mifugo iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa bwawa hilo lilitakiwa kujengwa kwa ukubwa wa mita 260 na limejengwa kwa mita 190, Kamati inashauri kuwa, kipindi hiki ambacho ni cha matazamio, Bwawa litanuliwe ili liweze kukidhi mahitaji halisi. Aidha, idadi ya mabirika iongezwe na kuboreshwa ili kukidhi mahitaji halisi ya aina zote za mifugo inayokusudiwa. Vilevile, kingo za bwawa ziimarishwe ili kuepuka kubomoka kipindi maji yanapoongezeka pamoja na kujenga uzio kuepuka mifugo kuvamia bwawa.

**b) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na kasi ya utekelezaji wa Mradi huu kwani hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umefikia **asilimia 7.5** ya utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Ukaguzi wa mradi huu, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali isimamie kwa karibu utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati;

(ii) Serikali ifanye tathmini na kuwalipa fidia wananchi wote ambao maeneo yao yamechukuliwa kwa ajili ya mradi ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima;

(iii) Serikali iweke mazingira mazuri ili kuwezesha wawekezaji kuja nchini kuwekeza kwa kujenga viwanda vya kuchakata samaki katika eneo la Mradi; na

(iv) Wakati wa Ujenzi wa Bandari, Mkandarasi awatumie vijana wanaotoka katika maeneo ya mradi kwa ajili ya kazi ambazo hazihitaji utaalam (vibarua).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba mradi huu ulichelewa kuanza kwa sababu ya mlipuko wa UVIKO- 19, bado Kamati inaona kuna haja kuwa ya kuongeza kasi katika utekelezaji na usimamizi bado inaona kuna tija kwani mradi ukikamilika na kuendeshwa kibiashara, utaleta manufaa kwa kufungua uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, Kamati inashauri miradi kutekelezwa kwa wakati kwani ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi unasababisha kuongezeka muda na gharama za mradi.

**Mheshiwa Spika**, Kwa ujumla, Kamati inapongeza jitihada za Serikali za kuendelea kuwafikishia wananchi miradi mbalimbali ambayo ina lengo la kutatua changamoto zinazowakabili.

**2.4 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Sekta ya Mifugo ilitengewa jumla ya **shilingi 92,050,824,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyofafanuliwa kwenye **Kielelezo Na. 2**. Aidha, jedwali hili pia linaonesha hali ya upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari 2023 katika utekelezaji wa bajeti.

**KIELELEZO NA 2: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa Sekta ya Mifugo na kiasi cha Fedha kilichopokelewa hadi Februari, 2023**

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 99 MWAKA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2022/2023** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2023** | **Asilimia ya Mapokezi** |
| Mishahara | 21,336,097,000 | 9,624,338,113 | 45.1 |
| (OC) | 23,983,679,000 | 13,015,295,502 | 54.2 |
| **Jumla Ndogo** | **45,319,776,000** | **22,639,633,615** | **49.9** |
| Fedha za Ndani | 46,592,173,000 | 22,909,167,131.18 | 49.1 |
| Fedha za Nje | 138,875,000 | | |
| **Jumla Ndogo** | **46,731,048,000** | **22,909,167,131.18** | **49** |
| **JUMLA KUU** | **92,050,824,000** | **45,548,800,746.18** | **49.4** |

***Chanzo: Uchambuzi wa Randama ya Sekta ya Mifugo – Fungu 99***

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa;

i. Jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Februari, 2023 ni **asilimia 49.4** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na

ii. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha hauoneshi ni kwa namna gani utekelezaji wa majukumu ya Sekta hii utafanikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na takwimu hizo, Kamati inashauri fedha zilizoidhinishwa na bunge zitolewe kwa wakati ili utekelezaji wa majukumu ya Sekta hii ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari 2023 katika utekelezaji wa bajeti kwa sekta ya Uvuvi inaoneshwa katika **Kielelezo Na. 3.**

**KIELELEZO NA 3: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa Sekta ya Uvuvi na kiasi cha Fedha kilichopokelewa hadi Februari, 2023**

| **UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 64 MWAKA 2022/2023** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2022/2023** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2023** | **Asilimia ya Mapokezi** |
| Mishahara | 27,803,186,000 | 8,268,040,134.16 | 29.9 |
| (OC) | 12,719,235,000 | 5,026,651,241.55 | 39.4 |
| **Jumla Ndogo** | **40,522,121,000** | **13,294,691,375.71** | **32.8** |
| Maendeleo (Ndani) | 98,682,025,000 | **6,470,525,355.71** | **4.8** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Maendeleo (Nje) | 36,996,737,000 | | |
| **Jumla Ndogo** | **135,678,762,000** | **6,470,525,355.71** | **4.8** |
| **JUMLA KUU** | **176,201,183,000** | **19,765,216,731.42** | **11.2** |

***Chanzo: Uchambuzi wa Randama ya Sekta ya Uvuvi - Fungu 64***

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Februari, 2023 ni **asilimia 11.2** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Hadi kufikia Februari 2023, fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa ni **asilimia 32.8** tu ya fedha zilizotengwa. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa ni **asilimia 4.8** tu ya fedha zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla sio wa kuridhisha na haioni ni kwa namna gani utekelezaji wa miradi ya maendeleo utafanikiwa. Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza shughuli zilizopangwa.

### 2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya Ushauri. Mfano wa Ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu kuondoa tozo kwenye uzalishaji wa maziwa yanayozalishwa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji zilionesha Serikali imeondoa tozo nane katika tasnia ya maziwa ambazo ni kuondoa VAT katika maziwa yanayozalishwa nchini; kuondoa VAT katika mitungi ya kusafirishia maziwa; kusamehe ushuru wa forodha katika mitamba na matenki ya kusafirishia na kuhifadhia maziwa.

Aidha, Kamati ilishauri pia Serikali kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji kwa ajili ya mifugo ambapo taarifa ya utekelezaji inaonesha kwamba Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na imekamilisha ujenzi wa visima 2 vya Matanzi (Mkuranga) na Lwami (Mwanga). Mabwawa 2 ya Kimambi (Liwale) na Matekwe (Nachingwea) yamejengwa na bwawa 1 la Mhanga (Itigi) limekarabatiwa. Aidha, ujenzi wa visima virefu 3 vya Kitaraka (Manyoni), Kapele-Kasinde (Momba), Kinamwigulu (Maswa) na mabwawa 11 unaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha biashara ya samaki nje ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zingine ikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imefanya jitihada za kujenga miundombinu ya vyumba vya ubaridi katika baadhi ya viwanja vya ndege. Kwa sasa tayari uwanja wa ndege wa Mwanza umewekewa miundombinu (cold storage facility) na zoezi hili linaendelea kwenye viwanja vingine vya ndege kwa kadri ya mahitaji na upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ushauri wa Kamati kuzingatiwa kwa sehemu, kuna maeneo ambayo Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wake. Mfano, ujenzi wa bwawa la Matekwe pamoja na kwamba limetolewa taarifa kwamba limekamilika bado lina mapungufu ambayo yasiporekebishwa tija iliyokusudiwa itakosekana.

Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kuzingatia Ushauri unaotolewa katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0. MAKADIRIO YA MADUHULI NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha na Bajeti inayomalizika. Uchanganuzi wa Maduhuli na Makadirio ya Matumizi hayo ni kama ifuatavyo: -

### 3.1. Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** mtoa hoja alieleza kuwa, jumla ya **Shilingi 42,105,000,000.00** zinakadiriwa kukusanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 5** ikilinganishwa na lengo la maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa katika **Kielelezo Na. 4.**

**KIELELEZO NA 4: Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na Mwaka 2022/2023**

| Na. | Fungu | Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 | Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 | Ongezeko/ Pungufu | Ongezeko/ Pungufu kwa Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | **Fungu 99** –Sekta ya Mifugo | 40,100,000,000 | 42,105,000,000 | 2,005,000,000 | 5 |
| **2.** | **Fungu 64** – Sekta ya uvuvi | 40,000,000,000 | 40,000,000,000 | 0 | 0 |
| | **JUMLA** | **80,100,000,000** | **82,105,000,000** | **2,005,000,000** | **2.5** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu 99 na Fungu 64*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umeonesha kwamba: -

(a) Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Sekta ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yameongezeka kwa **asilimia 5** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(b) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Sekta ya Uvuvi yapo sawa sawa na makadirio ya makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(c) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambao ulifikia asilimia 37.5 tu ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji, haitakuwa

rahisi kufikia lengo la ukusanyaji kwa mwaka 2023/2024 ikiwa mikakati ya ukusanyaji na vyanzo ni vilevile vilivyotumika kwa mwaka unaoisha.

**3.2. Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakadiria kutumia **Shilingi 98,184,966,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Uchambuzi umeonesha kuwa, katika Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuna ongezeko la Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa **asilimia 14.4** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganifu wa makadirio hayo unaoneshwa katika **Kielelezo Na. 5**

**Kielelezo Na. 5: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| Fungu | Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 | Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 | Ongezeko/ Pungufu | Ongezeko/Pungufu kwa Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu 99** –Sekta ya Mifugo | 45,319,776,000 | 50,122,670,000 | 4,802,894,000 | 10.6 |
| **Fungu 64** – Sekta ya uvuvi | 40,522,121,000 | 48,062,296,000 | 7,540,175,000 | 18.6 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA** | **85,841,897,000** | **98,184,966,000** | **12,343,069,000** | **14.4** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu 99 na Fungu 64*

**Mheshimiwa Spika,** takwimu hizi zinadhihirisha kuwa uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zimeongezewa msukumo katika Bajeti ili kuimarisha Sekta ya Mifugo na Uvuvi na kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika kulingana na malengo yaliyowekwa. Vilevile Serikali ihakikishe inaipatia Wizara hii fedha zilizotengwa kwa wakati ili iweze kutekeleza shughuli iliyojipangia kwa Mwaka wa fedha husika.

**3.3. Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 194,335,967,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 165,274,198,000** ni fedha za ndani, na **Shilingi 29,061,769,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **Shilingi 11,926,157,000** sawa na **asilimia 6.5** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo yamefafanuliwa katika **Kielelezo Na. 6**

**KIELELEZO NA 6: Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| Fungu | Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 | Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 | Ongezeko/ Pungufu | Ongezeko/Pungufu Kwa Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu 99** Sekta ya Mifugo | **46,731,048,000** | **61,924,107,000** | **15,193,059,000** | **32.3** |
| **Fungu 64** Sekta ya uvuvi | **135,678,762,000** | **132,411,860,000** | **(3,266,902,000)** | **2.4** |
| **JUMLA** | **182,409,810,000** | **194,335,967,000** | **11,926,157,000** | **6.5** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu 99 na Fungu 64*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba: -

a) Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezeka kwa **asilimia 6.5**. Ongezeko hili linaweza kumaanisha kuwa thamani au idadi ya miradi itakayotekelezwa imeongezeka ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

b) Bajeti ya Maendeleo ya Sekta ya mifugo imeongezeka kwa **Shilingi 15,193,059,000** sawa na **asilimia 32.3**; na

c) Bajeti ya Maendeleo ya Sekta ya Uvuvi imepungua kwa **Shilingi 3,266,902,000** sawa na **asilimia 2.4.**

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo; -

### 4.1. Ushauri wa Jumla

Kwa kuwa sehemu kubwa ya ongezeko la bajeti limetokana na fedha za ndani na mikopo kutoka nje, Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

a) Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato;

b) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo na Matumizi Mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, Taasisi na Idara zilizopo chini yake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

c) Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuongeza tija katika uzalishaji, ni muhimu kwa Watumishi wa Serikali kuzingatia nidhamu kwenye matumizi ya fedha kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kujielekeza kwenye mipango inayotekelezeka ili kuleta maendeleo kwa wafugaji na wavuvi;

d) Serikali iweke utaratibu mzuri wa ufuatiliaji na usimamizi wa wakandarasi katika hatua za utekelezaji wa miradi. Aidha, Serikali iongeze umakini katika usimamizi wa miradi kwa kushirikisha Halmashauri ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ubora uliokusudiwa na kukamilika ndani ya muda uliopangwa ili kuleta tija;

e) Kamati inashauri Serikali ianzishe Mamlaka mpya za usimamizi wa miradi chini ya Wizara ambapo kwa upande wa Sekta ya Mifugo pamoja na mambo mengine, wahusike na kusimamia mabwawa ya mifugo, majosho, minada, malambo,visima n.k na kwa upande wa Sekta ya Uvuvi ianzishe Mamlaka itakayoratibu shughuli zote za uvuvi baharini, kwenye maziwa na mabwawa;

f) Utekelezaji wa Mpango wa bajeti ya Wizara uzingatie umuhimu wa kutatua changamoto zinazoikabili nchi yetu na Dunia kwa ujumla ikiwemo tatizo la uhaba wa chakula, matatizo ya mabadiliko ya tabianchi na ukosefu wa ajira kwa vijana; na

g) Serikali iendelee kuwekeza na kuimarisha taasisi za utafiti katika Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini ili kuongeza tija katika Sekta hizo.

**4.2. Sekta ya Mifugo**

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Mifugo Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya maeneo ya malisho na mbegu za malisho ili kusaidia upatikanaji wa uhakika wa chakula cha mifugo na hivyo kuongeza thamani ya mifugo yetu kwenye ushindani wa soko;

b) Kutokana na umuhimu wa vitalu katika kuzalisha mifugo bora, Wizara ifanye jitihada za ziada kujiridhisha na kuhakikisha kwamba wananchi wanaogaiwa vitalu ni wafugaji kwa kuwa lengo lilikuwa kuwasaidia kupata maeneo ya uhakika ya malisho;

c) Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi iendelee na utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na watumiaji wengine ili kupunguza migogoro inayoweza kutokea baina yao;

d) Serikali ifanye Sensa ya mifugo ili kupata takwimu sahihi kujua idadi ya mifugo, aina ya mifugo na historia ya mifugo hiyo ikiwemo magonjwa ili kuweza kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Mifugo ikiwemo ya upatikanaji wa maeneo ya wafugaji pamoja na kupata soko la kimataifa; na

e) Katika kuanzisha na kuendesha vituo atamizi, Serikali izingatie ufugaji bora wa kisasa ambao utahakikisha bidhaa zetu za mifugo zinakuwa na ubora wa hali ya juu na kuweza kushindana katika soko la ndani na la nje.

**4.3. Sekta ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sekta ya Uvuvi Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iweke mpango mkakati wa kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya samaki ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara;

(b) Kutokana na kasi ya ukuaji wa kilimo cha mwani nchini na mwamko mdogo wa wananchi kuhusu zao hili, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) kuandaa mpango wa kutoa elimu kwa wakulima na wananchi kwa ujumla juu ya kilimo hicho kwa lengo la kuhamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga na kilimo hiki;

(ii) kuhakikisha pembejeo na mbegu bora za kilimo cha mwani zinapatikana kwa wakati; na

(iii) kuhakikisha soko la uhakika ndani na nje ya nchi linapatikana.

(c) Serikali iandae mpango mkakati wa kuhakikisha upatikanaji wa boti pamoja na zana nyingine za kuwezesha uvuvi bora ili kutumia fursa zilizopo katika vyanzo mbalimbali vya maji vilivyopo nchini kama vile maziwa, mito na mabwawa. Vyanzo hivi vikitumika vizuri vitaongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, Serikali iweke mkakati wa kuwawezesha wavuvi kupata mikopo nafuu itakayowawezesha wavuvi kununua zana bora za uvuvi;

(d) Serikali iandae mpango mkakati wa kuongeza mazalia ya samaki na kuhakikisha kwamba viwanda vya kuchakata mazao ya samaki vinavyojengwa nchini vinapata malighafi ya kutosha;

(e) Serikali iweke mkakati wa kudhibiti uharibifu wa mazingira unaosababisha mabadiliko ya tabia nchi na kuua mazalia ya samaki kutokana na ukataji wa mikoko, uhabirifu wa matumbawe na uchimbaji mkubwa wa maji;

(f) Ili kukabiliana na changamoto ya uvuvi haramu, Kamati inaishauri
Serikali:-

(i) Kuwawajibisha wafanyabiashara wanaoingiza nyavu zinazotumika katika uvuvi haramu ili kuepusha uharibifu wa mazingira ya bahari na kuathiri viumbe;

(ii) Iwekeze katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza nyavu nchini ili kupata nyavu zinazostahili kwenye uvuvi na kupunguza hasara zinazotokana na uvuvi haramu; na

(iii) Iongeze ulinzi kwenye suala la uvuvi.

(g) Serikali ifanye mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Sekta hii ambazo zimepitwa na wakati ili ziweze kuendana na mahitaji ya sasa.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0. HITIMISHO

### 5.1. Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyofahamika, Sekta za mifugo na uvuvi ni Sekta za uzalishaji ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa Sekta ya viwanda. Ukuaji wa Sekta hizi una umuhimu mkubwa katika kuimarisha biashara za mazao haya ndani na nje ya nchi na kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Malengo ya Maendeleo Endelevu na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020- 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mifugo inachangia **asilimia 7** ya pato la Taifa. Pato hilo linatokana na uzalishaji wa nyama ya ng`ombe, tasnia ya maziwa na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku. Vilevile, Sekta ya Uvuvi inachangia takribani **asilimia 1.8** ya pato la Taifa; Zaidi ya Watanzania **Milioni 4.5** wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku kutokana na

shughuli mbalimbali zikiwemo kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na Baba na Mama lishe. Aidha, Sekta ya Uvuvi huchangia **asilimia 30** ya protini inayotokana na mazao ya wanyama.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, endapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi itapewa fedha kwa ajili ya kufanya uwekezaji kikamilifu na kutumia vizuri rasilimali nyingi zilizopo nchini, Wizara hii ina uwezo wa kufanikisha mipango mbalimbali ya Serikali na kutengeneza faida ikilinganishwa na gharama zitakazowekezwa.

**5.2. Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao natamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:

1. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb
5. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb
6. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb
10. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mb

11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
14. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
16. Mhe. Ng'wasi Damas kamani, Mb
17. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb
18. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb
19. Mhe. Yahya Ally Khamis, Mb
20. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb
21. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega (Mb) na Naibu Waziri wake Mheshimiwa David Silinde (Mb) kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Riziki Shemdoe kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati. Shukrani za Kamati ziwaendee pia Watendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mipango madhubuti ya kuhakikisha Sekta za Mifugo na Uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija, kuchangia uchumi wa viwanda, kuinua kipato cha wafugaji na wavuvi pamoja na kuchangia kikamilifu katika malighafi ya viwanda na hivyo kuinua pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge - Ndg. Michael Chikokoto, *ndc*, Makatibu wa Kamati; Ndg. Elieka Saanya, Ndg. Thuwaiba Jumbe na Ndg. Asia Msangi na Msaidizi wa Kamati - Ndg.

Mwimbe John kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. David Mwakiposa Kihenzile
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BISHARA KILIMO NA MIFUGO**

02 MEI, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kusoma vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa ziada wa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo ambao ni Madiwani kutoka Kiteto; ambao ni Mheshimiwa Isaya Kilae, Mheshimiwa Paulo Litite na Mheshimiwa Christina Ngoibo.

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Babu Tale, Ndugu Ngandi Almas, Ndugu Ngereki Kisukari, Ndugu Augustino Lemomo, Ndugu Ngaiyo Kaunda, Ndugu Makairo Mgema, Ndugu Kandiri Zuberi, Ndugu Lucas Lemomo, Ndugu Maulidi Manga, Ndugu Muya Msurwa, Ndugu Emanuel Tabalo, Ndugu Parasoi Ndimba. Hiki ni Chama cha Wafugaji Tanzania na wanatokea Jimboni kwake kwa Mheshimiwa Babu Tale, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri anaendelea kuwakumbusha kuwa maonesho yanaendelea, mkapate ushauri mbalimbali wa ufugaji wa kisasa wa mbuzi, ng'ombe samaki na vingine.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia na Mheshimiwa Edward Olelekaita, ajiandae Mheshimiwa Lucy Sabu na Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema ambayo ametujalia na ninampongeze Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kwa nchi yetu. Kipekee kabisa kwa niaba ya wananchi wa Kiteto, Wizara ya Mifugo imetuletea majosho karibu Nane, bwawa kubwa la karibu Milioni 500. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunaendelea kumuombea Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema aongoze Taifa letu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Isdory Mpango kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kwa kuendelea kumsaidia Rais kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri wa Mifugo, rafiki yangu Mheshimiwa Ulega, kwanza ninampongeza kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii ya Mifugo na ninakupongeza kwa ziara mbili ulizofanya Kiteto. Umekwenda mpaka huko kabisa

machungani, ulitutembelea wakati wa majanga ya ukame na uliona mifugo na ukatutembelea tena wakati tunatembelea Bwawa la Kawa, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Pia ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde, nampongeza Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Mifugo kwa kuendelea kumshauri Mheshimiwa Rais.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niipongeze Timu ya Wananchi ya Yanga kwa kazi kubwa waliyoifanya na kuijengea heshima nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nijadili changamoto zinazotokana na Wizara hii ya Mifugo. Moja ni mabwawa na majosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 50, 51 na 53 tuliahidi Watanzania kwamba tutajenga mabwawa karibu 454 maana yake mwaka ni mabwawa 92. Ninaomba sana Serikali iiongezee Wizara hii pesa nyingi sana ili tuweze kutimiza ahadi hizi kwa Watanzania. Nachelea kusema kwamba Wizara hii inapata pesa kidogo sana, ninamuomba sana Mheshimiwa Rais na Serikali waongeze bajeti kwenye Wizara hii, angalau hata Bilioni 500 itasaidia ili Wizara hii iweze kutimiza yale yote ambayo tuliyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano majosho, tulisema kila kijiji chenye mifugo kiwe na josho. Kwa Wilaya ya Kiteto peke yake idadi ya mabwawa tuna upungufu wa mabwawa karibu 44, majosho 48. Pamoja na nguvu alizotusaidia Mheshimiwa Waziri hii inaonesha kwamba bado upungufu ni kubwa, mabwawa kama ya Dosidosi, Sunya, Njoro, Kinyungu, Matui, Sunya yote ni mabovu na kwa kweli Mheshimiwa Naibu Waziri tunaomba pesa kwa ajili ya mabwawa haya.

Mabwawa kama ya Dosi, dosi, ya Sunya, Njoro, kijungu, Matui. Sunya, yote ni mabovu na kwa kweli, Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaomba pesa kwa ajili ya mabwawa haya na Bwawa la Kaiwang Mheshimiwa Waziri endelea kufuatilia ili Watanzania wale wapate kunufaika na nguvu za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni maeneo ya malisho. Salama ya wafugaji nchi hii ni kuwa na maeneo salama ambayo yamelindwa kisheria. Kwa hiyo, naipongeza Wizara kwa kuendelea kufanya hivyo, lakini tuendeleze kasi. Hii itaondoa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wa ardhi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni suala la umasikini kwa wafugaji. Mheshimiwa Waziri alikuja Kiteto. Ukame ule kwa Kiteto peke yake tulipoteza ng'ombe karibu 25,000 na sasa tafiti zinasema; kwa sababu kuna dhana fulani watu wanafikiri wafugaji ni matajiri tu, lakini tafiti zinasema, asilimia 20 ya watu wanaomiliki mifugo; asilimia 20 wanamiliki asilimia 80 ya mifugo iliyopo. Kwa hiyo, hii ni picha tu inayoonesha kwamba *gap* lililopo, na siyo kwa sekta ya mifugo peke yake, hata kilimo. Kwa hiyo, vizuri Mheshimiwa Waziri hebu mlifanyie utafiti ili dhana zinazojengeka kwamba wafugaji ni matajiri ifahamike kwamba siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa kisasa unaozungumzwa kila wakati, kila Mtanzania angependa kufanya kitu chenye tija zaidi, lakini lazima tufahamu kwamba sekta ya mifugo tuna makundi matatu; kuna watu wanaofuga kiasili na kibiashara na ni sehemu ya maisha yao, ambao ndio Watanzania walio wengi, lakini kuna watu wanataka kujifunza biashara ya kufuga ng'ombe na kunenepesaha, na hapa wakiwemo Serikali. Serikali wanafanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotengeneza mikakati lazima tufahamu kwamba haya makundi matatu yapo. Kufanya biashara ya kunenepesha siyo kitu kidogo. *In fact* nimewatembelea wafugaji wawili ambao wanajaribu kufanya ufugaji huu unaoitwa ni wa kisasa. Mmoja mwenye hekta 100 amepiga *fence,* na miundombinu ame-*develop,* na kuweka ng'ombe hawa mnaowaita wa kisasa, ni karibu Shilingi milioni 400 mpaka 500, *investment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamtembelea mfugaji mwingine mdogo sana, ana hekta 20, anajaribu kutengeneza shamba. Hata hiyo, tunayosema ni kidogo ni Shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *at times* tukisema kwamba tufuge kisasa, mjue mkituletea hizo pesa, tuko tayari. *Otherwise* mfahamu kwamba mifugo ni sehemu ya maisha ya wananchi. Wakati mwingine tukisema tufuge kisasa bila kutuwezesha na tukapata nyenzo zinazohitajika, tunafikiri kama hamtufahamu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukamatwa kwa mifugo kwenye maeneo ya hifadhi, imekuwa ni kero kubwa sana. Namshukuru hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kauli aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, hebu fuatilieni vizuri sana kwa sababu kukamatwa kwa mifugo katika maeneo haya, imeanza kuwa kero kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanakamata tu ng'ombe, watu wanakwenda Mahakamani, wanashinda kesi, lakini hawapewi mifigo yao. Nina mwananchi wangu anaitwa Lenina, mpaka leo ni karibu miaka mitatu hajapata haki zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri mwangalie, mzungumze na Waziri wa Maliasili na Utalii, make, mtengeneze. Kama anapenda kukamata ng'ombe zaidi, aambiwe kuna kanuni zilitengenezwa na Wizara ya Mifugo chini ya Sheria inaitwa *The Animal Welfare Empowerment Animals Regulations of 2020.* Kama anaweza ku-*afford* kwenda kuwatunza hao ng'ombe kwenye maeneo ya hifadhi, afanye hivyo, lakini kama hawezi, aachie ng'ombe, awakamate wafugaji. Kwa sababu tunawafanya wafugaji wanakuwa masikini *unnecessarily.* Ni jambo la kukaa na kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mikopo na benki, Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kwamba twende kwenye benki. Kama kuna mradi ambao unafeli ni wa benki. Mfugaji anakwenda anataka mkopo, halafu unamwambia lete *security,* eti lete nyumba. Sasa kwani huyu mfugaji anafanya *real estate?* Kwa nini mifugo isiwe *security? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni mali kama mali nyingine. Kama kuna haja ya kutengeneza *insurance* ama bima kwa ajili ya mifugo ili tupate *security* tufanye hivyo, lakini hatupendi sana. Unakwenda una mifugo wazuri tu, eti mtu anakwambia nenda kalete hati ya nyumba au kalete shamba. Huyu hafanyi *real estate,* wala Halimi. Eeh, mtengeneze *module* ambayo inamfanya mfugaji aweze kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la chanjo. Ilani imezungumza habari ya chanjo hizi za magonjwa 13, lakini wakati mwingine tunahisi kama haiji kwa wakati. Kwa hiyo, lazima Serikali iweke mkakati wa kuleta chanjo hizi kwa wakati ili wafugaji wapate huduma hizi kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, nataka Mheshimiwa Waziri atengeneze wafugaji mabilionea. Wengine wametengeneza mipango mingi. Omba tu Mheshimiwa Rais akupe Shilingi bilioni 27,600,000,000/=, utapeleka katika majimbo yote 184. Karibu Shilingi milioni 150 watapewa vijana Hamsini Hamsini, watakuwa ni vijana 9,200 baada ya miaka miwili, utarudishiwa hizo pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua lazima tuwe *practical.* Hii habari ya kufanya tafiti na kufanya *workshop,* sijui na kufanya ma-*interview* ambayo yanapoteza muda, tafuta hizo hela, ukipeleka hiyo milioni 150 kila jimbo, mtuachie kazi ya ku-*recruit* vijana ambao wanafanya hizi kazi za mifugo. Ukifanya hivyo, baada ya miaka miwili hiyo pesa itarudi, lazima tuwe *practical.* Hatutaki tena mambo ya kusoma mavitabu haya na matafiti. *We have spent time, sixty years down the line,* tunasoma tu ma-*documents.* Tunataka tuwe *practical*. Kwa hiyo, ifike mahali, nakuombea pesa nyingi zaidi, ukipata nadhani itatusaidia sana kutekeleza hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa ahili ya *interest* ya muda, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lucy Sabu. Jiandae Mheshimiwa Charles Miwjage.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii nami niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuleta maendeleo kwa wananchi. Nampongeza zaidi kupitia hizi fedha za mafunzo kwa vijana. Kwa kweli mama anafanya kazi kubwa katika kuhakikisha kwamba anatengeneza vijana matajiri katika sekta hii ya mifugo na uvuvi. Nadhani sote tunatambua kwamba, ni moja kati ya sekta ambayo wananchi wetu wengi wamejiajiri katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara inayoongozwa na mtani wangu, Mheshimiwa Abdallah Ulega, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na mambo mawili ya kuzungumza. Jambo la kwanza ni vijana wanaopatiwa mafunzo ya unenepeshaji mifugo. Naunga mkono kupitia mzungumzaji aliyemaliza kuongea kwamba, ipo haja kubwa sana ya kuongezewa fedha kwenye huu mradi ili uweze kusambaa nchi nzima na uweze kuwanufaisha vijana wengi kupitia mradi huu. Ni mmoja wa miradi ambao una matokeo ya haraka kama ambavyo tumeona, unenepeshaji wa ng'ombe unahitaji miezi mitatu na ndani ya miezi mitatu unaweza kuuza ng'ombe kwa kuhakikisha kwamba tunapata fedha katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Wizara kwamba vijana kama ambavyo tumeona wanahusishwa kwenye jambo hili la huu mradi wa unenepeshaji wa ng'ombe, ipo haja kubwa sana tuweze kuona uwazi wa vijana hawa ambao wanachaguliwa kwenda kwenye haya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye hotuba kwamba tuna vituo nane na viko katika mikoa mitatu; Tanga, Mwanza, na Kagera. Bado vituo hivi ni vichache na

havijasambaa nchi nzima, na vijana wengi wanahamasika katika eneo hili ili waweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema, hadi kufikia Machi, 2023 vijana 238 wako kwenye huu mradi. Bado hii idadi ni ndogo sana, na kwa mwenendo huu, tija yake haiwezi ikaonekana kwa haraka. Hivyo basi, nashauri ushirikishwaji, ama waongeze idadi ya vijana wengi waweze kuwa-*recruit* kwenye huu mradi ili basi tuweze kuona tija yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema kwamba mnufaika atapewa ng'ombe 10 wa kunenepesha na kuwauza kila baada ya miezi mitatu, basi Wizara iongeze fedha za kutosha ili basi vijana wengi waweze kuhusishwa katika mradi huu. Nashauri Waziri wa fedha aongeze fedha katika mradi huu uweze kuinua vipato vya vijana wengi na kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo kwenye ufugaji wa vizimba, tunampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akizungumzia mara kwa mara juu ya mradi huu, mradi ambao utawanufaisha vijana wengi. Nasisitiza zaidi kwamba Wizara iweke mpango mzuri ambao utawasaidia vijana wengi waweze kujiajiri katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo napenda kuzungumzia ni zoezi la utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, ukurasa wa 27, nanukuu: *"Aidha tarehe 3 Novemba, 2022 Serikali ilisitisha zoezi la utambuzi wa mifugo kwa muda ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza hapo awali." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri hajatupatia *way forward,* baada ya haya yote, nini changamoto waliyoiona? Wamejipangaje hususan katika ku-*resume* jambo hili ili liweze kufanukiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba ni takwa la kisheria kuweza kupitia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba jambo hili ni muhimu ili tuweze kuwa na taarifa sahihi ya mifugo katika maeneo yetu. Pia, Serikali iweze kuboresha sera ama kuweza kuwa na idadi kamili ya mifugo tuliyonayo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba, zoezi hili lilikuwa lina changamoto mbalimbali kama malalamiko katika ada, upungufu wa kanuni, usimamizi, na utekelezaji wake. Sasa tungependa kufahamu ama kusikia wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hoja yake tuweze kujua wamejipangaje katika zoezi hili ili kusaidia wafugaji wetu? Ama Serikali yetu kumsaidia mfugaji na kuboresha miundombinu ya wafugaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuhesabu mifugo ni muhimu sana. Baadhi ya wananzengo ama wananchi, wamekuwa wakilitafakari na wakihoji kwamba mwaka 2022 tumetumia zaidi ya Shilingi bilioni 200 katika zoezi la sensa, na zoezi hili lilifanikiwa kwa asilimia 100. Sasa kwa mwananzengo wa kawaida, anajaribu kufikiria kama katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi tumehesabiwa bila kutoa chochote, iweje sasa unakuja kuhesabu mifugo unaanza kuweka mambo ya ada?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali, kwa sababu hii imekuwa ni kero kubwa kwa wafugaji, Serikali iweze kuona ni namna gani itaendesha zoezi hili ili kila mfugaji

aweze kuondokana na changamoto hiyo ya ada mbalimbali ambazo zimekuwa zikitozwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhesabu mifugo ya mwananchi na kuweka ada ni jambo ambalo limekuwa kikwazo sana kwa wananchi na Serikali inatakiwa ije na mpango mzuri ambao utawasaidia wafugaji waweze kutoa ushirikiano mzuri. Kwa sababu, kama zoezi hili litaendeshwa bure, nina imani wafugaji wote; sioni kama kuna mfugaji yeyote ambaye hatatoa ushirikiano kwenye zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasisitiza Serikali iandae utaratibu mzuri, na sidhani kama kuna mfugaji yeyote ambaye hatatoa ushirikiano kwenye zoezi hili kwa sababu, ni zoezi ambalo lina manufaa kwao kuweza kutengenezewa mazingira mazuri katika maeneo yao ya mifugo na suala zima la utoaji wa chanjo, na udhibiti wa magonjwa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda kuzungumzia, naishukuru Wizara kwa kuja na mpango mzuri wa kuzalisha nyasi kwenye mashamba makubwa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri katusomea kwenye hotuba yake. Jambo hili ni zuri sana na litasaidia kuondokana na migogoro kati ya wakulima na wafugaji, kama endapo tutakuwa na maeneo makubwa ambayo nyasi zinazalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufanikisha jambo hili, ipo haja ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, na Wizara ya Kilimo, waone namna gani ambavyo watashirikiana kupitia vijana ambao wanafanya ule mradi wa Jenga Kesho Bora wa *BBT,* ili kuwe na *coordination* nzuri ambayo itasaidia Wizara, vijana hawa kupitia mafunzo wanayoyapata waweze basi kupatiwa na namna gani wanaweza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Ni kengele ya pili.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, halafu Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Kanyasu wajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hii Wizara muhimu, Wizara moja ya sekta za kiuzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma sana randama ya Wizara hii. Nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimesoma maandiko yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema, naunga mkono hoja ya Wizara hii. Nataka kusema, naunga mkono hoja Wizara hii ipite.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika randama, Ukurasa wa 17, ukurasa wa 18 na ukurasa wa 32, mara tatu, Waziri ametamka kwamba, yeye migogoro ya Rutoro na Mwisa ameshaachananayo anasubiri huruma ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, waende wapime, wananchi wa Rutoro na Mwisa waishi kwa amani. Amesema mara tatu. Naunga mkono hoja ya Waziri kwa misingi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaingia karne ya 21, tuliandika Dira ya Taifa. Hayati Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, aliandika

dibaji, nitanukuu sehemu ya dibaji, kwamba, "Tunapokwenda kwenye ile karne ya 21 lazima tuwe na nguvukazi yenye ustadi mkubwa na hulka ya kujituma." Nguvukazi yenye ustadi mkubwa na hulka ya kujituma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeunga mkono bajeti ambayo Waziri anakiri kabisa kwamba idadi ndogo ya Watumishi katika Sekta ya Uvuvi ikilinganishwa na mahitaji ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani alivyosema Mzee Mkapa mmemsikia; mtu ambaye nimemuunga mkono, amekiri kabisa kwamba, rasilimali watu aliyonayo, haimtoshi. Namuunga mkono Mheshimiwa Rais anaposema kwamba, mifugo na uvuvi ni utajiri mkubwa. Nikipata muda nitawaonesha. Kuwa na utajiri siyo hoja, kuchota utajiri ndiyo ngoma ilipo. Hatuna rasilimali ya kuchota rasilimali zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali Wizara hii, nitawaonesha rasilimali zilipo, waongezewe pesa, kwani hizi pesa hazitoshi. Waongezewe pesa kwa ajili ya kutengeneza rasilimali, na zana za kuchota raslimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumze na hili ni kwa Wizara zote; sekta zote za kiuzalishaji. Mnapotuletea bajeti, mnapojinasibu mahali popote, pamoja na kazi nzuri ambazo Wizara hizi zinafanya, kuleta chakula, kutengeneza ajira, malighafi za viwanda, mtueleze *clearly* ni kiasi gani tunapata pesa za kigeni? *In bolded font.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna-export na kupata pesa za kigeni dola bilioni 10 hazifiki, ni tisa na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukraine ana-*export 68 billion dollars;* sisi tunapata nini? Madini tuliwasikia lakini kwa kufichaficha, tunapenda tujue, tuige mfano ule wa Ajenda 10/30. Ajenda 10/30 anakueleza malengo yake atapata kiasi gani kwa dola ambayo na mimi sikubaliani naye, nasema amejiwekea malengo kidogo. Lakini ninapenda hii iwekwe wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kwa kampuni ya maziwa ya Asas. Kazi mliyofanya ujombani Busokelo, Rungwe nzima ni nzuri. Waheshimiwa Wabunge, Kampuni ya Asas inaagiza ng'ombe wa maziwa kutoka Afrika Kusini, ng'ombe mmoja ukimlisha unapata kilo 25, anawakopesha watu wanafuga halafu wamrudishie. Mheshimiwa Waziri, kama unaijua Kampuni ya Asas na tunagombania mwisa, nakuomba mjomba leta *Asas Company Ltd.* tumpe aardhi awagawie wananchi wa kwetu wa Kagera hao ng'ombe na ajenge viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze watu, hawaelewi; hekta 600,000 za *NARCO* nusu yake ziko Kagera. Kwa hiyo, wananchi waliozoea kutumia ardhi ile, imetwaliwa. Sasa niko tayari kufanya kazi nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na wewe nikuombe umweleze Waziri kwamba kwenye mabanda yale wasituoneshe ila waweke na banda la watu kutoa maoni na kubadilishana uzoefu kwa sababu tuna uzoefu tofauti. Tusiende kuangalia, turuhusiwe kutoa maoni yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafanya fujo, nilindie muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017 Tanzania tuliuza nje samaki wenye thamani ya dola milioni 193 kwa takwimu nilizonazo. Na hizi ni takwimu za *World Fish Center.* Rasilimali ya maji tuliyonayo sisi Tanzania siyo wa kuuza kiasi hiki. Mahesabu yanakuonesha wewe kuuza dola milioni 800 inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi ya Morocco ambayo tunawazidi kwa wingi wa maji wanauza samaki duniani *2.5 billion dollars.* Sisi tuna maji mengi kuliko Morocco, ndipo linapokuja suala la rasilimali. Ukiweka shilingi katika sekta hii unapata shilingi 2.5. Serikali muweke shilingi kwenye sekta hii ili tupate pesa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kiburi cha Taifa lolote ni uwezo wa kuuza nje, na imeandikwa hata kwenye Dira ya Taifa, huwezi kujenga uchumi shindani kama huna huo uwezo wa kuuza nje. Kwa hiyo, nilikuwa nawaeleza hiki kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kwenye sekta hii ni kwamba asilimia 97 ya wanaozalisha hawa samaki tunaowazungumza ni wafugaji wadogowadogo, wavuvi wadogowadogo. Kwa hiyo, Serikali mpeleke pesa kule kwa wafugaji hawa wadogowadogo, kwa wavuvi hawa wadogowadogo, ili hao watu sasa watusaidie kujenga uchumi jumuishi. Uvuvi wa samaki utakaoleta watu wengine wakawatoa hawa ndani ya shughuli patakuwa hapakaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa nini tuko hivi; moja wapo ya changamoto za Wizara hii au sekta hii ni uvuvi haramu. Lakini uvuvi haramu siyo suala la Tanzania tu, hoja hapa siyo kwamba tuna uvuvi haramu, hoja ni kuu-*manage,* tunau-*manage* namna gani. Uvuvi haramu duniani, *overfishing,* unasababisha mapungufu ya *83 billion US Dollars;* hizo ni taarifa za *World Bank.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utaona kwamba hii 193 niliyowaambia ya mwaka 2017, tungefanya kazi kwa tija, kwa kuzuia *overfishing* na uvuvi mwingine haramu, tungeweza kuchupa na kwenda kwenye nafasi nzuri. Nilimueleza Mheshimiwa Waziri nikiwa Goziba kwamba nitakuja nimuoneshe nilichokiona Goziba. Uvuvi haramu umezidi mipanga na Wizara hii peke yake haiwezi kuutatua, mnahitaji kupata msaada wa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikaomba aweke banda la maonyesho pale ili nije wasionioneshe, na mimi niwaoneshe nilichokiona Goziba, Bumbire, Kelebe, Makibwa na Nyamburo**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye sekta ya nyama, hesabu zangu za haraka – nisije nikakosa muda – sekta ya nyama kirahisi inaweza kutuingizia dola bilioni tano. Kama kuna mtaalam katika Wizara hii ana mashaka, tukakutane kwenye banda pale nimuoneshe kwa mahesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuwa na ng'ombe milioni 35 halafu ukashindwa kuuza nyama inayofikia bilioni sita kwa mwaka. Hata ungewachinja wale ng'ombe kwa kipindi cha miaka kumi, chukua ng'ombe milioni 35 wagawe namna hiyo, utaona hizo *figures.* Nitakuwa kwenye banda la maonyesho pale, niwekeeni zulia nije niwaeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kufanya nini; mmeizungumzia *NARCO* kwamba itawataka wawekezaji waje na *business plan;* hakuna. Ninyi ndio muwape *NARCO* masharti watakayoyafuata, wewe ndio uandae *business plan.* Ndiyo maana hata watu wa *estate* mtu anajenga nyumba, iwe hoteli, iwe hospitali au klabu, watu waende kucheza. Huwezi kufanya klabu ukaigeuza kwamba ni hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo *NARCO* ianzishe *business plan* ili watu waje wafanye nini. Na hiyo *business plan* iwahusu hawa waliopewa vitalu na wale watakaokuja. Siyo unajenga kitalu cha kufuga ng'ombe mtu analeta ng'ombe analingana na mbuzi; haiwezekani. Ufugaji wa kuweza kufikia malengo niliyowaeleza inatokana na malisho, mbegu utakayoleta na utunzaji wake, ili tuweze kufuga nyama tupate nyama inayoweza kufikia hizo dola bilioni tano ambazo nakueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, umezungumza Mheshimiwa Waziri nakuunga mkono, watu sasa wanataka nyama inayozalishwa Tanzania. Na jambo la faraja ni kwamba katika nyama wanayohitaji ni wanyama wanaofugwa kirahisi; anaongoza mbuzi, anakuja kondoo, ng'ombe ni wa tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kote nilikokwenda kujifunza – siwaambii tena mambo ya Uganda – hapahapa Tanzania, hapahapa Iringa, kuna Watanzania wamefanya maajabu, Asas anawaongoza na wengine wanafuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema mwanzo na awali kwamba naunga mkono hoja, naendelea kuunga mkono hoja. Nimemuona Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ananiangalia, na yule wa Ofisi ya Waziri Mkuu ananiangalia; naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Kitandula, jiandae Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye imempendeza ameturuzuku uhai kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kwenye Wizara hii ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu na ni muhimu sana kipekee kwa sisi watu wa Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali, tulikuwa na kilio cha muda mrefu cha kutokuwa na mnada wa uhakika pale kwenye *border* yetu ya Horohoro. Mnada ule umekamilika, tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na kukamilika kwa mnada ule na wananchi wale kufurahia jambo lile, lakini mnada ule umekuwa kero kwa sababu tangu kukamilika kwa mradi ule mwanzoni mwa mwaka huu mpaka leo mnada ule haujafunguliwa. Mheshimiwa Ulega, hili unaliweza, nakuomba sana. Tukimaliza tu Wizara yako, *assignment* ya kwanza nakuomba ndugu yangu twende tukafungue mnada ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi yule anakataa kukabidhi kwa sababu anatudai karibu milioni 100. Hizi tuna uwezo nazo, twendeni tukafungue mnada ule. Tunapoteza fursa ya mapato kwa sababu hali ya upande wa pili kwa wenzetu Kenya ni mbaya kwenye minada yao. Kwa hiyo, tukifungua mnada ule tumepiga bao. Twende tukafanye jambo hili kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tuliomba majosho kumi tukapata mawili, si haba, tunaishukuru Serikali tulipata jumla ya milioni 46 tukapeleka Kibewani na kule Mkota. Tunaomba yale yaliyobakia mtufikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile pale Duga tuna josho ambalo tulilijenga tangu mwaka 1972; limechakaa. Nakuomba sana josho lile ni muhimu lifanyiwe kazi kwa haraka hususan kwa hili ambalo mmelifanya jambo kubwa la

kuleta mnada mkubwa pale Horohoro. Tunaiomba sana Serikali iangalie eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali na sisi ni wanufaika kwenye maeneo yale ya kupata boti. Pale Zingibari ndugu zangu wamepata maboti, ndugu zangu wa Mwaboza wamepata boti na tunaye mvuvi mmoja mwingine binafsi na yeye amepata boti; tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mmekuwa mkitusaidia kutoa mbegu kwa wakulima wetu wa mwani, tunashukuru sana. Lakini tunahitaji kuongeza jitihada. Mwani unazalishwa kwa wingi lakini uongezaji wa thamani ni mtihani. Tunaomba sana Serikali mliangalie eneo hili; kuongeza thamani ya mwani wetu ili wananchi wale waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu, Mheshimiwa Ulega, mlituahidi kwamba mtatujengea kituo cha kutotoa vifaranga. Ahadi hii kama umeisahau vile; nakuomba ikumbuke ahadi hii. Tunashukuru mnatuletea Mradi wa Bahari Mali kwa kushirikiana na wenzetu wa *IUCN* ambapo vikundi vyetu vitatu vitakuwa sehemu ya mradi ule; tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba – ndugu yangu Waziri unajua, ukipeleka jambo zuri kama hili kwa watu wenye uhitaji ambao ni wengi, jambo lile badala ya kuwa neema linageuka kuwa kero. Ninawasihi sana, sambamba na mradi huu, Serikali angalieni maarifa mengine ya kuongeza ukubwa wa mradi huu ili wananchi wetu wa Ukanda wa Pwani waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nimeisikia bajeti yako, eneo moja limenisikitisha; tumeingiza lita milioni 11.6 za maziwa zenye thamani ya bilioni 22. Hizi ni fedha

ambazo tungeweza kuwasaidia wananchi wetu tukazalisha maziwa kwa wingi ndani ya nchi tukaokoa fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesafirisha maziwa kwenda nje lita 278,000. Kwa hiyo, ukiangalia uwiano tumeingiza zaidi kuliko tulivyouza nje. Tuliangalie vizuri eneo hili, hatuna sababu ya kuagiza maziwa nje, tuna uwezo wa kuzalisha maziwa ndani ya nchi yetu tukajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia makusanyo ya Wizara, na Kamati imefanya kazi nzuri, imetuonesha; hali hairidhishi. Tulikusudia kukusanya bilioni 80, tumekusanya bilioni 30; *only 37 percent;* hii haiwezi kuwa sawa. Tuongeze maarifa zaidi tukusanye zaidi, tuna uwezo wa kufanya hivyo. Na hasa kwenye sekta ya uvuvi, tulikusudia kukusanya bilioni 40, tumekusanya bilioni 13; *only 33 percent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage amesema pale; kwenye eneo hili la uvuvi na ufugaji wa samaki hatupaswi kuwa na kiwango hiki. Yaani mchango wa sekta ya uvuvi kuwa asilimia moja haiwezi kuwa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sekta ambayo ulimwenguni uingizaji wake ni mkubwa sana, hatujafanya vizuri, tuongeze bidii kwenye eneo la ufugaji wa samaki ili tuondoe umaskini kwa wananchi wetu, tujihakikishie usalama wa chakula na lishe katika nchi yetu. Sekta hii ina uwezo wa kututoa. Hatuwezi kusifiwa kuwa nchi ya maziwa makuu, hatuwezi kusifiwa kwamba ni nchi yenye ukanda mkubwa wa bahari lakini ufugaji wa samaki haueleweki; hii haiwezi kuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu, Mheshimiwa Ulega na timu yako uliyonayo sasa, najua tukiamua kuweka

mkazo kwenye eneo la ufugaji wa samaki tunaweza kupiga bao. Na hiki kigugumizi cha ufugaji wa samaki kwenye Ukanda wa Pwani kinatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ulega, wewe mtu wa pwani, unajua umaskini wetu watu wa pwani wakati tuna rasilimali ya bahari. Twendeni tukafanye kazi ya kuwaondolea wananchi umaskini kupitia ufugaji wa samaki kwenye eneo la ukanda wa bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru; ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Kanyasu, wajiandae Mheshimiwa Regina na Mheshimiwa Boniphace.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, naomba nianze kwanza kwa kusema ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwa kweli pia maandiko mbalimbali ambayo Mheshimiwa Waziri amewasilisha na nimemsikiliza vizuri kwenye hotuba yake ambapo kuna wakati alikuwa anaacha kusoma anatuelezea anachokifikiria kufanyika. Ninampongeza kwa maoni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba uvuvi mpaka leo unachangia pato la Taifa kwa asilimia 1.8. Ukitazama namna ambavyo nchi yetu imebarikiwa, namna ambavyo tumezungukwa na maji karibu nchi nzima ukianzia Ziwa Victoria, ukaenda Tanganyika, ukaenda Nyasa, ukaenda baharini na vibwawa vidogovidogo vilivyopo katikati ya nchi, ungetamani kuona

mchango wa sekta ya uvuvi unafika asilimia 10 kwenye Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na tumefeli wapi; amezungumza hapa mzungumzaji aliyetangulia kwamba sisi tungeweza kuwa tunaongoza katika mauzo lakini pia tungeweza kutawala soko la Maziwa Makuu. Jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Waziri nataka kukuhakikishia kwamba tumefeli; kwanza, tumekuwa na usimamizi mbaya wa rasilimali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sasa hivi tunazungumzia kushamiri kwa uvuvi haramu; miaka michache nyuma tulifaidika na takwimu za mauzo makubwa nje – amesema Mheshimiwa Mwijage – tukafaidika na takwimu za ongezeko dogo la samaki Ziwa Victoria, kwa sababu tulitumia nguvu kubwa ya operesheni kwenye kufikisha ujumbe wa namna ya kutunza maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa matokeo ya operesheni ni yapi. Kwanza, tulipata ongezeko la muda la mauzo ya samaki nje, tukaongeza mapato kutokana na faini kwa sababu tulikuwa tunapiga sana faini. Sasa matokeo yake ni kwamba wavuvi wakubwa wote waliokuwa Ziwa Victoria wakaacha kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na wanapoacha kufanya hiyo kazi kutokana na kufilisika – na kwa kweli walifilisiwa na Serikali, maana yake ni kwamba wanaokuja ni wavuvi wadogowadogo ambao hawana uwezo wa ku-*access* gharama kubwa ya zana za uvuvi na lazima watavua kwa uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatuwezi kuja leo tunashangaa kupungua kwa samaki, *genesis* yake tuliitoa

huko. Tulipaswa kuja na programu ambayo itadumu ya kudhibiti uvuvi haramu na kuhakikisha kwamba tunalinda maliasili katika maziwa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaja na zimamoto ya operesheni ambayo ninafikiri Mheshimiwa Waziri usipozingatia ndio utakuwa ushauri wako utakaopewa na wataalamu, na operesheni iliwafaidisha zaidi watu wako wa chini ambao walitumia operesheni hiyo kuonea watu na matokeo yake watu wote wakaona uvuvi siyo kazi ya mtu mwenye akili timamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Mwijage amezungumza habari ya ongezeko la *illegal fishing,* amezungumzia ongezeko la *bycatch*. *Bycatch* kwa nini ni nyingi; ni nyingi kwa sababu watu wa *BMU* hawafanyi kazi huko chini tulikuwa na *BMU* zamani na kazi yao kubwa ilikuwa ni kuhakikisha wanamlinda mvuvi wao wenyewe, Wavuvi wenyewe wanalindana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, hatuna wataalam. Ukiangalia ajira za Serikali zote zinazotoka ni kama vile uvuvi tume u-*abandon,* yaani kama si jambo muhimu. Watu wanasoma kwenye vyuo hawaajiriwi. Unatembea mialo kumi afisa uvuvi mmoja, halafu unategemea kudhibiti Uvuvi haramu, unaudhibiti vipi? Haiwezekani; uvuvi haramu unatoka wapi; ni kutokana na dhana kupanda, wasimamizi hawapo, na ukianzisha *operation* unakwenda kuonea watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka kushauri; uwepo wa, kuzungungukwa na maji katika nchi yetu bado haijawa baraka, bado sisi tunaona kama vile ni laana. Tunachotaka ukifanye sasa hivi, hakikisha tunapata dhana za uvuvi kwanza kwa bei nafuu, lakini watu wako walioko huko chini waimarishe zaidi kwenye kutoa elimu kuliko kwenye kufanya

*operation* kwa sababu mtu akipata elimu ataambukiza kizazi chake na kizazi kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, na jambo lingine ni lazima *to control* hizi *breeding areas*. Maeneo yote ambayo zamani yalikuwa ni mazalia ya samaki sasa hivi yamevamiwa. Hii ni kwa sababu ile *operation* baada ya *operation* namna tena mtu anafanya kazi kule ziwani. Mimi nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri ukilisimamia hili samaki watarudi ziwa Victoria, lakini yako mambo ambayo lazima tufanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani sasa hivi hawategemei tu mazalia ya samaki ya *natural* kutokana na uharibifu wa mazingira, ndiyo maana unaona watu wana-*invest* kwenye *cages* kwenye uvuvi wa vizimba, ufugaji wa vizimba. Lile Ziwa Victoria na ukubwa wake ukiweka vizimbaa kila kona hatuwezi kuwa na kilio cha samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la samaki liko *obvious* Tanzania kuna soko la samaki na nje ya nchi kuna soko la samaki. Hatuwezi kuendelea kutegemea kwamba wale wanaozaliwa mle kwa sababu ya asili ndio tuendelee kuwategemee kuuza nje haitawezekana. Ukienda nchi zote ambazo ni *leading export* wa samaki wanatumia vizimba, kwa hiyo weka fedha nyingi hapo. Shida tuliyonayo Tanzania sasa hivi vizimba ni bei ghali sana, chakula cha kuku ni bei ghali sana; lakini kuna urasimu mkubwa kwenye kufikia malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu ya muda na kwa sababu sitaki kuacha kuzungumza habari ya mifugo, nataka nikushauri hapo kwamba lazima utakapoamua kulisimamia jambo hili huko chini watu wako miiko ambayo wanapelekewa; lazima tuongeze idadi ya *staff* lakini watu walitumia vibaya sana madaraka yao na

matokeo yake tukawa na mafanikio ya muda yaliyopelekea watu wengi kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusu suala la mifugo. Nimeangalia takwimu zako za mapato ya mifugo, kwa mtu akikusikiliza ambaye haijui Tanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango mzuri, ya pili hiyo. Mheshimiwa Regina, jiandae Mheshimiwa Boniface.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante ili na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameendelea kuweka mikakati katika Wizara hii na kuhakikisha suala zima la mifugo katika nchi hii linakuwa endelevu na lenye tija. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa namna walivyoanza vizuri kufanya kazi. Pia nipongeze kwa ripoti nzuri hii ambayo imewasilishwa katika Bunge hili, iliyojaa mikakati na namna ya kwenda kumkomboa hasa mfugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu, wafugaji, hasa wafugaji wa asili, wanategemea mifugo kwa kila kitu. Wanategemea mifugo katika mahitaji ya kujisomesha na kwa ajili ya chakula; na kwa kila kitu mfugaji wa asili anategemea mifugo ili aweze kujikwamua kiuchumi. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba

tunapoongelea mifugo maana yake tunaongelea uchumi, sasa ni uchumi upi tunao uzungumzia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwa na chanagamoto nyingi sana. Jambo ambalo linawakwaza wafugaji wasione suala zima la ufugaji kama linaleta tija na kuweza kujikwamua kiuchumi ni kwa sababu wafugaji wa nchi hii wamekuwa ni watu ambao ni wakukimbizana hapa na pale wakiwa ni watu waliosahaulika, kwa sababu wafugaji wanakuwa ni kama wakimbizi katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu kumekuwa na migogoro mingi sana baina ya wafugaji pamoja na hifadhi zetu. Lakini tunashukuru kwa sababu migogoro mingi kati ya wafugaji na wakulima sasa imepungua kwa asilimia kubwa. Hata hivyo haya yote yanatokana na sababu kwamba Serikali haijaweka mkazo katika kuhakikisha maeneo yote ya malisho katika halmashauri zetu yametengwa. Haya ninayasema kwa sababu mamlaka zetu hazijasimamia kuhakikisha kila halmashauri kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya malisho. Hii imesababisha migogoro kuendelea kila siku katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema haya kwa mifano hai. Tuna mifano ya wafugaji ambao wamekuwa wakikamatwa mara kwa mara na mifugo yao ikiendelea kutaifishwa na kupigwa minada. Baada ya kutaifishwa na kupigwa minada wafugaji wanabaki wakiwa maskini, kitu ambacho kinasababisha wale wafugaji waone kwamba kazi ya ufugaji si kazi ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu sasa kwa Serikali, niombe sasa mamlaka husika wakasimamie maazimio ya mikutano ilifanyika baina ya wadau wa ufugaji

pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye aliongoza ule mkutano uliohudhuriwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya; kwamba kila Wilaya sasa iende ikatenge maeneo ya malisho ili kuondoa migogoro. Migogoro hii inasababisha mifugo mingine kukatwa, kujeruhiwa na kufa. Migogoro hii imesababisha hata wafugaji wengi kupoteza maisha na wengine kuwa walemavu. Kwa hiyo niombe sana mamlaka hizi zikasimamie ili walau wafugaji waone wana haki ya kufuga na kujipatia kipato katika familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nipende kugusia suala zima la utambuzi, usajili na ufatiliaji. Tusiposimamia suala hili katika nchi yetu tuna uhakikia hata masoko ya nje hatutaenda kufanya vizuri. Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba utaratibu wa kuweka hereni katika mifugo ulisitishwa; lakini sasa, mkakati wa Serikali ni nini? Tunaendaje kutambua mifugo yetu? Tusipofanya hivi ni lazima sisi hatutaingia kwenye soko la ushindani na hatma yake hatutaweza kuingiza kipato katika nchi hii na masoko yetu hayatakubaliwa. Tukiweza kuwatambua wanyama wetu itatusaidia kuweka mkakati na kuwatambua, kwa mfano, suala la usalama kwa wanyama wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wanyama kuna nchi zingine bila kuwa na hereni hawawezi kupokea mnyama, hawakubaliki kwa sababu hawatambuliki na hawana uthibitisho. Kwa hiyo niombe Serikali sasa ije na mpango ambao hautakuwa na maumivu kwa wafugaji ili suala hili la kuweka alama na kuwatambua wanyama wetu iende kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, pamoja na kuwa na mifugo mingi katika nchi yetu, lakini kama nchi tumeshindwa kupata faida kubwa kutokana na mifugo. Hii ni kwa sababu sisi hatujawekeza lakini tumekuwa na ushuru na

utitiri mwingi wa tozo katika nchi yetu ambayo inafanya wafanyabiashara wengi wa nyama kushindwa kufanya biashara ya nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano; ukiangalia tozo zilizopo katika nchi yetu na nchi jirani ya Kenya, Tanzania kuna tozo zaidi ya kumi lakini wenzetu wa Kenya wenyewe wana tozo tatu. Hii inasababisha na kurahisisha sasa hata mfanyabiashara wa nyama wa Tanzania kuona ugumu kufanya biashara Tanzania na kukimbia nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ghrama zetu pia ziko juu sana. Kwa mfano suala la kuchinja mbuzi; Tanzania tunachinja mbuzi kwa shilingi 6,500 lakini Kenya wao wanachinja kwa 150 ambayo ni sawa na shilingi 2,700 kwa bei ya Tanzania. Hili suala naomba Wizara iliangalie ili kurahisisha wale wafanyabiashara wanaosafirisha nyama waweze kufanya biashara hii zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna tozo ambazo hata hazina umuhimu sana. Kwa mfano *autonics certificate* kuna hizi za *meat crown* ambazo zingeweza kufanywa kupitia zile tozo za uchinjaji ili kumrahisishia mfanya biashara aweze kufanya biashara bila kupata maumivu yoyote. Pia suala pia la usafirishaji limekuwa la gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie namna Wizara inavyoweza kufanya ili kuweza kuinyanyua hii sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, kwanza kuhusu minada. Minada yetu haimpi faida mfugaji, anayepata faida ni yule anayeuza nyama. Mfugaji anapokwenda mnadani kuuza nyama hawatumii kipimo chochote isipokuwa ni

makubaliano tu, kwamba huyu ng'ombe anafaa kuuzwa laki tano au milioni; lakini yule anayeuza nyama lazima aweke kwenye kilo. Kwa hiyo moja kwa moja ukiangalia mfugaji hapati faida, anayepata faida ni yule anayeuza nyama. Sasa, niiombe Serikali iweke mizani katika minada yetu ili ng'ombe wapimwe kilo wakati wa mauzo, walau hata sasa na mfugaji anaweza akapata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni ombi, hasa katika Mkoa wetu wa Manyara. Kwamba, katika miaka miwili mitatu tumekumbwa sana na suala la ukame. Niiombe Serikali iwachimbie wafugaji mabwawa ya kutosha ili inapofika msimu ule wa ukame wanyama waweze kupata maji ya kutosha na waweze kuhimiri...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kwa mchango wako mzuri, kengele ya pili. Mheshimiwa Getere. Kama muda utabaki ataingia Mheshimiwa Tauhida.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa heshima na mimi kuchangia Wizara ya Mifugo. Kwanza naishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi, namshukuru Mheshimiwa Ulega, bajeti yake kwakweli ameisoma kwa uchungu sana, na ameonesha kwamba ni kijana ambaye amedhamiria kufanya kazi kubwa, nakushukuru sana. Na mimi nadhani Mama Samia hatua anayoenda nayo kuna watu anawaona moyo wao unataka nini. Nadhani alikuona moyo wako unataka kuimarisha na kuwakomboa wafugaji kwenye mateso waliyonayo sasa hivi na watu wa uvuvi, nadhani unafanya kazi vizuri. Kwa maana hiyo moja kwa moja naunga mkono hoja yako kabla sijaendelea, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kufanya kazi kubwa ya kuwaamini Mawaziri wake. Mimi nadhani katika uongozi huu kama Waziri hata *perform* huyo atakuwa na shida yake binafsi. Mheshimiwa Rais anawaamini sana, anawapa ninyi mumpelekee mawazo. Kwa hiyo Mheshimiwa Ulega mpelekee mawazo ya wafugaji; kwamba kama tuna kopa kwa ajili ya mambo mengi hakuna eneo la kukopea kama kukopa kwa ajili ya kuimarisha mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Rais anaweza kukopa popote, kwa sababu ukichukua wafugaji wote, mali zote za wafugaji ng'ombe, mbuzi na kila kitu ulichotaja hapa ni trioni 25, na ukichukua samaki peke yake ni trioni 846. Sasa, trioni zote hizo manashindwaje kukopa kuimarisha, tuna shida gani ya kukopa ili kuimarisha trioni za fedha? Sasa unapewa milioni 200 ndugu yangu, sijui bilioni mbili, sijui bilioni tatu inatosha wapi? Haitoshi. Kama nchi inaweza kukopa ikope kwa ajili ya kuimarisha ufugaji na uvuvi. Mimi nadhani hilo ni jambo zuri sana la kufanya katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda mbali nataka nizungumze jambo moja tu. Mheshimiwa Waziri umesema habari ya kupeleka mizani kwenye minada; na umezungumza kwa uchungu sana nimeiona moyoni mwako. Nataka nikupe tahadhari, tena tahadhari kubwa. Usipokuwa makini ukipeleka hiyo mizani bila kuwapa elimu wafugaji utakuta minada iko mitupu, na hasa minada ya vijijini. Mauzo ya ng'ombe hayategemei mizani peke yake. Nataka nikupe mfano; mimi nikiwa na maksai kumi inawezekana maksai sita ndizo zenye uwezo wa kununua milioni moja, maksai nyingine zote zinakuwa chini ya milioni moja, labda inakuwa laki nane au laki saba. Mimi nikikutana na mfugaji anayenunua ng'ombe yule mnunuzi namuuzia maksai kumi zote kwa milioni moja, zile zingine zote zinabebwa na maksai sita. Kwa

hiyo ukienda kwa mizani inawezekana mtu asiuze ng'ombe zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, achunge sana hili neno; kama anakwenda huko afanye utafiti kwanza kabla hajapeleka mizani vinginevyo atakwenda kuua minada; watu watauzia majumbani hakuna mtu atakayepeleka ng'ombe mnadani. Lazima twende tuwaelimisha wafugaji juu ya hasara anayoweza kuipata kutokana na hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amezungumzia habari ya mashamba darasa. Mashamba darasa maana yake ni kwamba uwe na maafisa ugani wa kutosha. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeseme 2025 tuwe na afisa ugani kwa kila kijiji. Tuna vijiji 12,319, unao? Unao wa mashamba darasa? Asilimia 35 ya maafisa ugani ndio walioko vijijini sasa hivi; unao hao wa mashamba darasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani imesema tupeleke majosho kwa kila kijiji. Tuna vijiji 12,319. Kwenye jimbo langu katika vijiji 35 ambavyo vina wafugaji wa kutosha ni vijiji 10 tu ndivyo vina majosho, na majosho yenyewe mnaenda kufanya nyie watu wa Wizara. Siku hizi mna mtindo mnapeleka milioni 22 mnaenda kuchimba majosho. Unachimba josho la milioni 22 halina kisima, halina kibanio halafu unaliacha hapo, halafu fedha yenyewe inatoka Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemuona hapo Mheshimiwa Waziri, aende akafumue huo mtindo. kwa nini fedha ya kijijini ikae Wizarani? Walaji gani wanakaa Wizarani na fedha haiji kiasi kwamba josho linajengwa kwa miaka miwili hadi miaka mitatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kata ya Salama kuna josho limebomoka, naomba aende alitengeneze. Kwenye Kijiji cha Salakwa hamna josho, kwenye Kijiji cha Maliwanda hamna josho, vijiji takriban 20 havina josho. Nitamletea aweze kuangalia kwamba kwanini inafanyika hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzungumze mashamba ya *NARCO;* sasa najiuliza, *NARCO* ni biashara au ni nini? Mashamba ya Serikali ya *NARCO* na mashamba mengine ya Serikali mliyonayo ni ya biashara au ni ya watu? Ni ya watu au ni ya Serikali au? Mimi sielewi sasa Kwa sababu kama mna ng'ombe, mashamba yenye kutunza ng'ombe milioni 42 leo mnatunza ng'ombe 19,000. Sasa mimi nashindwa kuelewa haya mashamba ni ya nani? Kila mtu shamba lake, kila meneja shamba lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri, kama anaweza kama anaitendea haki hii Wizara aanzishe mamlaka ya wafugaji. Mimi nashindwa kuelewa, hivi leo nchi yetu inashindwa kuwa na mamlaka ya Samaki na ng'ombe ilhali tuna Mamlaka ya *TAWA*, tuna *TARURA*, tuna *RUWASA* na tuna *TFS*. Mna mali ya kutosha kutoka kwa wafugaji lakini mnashindwa kuweka mamlaka, kwa sababu gani? Sijawahi kuona nchi ina mamilioni ya fedha kwenye maeneo kama hii…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi uko salama hapo? *(Kicheko)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko salama kama ambavyo Singo yuko salama.

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru, nashukuru. *(Kicheko)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipunguza sauti sawa. Kwa hiyo naomba nchi yetu itengeneze mamlaka ya wafugaji ili iwalinde wafugaji, wafugaji wanashida. Waheshimiwa Wabunge wa *CCM* na wale wa *NEC* mliomo humu ndani, katika eneo ambalo hatujafanya vizuri Tanzania ni la wafugaji. Wafugaji hatuwafanyii vizuri, hatuwatendei vizuri kabisa. Tunaomba hii Wizara mama aitendee vizuri, tunamuomba sana Mheshimiwa Rais na Halmashauri Kuu ya CCM Taifa. Mimi nimekuja na kitabu hapa, ninacho hapa. Katika eneo la wafugaji hatujafanya vizuri; tuna ilani hapa hatujafanya vizuri katika eneo la wafugaji. Tuwalinde wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja hapa na lile suala la herein; sasa katika ilani inasema hivi, tuwatambue wafugaji wenyewe, mifugo yao na wafugaji yenyewe. Sisi hereni tunawekea ng'ombe tu mfugaji hatujui tunamwekea nini, au na yeye tuna mwekea hereni? Sasa unawezaje kumwekea herein, *is not sustainability*. Unawekaje hereni kwenye mfugo, uweke leo kesho usijue unaweka nini? Ndama anazaliwa leo hakuna hereni. Tunaanzisha vitu ambavyo havina maana. Hata kama tungeuza hereni kwa bei nafuu lakini *where is sustainability*? Iko wapi sasa? Leo mtu anazalisha ng'ombe unampa hereni moja kesho kutwa anauwezo gani wa kuangalia?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa, ni wapi taarifa. Haya Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Anazungumzia suala la heleni hawa ng'ombe wako madume na majike, sasa heleni wanatakiwa wavikwe. Je, watavishwa madume peke yake au na majike? Kwa sababu wakivishwa majike…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Getere.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** …akivishwa dume inakuwa ni hatari kama atavaa heleni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE**: Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa heleni sio mbaya, ni mzuri kwa maeneo yaliyoandaliwa, ni mzuri kwenye ranchi ni mzuri kwa maeneo yaliyoandaliwa siyo vijijini. Mtu hana simu hana nini eti unamlazimisha kununua heleni halafu anaiona ng'ombe wake…

**MBUNGE FULANI:** Taarifa, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa mnamchukulia muda wake, endelea Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili jambo la hereni nalo tuliwekee utaratibu mzuri ili tuweze kwenda nalo.

Mheshimiwa Waziri umezungumza habari ya mikopo ya wafugaji; ni kweli benki ya NMB inakopesha wafugaji kwa asilimia tisa, ni kweli, lakini masharti ya kupata mkopo eh! kazi ipo; kupata mkopo kazi ipo. Ni kweli benki ya NMB inafanya

kazi nzuri, hata kwenye jimbo langu inafanya kzi nzuri sana ya kukopesha mikopo lakini nani anawasimamia wafugaji wapate mikopo. Kwanza unapewa masharti uwe na *clearance,* uwe sijui na vitu gani. Unatumia kama laki tano laki sita halafu unaomba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, ahsante kwa mchango mzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa kuna wageni wa Mheshimiwa Ulega, Waziri wa Mifugo, wamekuja tena ambao ni; Chama cha Wafugaji kutoka Tanzania, Chama cha Wavuvi, ndugu Blody Masingisa, Wadau wa Viwanda, Wakurugenzi wa Viwanda vya Chanjo, Kikundi cha Wafugaji na Wadau mbalimbali ambo wamekuja karibuni Dodoma.

Wageni 23 wa Mheshimiwa Dkt. Ritha Kabati ambao ni Kwaya ya *Bible Study* kutoka jijini Dodoma wakiongozwa na kiongozi wao Reverent George Otieno.

Wageni 32 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wana maombi kutoka Jijini Dodoma.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Kamani ambao ni ndugu zake kutoka jijini Mwanza.

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, walimu watatu na wanafunzi 120 wa shule ya Dodoma Sekondari ya Jijini Dodoma, karibuni.

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa wadau wa Wizara ya Mifugo

na Uvuvi kupitia dawati la sekta binafsi la Wizara wako katika viwanja vya Bunge katika eneo tunalofanya sherehe za Bunge kwa ajili ya kuonesha huduma za bidhaa wanazozizalisha pamoja na teknolojia bunifu mbalimbali zinazolenga kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya mifugo na uvuvi. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mheshimiwa Edwin Swalle na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile.

Nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu tunaanza na Mheshimiwa Tauhida Gallos, Mheshimiwa Miraji Mtaturu na Mheshimiwa Edwin Swalle wajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu wake. Niwapongeze kwa muda mfupi Mheshimiwa Waziri na mabadiliko ambayo tunayaona tukipitia Kamati yetu ambayo yanakwenda kutokea ndani ya Wizara ya Uvuvi. Vile vile nichukue nafasi hii nimshukuru na kumpongeza kwa kumwalika Waziri kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limetupa moyo hususani kwa sisi tunaotoka Zanzibar. Mheshimiwa Waziri nimpongeze amekuwa Waziri wa mfano kwenye suala hili. Wanapoalikana kwenye vikao kama hivi, wanajenga umoja na kazi kuifanya iwe ya pamoja. Hata hivyo, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amealikwa na yeye yupo ajifunze kupitia hili. Sio vibaya, sio kosa, sio dhambi kusema kwamba kuna baadhi ya Mawaziri ambao shughuli zetu zinaingiliana kuweza kuwaalika ndani ya Baraza la Wawakilishi. Huu kwa Mheshimiwa Waziri umekuwa mfano, naamini wengine watasoma kutoka kwake na Mawaziri wengine watasoma kutoka kwake. Hili liwe endelevu kwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii zaidi kuishauri Wizara, kwa muda huu mambo makubwa ambayo nimeyaona ni ya kushauri, kwa sababu Waziri kwa muda mfupi ambao amekabidhiwa Wizara, sisi tukiwa kama Wajumbe wa Kamati tumeanza kuona mabadiliko na mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hakupewa Wizara hii kwa bahati mbaya. Tunatamani atimize kiu ya Watanzania kwenye Wizara hii. Wizara yake pia imebeba sera za vijana, kiu za vijana ni ajira, kuondokana na matatizo ya ajira. Wizara hii ina majibu tosha kwenye suala la ajira. Uvuvi ni ajira, ufugaji ni ajira tena tuchukue fursa hii na

nimshauri Mheshimiwa Waziri, atumie fursa kubwa kuwaonesha vijana kuna nini ndani ya ufugaji na kuna nini ndani ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Watanzania hawaelewi thamani ya kufuga ni nini? Mtu yeyote ambaye ni mbaya anamtazama mfanyabiashara anaekwenda kufanya biashara, jioni anamfikiria kakusanya shilingi ngapi? Mtu mbaya ndipo anapoelekea au jambazi, lakini Tanzania hii hii tuna wafugaji asubuhi mpaka jioni anatembea na mabilioni ya fedha anaongozana nayo. Watanzania au vijana wa Tanzania hawafahamu kama almasi, lulu na ule ufugaji pia ni almasi lulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri achukue muda huu awaelimishe vijana wa Tanzania wafunguke. Mtu akisikia suala la ufugaji, akisikia suala la uvuvi anadhani kwamba, watu wa aina fulani au tabaka la aina fulani ndio wanaohusika na kuvua, lakini pia wanahusika na suala la ufugaji. Haipo hivyo, uvuvi ni utajiri, lulu inakaa baharini, sawa na mchimba madini anapokwenda kutafuta madini ya kuchimba. Lulu iko kwenye bahari, samaki ni lulu yetu Watanzania, ufugaji ni lulu yetu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunazungumza madini, lakini na haya kwetu ni madini na yanaweza pia kuwavusha Watanzania. Tanzania kila siku tukiamka asubuhi vijana tatizo kubwa ni ajira, ajira, ajira. Tumejielekeza ili uonekane unafanya kazi na umeajiriwa ufanye kazi ofisini, Wanadhani kwamba ufugaji sio sehemu ya ajira. Ufugaji una majibu ya ajira kwa vijana. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, woneshe dira kwa vijana, umri wao unatosha kutufungulia njia Watanzania, umri wao unatosha kuwaonesha vijana wenzenu wa Tanzania ufugaji una fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mtanzania mfugaji anamiliki mifugo anakwambia mifugo 10,000, mimi Mzanzibari nashangaa hee! Ng'ombe 10,000 tena! Ng'ombe 10,000 mpigie mahesabu ana mamilioni mangapi ameyaweka nyumbani? Namaanisha nini? Namaanisha hata mfugaji anahitaji kupewa elimu. Anahitaji kuelimishwa ili mifugo yake iwe mafunzo kwa wengine. Maana kama atauza kwa faida na kuonesha faida yake kwa Watanzania vijana wengi watashawishika kuingia kwenye suala la mifugo, lakini vile vile watauona umuhimu wa kuvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumwambia Mheshimiwa Waziri, vijana kiu yao yote ndani ya Tanzania, yote tunayoyafanya tisa, kumi wanataka suala la ajira. Tuwaoneshe ajira ya Watanzania iko hapa. Kaka yangu Waziri ni msikivu, Naibu Waziri wake ni msikivu ndio maana wametumia mezi michache kuanza kuleta chachu ya mabadiliko ndani ya Wizara. Siri ni moja tu, kama wataendelea hivyo watatuvusha na watampa matumaini aliyewateua. Usikivu wa Waziri ndio unaomfanya Waziri aweze kuwavusha watu salama. Sikiliza maoni ya watu ingawa sio maoni yote unaweza kuyakubali, lakini kwa sehemu usikivu wa Waziri na akichukua ushauri wa Kamati atafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshauri Waziri, tutumie muda kwanza kuwaelimisha wafugaji wetu juu ya suala la chanjo. Mambo mengi ukiyaona Tanzania yanagoma tatizo lake ni Mtanzania kutopewa elimu. Ukimwelimisha vya kutosha, ukampa fursa akuulize maswali umjibu aridhike, Mtanzania hana shida. Hivi mfugaji gani utakaemwambia ng'ombe hawa, mbuzi hawa, kondoo wakichanjwa tunaboresha nyama yake tunapata soko

kubwa la nje, Mtanzania gani atakataa? Mfugaji gani atakataa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililokuwepo tunajiaminisha kwenye mipango yetu. Tukishapanga maofisini tunatumia nguvu kwenda kutoa maamuzi. Hili kwetu halitatufikisha kokote. Muda Waziri anaotaka kutoa maamuzi hususani yatakayowahusu wavuvi na wafugaji awafuate kwanza, awashauri wakubaliane, wazungumze hatopata pingamizi sehemu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini kama mfugaji wa sasa tena Mungu kajalia leo wapo hapa wengi, wafugaji wa leo umwambie kwamba baada ya ng'ombe kumuuza milioni moja utamuuza milioni moja na laki tano maana nyama yake itakwenda nje ya Tanzania, hawezi kukataa. Anakataa kwa sababu mara nyingi tuna maamuzi ya kibabe. Unaamua, unapanga halafu unamtolea maamuzi, ng'ombe wake, halafu wewe ndio unamtolea maamuzi, sio sahihi. Tushirikishe kwenye maamuzi, Waziri apange naye, azungumze naye, waone nini wanafanya atakuwa hana tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimekuja hasa na mambo ya kushauri, nimshauri Waziri, Taasisi zake nyingi ziko katika maeneo ya kukodi, wanakodi majengo hususani hapa Dodoma. Mheshimiwa Waziri, alipe kipaumbele suala la kujenga Ofisi kubwa ambayo taasisi zake zote ataziweka hapo. Leo mfugaji anatoka Mara anamtaka mtu wa uvuvi, sijui sekta gani iko jengo gani, sijui sekta gani iko jengo gani, sio sahihi. Ajenge jengo la Ofisi Dodoma ndiyo tumekwishahamia, bado hawajaamini kama tumehamia? Ndio tumeshafika. Wajenge jengo ambalo litakusanya taasisi zao zote ili waweze kufanya kazi na kuleta ufanisi na tija ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia ndani ya bajeti hii ili Mheshimiwa Waziri, aende vizuri, mipango yake iende vizuri lazima awe na ofisi nzuri, lazima awe na sehemu ambayo wafanyakazi wanafanya kazi vizuri. Leo unaenda hata huko kwa mpangaji kuna masharti, siku nyingine anaamua tu kufunga ofisi yake, siku nyingine anaamua tu leo hatufanyi kazi. Kwa hiyo, masharti ya wapangaji ni mengi. Dodoma tumeshafika, ndiko Makao Makuu ya Nchi, tunataka Waziri ajenge na taasisi zake zote zilizoko ndani ya Wizara yake zifanye kazi ndani ya jengo hilo. Ajenge jengo moja kubwa lilete faida, lilete tija kwa Watanzania ili kazi ziweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la sensa kwa mifugo. Suala la sensa kwa mifugo lina faida yake, lakini kwa nini Waziri kuna baadhi ya mambo hapati ushirikiano? Ni pale pale ninaporudi, kwa sababu hawatoi ushirikiano kwa watu wa chini. Kwa usikivu wao nawaomba suala la sensa litaenda kutupatia majibu ya kuona ng'ombe wangapi wako Tanzania na wanamilikiwa na akina nani? Hata hii migogoro ya kila siku ya wafugaji na wakulima itaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitegemei mfugaji halisi wa Tanzania ataenda kuingiza ng'ombe ndani ya shamba ya la Mtanzania mwenzie. Tuwape elimu wafahamu kwamba sote rasilimali ya Tanzania ni ya kwetu, haya mambo mengine yanasababishwa na watu waliokuwepo ndani ya mipaka ya Tanzania. Hata hivyo, ile migogoro likija zogo la wafugaji utasikia fulani, fulani ni wafugaji, Hapana, wengine ni wahamiaji, majirani zetu. Waziri afanye sensa tujue kitongoji, kata ina wafugaji wangapi, wenye kata yao wapange hapa mtafuga, hapa mtalima. Tatizo litatokea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mfugaji wa leo kweli atakataa kuambiwa hapa fuga, hapa nywesha maji?

Mpelekee maji ng'ombe wake, mihangaiko anayohangaika kuna muda hata ng'ombe anashindwa kunywa maji, watengeneza mabwawa, wawaoneshe maeneo ya kufuga hawana shida. Hii nchi ya Tanzania iko salama, ina amani kwa sababu watu wa nchi ya Tanzania ni wasikivu, waelewa, ndio maana ukaona mpaka leo Tanzania ina amani. Usikivu wao tuutumie vizuri kwa kuleta maendeleo kwao. Kama tutawasimamia vizuri Waziri na Naibu Waziri wakishuka chini, Wizara ya Uvuvi itabadilika, uvuvi hautodharauliwa na vijana na watu wataung'ang'ania kama wanaenda kuchimba dhahabu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida, kengele yako ilikuwa imelia.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Miraji Mtaturu baadaye atafuatia Mheshimiwa Edwin Swalle na baadaye Mheshimiwa Simon Songe ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja lambayo iko mezani. Kwanza nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwaongoza Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kaka yangu na swahiba wangu Abdallah Bin Ulega pamoja na Naibu wake ndugu

yangu David Silinde pamoja na Wizara nzima kwa ujumla kwa hotuba nzuri yenye maono, yenye uelekeo mzuri ambayo inaonekana wazi kwamba tunapata mapinduzi makubwa kwenye Sekta ya Uvuvi pamoja na Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu nimeipitia hii hotuba na nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri, nimesikiliza pia maoni ya Kamati ambayo mengi yameipongeza Wizara. Nasema kama haya waliyoyaandika ndani ya hii hotuba wataenda kuyatengenezea mpango kazi, Mheshimiwa Waziri tutatoka kidedea na tutaona namna ambavyo sekta hii itafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kama ambavyo wamepongeza wengine kwa uteuzi alioupata pamoja na wenzake lakini niamini kwamba kwa nguvu aliyonayo, maono aliyonayo, hamu aliyonayo, Wizara hii itaenda kubadilika na italeta matokeo chanya yaliyotarajiwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia taarifa ya Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri sana imejieleza kwenye Kamati, kuna malengo waliyojipangia hawakuzidi asilimia 40, kwa maana kwenye mapato, kwenye maduhuli ambayo walitegemea. Pia kuna mipango mingi ilikwama katika mwaka wa fedha uliopita. Hiyo ni kwa sababu ya rasilimali fedha, lakini mipango yao inawezekana haikufika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini mwaka huu wamejifunza na wamefanya tathmini, tunaamini mwaka mmoja ujao tutakuwa na mabadiliko mengine ambayo tumeeleza. Hata hivyo, nikiangalia katika hili tunayo mifugo mingi sana, tunao ng’ombe milioni 36 kwa mujibu wa taarifa ambayo tumeiona hapa. Tunaona tuna mbuzi wa kutosha,

tuna kondoo wa kutosha, lakini kama haitoshi tuna rasilimali kwenye Bahari pamoja na Maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tukitumia vizuri hii mipango tuliyoipanga, tutakuwa na matokeo makubwa na Wizara hii itachangia fedha nyingi kwenye pato la taifa. Tumeona wamesema ni asilimia saba tu inachangia kwenye pato la Taifa, bado ni ndogo. Kama walivyosema wengine ni kwamba mifugo tuliyonayo inawezekana kuna changamoto ambayo tunapaswa twende nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo nimeliangalia kidogo, ni upande wa ukusanyaji maziwa. Ukiangalia Nchi za Afrika Mashariki wenzetu wa Kenya wameweza kukusanya lita 1,241,000, watu wa Uganda wamekusanya maziwa Lita 707,560, lakini sisi Tanzania tumekusanya lita 64,837. Sisi tunasema tuna ng'ombe wengi, tunasema tunayo rasilimali nyingi, tuna eneo kubwa la kufugia, lakini bado tunaweza kukusanya maziwa kiasi hiki kidogo, maana yake bado kuna kazi hatujafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Sisi tunafanya ufugaji wa kienyeji. Ng'ombe wetu si kwamba tunawaona kwa mazingira, ng'ombe wetu ni wadogo, hawana kilo nyingi, nyama zao hazivutii kuliwa. Tukienda kuchoma mnadani tukala tunaamini nyama nzuri, lakini ikienda kwenye vipimo na vipimo vinavyotakiwa nyama ile ni kama haitakiwi. Nini tunatakiwa tufanye? Lazima tupige hatua moja mbele na ndio maana nakuja na ushauri. Mheshimiwa Waziri, amefanya kazi nzuri, mipango ni mizuri, lakini nimeona nami niweke mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni eneo la *Ranch* za Taifa. Mheshimiwa Waziri *Ranch* zetu hazifanyi kazi, ni kama

hazipo, yamebaki kuwa mapori tu. *Ranch* hizi ziliwekwa makusudi ili zisaidie mapinduzi ya ufugaji nchini. Kulikuwa na uwezo wa wafugaji wetu kwenda kujifunza, maeneo mengi leo *Ranch* zimebaki kuwa na walinzi tu. Mameneja wale wapo tu wanaangalia kulinda angalau wasije wakaibiwa majengo yale ambayo yako pale. Hii sio sawa. Hata ukiangalia leo Waziri ametuambia hapa *Ranch* ya *NARCO* amenunua vitu lakini vitu venyewe vilivyonunuliwa ni vichache, yaani bado hawezi kujivunia kwamba kuna hatua watapiga. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba *Ranch* zetu zingine ziko *grounded* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ninayotaka kusema ni hii, huu mpango mnaokuja nao wa kuwasogeza wawekezaji ambao watakuja kufanya na sisi ili waweze kutumia miundombinu tuliyoiweka kama Serikali kuweza kunenepesha ng'ombe, kuweza kuongeza utaalam, uhamilishaji na vile vituo kwa sababu viko karibu na wananchi, wananchi waje wajifunze pale. Mheshimiwa Waziri hapo ndiyo atakuja kuleta mapinduzi makubwa ya ufugaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hili walilokuwa wanataka kulianza la kuhakikisha kwamba wanakwenda kuwakaribisha wawekezaji ambao watakwenda kusimamiwa na wataalam wetu wengi ambao wako Wizara ya Mifugo, Wizara ya Mifugo ni kama Wizara ya Kilimo ina wataalam wengi sana. Mheshimiwa Waziri awatumie hawa waweze kuleta mapinduzi ya ufugaji katika nchi yetu. Nilitaka nieleze hilo kwa upande huu wa *Ranch* zetu, najua mipango wameshai-*set,* lakini naongezea eneo hilo. Wafanye vizuri, wakaribishe wawekezaji, wawasimamie, naamini tutapata matokeo ambayo tunayatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni miundombinu. Tumekuwa tukijenga majosho, tumekuwa tukijenga mabwawa, tumekuwa tukijenga miundombinu mbalimbali inayosaidia ufugaji wetu. Hata hivyo, hizi fedha tumekuwa tukizitupa kwenye halmashauri, kule hakuna *mechanism* ya kuzisimamia, leo majosho mengi yamekufa, mabwawa mengi yamekufa hatuna uwezo hata wa kuyakarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba tuunde kama ikiwezekana Tume maalum kama ilivyokuwa Tume ya Umwagiliaji, tuwe na Tume ambayo itaenda kuratibu rasilimali ya mifugo kule kwenye Halmashauri zetu. Kule kwenye Halmashauri unakuta Afisa Mifugo yupo mmoja tu wakiingia pale Mkurugenzi vipaumbele vinakuwa ni sekta nyingine lakini sekta ya mifugo haiangaliwi ambayo ndiyo inabeba watu wengi kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri eneo hili muone namna ambavyo mtaweza kufanya, kuundwe Tume fulani mfano kwenye maji tuliona tatizo tukaunda *RUWASA* tuliona kuna matatizo tukaunda *TANROADS* leo hii kuna barabara zinajengwa, leo hii unaona kuna ufuatiliaji na mambo kama hayo, kwa nini tusifanye kwenye mifugo inawezekana tukiamua ili fedha nyingi zinazoenda kule zikasimamiwe na tume maalumu ambayo italeta matokeo ambayo tunayatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili pia nina maombi yangu katika Wilaya yangu ya Ikungi, eneo hili kama wafugaji tunao tunahitaji majosho, tunahitaji mabwawa lakini tuna maeneo ya Kata za kimkakati ambazo tukiwekewa majosho haya yatasaidia kuleta mapinduzi. Mojawapo ni Kata ya Siuyu, Kata ya Mang'onyi, Kata ya Isuna, Kata ya

Mkiwa na Kata ya Misughaa maeneo haya Mheshimiwa Waziri yanao wafugaji wengi wakiwekewa miundombinu ya mabwawa, wakiwekewa majosho utaona mabadiliko ya ng'ombe wetu na utaalam ambao unataka kutuletea wa yale madume ya mbegu ambayo yataenda kubadilisha kizazi cha mifugo ninaamini kabisa tutabadilidha ufugaji wa watu wetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nimalizie kuhusu uvuvi pamoja na kuwa sisi hatuko Pwani, pamoja na sisi tuko Kati huku Mheshimiwa Waziri lakini na sisi tuna mabwawa na tuna maziwa, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri ninalo bwawa langu linaitwa Muyanji liko pale Singida, bwawa hili limejengwa toka enzi za ukoloni, bwawa hili tumekuwa tukipata kitoweo cha samaki lakini hapa katikati tumekuwa tukipata *ups and down*s kwa sababu hatupati samaki wazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 tulipeleka vifaranga 3,500 kupitia Halmashauri yetu tukapandikiza mle ndani, wananchi wameendelea kupata kitoweo pale, vijana wetu wanapata shughuli za uvuvi pale, ninakuomba sana ikikupendeza bwawa lile limepungua kina nikuombe sana tupate fedha tukatoe zile tope zilizoingia mle ndani, tuliboreshe vizuri kwa kujenga miundombinu sehemu ya kunyweshea mifugo iwekwe ili isiendelee kutifuatifua udongo utakaoingia ndani ya bwawa lile, ili bwawa lile la Muyanji liendelee kutoa Samaki, kwa sababu Wizara yako inatusaidia kwenye protini na samaki kule pia tuwapate kwenye Wilaya yetu ya Ikungi na hasa kwenye eneo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye eneo hili ukilifanyia kazi utakuwa umetufanyia vizuri, baada ya maeneo haya nakushukuru, naunga mkono hoja, nakushukuru nakutakia kila la kheri.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Miraji Mtaturu, nilimtaja Mheshimiwa Edwin Swalle halafu Mheshimiwa Simon Songe ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza Kaka yangu Mheshimiwa Ulega pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii na timu yote ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nimekwenda kwenye mabanda pale nje kumenoga kweli kweli, kwa kweli Mheshimiwa Waziri umetuthibitishia kwamba hii ni Wizara ya vitoweo, hongereni sana kwa ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kwenye eneo la sekta hii ya maziwa. Jimbo la Lupembe na Mkoani Njombe kwa ujumla wake huko nyuma tulikuwa na kiwanda kizuri sana cha maziwa, kiwanda hiki cha maziwa kilikuwa kinatoa ajira nyingi kwa wananchi wetu, kilikuwa kinatoa kodi kwa Serikali na kadhalika, lakini kiwanda hiki ambacho kilikuwa ni msaada mkubwa kwenye kuchakata mazao ya mifugo leo hii kimefungwa. Mkoa wa Njombe tangu wakati wa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kule Makete *ranch* ya Kitulo kulishakuwa na *ranch* nzuri kwa ajili ya mifugo na Mheshimiwa Waziri anajua, *ranch* hii ya Kitulo ilikuwa ni kwa ajili ya kunenepesha ng'ombe tulikuwa na ng'ombe wakitoa maziwa mpaka lita 40 kwa siku, *ranch* hii imeendelea kushuka imeendelea kuwa haina tija kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu amekuja kuipa nguvu sekta hii ni vizuri akaenda Mkoani Njombe akasaidie kufufua

kiwanda cha maziwa kilichoko Njombe, Serikali kupitia Waziri kwa sababu mnayo nia njema ya kupeleka mbele sekta hii ya mifugo na uvuvi ninaamini kiwanda hiki ambacho kinapigwa danadana, kimejawa na mambo mengi, wataalam wako Mheshimiwa Waziri ukiwauliza wanajua, ukifia Njombe utakuja kukikwamua kiwanda hiki ambacho kipo na mitambo ipo, badala ya kupanga mambo mapya ningeomba bidhaa tulizonazo, vifaa tulivyonavyo tukaboreshe vianze kutoa ajira kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka nitumie nafasi hii pia kupitia wewe nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake njema ya kuboresha sekta ya mifugo na uvuvi. Halmashauri ya Njombe kwa mara ya kwanza Halmashauri ya Njombe *DC* tumepata mradi wa mabwawa manne ya kufuga Samaki, huu ni mpango ambao sekta hii ya uvuvi na mifugo imeamua kwenda mbele na kuboresha maisha ya wananchi wetu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu umeanza vizuri, utakapokuja Njombe utembelee mabwawa haya ili uone pia namna ya kuongeza fedha na kuongeza tija kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la lingine ninataka pia niseme kuhusu mifugo kwamba ni kero. Nakubaliana na Waziri kwamba mifugo ni utajiri, mifugo ni uchumi lakini mifugo pia ni kero. Zipo kero tatu kwenye mifugo, kero ya kwanza hii mifugo imekuwa sababu ya ugomvi kati ya wakulima na wafugaji. Jambo la pili, kero kwenye mifugo ni kwamba mifugo imekuwa ni sababu ya ajali mbalimbali barabarani, Wabunge ninyi mnakumbuka Mheshimiwa Kigwangalla yuko hapa alipata ajali kwa kugongana na mifugo barabarani, Mheshimiwa Waziri ujumbe wangu ni nini, tunakuomba uibadili sekta hii ya mifugo…..

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mwita Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba mifugo siyo kero, ila wanaotunza mifugo hiyo ndiyo wana kero, kwa hiyo watu waelimishwe tu kwamba mifugo haina akili watu ndiyo wanaitumia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Swalle unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa heshima ya Mheshimiwa Getere ninachosema ni kwamba Mheshimiwa Waziri ninakuomba uifanye sekta hii kuwa na utulivu tusiache mifugo iendelee kurandaranda kila mahali, leo hapa Dodoma kwa mfano ukiingia katikati ya mji mchana unaweza kuona ng'ombe, hata ukiingia Dar es Salaam unaweza ukaona mbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni nini? Kwa kuwa Serikali yako maeneo mengi tumepanga maeneo kwa ajili ya majumba ya makazi, yako maeneo kwa ajili ya mahoteli, ninayo imani kwamba Mheshimiwa Waziri mnaweza kupanga vizuri maeneo kwa ajili ya malisho na maeneo kwa ajili ya wakulima. Jambo hili Mheshimiwa Waziri linawezekana kwa dhamira njema ambayo unaweza kuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia jambo lingine kwamba mwaka huu kwenye mbio zetu za Mwenge, kauli mbiu za mbio za Mwenge mwaka huu 2023 zinasema

"Tutunze mazingira, tuokoe vyanzo vya maji, kwa ustawi wa viumbe hai na uchumi wa Taifa". Kauli mbiu hii ya kutunza mazingira inaendana na kudhibiti uzuraraji wa mazao ya mifugo, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri ujitahidi kuweka mpango mzuri ili kusimamia sekta hii ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu na hili ni muhimu sana, nimesoma kwenye taarifa ya Waziri hapa amesema namna sekta ya mifugo na uvuvi inavyochangia uchumi wa Taifa. Mifugo inachangia uchumi kwa asilimia Saba na lengo la Serikali na Waziri na timu yake yote ninaamini tunataka kulikamata soko la Kimataifa, lakini nitoe wito kwenye Wizara hii kwamba soko la Kimataifa lina vigezo vya kuuza bidhaa za wanyama duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vigezo hivyo ni kuwatambua wanyama hawa kuwasajili na kujua hawa wanyama ni mali ya nani, huwezi kupeleka biashara kwenye soko la Kimataifa bila kujua mmiliki ni nani kwa usajili alionao. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri umesema kwenye taarifa kwamba mlikuwa na mpango wa kuwatambua wanyama na mpango huu umesimamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwako mnaweza kukaa kwenye Wizara yenu kama gharama ni kubwa ya kulipia usajili na utambuziwa wa Wanyama, mnaweza kama Serikali kusaidia kama ambavyo tumefanya kwenye sekta yetu ya kilimo, mkatoa ruzuku kwa kiasi fulani ili mkulima alipe bei kidogo. Kwa hiyo, kama ni 1,500 Serikali mnaweza kutoa ruzuku shilingi 1000 na huyu mfugaji akatoa 500 au 300, lakini ni lazima mifugo yetu itambuliwe, ifanyiwe ufuatiliaji ili soko la Kimataifa liweze kutuelewa kwamba tuna sifa ya kuingia kwenye soko la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine nataka niseme kidogo kuhusu mpango wa mbele wa kutoa elimu ya ufugaji. Hivi karibuni kumekuwa kuna mpango wa Serikali wa kujenga vyuo vya *VETA* nchini, vyuo vya *VETA* ni kutoa ufundi na ujuzi kwa wananchi, ninataka nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Wizara yake kwamba washirikiane na Wizara hii ya Elimu na Sayansi vyuo hivi vya *VETA* kwenye maeneo mengine ni Mikoa ya wakulima, Jimbo la Lupembe kwa mfano tumepata chuo cha *VETA* kile chuo ni muhimu kikawa chuo pia cha mifugo na uvuvi ili wananchi wetu wasome habari ya umeme, wasome habari ya ujenzi lakini pia wasome na kilimo kwa sababu kilimo ndiyo shughuli yao ya kila siku kwenye maeneo yale, tukifanya hivyo vyuo hivi vitakuwa na tija kwenye kila eneo ambako vipo

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pia kwa kumalizia nitumie nafasi hii kumsihi sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Mifugo na Uvuvi, kwamba ubunifu alioanza kuufanya leo kwa kutuonesha kwa vitendo uzuri na ubora wa Wizara hii uigwe na Wizara nyingine huko mbele ambako tunakwenda, ubunifi huu Mheshimiwa Waziri ndiyo kitu pekee ambacho kitakupeleka mbele na ktoa tija kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Swalle. Nilimtaja Mheshimiwa Simon Songe Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa. Dkt. Christine Ishengoma wajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna alivyokuja na mpango wa kuhakikisha kwamba tunawekeza sana katika Wizara hii, pia niwapongeze Waziri pamoja na Naibu kwa kazi kubwa ambayo mmeonesha kuanza kuifanya, pia nimpongeze sana Katibu Mkuu Shemdoe kwa kazi ambayo anaendelea kuifanya, akili kubwa aliyoitumia TAMISEMI basi akaendelee kutumia akili kubwa hivyohivyo kwenye Wizara ya Mifugo ili tuweze kupata pato kubwa kutokana na mifugo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema mchango wa mifugo pamoja na uvuvi kwenye Serikali yetu ni asilimia saba ya pato la ndani, asilimia hizi ni chache sana ukilinganisha na idadi ya mifugo tuliyonayo. Ukichukua tu mifugo tuliyonayo inatosha kabisa kutupa pato kubwa ikilinganishwa na pato ambalo tunalipata sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo pia imekuwa ikiongezeka mwaka kila mwaka lakini pato ambalo linachangiwa kutoka kwenye Wizara hii linateremka kila mwaka. Kwa mfano, ukichukua 2016/2017 mchango wa pato ulikuwa asilimia 7.6, ukienda mwaka 2017/2018 asilimia 5.4, ukienda mwaka 2018/2019 asilimia 7.2, ukienda mwaka 2019/2020 asilimia 7.4, 2020/2021 asilimia Saba na 2021/2022 asilimia Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi kuchangia asilimia Saba peke yake kutokana na mifugo pamoja na uvuvi, tunatamani kuona mwakani mchango wa Wizara hii unafika angalau asilimia 10, asilimia 12 mpaka asilimia 15 tuwekeze kwenye mifugo ni sehemu mojawapo pia ambayo tunaweza kupata rasilimali nyingi za fedha kutokana na Wizara hii ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana Waziri angalia hili ni jambo ambalo tunatakiwa sasa tuwekeze kama ambavyo tumewekeza kwenye kilimo pia tuwekeze kwenye mifugo ili tuweze kupata pato kubwa litokanalo na mifugo. Kama walivyosema wenzangu pia hakuna tutakapokwepa kuwatambua wanyama, haiwezekani tukaacha kuwatambua wanyama halafu tunategemea kuongeza pato katika nchi yetu haitawezekana! Ili tuongeze pato katika nchi yetu ni lazima tuwatambue Wanyama, ni lazima tuwasajili Wanyama, pia ni lazima tuwafuatilie kwa sababu hatutaishia kwenye kuwatambua, unawatambua *so what?* Hatutaishia kwenye kuwasajili, unawasajili ili iweje? Tunatakiwa twende mbele zaidi kuwafuatilia

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta Afisa Mifugo yupo ofisini anaamka asubuhi hajui wala ratiba yake, hajui aende wapi, hajui aende kwa nani, hafahamu! Inatakiwa ifike sasa sehemu Afisa Mifugo akiamka asubuhi anajua kabisa kwamba naenda kwa mfugaji Songe ana ng'ombe 200, naenda kufanya kazi moja, mbili, tatu nne, tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwape elimu kwa sababu kama watakuwa wanafuga bila elimu, tutafuga ng'ombe 10,000 lakini mwisho wa siku tutaenda kwenye '*inversely proportional to x*' tulikuwa tunasoma kwenye hesabu miaka fulani hivi kwamba x *is inversely proportional to y,* yaani kadri *speed* ya gari inavyoongezeka na muda unapungua. Kwa hiyo, kadri ya ng'ombe wanavyoongezeka wengi na pato nalo linapingua *so what?* Tunategemea ng'ombe wakiongezeka na pato liongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna muda mwingine lazima tuwasaidie hawa wafugaji, Mheshimiwa Waziri tuangalie sana kuwasaidia wafugaji, Maafisa Mifugo walioko huko wawe na ratiba ya kuwatembelea wafugaji ili

wawasaidie, hata hili suala la hereni limefeli kwa sababu mwananchi anasema, *so* ukinivalishia hereni inakuwaje sasa? Wakipata Elimu mimi nafikiri ni jambo jema lakini kwa sababu hawajapate Elimu hawajui kwamba ukimvalisha heleni ng'ombe wake halafu mwisho wa siku inakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anatakiwa aambiwe tunataka tuwafahamu lakini pia tunataka tujue eneo hili kuna mifugo mingapi ili tuweze hata kuweza kutengeneza mabwawa kwa ajili ya maji, anajua oooh! Kumbe kutakuwa na faida, anajua kabisa kwamba hata yakitokea magonjwa anakuwa anafahamu kwamba eneo hili kuna ng'ombe kadhaa tupeleke dawa kadhaa, Hiyo ndiyo maana ya kuwatambua ng'ombe wetu ndiyo maana ya kutambua mifugo tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tuangalie, tuje na mpango ili tuweze kuwatambua. Niwaambie Watanzania wenzangu kama tunataka Pato la Taifa liongezeke kutokana na mifugo ni lazima tukubali kuwatambua mifugo, lazima tukubali kuwasajili mifugo, lazima tukubali kuwafuatilia mifugo bila hapo hatutapandisha pato kutokana na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kidogo kwenye eneo la uvuvi. Mimi kila siku najiuliza kuna hawa watumishi ambao mmepeleka kwenye Wilaya zetu wanaotoka Wizara ya Uvuvi wako chini ya Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi ni sawa kabisa, lakini wakienda huko wanakuwa tofauti kabisa na Maafisa Uvuvi walioko kwenye Halmashauri, kila mtu utekelezaji wake anatekeleza tofauti. Huyu akienda huku anakuwa *boss* huyu akija huku anakuwa *boss* haiwezekani tukafika kwa stahili hiyo? Mheshimiwa Waziri liangalieni hili kama inawezekana wekeni *agency,* hawa waliopo Halmashauri waungane na hawa ambao wanatoka

Wizarani wafanye kazi moja. Wanakamata watu, ukimuuliza ambae mimi namuuliza kila siku wa Halmashauri anasema sijui, kwa nini asijue wakati wanatekeleza wote sheria moja? Ni lazima wafanye kazi kwa Pamoja, ni lazima wafanye kazi kwa kushirikiana ili tusonge mbele na kuacha kuwanyanyasa wavuvi na kuwakatisha tamaa, tukitaka wavuvi wafanye kazi ni lazima tukubali kuwasaidia. Tukitaka wavuvi waweze kuleta pato katika nchi yetu ni lazima tukubali kuwapa semina, wamefika huko wanafika kukamata hatuwasaidii, nami nitakuwa wa mwisho kujisifu kuongeza pato eti kwa sababu ya faini, nitakuwa wa kwanza kushabikia kupunguza pato kwa sababu watu wametii sheria bila shuruti, hakuna sababu ya kujisifu kwamba tumekusanya hela nyingi zinazotokana na *penalty* tumekusanya fedha nyingi zinazotokana na faini maana yake makosa yameongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiwasaidie wavuvi kuwaelimisha badala ya kuwa na makosa mengi wawe na makosa kidogo ili tuweze kuwasaidia, tunawafilisi bila sababu za msingi. Halafu unakuta ana uvuvi haramu na huyu anaenunua nyavu dukani, hazijawahi hata kusikia mwenye duka kafilisiwa, hatujawahi kusikia mwenye kiwanda kafilisiwa lakini anaefilisiwa ni mvuvi kwani hamjui maduka yanayouza nyavu hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnayajua maduka haya nendeni mkashughulike nao tuwasaidie wavuvi, tuwasaidie watu wa Busega, tuwasidie watu wa Mafia, tuwasaidie watu wa Mwanza ili waweze kuvua wakiwa na amani kuliko sasa hivi kila siku wamekuwa watu wa kukimbia kimbia, nakumbushwa hapa na Kigoma. Mheshimiwa Waziri tulifanye hili ili tuweze kuwasaidia, hamna sababu ya msingi ya kukimbizana na wavuvi, wanakufa humo ndani ya maji kwa sababu ya kukimbizana, tuwasaidie kuwashauri, tuwasaidie kuwapa semina, tuwasaidie kuwapa elimu, ikifika sehemu ya

kumpiga faini basi tumpige faini lakini tuanze kwanza kwa kumsaidia huyu mvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni hilo la mikopo kwa vikundi vya wavuvi. Eneo hili na lenyewe lina ukiritimba mwingi bila sababu za msingi. Hebu Mheshimiwa Waziri angalieni hili, watu wa Busega huko wameomba mpaka wamechoka. Sasa wanaopewa hii mikopo ya vikundi ni watu gani tofauti na Watanzania? Tunaomba kama inawezekana, tu – *review* namna ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya wavuvi wetu ili waweze kupata, kwani wameunda vikundi lakini upatikanaji unakuwa mdogo. Upatikanaji wake unakuwa wa kufuatilia, mwisho unafuatilia mpaka nusu ya gharama ya ule mkopo utakaopewa inaisha. Unafuatilia, unafuatilia, bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie hili ili tuweze kuwasaidia wananchi hawa, ambao ni wavuvi ili waweze kuleta tija. Tunatamani mwakani akija hapa aseme mapato yamepanda kutoka asilimia saba ya mchango wa Wizara yake, imefika asilimia 10. Mimi nitakuwa wa kwanza kupiga makofi na wa kwanza kwenda kumpongeza nyumbani kwake, kwa sababu tutakuwa tumeona kweli amedhamiria kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simon Songe. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, halafu Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Tunza Malapo, wajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwanza napenda kuipongeza Wizari yetu hii ya Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote wa Wizara. Kwa kweli wametuletea bajeti ambayo imegusa kila sekta na matarajio yetu wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiona Sekta hii ya Uvuvi na Mifugo kwamba hii ni sehemu ambayo Serikali yetu itainua kipato cha mwananchi mmoja mmoja, kitaongeza ajira, na lakini pia kitaleta uchumi mkubwa ndani ya Nchi yetu. Tunafahamu kwamba kuna baadhi ya nchi hapa duniani zinaendeshwa kwa uvuvi tu na nyingine kwa mifugo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na pia nampongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar kwa sababu kwenye uvuvi wa Bahari Kuu ni chombo cha Muungano na ndiyo maana Mawaziri wetu wote wawili wako hapa na kila mwaka tunawaona. Nawapongeza sana kwamba na kule Zanzibar sasa kuna mikakati madhubuti ya kuhakikisha Zanzibar nayo kwa kushirikiana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia chombo hiki cha uvuvi wa Bahari Kuu kinataka kuwekeza kwenye Sekta hii ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Nawapaongeza sana Serikali zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, naipongeza Wizara kwa kusamehe na kuondoa tozo mbalimbali katika Sekta zote; za Uvuvi, Mifugo na mambo yanayohusiana na mazao hayo, ikiwemo Sekta ya Maziwa. Sekta ya Maziwa ilikuwa ina changamoto nyingi sana huko nyuma kutokana na tozo mbalimbali ambazo zinakwamisha ukuaji wa sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo nane zimesamehewa au zimeondolewa katika Sekta ya Maziwa. Ninachokiomba sasa, tuendelee kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya maziwa kwa maziwa yanayodumu kwa muda mrefu ili kuokoa maziwa ya wafugaji wetu yasiharibike na sisi kuepuka kuingiziwa maziwa ambayo virutubisho vyake vimeongezwa baadhi ya mambo ili kuathiri afya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa chakula pia unapatikana kwenye Sekta hizi mbili; Mifugo na Uvuvi. Naipongeza sana Serikali kwa kutaka kuwekeza katika Sekta hizi. Nikiendelea, Serikali inawekeza fedha nyingi sana kwenye Sekta ya Ufugaji kwa kuwajengea mabwawa wafugaji wetu huko waliko. Cha kusikitisha, uwekezaji ule unatuvunja moyo kwa maana haufikii viwango vile ambavyo vinatarajiwa. Ninachokiomba kwa Wizara, pamoja na kwamba maeneo ya wafugaji yako ndani sana, wawe na ufuatiliaji wa mara kwa mara kuhakikisha malambo na mabwawa hayo yanajengwa kwa viwango vinavyostahili ili kuzuia kupoteza fedha za Serikali, na walipa kodi ambao ni wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta hii ya Mifugo, bado mfugaji hafaidiki na soko au fedha kutokana na bidhaa yake ya ufugaji. Tumepata masoko kutoka nje ya nchi, majirani zetu tunao, lakini kiunganishi hapa kinakuwa kikwazo, kwa sababu wanakutana na madalali. Madalali ndio wanaokwenda kwa wafugaji, wanawachukua ng'ombe mpaka Dar es Salaam, wanawakabidhi wale wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hii ni Sekta binafsi lakini kuwe na kiungo, kama kituo kuhakikisha mnunuzi anajua afike wapi ili aweze kuwapata hawa ng'ombe kupitia kwa mkulima au mfugaji mwenyewe ili afaidike zaidi yule

mkulima na mfugaji, sio dalali. Kuna udalali mkubwa hapo unaofanyika kwenye Sekta hii ya Mifugo. Kwa hiyo, tuendelee kuimarisha sekta zetu au tasnia zetu za utafiti kwenye uvuvi na kwenye mifugo. Hapo ndiyo tutapata malisho bora, tutapata mbegu bora, na mazao bora kwa ajili ya sekta zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie uvuvi wa Bahari Kuu. Muda mwingi tulikuwa tunapiga kelele kuhusu sekta hii kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu. Naipongeza kwa dhati Serikali, sasa imejikita kuingia kwenye Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu, kwa maana ya kwamba imeagiza meli mbili za uvuvi kwenye ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kule Kilwa, tumeona mambo yameanza. Tunachoomba sasa, Serikali iwekeze fedha kwa haraka ili bandari ile imalizike, meli hizo zinunuliwe, na vifaa vyake vingine vijengwe ili tuingie kwenye Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu, nasi tuweze kufaidi rasilimali alizotupa Mwenyezi Mungu kwa kupitia bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye uvuvi wa Bahari Kuu, izungumzie Shirika la *TAFICO*. Nimeona mipango mingi ambayo imepangwa kwa ajili ya kulifufua hili Shirika ili lianze kazi. Shirika hili linahitaji uwekezaji mkubwa, linahitaji fedha nyingi kwa sababu miundombinu yake inatumia gharama kubwa. Tusione shida kuwekeza, kwa sababu tukiwekeza leo tutafaidika kesho. Tunapowekeza zaidi kwenye Shirika la *TAFICO* tutavuna zaidi mabilioni kwa mabilioni ya fedha na tutaongeza ajira, tutaongeza ukuaji wa uchumi na pato la Taifa. Shirika hili ni muhimu, litatukomboa kwenye sekta ya uvuvi, tutakapoingia kwenye uvuvi wa Bahari Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanye hili Shirika lianze kazi haraka, liungane na bandari ya uvuvi tuingie kwenye uvuvi wa Bahari Kuu, tufaidi. Tusiwe kila siku tu tunapiga kelele,

Bahari Kuu, Bahari Kuu! Bahari imejaa Samaki, nchi za nje wanakuja na meli zao wanavua, sisi tumekaa. Mwenyezi Mungu katuruzuku hii rasilimali, tuitumie, tuwekeze, tukavuna zaidi ya tunachowekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, nimeona kwenye Wizara, Serikali ina mipango ya kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kwa zana za uvuvi. Tuendelee kuwasaidia wavuvi wetu kwa mikopo nafuu ili waingie kwenye Sekta ya Uvuvi na wao wafaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ni kazi ngumu. Unapotoka kwenda kuvua, unajua kwenda, hujui kurudi. Ikikukuta dhoruba huko, unaweza ukapotea baharini na usirudi, au kwenye visiwa usirudi, au ukapotelea nchi jirani baada ya miezi mitatu ndiyo unaokotwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi una hali ngumu, tuwawezeshe wavuvi wetu wavue kisasa na kwa tija. ikiwepo kuzifanyia marekebisho sheria na sera mbalimbali za uvuvi, iwe ni yenye manufaa kwetu na wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, kuna mfumo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umemalizika.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema, tuendelea kuvua na kufuga kwa kuhifadhi mazingira ya nchi, ili kunusuru nchi yetu isije ikawa jangwa na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, halafu Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Joseph Kamonga wajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia Sekta hizi za Mifugo pamoja na Uvuvi. Nianze kwanza kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mambo mengi mazuri anayoyafanya kwenye sekta hii, kwa sababu tulivyoona Bajeti ya Mifugo imeongezeka, ingawa Bajeti ya Uvuvi imepungua kidogo; lakini yote ni mazuri, Wizara hii inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mahususi sana kwa sababu inachangia asilimia saba kwa upande wa mifugo na asilimia moja kwa upande wa uvuv; na inachangia ajira kwa wananchi, pia na pato kwa wavuvi pamoja na wafugaji. Kwa hiyo, hii ni sekta mahususi kwa sababu inainua hata lishe ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, hotuba yake aliyoisoma ni nzuri sana, imejaa vipaumbele vizuri sana, imejaa mikakati mizuri sana ya kuendeleza miradi kama ilivyopangwa. Ushauri wangu ni kuwa, mambo yote yaliyopangwa yaweze kutekelezwa kwa wakati na pia bajeti ambayo tunaomba, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuweze kuipitisha kwa sababu hii ni sekta mahususi, na ni sekta nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo ina mambo mengi. Ukitaka kupata mifugo bora lazima ufuate kanuni

mbalimbali ambazo lazima mifugo iwe nazo. Kwa upande wa kwanza lazima iwe na malisho. Nimeona Mheshimiwa Waziri kwenye sekta yako una mipango mizuri sana ya kuboresha malisho. Malisho kwa upande wa sekta binafsi pamoja na malisho kwa upande wa Serikali, na malisho yanayoanzishwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kuwa jambo muhimu sana hapa ni malisho. Malisho yaangaliwe kwa umakini sana. Malisho yasitengwe kwenye mikoa fulani au kwenye Halmashauri fulani. Yawepo mashamba darasa ya malisho, na ikiwezekana mashamba darasa kwenye kila Halmashauri, kwa sababu mtu akiona, anaweza akaenda aka-*practice* yeye mwenyewe akaweza kuwa na malisho. Kwa upande wa malisho, pia kuna suala la mbegu. Kama wanavyosema, bado kuna tatizo la mbegu, lakini naona kwenye hotuba kwamba kuna mashamba ambayo yametengwa kuzalisha mbegu pamoja na shamba la vikugwe na mashamba mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hizo mbegu ziweze kupatikana madukani kusudi wafugaji waweze kupata mbegu na kuwa na mashamba na hii itapunguza migogoro mingine ambayo inaendelea au isiyo na lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ili wafugaji waweze kufuga kwa tija lazima waangalie yale mambo ya afya ya mifugo. Hii inaenda pamoja na chanjo na maji. Hapa nasemea upande wa mabwawa na malambo. Ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malambo na mabwawa yanachimbwa. Tumetembelea mabwawa mbalimbali, lakini unakuta mwisho wake yanakuwa siyo bora, kwa nini?

Nilikuwa nashauri ianzishwe mamlaka kama Mheshimiwa Waziri alivyosema kwenye hotuba yako. Hiyo mamlaka shughuli zake hasa, ziwe ni ufuatiliaji wa miradi hii ambayoe ni majosho, malambo ili kusudi yaweze kuendelea vizuri. Miradi ipo, lakini ufuatiliaji wake siyo mzuri. Naamini ikianzishwa mamlaka, mambo yatakuwa mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa madume bora ni jambo muhimu sana. Nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri; najua kuwa madume bora 366 yameshanunuliwa na kusambazwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kuwa hata hivyo, kuna wafugaji wazuri ambao wanaweza wakazalisha na madume bora kusudi hawa wananchi wafugaji hasa waweze kupata elimu ya kutumia madume bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye madume bora, kuna uhimilishaji. Wananchi wengi hawana elimu ya uhimilishaji. Nilikuwa namshauri Mheshimiwa Waziri kuwa Maafisa Ugani tulionao ambao ni wazuri, ni wasomi, wanafanya kazi nzuri, waweze kuwafikia wakulima na wafugaji, na kuwaelimisha kuhusu mambo ya uhimilishaji. Kwa mfano nina ng'ombe mmoja na una ng'ombe mmoja; natoa mfano wa *ASAS* mwenye ng'ombe wengi, lakini unakuta lita kwa ng'ombe mmoja anapata lita ya maziwa 36 kwa siku. Kwa nini uwe na ng'ombe wengi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja tena kwenye upande wa Maafisa Ugani. Nashukuru kwa Serikali kuwapitia pikipiki 1,012 hivi ambazo wamewanunulia. Ni jambo zuri sana. Mmewapatia na simu za kinganjani, mkiwemo na wenyewe kama Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, naomba, ingawa wako TAMISEMI, lakini Wizara pamoja na Serikali waweze kuwafuatilia kuona wanawafikia wafugaji. Wakati mwingine hawafiki kwa wafugaji, mpaka uwaite wewe mwenyewe,

lakini kwa sababu wamepatiwa pikipiki, naamini watafika kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili twende na sayansi na teknolojia, ni lazima tuboreshe huduma za mafunzo pamoja na utafiti. Kwa hiyo, fedha za bajeti zilizotengwa kwenye mambo ya utafiti, naomba zikishatolewa zote, waweze kupata bila kukata hata senti moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wafugaji na wakulima pamoja na watumiaji wa ardhi, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi naamini unanisikia, uweze kushirikiana pamoja na Wizara hii ya Mifugo kusudi hawa wafugaji waweze kutengewa ardhi yao waimiliki, wasibughudhiwe kusudi waweze kupata malisho yao, waweze kupanda malisho yao kwenye ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru mmetatua migogoro mbalimbali kwa upande wa Morogoro na wenyewe umetatua lakini kwa upande wa Morogoro, kwenye Bonde la Kilombero kwa upande wa Kilosa, Mabwelebwele, Tindiga, Kilangali bado migogoro ipo. Mheshimiwa Waziri naomba ulifanyie kazi kusudi tuweze kulitatua hilo pamoja na sehemu nyingine ambazo sikuzitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa utambuzi wa mifugo,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nasisitiza, kwa faida yake, utambuzi wa

mifugo uweze kuangaliwa, na mwisho ni uchumi wa bluu, na ufugaji wa vizimbani pamoja na malambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki wanapotea, lakini tukifuga kwenye vizimba, naamini tutapata samaki wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma. Nilimtaja Mheshimiwa Tunza Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa Kenneth Nollo, ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi hii ya uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Sina shida na hotuba, imeandikwa vizuri tu, kama kuandika, Mheshimiwa Waziri umeandika. Tatizo linakuja kwenye utekelezaji wa yale ambayo anayaandika. Yaani kama kwenye kuandika, kupangilia hoja, aah uko vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia dhima ya Sekta ya Uvuvi inasema, "kuhamasisha, kuwezesha na kusimamia uvuvi endelevu, ukuzwaji viumbe kwenye maji, uzalishaji bora wa viumbe wakuzwao kwenye maji pamoja na mazao yake." Tatizo linaanza hapo. Kule Mtwara na sehemu nyingine za nchi yetu wananchi wamehamasika kufuga viumbe wa majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kule kwetu Mtwara, watu wako tayari kulima mwani, na kufuga

majongoo bahari. Kasheshe inayowakumba, ndiyo hayo ninayokwambia kwamba kuandika siyo hoja, hoja ni kutekeleza. Watu wamehamasishwa, Mheshimiwa Silinde tuliongea, ulienda kuzindua. Hivi tangu umeenda kuzindua, umewauliza hata wanaendeleaje? Tangu umeenda kuzindua mpaka leo, hivi vifaranga vya majongoo havijapatikana na hawajui hatima yao. Ukumbuke wale watu wamewekeza fedha zao. Huko huko tunapohamasisha kwamba watu wakuze viumbe vya majini, walime mwani na kadhalika, lakini wameweka vile vizimba vizuri, wanawalipa walinzi, wanafanya uangalizi mbalimbali; majongoo, vifaranga vitoke Bagamoyo, vikifika Mtwara vimekufa, lakini mnawaambia wafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasubiri watakuja; watakuja lini? Kwa hiyo, unapokuja kuhitimisha Mheshimiwa Waziri wafugaji wale wa majongoo Mtwara wanataka wapate jibu la uhakika, suala lile linafikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kuhusu mwani, pia wamehamasika sana, tatizo linakuja kwenye masoko ya uhakika. Suala siyo kuuza kwa sababu hata ukiuza shilingi 200 si umeuza? Tunataka wauze kwa bei yenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko kwenye mazao ya bahari kuna fedha nyingi ambazo Serikali inazipoteza. Kuna fursa nyingi ambazo Serikali ingewekeza ingeweza kupunguza baadhi ya matatizo ya ukosefu wa ajira kwa sababu watu wamehamasika na watu wanatamani wafanye, wanachoshindwa ni uwezeshaji na uwezeshaji huu ndiyo huo ninaosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Hotuba ya Mheshimiwa Ulega, utaona sisi tunaenda kuwa matajiri lakini mwaka jana hapa niliongea vizuri sana nikasema *issue* siyo

kutenga, *issue* kutekeleza. Sasa nataka nikupe mifano michache kama kawaida, nasoma yule ambaye hakupitia aone hali halisi ya Sekta ya Uvuvi. Sisi tunatoka kwenye bahari tunajua umuhimu wa Sekta ya Uvuvi! Kwa nini Serikali hii haioni umuhimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo, hiyo bajeti hiyo tulitegemea iende ikajenge Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko. Hiyo bajeti tulitegemea hiyo ya maendeleo tulitegemea itoe mafunzo itafute masoko, ijenge majengo ya utawala kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza humu ndani kila siku tunaimba, uchumi wa buluu na uchumi wa buluu ni mtambuka kwa sababu unahusu vitu vingi. Kuna utalii ndani yake, kuna ufugaji wa samaki na uvuvi wake na mazao yote yanayoendana humo. Kuna mambo mengi. Bajeti ya maendeleo, Mradi wa Uchumi wa Buluu. Kwanza fedha zenyewe zinazotegemewa za nje. Walitenga shilingi ngapi? Shilingi bilioni 13, mpaka hapa ninapoongea hakuna hata shilingi kumi iliyotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikaa humu tunaimba uchumi wa buluu na kwenye hotuba yake Mheshimiwa Ulega ameandika uchumi wa buluu sehemu nyingi lakini hakuna fedha hata shilingi kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, ilitengewa shilingi ngapi? Shilingi bilioni 50, hapa leo tunapoongea kuna shilingi ngapi ambayo imetoka? Hizo fedha za ndani. Shilingi bilioni 50 imetoka shilingi milioni 426 sawa na 0.9% hata asilimia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nikawa naongea na wenzangu, kwa hiyo, ukijumlisha hizi fedha zote za maendeleo hizi shilingi bilioni 135 kwenye Fungu 64 Uvuvi mpaka sasa hivi fedha iliyotoka nimekwambia shilingi bilioni 135 fedha za maendeleo, mpaka sasa hivi fedha iliyotoka ni shilingi bilioni 6.47 sawa na 4.8%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa asubuhi nilikuwa nawauliza watu kama mambo ndiyo haya, kuna haja ya kukaa hapa kujadili bajeti ambayo haitekelezeki? Tungesema tu kwamba ikifika kwenye mifugo na uvuvi akamalizie kwanza hiyo ya mwaka jana. Akishamaliza ndiyo arudi hapa. Tunakuja kujadili nini kitu ambacho hakitekelezeki? Ndiyo swali langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo kwenye huo ujenzi wa bandari ya uvuvi umetenga shilingi bilioni 50 umetoa shilingi milioni 426. Leo tena kaweka shilingi bilioni 50 zingine, hizi huku hata 1% haijafika. Tunaenda kuipitisha tunaenda kukubaliana ndiyo? Ndiyo hiyo inahusu nini wakati utekelezaji wake hafifu namna hii? Ndiyo swali langu mimi hilo la msingi. Ikibidi naelewa kwamba bajeti yetu sisi ni *cash basis* kwamba tukusanye ndiyo tutumie, naelewa wala sina shida juu ya hilo lakini najiuliza; Serikali haijaona umuhimu wa Sekta ya Uvuvi? Ndiyo swali langu ambalo najiuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nyingine nayokupa, Serikali ilisema itanunua maboti 158 igawe kwa wavuvi. Kule kwetu Mtwara Mheshimiwa Ulega Manispaa ya Mtwara watu mpaka sasa hivi wako kwenye michakato tu. Kuna boti limeenda kule? Halipo, wako kwenye michakato tunapitisha bajeti nyingine ile ya mwanzo haijatekelezwa. Kwa nini Mheshimiwa tunafanyiwa hivi hasa kwenye Sekta hii? Sisi wengine hatuna madini, hatuna nini tunategemea uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu hapa, ombi langu, yale maboti ile michakato ifike mwisho. Vile vikundi wale watu binafsi wapatiwe ili waweze kufanya kazi zao za uvuvi, hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila nikitamani kuongea, kila nikitamani kuongea najikuta ninahuzunika kwa sababu kuna wataalam wengi sana kwenye Sekta ya Uvuvi ambao wangekuwa wanawezeshwa imani yangu tungekuwa tunasonga mbele sana. Wakati anatoa hotuba yake Mheshimiwa hapo kawataja wengine walimu wake, wengine nini lakini wamekaa tu hawatekelezi kwa sababu hawana fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *TAFIRI* hakuna fedha, *FETA* hakuna fedha, ukienda *TAFICO* hakuna fedha lakini wale watu wanalipwa mishahara, wale watu wana *other charges* fedha ambazo wanazitumia kwa matumizi mengine lakini hawafanyi kazi zao kwa sababu hakuna fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali pamoja na kwamba keki ya Taifa inaenda kwenye mambo mengi, wangejitahidi angalau hata isipungue 20%, 30%, 40% lakini unapotoa bajeti 4.8% unategemea wafanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana. Mheshimiwa Ulega wakati unaandika naomba pia uende kwenye mamlaka wakupe fedha utekeleze, kuandika bila vitendo sawa na hakuna kitu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tunza Malapo. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mheshimiwa

Kenneth Nollo na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya hata wananchi kule Ludewa wanaziona na leo wamefurahi kuona kuna Wananchi wa Ludewa walipewa mwaliko wa Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya mikopo ya maboti. Hili ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze pia Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu *Professor* Shemdoe, hongereni sana kwa kazi nzuri. Sisi Ludewa tuna kata nane ambazo zimezunguka Ziwa Nyasa, kuna Kata ya Lumbila, Kilondo, Lifuma, Lupingu, Iwela, Manda na Ruhuhu. Kwa hiyo, kuna idadi kubwa sana ya wananchi ambao ajira yao inategemea maji, inategemea kwenye uvuvi. Kwa hiyo, bajeti hii ni muhimu sana ndiyo maana nimesimama niweze kuwasemea wale wavuvi wa jimboni kwangu na wa maeneo mengine hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisoma ile Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri nimeona amezungumzia mwaka 2021, Sekta ya Mifugo ilikua kwa 5% na kuchangia 7% ya Pato la Taifa. Hii ipo kwenye ukurasa wa 69 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Vilevile ameonesha kwamba Sekta ya Uvuvi kwa mwaka 2022 ilikua kwa 2.5% na ilichangia 1.8% kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Wabunge wenzangu waliozungumzia Sekta hizi mbili kwa maana ya Uvuvi na Mifugo kwamba sekta hizi zinazo nafasi na uwezo mkubwa wa kuchangia zaidi kwenye Pato la Taifa iwapo zile

changamoto ambazo zinaikabili Wizara hii kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameainisha na kamati imeainisha zikafanyiwa kazi na kuongezewa fedha kama ambavyo Wajumbe wengine wamependekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amezungumzia ana upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Hili hata kule Ziwa Nyasa Jimboni kwangu tuna watumishi wawili tu ambao ni wataalamu wa uvuvi katika kata nane. Kwa hiyo kutegemea hapa tutapata tija ni changamoto sana. Kwa hiyo, ningeiomba sana Serikali iweze kuongeza watumishi kwenye Sekta ya Uvuvi ili waende kusimamia tija kule kwa wananchi ambako wanafuga samaki na wanavua kutegemea asili kwenye Ziwa Nyasa na maziwa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia hata vyuo ambavyo vinatoa mfaunzo ya uvuvi ni vichache sana hapa nchini hasa hizi kada za kati. Ukienda pale Sokoine utaona wana kitengo wanafanya vizuri lakini hizi kada za kati wale ndiyo hasa ukimwambia nenda Lumbila ukahudumie wananchi wa kule atakwenda na atafanya kazi yake kwa uaminifu mkubwa. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Serikali kuongeza hizi kozi za kati ngazi ya cheti, ngazi ya *diploma* ili tupate wataalamu wengi zaidi na hii itasaidia sana kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi kwenye Pato la Taifa vilevile kuongeza ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imebainika kwamba Watanzania milioni 4.5 wanategemea Sekta ya Uvuvi. Hii ni idadi kubwa ya Watanzania ambao tunatakiwa tulinde ajira zao kwa nguvu zote. Kwa hiyo, tukiwaongezea wataalam tukawapa vitendeakazi, sekta hii kwa kweli inaweza ikakua kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ambalo ningependa kulizungumzia ambalo Wabunge wengi pia wamezungumzia ni eneo la kuanzisha kwa mamlaka ambayo itasimamia Sekta ya Uvuvi, itasimamia Sekta ya Mifugo. Tukiangalia upande wa maliasili, samaki ni maliasili, misitu ni maliasili. Kwa hiyo, misitu, wanyamapori wana mamlaka ambazo zinasimamia kwa sababu kule kunakuwa na wataalam ambao wao kazi yao wakilala wakiamka wanafanya mambo kwa utaalamu kwa kuzingatia tafiti tukamwacha Mheshimiwa Ulega anahusika na sheria na mambo ya sera. Hii mamlaka sasa ndiyo itasimamia kule kwenye uvuvi kwa sababu samaki nao tumesema ni maliasili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watapewa mafunzo kwa sababu shughuli ya kwenye maji inahitaji ukakamavu kidogo. Kwa hiyo, ni muhimu wakapata pia mafunzo kama ambavyo imefanyika kwenye Sekta ya Misitu. Kwa hiyo, tukiangalia mwaka ule 2009 katika Gazeti la Serikali Na. 135 ilianzisha hiyo Mamlaka ya *TAWA* kwa hiyo nimshauri sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Sekta hii ya Mifugo na yeye nimeona kwenye ukurasa wa 106 wa hotuba yake amezungumzia dhamira yake ya kuanzisha hii mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili ni muhimu sana ambalo Serikali ningeishauri iweze kutoa msukumo wa dhati kuhakikisha mamlaka hii inaanzishwa ili Sekta hii ya Mifugo, Sekta ya Uvuvi iweze kuajiri Watanzania wengi zaidi ambao vijana wetu sahizi wanahangaika ajira lakini vilevile itoe mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa letu. Hii 7% bado tuko chini sana ukizingatia takwimu zinaonesha kwamba nchi yetu ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo barani Afrika. Kwa hiyo, nadhani tulipaswa tunufaike sana na idadi hii kubwa ya mifugo ambayo tunayo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ningependa kushauri Serikali ni eneo la uhifadhi wa mazingira kwenye maziwa yetu haya ili kuweza kuhifadhi maeneo ya kuzalia kwa samaki, mazalia. Kwa sababu wananchi wengi bado wanategemea ule uvuvi wa asili *(nature)*. Kwa hiyo, ningeishauri Serikali kupitia Wizara hii ya Mifugo ishirikiane na Wizara inayohusika na mazingira waweze kuhifadhi vizuri yale mazalia ya samaki kwenye maziwa yetu ili kuweza kufanya samaki wawe wengi zaidi na wakati ule mpango mwingine wa ufugaji wa samaki nao unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo maeneo yote ambayo yanafaa kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwenye vizimba labda kama watatumia njia ya kufuga nchi kavu. Kwa mfano kama Ziwa Nyasa lina mawimbi makali sana kwa hiyo kuna maeneo ambayo yanahitaji Wizara iende ikayafanyie utafiti zaidi iweze kuongeza nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tulisema hizi sheria za uvuvi ndizo zinazosimamia ufugaji wa samaki. Hii ni changamoto kubwa sana, kwa hiyo ningeshauri Serikali iweze kufanyia marekebisho tuwe na Sera, kanuni na sheria zinazosimamia eneo la ufugaji wa samaki kwa sababu utaangalia kuna nyavu ambazo zinatumika kutengeneza vizimba. Ukija kuangalia kwenye Sheria ya Uvuvi ni nyavu haramu. Kwa hiyo, tunakuwa tunajichanganya na hapa nchini hazipatikani kwa hiyo wananchi wanahangaika kwenda kununua nchi jirani kwa njia za magendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunaona hapa kuna umuhimu mkubwa sana kwa Serikali kufanyia kazi hizi kanuni licha ya kuwa walifanyia mabadiliko mwaka 2020 lakini hili eneo sasa la ufugaji wa samaki ni vyema lilkawa na sheria zake mahususi na kanuni zake ikiwezekana na sera yake ambayo itaenda kuangalia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan na Mheshimiwa Shally Raymond wajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kunukuu kupitia Karl Marx na Engels wote wanakubaliana kwamba, naomba kunukuu kwamba *"Despite the capitalist economy, the economic modes of production define the class structure of the society."* Pamoja na kwamba na mfumo wa kibepari lakini mfumo uliopo wa kiuchumi katika jamii fulani unatoa madaraja ya jamii ile kwamba namna gani ilivyokaa katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika nchi yetu tukiweza kuwapanga wafugaji kwenye mfumo wetu wa uzalishaji na mfumo wetu wa uchumi, wafugaji ndiyo wanaotokana katika daraja la mwisho zaidi la uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua kigezo kwamba mfugaji hakopesheki kwenye mabenki na tukianza na wafanyabiashara wakubwa wenye viwanda wanakopesheka kwenye mabenki. Wafanyabiashara wa kawaida wachuuzi wanakopesheka kwenye mabenki lakini siku hizi tumeweka na wajasiriamali na wamachinga humo humo wanakopesheka kwa kiasi fulani kwenye mabenki. Wanakuja wakulima wanakopesheka kwenye mabenki lakini mtu ambaye hakopesheki kwa sababu ya kutokuwa na anwani ni mfugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba tu lakini ni namna gani sisi wenyewe tumemtengenezea mfugaji asiaminike, mfugaji asikopesheke na mfugaji asiwe na anwani. Nataka kusema kwamba nchi yetu tuna mifugo mingi na tuna wafugaji wengi lakini kwenye uzalishaji bado hatambulilki katika mfumo wa kiuzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Serikali ilikuja na utaratibu wa utambuzi wa mifugo ile inaitwa *Ear tag Electronic System.* Mfumo huu umefanikiwa sana katika Nchi ya Botswana kwamba mifugo inavyozaliwa baada ya miezi mitatu anapewa *electronic tag* na ile *electronic tag* inakuwa na habari mbalimbali. Aina ya mifugo, inamilikiwa na nani lakini vilevile kwa ajili ya kupata dawa, *traceability* na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosababisha wafugaji wetu wasiweze kukopesheka ataenda benki anataka kukopa lakini benki wanataka wajue ana mifugo kiasi gani? Sasa mifugo kiasi gani ni lazima kuwe na mfumo ambao unatambua kwamba ana mifugo kiasi gani ambayo imethibitishwa na mfumo halali. Sasa mfugaji huyu akienda kutaka kukopa baada ya siku mbili, tatu anahama kutoka Shinyanga… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuzungumze kwa taratibu ili wachangiaji wasikike vizuri.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anahama kutoka Shinyanga anaenda Mtwara kwa hiyo hata benki haiwezi kumkopesha. Kwa hiyo, nilichotaka kusema ni kwamba Serikali mfumo huu ni lazima kama ilivyousitisha iurejeshe. Jambo la msingi Serikali iongeze ruzuku kwenye zoezi ili kwamba wafugaji wetu waweze kusajili mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni zuri kwamba Serikali itakuwa inapata mapato kwa sababu mfugaji anavyoenda kuuza inawezekana kukawa kuna namna gani anaweza kuchangia katika kulipia ushuru mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, jambo hili limezungumzwa kwamba katika mwaka 2025 kutakuwa na utambuzi wa mifugo. Kwa hiyo, jambo hili lipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kwa dhati niipongeze Wizara ya Mifugo. Wizara hii imekuwa haipati fedha za kutosha. Bajeti ya mwaka huu ina bilioni 290 tu, ambayo ni kidogo sana. Ukienda Taasisi ya Utafiti wa Mifugo TALIRI ina fedha haizidi bilioni moja; yaani taasisi ya kufanya utafiti wa mifugo haipati fedha, hata bilioni moja haifiki. Kwa hiyo naomba Serikali iangalie sana, kwamba sekta hii ya mifugo iweze kutoa fedha. Na nataka niipongeze Wizara hii, imefanya kazi kubwa ambazo pamoja na kupata hela kidogo lakini wameonesha uwezo mkubwa wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kinachowaangusha wafugaji wetu ni kwamba maeneo ya malisho hayajapimwa, na tukiri kwamba Wizara ya Ardhi ina sura ya Wizara ya migogoro ya ardhi, si Wizara ya kupima maeneo. Sasa kama inawezekana itengenezwe mamlaka kwa ajili ya upimaji wa maeneo ya mifugo, mamlaka ambayo itashirikisha kati ya Wizara ya Mifugo na Wizara ya Ardhi ili kwamba wafugaji wetu waweze kupimiwa maeneo na waweze kuweza kulisha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie jambo hili limeshuka hata maeneo yetu tunayokaa; wafugaji wanaishi kwa kutangatanga. Njia ya wafugaji kiasili zilikuwepo tangu zamani, siku hizi watu wanaamua kulima hata njia za wafugaji, tunaita mapalio, hamna mapalio sasa, kwa hiyo mfugaji anaishi kwa kutangatanga, naomba jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusu suala la majosho na maji, mabwawa, malambo, jambo hili nalo liangaliwe. Mimi Kata yangu ya Chifutuka ina ng'ombe zaidi ya 2,500 lakini hakuna sehemu ambapo mifugo inaenda kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea sekta hii lakini hii ni sekta ambayo kwa kiasi kikubwa tumeitelekeza. Bado tunachukulia kwamba mfugaji ni mtu ambaye yuko kienyeji na Serikali bado haijaangalia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, kwanza kwa kuanza kiufufua *Ranch* ya Kongwa na mwaka jana kulikuwa na tatizo la kutaka kuibadilisha ranchi yawe mashamba ya alizeti. Kwa vitendo amefanya, amepeleka matrekta matano, amepeleka ng'ombe 1000 kwa hiyo huko ndiko tunakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri na nataka niseme nchi yetu ina utajiri mkubwa wa mifugo, masoko yameshafunguka sasa, kama vile Saudi Arabia, Vietnam na kwingineko, tutumie fursa hii. Ng'ombe wa Tanzania walikuwa hawauziki kwa sababu hatuna *traceability,* kwamba huyu ng'ombe ametibiwa haijulikani, na ndiyo maana wenzetu wanaangalia namna gani nyama

yetu inavyokuwa. Kwa hiyo tayari tuko katika nafasi nzuri kuendelee kuipatia fedha Wizara hii ili iweze kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu migororo ya wafugaji na hifadhi zetu. Mimi wiki iliyopita ng'ombe 191 walikamatwa wameingia kwenye hifadhi, na bahati mbaya walivyokamatwa inatakiwa ng'ombe mmoja alipiwe laki moja. Sasa utaona kiasi gani mkulima huyu mfugaji anaweza kutoa. Lakini chanzo cha kwenda kwenye hifadhi ni nini? chanzo cha kwenda kwenye hifadhi ni kutafuta malisho. Kwa hiyo Serikali iangalie, kama nilivyosema mwanzo, namna gani inaweza kudhibiti tatizo hili la wafugaji kupeleka ng'ombe kwenye hifadhi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kenneth Nollo. Nilimtaja Mhehimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimia Daimu Mpakate ajiandae.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kabla ya kutoa mchango wangu niitumie fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mama Samia

Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuendelea kuiletea maendeleo Tanzania wananchi wa Zanzibar hawa wa Jimbo la Chakechake, tunaona jitihada na nguvu wanazozitumia kwenye kuiletea maendeleo Taifa hili. napongeza pia jinsi anavyoshirikiana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi kwenye kuisaidia Zanzibar kusogea kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mchango kwenye jambo moja tu. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri alivyokuwa akisoma leo hapa, na ukisoma kwenye kishikwambi, kuna ongezeko kubwa sana la idadi ya mifugo kutoka mwaka jana hadi mwaka huu. Kwa mfano kwenye ng'ombe tumetoka milioni 35.3 mpaka milioni 36.6. Kwenye mbuzi tumetoka milioni 25.6 mpaka milioni 26.6, kwenye kondoo tumetoka milioni nane mpaka milioni tisa, kwenye kuku tumetoka miliono 92 mpaka milioni 97. Ukuaji wa sekta umeongezeka kwa asilimia tano, lakini cha kusikitisha moja katika eneo ambalo halifanyi vizuri kwenye kukua na kuongezea Pato la Taifa *(GDP)* ni eneo hili la sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *National Bureau of Statistics of Tanzania (NBS)*, *statistics* zinaonyesha tangu mwaka 2019 *GDP* haijaongezeka kupitia sekta ya mifugo, yaani sekta ya mifugo haijaongeza tija katika kuongeza *growth development product* yatu. Kwa hiyo hili ni jambo ambalo Wizara wanatakiwa walichukue kwa uzito na kuona ni jinsi gani sekta italeta maendeleo kwenye kukuza uchumi na kukuza *GDP* yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamechangia hapa, Mheshimiwa Kamonga ametoka kusema hapa, kwamba Tanzania ni nchi ya tatu kwa idadi ya mifugo barani Afrika. Zipo nchi tunazipita kwa idadi ya mifugo, lakini hizo nchi zinafanya vizuri zaidi yetu kwenye uuzaji wa bidhaa za

mifugo, hasa nyama kwenye soko la kimataifa. Kwa mfano *South Africa* ambao hawapo hata *top tena* wanauza kwa dola za Kimarekani milioni 89.2 kwa mwaka, sisi ni dola milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sudan wenye idadi ya takriban mifugo milioni 31 tu ambao sisi tunawapita kiujumla, wanauza kwenye soko la dunia takriban Dola za Kimarekani milioni 51, kwenye idara moja tu ya nyama. Misri ambayo nayo haipo hata kwenye *top ten* tunalingana kwenye uuzaji wa bidhaa za mifugo kwenye soko la kimataifa, hii ni kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa. Sasa kinachosikistisha, kuna watu tunawapita kwa idadi ya mifugo lakini wanapofika kwenye soko la kimataifa wao ndio wanatuongoza na wanajipatia fedha nyingi zaidi ya sisi, tunakosea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya ambao ni majirani zetu wao wana kuku karibia milioni 21 tu tunawapita mara nne ya idadi ya kuku wetu takriban milioni 92, lakini wao pato lao wanafika Dola za Kimarekani milioni 71 zinazoingia kupitia mauzo tu ya kuku. Sasa kuna mahali tunakosea kama Taifa, kwa hiyo ndio hapo napotaka sasa Wizara watusikilize na wachukue ushauri wetu wakaufanyie kazi kwa ajili ya kutaka kuboresha sekta hii itusaidie kwenye kukuza uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi moja ya jambo lililoahidiwa kwenye sekta hii ni kwamba tutabainisha na kutenga maeneo ya ufugaji kwa kuyatambua na kuyapima, kuyasajili na kuyamilikisha ili kuongeza maeneo yaliyotengwa kutoka hekta milioni mbili na laki saba hadi hekta milioni sita. Moja kati ya mwarobaini wa kukuza pato letu kupitia sekta hii ya ufugaji ni kuwa maeneo tengefu kwa ajili ya ufugaji. Tumeshaingia kwenye migogoro mingi kwa miaka mingi, tumeona ufugaji wa

kuhamahama hauna tija. Ilani imetuelekeza tuyatenge maeneo maalum, tuyaweke tuyarasimishe, tuyapime na tuwape wafugaji wetu wapime, tuwawekee miundombinu mizuri tuwape maji ili waongeze tija kwenye uzalishaji wa bidhaa za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafeli tunapokwenda kuliendea soko la kimataifa kwenye bidhaa zetu za mifugo. Kuna kitu amekisema hapa mchangiaji aliyepita, kwamba tumeshindwa kuwa-*label* na kuwa-*trace* wanyama wetu. Soko la kimataifa linataka uwajue wanyama wako tangu walivyozaliwa, umri wao wanavyokuwa, wanachokula, ukienda uwe na hizo kanzidata za kutosha kwenye soko la kimataifa unapokwenda kuuza hizo bidhaa. Sasa zote hizo hatuna, hatuzijui, kwa hiyo inafanya *quality* ya bidhaa zetu iwe ndogo na hivyo kufanya *competition* ya kwenye soko la kimataifa pia nayo iwe ndogo. Kwa hiyo moja katika maeneo ninayoishauri Wizara ni kuongeza tija kwenye kufanya hiyo kwa ajili ya kusaidia ubora wa nyama inayotoka Tanzania ilii iwe juu na hivyo soko la kimataifa tuweze kuliendea kwa usahihi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio mchango wangu naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhan Suleiman. Nilimtaja Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Yustina Rai ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana; kipekee namshukuru Mungu kwa upendeleo wa zawadi ya pumzi ya uhai ndiyo maana tuko hapa na tunajadili jambo hili kubwa. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lake la hotuba nzuri na iliyoeleweka; na niseme kwamba mengine ya mwaka jana

pia akiwa kama Naibu Waziri yalitekelezeka, kwa hiyo naipongeza sana Wizara hii kwa ujumla, yeye na timu yake ya Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu mwaka huu tufanye zaidi Mheshimiwa Waziri kwa sababu mifugo ni afya, mifugo ni kilimo, mifugo ni lishe, mifugo ni biashara, mifugo ni utalii, mifugo ni usafiri, wakiwepo punda wanaosaidia usafiri, lakini mifugo ni ulinzi; yaani mifugo ni kila kitu, ni Wizara mtambuka. Zaidi sana ni kama walivyotuambia asubuhi, mifugo ni utajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namwambia Waziri wetu kwamba utajiri huu haujawa sasa na uwiano. Kwamba wanaofuga katika kiwango kikubwa watajirike na wale wanaofuga kidogo kule nyumbani watajirike. Mimi natoka hapa hapa kwenye ufugaji mkubwa na kwenda kwenye ile hoja yangu ya kila mtu afuge na ikiwezekana afuge angalau hata kuku wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiamka nyumbani hata kama una hiyo saa yako ya kuweka *alarm* lakini kabla ya *alarm* haijalia jogoo ameshawika. Kwa hiyo, unaona ni jinsi gani kuku walivyo muhimu kwetu Watanzania, asubuhi tunaamshwa na jogoo. Lakini jogoo huyo wa kienyeji tunaambiwa amekuja ameboreshwa; kuna wale majogoo wa *kuroiler* nao sijui kama wanajua kuwika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeleta kilio kutoka mkoani kwangu. Tangu wameniona Bunge hili wanawake wa Tanzania wananiona nikiomba vifaranga vya kuku ili kila Mtanzania afuge, lakini jambo hili halijaweza kutekelezwa kiuhakika. Mwaka jana Wizara hii ya Mifugo iliweza kupeleka Kilimanjaro kwenye vikundi saba tu na mashamba darasa mawili. Sasa ile ni kitu kidogo mno. Ninaomba kwa upendeleo

mwaka huu twende tupeleke mifugo hii, kila nyumba iwe na kuku. Nilishawaomba sana, ikiwezekana hata tugawe hivi vifaranga kwenye shule za *primary* maana kuku wa kienyeji hawana gharama, wanachakua tu wanajilisha wenyewe. Sasa kwa nini nyie Wizara ya Mifugo msisaidie wanawake wa Kilimanjaro kufuga? Naomba nipate jibu la sivyo hatujafika kushika vifungu na baba Tulia sitaki mimi kukushikia kifungu nakuheshimu sana. Naomba wanawake wa Kilimanjaro wapelekewe vifaranga wafuge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna hela zile ambazo sasa hivi zimesitishwa 4:4:2. Hapa leo tunalia mifugo haikupewa fedha za kutosha, hata mimi nawaombea, na tena niseme rasmi naunga mkono hoja na nataka mpate fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ikiwezekana, badala ya kuwapa wale wanawake, vijana na wenye ulemevu 4:4:2 tuwape miradi, na miradi hiyo si mingine ila miradi inayotokana kwenye Wizara ya Mifugo. Muongee na TAMISEMI mwende kwenye halmashauri, marejesho yatakuwa mazuri, kuliko sasa hivi tumesimama, hamna kinachoendelea, tunangoja sera itengenezwe ilhali hela haikusubiri inazidi kupungua thamani. Naomba sana Wizara ya Mifugo izungumze na TAMISEMI, mtakubaliana tu, hizo hela zitumike tuletewe Tanzania nzima wanawake, vijana na wenye ulemavu tupatiwe miradi, si ya kuku tu tunaweza pia tukapatiwa miradi ya ng’ombe, mbuzi wa maziwa, miradi ya kondoo mpaka ya nguruwe mmesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nilikuwa naiomba sana wizara hii ishirikiane pia na watu binafsi. Kuna mashamba ambayo yanalelewa labda na *mission*. Kuna wanaozalisha vifaranga lakini pia kuna watu binafsi wanaofuga. Leo tumewaona pale, na nikushukuru sana

Mheshimiwa Waziri, tumepata shule kweli kweli, pale nje tumepata darasa, tukaoneshwa jinsi gani *ASAS* anafanya vitu vyake. Kuna shule ambazo anazilea kwa maziwa yale ya ruzuku, anawapa tu; shule zile vijana wale wana afya nzuri kuliko hata wale wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumejifunza, kwamba kuna magonjwa ambayo kama maziwa hayajapitiwa kiwandani, yakafanyiwa *treatment* yanaleta magonjwa yanayoambukiza. Kuna ugonjwa wa *brucellosis* ambao sasa kama ng'ombe yule alikuwa inatupa mimba na mama pia akinywa na yeye pia anapata uharibifu wa kile kiumbe ndani yake, lakini kama maziwa hayo yamepitishwa kiwandani inakuwa salama. Ila tatizo lililo Tanzania ni asilimia tatu tu ya maziwa yanayozalishwa rasmi ambayo yanapita kiwanda, mengine yote 97 hayako rasmi. Matokeo yake unakuta hata Serikali inapoteza mapato. Sasa shida iko kwenye Wizara ya Mifugo, vile vituo vya kuokota maziwa sasa vya kukusanyia maziwa, ambavyo vimesambazwa bado ni vichache sana. Vinahitajika 770 lakini mpaka sasa hivi ni theluthi moja tu vimepatikana. Hapo mnatuambia nini Wizara ya Mifugo Tanzania nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wangetaka maziwa yao yafike kwenye vituo ambavyo vinaweza vika-*process*. Kule Kilimanjaro wafugaji wote wa ng'ombe wangependa maziwa yao yaende Nronga au yaende pale Kalali, lakini haiwezekani. Tunaomba mtujengee hivyo vituo ili maziwa hayo yaweze kupitia kwenye hiyo *process,* maziwa yawe salama na sisi pia tuweze kuwa na maziwa mazuri kila mahali, watoto wanywe maziwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeona sasa hivi tunazungumza tatizo la watoto kuwa na tabia zisizoeleweka ni pamoja na lishe ambayo haieleweki. Lishe ambayo

haijawa katika hali nzuri haiwawezeshi kabisa vijana kuwa vizuri, watakuwa *hipper* tu; na tutapiga sana kelele hapa lakini mtaona kwamba haiwezekani mpaka ninyi Serikali mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko viwanda vingi vya maziwa ambavyo tunatumia maziwa yake nchini, lakini pia ukienda *super market* unakuta kwamba maziwa mengine pia ni *imported.* Ukiangalia uwiano wa maziwa ambayo sisi tume-*import* na tulio-*export* mengi sisi tumeleta. Wizara hii sasa iangalie, kama tumesafirisha lita 200,000 lakini tukaleta lita milioni 1.6 hapo kuna shida. Ninaomba Wizara na wale watafiti waliofanya kazi ya utafiti waone ni jinsi gani tunakwenda kuboresha mifugo yetu ili tuweze ku-*export* zaidi tuweze kupata hela za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na niseme wazi mwananchi wa kawaida au mfugaji wa kawaida tu hawezi kununua mtamba wa Tanzania. Niiombe Serikali hii yenye usikivu sana, chini ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan afikirie kuona upendeleo kwa wafugaji ambao ni *zero grazing,* wao mifugo yao haitoki nje, maana yake hata haya madume yaliyoletwa, tumeambiwa yatakwenda *ranch*. Mengine yatakwenda kwa wale waliojengewa vituo, lakini wale wanaofuga ndani ikiwemo Mkoa wa Kilimanjaro, sijaona hiyo *allocation* ya haya madume bora. Hii inanikumbusha na namkumbuka Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa nasikia machozi, nasikia uchungu, alileta madume yaliyofanya *cross breeding* yalikuwepo madume ya *Friesian*, yalikuwepo madume ya Boran, yalikuwepo madume ya aina nyingi na sasa yanaishia na kila siku maswali nimeuliza hapa ndani, lakini sioni wakiitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona wenzetu majirani wameendelea kuboresha na kuboresha vizazi vya ng'ombe

na kuboresha maziwa. Tanzania tuna shida gani? Shida iko wapi? Tuna shule vijana wetu wanasoma vizuri sana. Wanasoma *SUA*, wanasoma shule nyingine, lakini mapokeo ni kidogo. Niombe sana hii Wizara inayoongozwa na vijana hawa, yuko Mheshimiwa Waziri, yuko Naibu Waziri, wachapakazi, wazuri, sina wasiwasi nao, timu ya Katibu Mkuu iko vizuri lakini pia…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Naomba niliyosema wanisikie na naunga hoja mkono. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mheshimiwa Yustina Rahhi na Mheshimiwa Zacharia Issaay wajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala* aliyeniwezesha kusimama na kuweza kuongea mbele ya umati huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha Wizara hii ya Mifugo kuwa na bajeti nzuri ambayo inaleta matumaini. Naungana na Taarifa ya Kamati, mashaka yao juu ya utekelezaji wa yale yote waliyoandika kutokana na utekelezaji wa mwaka uliopita ambao unaishia sasa ambapo kwenye Miradi ya Maendeleo mpaka sasa umefika asilimia

58, lakini sina mashaka Waziri wa Fedha yupo, Watalam wake wanasikia, wataisaidia hii Wizara kufikisha malengo yale ambayo yamekusudiwa ili jopo la wasomi waliopo kwenye Wizara hii waweze kufikisha kwa wananchi tunaowatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini katika Wizara ambayo najua ni muhimu sana ambazo zina wasomi wengi Maprofesa, Madaktari leo wameonesha umahiri wao kwa kuleta bajeti nzuri ambayo inahitaji fedha tu kutekeleza ili uvuvi na mifugo ianze kupiga kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitaongea jambo moja tu, jambo hili ni suala la mifugo. Tunduru Mwaka, 2008 tulianza kupokea mifugo kutokana na Serikali kuwahamisha wafugaji kutoka Bonde la Ihefu. Wengi walikuwa wanapita njia wanaenda Mkoa wa Pwani na wanaenda Mkoa wa Lindi. Kilichojitokeza wafugaji wengi walibaki katika maeneo ya Namtumbo, walibaki katika maeneo ya Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Tunduru walivyokuwa waungwana kwa kuona tatizo lipo mwaka 2017/2018 walitenga maeneo ya vitalu. Vitalu ambavyo vilitengwa vilikuwa jumla 279 ambavyo kila kitalu kimoja kilikuwa na hekari 500 kwa jinsi watu wa Tunduru walivyokuwa na uungwana na kuwapenda wafugaji wenzao, wakaruhusu vitalu hivyo vitengwe katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyojitokeza baada ya makubaliano na wafugaji hao na mfahamu kwamba Mkoa wa Ruvuma ni Mkoa wa Kilimo, kwa hiyo Mkuu wa Wilaya ya Tunduru kutoa eneo kwa ajili ya wafugaji ilikuwa ni uungwana ili nao wenzetu waende kuishi vizuri kama wengine. Kilichojitokeza katika vitalu vile tulikubaliana

na wafugaji kwamba kila kitalu kimoja watalipia laki moja na nusu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea kupata milioni 41 katika vitalu vile kwa mwaka, lakini mwaka wa kwanza vitalu vile vilitoa milioni 15, mwaka wa pili vikatoa milioni tisa, mwaka wa tatu ikatoa milioni sita. Mwaka, 2021/2022 ambapo sasa vurugu za wafugaji kuvamia maeneo ya wakulima ikawa kubwa, basi ili mshike mshike ya kuwarudisha wenzetu kwenye maeneo yao tumefanikiwa kukusanya milioni 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ya hivi vitalu au wafugaji kutokwenda yamekuwa ni makubwa sana katika Halmashauri yetu ya Tunduru, migogoro ya wafugaji na wakulima imekuwa ni mikubwa. Watu wanakufa kwa ajili ya kugombana, mazao ya wananchi yanaliwa na hawa wafugaji. Pamoja na yote na jitihada nzuri za wenzetu wale wa Tunduru kutoa maeneo yale kwa hiyari na kwa makubaliano, lakini bado wale wafugaji wameendelea kukaa maeneo ambayo siyo rasmi ambayo yamesababisha migogoro na wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya madhara yake, maeneo makubwa ya Wilaya ya Tunduru sasa yamegeuka jangwa. Ukienda Jimbo la Tunduru Kusini mpakani mwa Ruvuma mwote, sasa hakuna kilimo kinachoendelea na awali nimesema Wilaya ya Tunduru ni eneo la kilimo. Kwa hiyo naiomba Serikali, mgogoro huu kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Madiwani walikubaliana kufuta vitalu hivi kutokana na yale matarajio yao ya kupanga vile vitalu, faida yake haikupatikana. Moja, fedha hazikuweza kupatikana ndani ya miaka hiyo mitano tumekusanya milioni 54 tu kati ya milioni 109 ambazo zilitarajiwa kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wafugaji hawa sasa wamesambaa kwenye mashamba ya watu, migogoro imekuwa ni mikubwa, wengine wameenda mpaka maeneo ya hifadhi ambayo sasa wamelazimisha tembo kurudi kwenye maeneo ya makazi ya watu na kusababisha majanga makubwa kwenye mazao ya wakulima hata vifo kwa baadhi ya maeneo ya watu. Juzi tu Waziri wa Maliasili nilimweleza kwenye eneo langu amekufa mtu mmoja kwa ajili ya tembo, lakini changamoto kubwa maeneo ambayo tembo ndiyo anapaswa kukaa basi wako wale ngo'ombe wanakaa kule, matokeo yake sasa wanasababisha madhara hayo tembo kuja kudhuru maeneo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali, jambo hili liliwekwa kwa nia nzuri, halmashauri iliamua kutenga maeneo ili isaidie wafugaji wetu wakae, hawataki kukaa kwenye maeneo ambayo wananchi na Serikali imewatengea. Kwa hiyo tunaomba sana Serikali ilichukulie hili, Serikali Kuu na namwomba Waziri nilimwambia mara chungu nzima, naomba safari huu tufuatane mguu kwa mguu, akasikilize kero hizi za ng'ombe kwa wakulima, wafugaji wenyewe pamoja na Baraza la Madiwani ambao waliamua kwa hiyari na kwa azimio kufuta vitalu vile kwa sababu havina msaada wowote, wafugaji wale wote hawapo kwenye maeneo yale yaliyokusudiwa. Pia ile faida iliyotakiwa ipatikane kutokana na ada kwenye vitalu vile haipo, ndani ya miaka mitano tumekosa milioni 154 ambazo zingeweza kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la mifugo naomba, tumezungumza hapa suala la wafanyakazi. Jimbo la Tunduru Kusini zina kata 15, ni kata mbili tu zina watalam, halmashauri nzima ina kata 39, tuna Maafisa Ugani upande wa mifugo 14, watatu wako pale halmashauri, wawili wako kusini na wengine waliobaki wako kaskakazini. Sasa naomba

hili ufanisi mzuri uonekane kwenye kazi hii ya mifugo, basi tuongeze idadi ya Maafisa Ugani kwenye maeneo mbalimbali ya kata zetu ambao watasaidia kuwapa msaada hao wafugaji wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hawana vitendea kazi. Nashukuru kwenye Hotuba ya Waziri ameongea vizuri kwamba watanunua pikipiki kuwawezesha, lakini siyo pikipiki. Tunduru ni kubwa eneo lake linazidi Mkoa wa Mtwara. Kwa hiyo kumpa Afisa Ugani pikipiki atoke Tunduru Mjini amfuate mkulima zaidi ya kilomita mia ni adhabu kubwa, hasa unaposema Afisa Ugani wa Wilaya. Naomba Waziri ajitahidi kwenye bajeti yake kama hakupanga basi atuchomekee hata angalau kigari moja kisaidie kutoa huduma kwenye maeneo mbalimbali pamoja na hizo pikipiki ambazo zitawasaidia Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti, nimeona Waziri ametenga maeneo kwa ajili ya mashamba darasa mia moja. Tunduru tuna shamba pale Masonya, tuna shamba Mowesi, Shamba la Masonya lina zaidi ya ekari 3,200, linafaa kabisa kuweka shamba darasa. Tunaomba katika mpango wa Waziri, basi aliangalie kwa huruma shamba hili, liko *idle,* mkulima na mfugaji mmoja ana ng'ombe wasiozidi 2,500 tuseme, yuko pale, liko *idle* kwa hiyo linaweza kufaa kuwa shamba darasa, likawasaidie wakulima wadogo wadogo ambao wako ndani ya Wilaya ya Tunduru ili waweze kujifunza. *(MakofI)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nanaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na wachangiaji wanaofuata, naomba niwatangaze wageni ambao wametutembelea jioni hii hapa Bungeni, ambao wageni hao ni wawakilishi wa wadau kutoka Sekta Binafsi ya Mifugo na Uvuvi ambao wanaratibiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Karibuni sana wawakilishi wote ambao ni wadau kutoa Sekta Binafsi hapa nchini, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Yustina Rahhi, Mheshimiwa Zacharia Issaay na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo wajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo. Napongeza kazi kubwa iliyofanyika na Wizara hii, wametuletea bajeti nzuri na kutuonyesha maeneo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kama kuna maeneo Tanzania hatutajutia kuwekeza maeneo yenye *risk* ndogo, basi ni Sekta ya Mifugo. Ukiwekeza katika Sekta ya Mifugo siku zote ujue kwamba *risk* ni ndogo unaenda kuwekeza na unapata faida ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa mfano, tukanunua meli tukafanya Uvuvi wa Bahari Kuu, si tunanunua, tunavua, tuna-*export* Samaki, tunapata kipato au tukaamua kunenepesha mifugo, tunanenepesha tunawauza tunapata fedha. Kwa hiyo Sekta ya Mifugo ni sekta ya kuleta uchumi, lakini ni sekta ambayo tukiwekeza hatutajutia. Mheshimiwa Waziri ametuonyesha maeneo ya kuwekeza katika sekta hii ili kuweza kuleta mapinduzi makubwa katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji *transformation* katika Sekta hii ya Mifugo, lakini sasa sijui kwa nini anafanya vidogo vidogo, pengine na bajeti hii ni ndogo, maana na bajeti ametengewa bilioni 295.9. Kwa mfano, ameeleza kabisa kwamba, tija ni ndogo kutokana na mifugo. Tunaona kwamba pato la Taifa bado limebaki kuwa kwa asilimia saba na sekta inakua kwa asilimia kidogo na tija ni ndogo, tumeona sababu mbalimbali, lakini mojawapo ni hili la kwamba aina ya mifugo yetu tuliyonayo hata tungefanya nini bado watakuja na tija ndogo. Aina ya mifugo tuliyonayo ambayo ni mbari za mifugo na kosafu. Kila siku nazisema, hata ungemlisha ng'ombe wa kienyeji namna gani, bado utakamua nusu lita mpaka lita mbili ya maziwa. Tunahitaji kubadilisha aina hii ya kosafu za mifugo yetu, hata ukimlisha namna gani ng'ombe huyu wa kienyeji ataishia kwenye kilo mia, mia na hamsini hazidi mia mbili, hata huwezi kumchagua kwenda kunenepesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona mpango wa Waziri hapa ni kufanya uhamilishaji katika kubadilisha kosafu za mifugo, lakini analenga mifugo laki moja tu, sasa najaribu kuona kwa nini laki moja tu? Laki moja ni kidogo sana, tena na anataka kufanya katika mikoa 26 ya Tanzania. Ukilinganisha na mifugo tuliyonayo milioni 36, laki moja ni wachache na *trend* ya uhamilishaji naona inazidi kushuka, sijaelewa ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu imeonesha kwenye jedwali la Waziri mwaka 2019/2020 alihamilisha mifugo elfu sitini na saba na pointi. Mwaka 2021 alihamilisha ng'ombe 77, lakini mwaka uliopita alihamilisha ng'ombe 60,600. Sasa *trend* ya Waziri inazidi kushuka. Nafikiri kuliko kutawanya hizi nguvu ndogo katika mikoa yote 26, ni kwa nini wasifanye kampeni, akafanya uhamilishwaji kwenye mikoa miwili au mitatu wakaboresha mifugo ya pale, kwa

sababu kuboresha mifugo ni kumbadilisha mfugaji kwenye mitazamo yake. Tukambadilisha mfugaji akaona ubora na wafugaji wenyewe wataazimana, akiona sehemu ambayo mifugo imekuwa bora, wataazimana mbegu, wataazimana madume. Kwa hiyo hili ni muhimu sana na hii ni pointi ya kuleta *transformation* katika ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tu kwamba mifugo imeongezeka, kuna mmoja amesema mifugo ni kero, mimi sitaki kusema mifugo ni kero. Mifugo ni benki kwa wafugaji, lakini tujue tu kwamba Tanzania ardhi yetu ni ile ile tuliyopewa na Mungu na sisi tunaongezeka na nyanda za malisho haya ndiyo hizi hizi kila siku zinasogezwa zinakuwa maeneo ya kilimo, ndiyo hizi tunaendeleza maeneo ya makazi na zinazidi kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukisema tu kwamba tuko *proud* pengine na mifugo kuongeza ni nzuri na nakubaliana, lakini bado haijawa mifugo yenye tija na sababu ndiyo hizi hizi. Kwa hiyo kuwabadilisha mitazamo wafugaji ni muhimu, wanatakiwa kuona kwamba watoke kwenye mifugo hii ya kienyeji ambacho kipato chake ni kidogo, waende kwenye dume ambalo wataliona ni zaidi ya kilo mia nne au mia sita kama wanavyoweza kuiona Nane Nane ndiyo watabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *efforts* ziongezwe kwenye uhamilishaji kubadilisha kosafu za mifugo, hili ni muhimu sana na nalirudia, lakini pia Waziri ameeleza kwamba atanunua madume 200, sasa madume 200 ni wachache sana. Haya madume 200 kama atagawa tena kwenye mikoa 26, ina maana kila mkoa utaenda na madume saba saba. Hata kama ni Manyara ina maana kila Mbunge ataondoka na dume moja, sasa kweli mpaka hii mbegu ienee ni leo? Hawa wafugaji wakiweza kuwaelekeza

ni wapi madume bora wanapatikana na wakawapelekea watakuwa tayari wao wenyewe kuwanunua *at least* kubadilisha. Pia nimeona kwamba Waziri anaongeza mitamba 1,200, nami natamani Mradi wa Ng'ombe wa Maziwa ungewasaidia sana akinamama waweze kusambazwa, wauze maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenyewe umetoa kibali cha kuingiza maziwa kwa kipindi kilichopita lita milioni 11.6 kwa fedha za Kitanzania bilioni 22. Hii inaonyesha kabisa tu kwamba uzalishaji wa maziwa katika nchi yetu ni mdogo na ndiyo maana tuna-*import* maziwa, ya kwetu yenyewe hayatoshi kwenye viwanda vya usindikaji, lakini tuna fursa kubwa sana ya kuzalisha maziwa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mtanzania unatakiwa unywe maziwa hata lita 200 kwa mwaka, lakini tunakunywa chini ya kiwango na watoto wetu wanapata udumavu, ujue Tanzania nayo iko kwenye orodha ya udumavu. Tunapaswa kuongeza uzalishaji kwa kuleta madume bora, mitamba bora, lakini pia kwa kufanya uhamilishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kwamba changamoto nyingine iliyoko kwenye mifugo ni hii ya magonjwa. Magonjwa ni mojawapo ya sababu inayorudisha nyuma Sekta hii ya Mifugo. Tunashindwa kuuza mifugo yetu nje kwa sababu wanahitaji kujua *background,* hii mifugo iliwahi kuugua labda magonjwa ya mdomo na miguu *(FMD)* na vitu vingine. Mifugo inayoumwa siku zote *quality* yake ni ndogo, nyama yake ni ndogo, maziwa yake ni kidogo. Sasa inatakiwa kukomesha kabisa au kupunguza magonjwa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kabisa tu kwamba wataalam hatuna. Kwa mfano, kwenye wilaya nzima hatuna Madaktari wa Mifugo, wale wa *veterinary per se,* kuna kada za mifugo huko ziko za *Animal Production, Range Management* na zingine, lakini hawa wa *veterinary* hawapo. Ndiyo maana wafugaji wetu siku zote wanapata shida. Nimeona wafugaji wakihangaika kutibu mifugo yao wenyewe, yaani kwa ugonjwa mmoja mfugaji anatumia uzoefu wake, atatumia aina tatu za dawa, atanunua *oxytetracycline (OTC), penicillin,* sijui *gentamicin* zote anakwenda kumdunga ng'ombe mmoja kwa dozi anayoijua kwa sababu hana sehemu ya kupata utaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeua *Veterinary Centers,* hata kama haiwezekana kwenye kata, hizi *Veterinary* Centers ziwepo basi kwenye halmashauri ili tuweze kuchunguza magonjwa hasa ya mlipuko. Ugonjwa wa mlipuko ukitokea katika halmashauri mpaka *sample* ipelekwe mkoani na ilete majibu ndiyo ianze kushughulikiwa, hebu tuboreshe kwa sababu tatizo limekuwa kubwa. Kwa sababu wataalam hawa ni wachache kwa nini Wizara sasa isifikirie kuwafundisha ma-*para professional* wengine kwa kila kijiji ili waendelee kusaidia wafugaji, wasiendelee kuhangaika na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili la majosho ili kuweza kupunguza magonjwa ya mifugo. Nampongeza ameweza kujenga majosho ya kutosha na kuwa na majosho ni jambo jema, naomba aongeze majosho kwa sababu ng'ombe hawatakiwi kutembea mbali na maeneo yote ni mashamba, ingewezekana hata kila kijiji kikawa na josho kama siyo kila kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu majosho kuwepo ni jambo moja bado matumizi ya josho hayajawa mazuri,

majosho yapo lakini watu hawaogeshi, naomba Mheshimiwa Waziri afanye utafiti tatizo ni nini? Wakipewa dawa ya ruzuku pengine kwa mara ya kwanza wataogesha, baadae wanaacha kwa sababu kuogesha ni kwenye majosho na majosho ndiyo namna nzuri ya kuweza kupambana na magonjwa ya kupe, tujue sababu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo sheria lakini sheria zetu zimekaa kwenye vitabu, mara pengine ni vizuri kutumia sheria kuogesha ili watu wakaogeshe mifugo, kwa sababu kama nyumba moja inaogesha nyingne haiogeshi na sehemu ya malisho ni moja bado mzunguko wa kupe utaendela kuwepo pale, kwa hiyo hilo mimi naomba uliangalie.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine labda ni ubora wa madawa. Hebu tuangalie ubora wa madawa, kwa sababu mifugo hii inaogeshwa ile *ratio* ya dawa ya kuogesha hii, unaweza ukasema *CC* Mbili labda kwenye lita moja ya maji, lakini unaogesha ng'ombe au unampeleka kwenye *deep* anatoka pale bado ana kupe. Tujue tatizo ni nini? Ndiyo maana ukiona kwenye dawa pengine maelekezo ni kuchoma *CC* 10 kwa ng'ombe, wafugaji wananchoma mpaka 20 na 30 kwa sababu akichoma hiyo 10 kama ilivyo kwenye maelekezo anaona ugonjwa huo hautibiki. Pengine kuna uchakachuaji kwenye madawa haya ya mifugo naomba ufatilie.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Yustina.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga hoja mkono.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay nilimtaja, Mheshimiwa

Vedastus Manyinyi Mathayo na Mheshimiwa Abeid Ramadhan Ighondo ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa inayofanyika kwa kila sekta katika nchi yetu. Kwa kweli ni kazi nyingi zimefanyika na ina matokeo chanya kutatua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya, wamejitahidi kufanya kazi kubwa na sekta hii sasa inaelekea pazuri na mafanikio yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona eneo kubwa kwenye eneo hili la hotuba yake pamoja na bajeti aliyoiwasilisha tunao wajibu mkubwa kwanza wa kutazama ikama ya watumishi, hali yetu siyo nzuri kwa Maafisa Ugani, na hatuwezi kufanikiwa bila kuwa na wataalam, rasilimali mbalimbali pia vifaa na vitendea kazi pamoja na fedha kwa ujumla. Kwa hiyo naona kuna umuhimu mkubwa kwa sababu eneo lenyewe kwa mfano, Jimbo la Mbulu Mji lina watumishi Watano tu lakini lina Kata 17, lina Vijiji 34 na mitaa 58. Eneo kubwa la Jimbo langu wengi ni wakulima na wafugaji, wale wafugaji wana mifugo, kwa hiyo tatizo kubwa tulilonalo hatuna wataalam. Pia na najua siyo Idara yake yeye lakini wana jukumu kubwa la kuangalia idadi iliyoko kwa watumishi walioko ili tuone namna gani basi wale wachache wanaweza wakahudumia Watanzania na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kufanikiwa au kupata mafanikio bila kuwa na wataalam hao, vitendea kazi na rasilimali nyingine pia tuje na mpango kabambe, wafugaji wanahama sana, wanahama sana mifugo wanapata matatizo, mifugo yao wananyang'anywa, wanakamatwa misituni, siyo kwamba wanaingia kwenye misitu kwa nia mbaya ni kutokana na majanga ya ukame yanayoikabili ulimwengu kwa ujumla lakini pia mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili Mheshimiwa Waziri kama hatutakaa chini tutapata tatizo kubwa sana kwa ajili ya wananchi wengi na hasa wafugaji hao wanapopoteza mifugo yao na mwisho wa siku wale wa misitu wanavyowakamata wananauza bila hata kuangalia pande zote mbili na athari zinazotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuona tunajipangaje kwa hali tuliyoona Afrika Mashariki kwenye majanga yale ya ukame mifugo imekufa sana kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kwetu tuna kazi kubwa ya kubadilisha koo za mifugo, kupunguza idadi ya mifugo wengi wa kienyeji, kuja kwenye ufugaji wa tija pia kuangalia ufugaji unakuwa na tija na mifugo wanaopungua wale wanakuwa bora zaidi kulingana na mahitaji ya wakati wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu kabisa tatizo hili la wingi wa mifugo litazidi kuongezeka kama taarifa yake ilivyosema leo, kama hatutachukua jukumu la kuwa na mashamba darasa ya kupunguza idadi ya mifugo pia unenepeshaji na namna ya kubadilisha koo za mifugo basi moja kwa moja tatizo hilo litakuwa kubwa kwa nchi yetu na mwisho wa siku umaskini utakuwa unaendela kukabili kundi hili la wafugaji ambao ndiyo kundi kubwa na mifugo hawa tunawategemea kwa namna mbalimbali kama

ambavyo tunajua katika maisha yetu ya kila siku na ndiyo uchumi na maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais katika ziara yake Mkoani Manyara, aliagiza maziwa yale ya Babati, Tlawi kule Mbulu na Bassotu aliagiza wataalam waende kuangalia namna ya kunusuru yale mabwawa kwa ajili ya shughuli za uvuvi lakini pia uwepo wa rasilimali hiyo. Timu yako ilikuja tunakupongeza sana, ilifanya kazi nzuri sana, ilitembea na wataalam wa Wilaya zetu lakini taarifa ile nadhani sasa ni karibu miezi Sita hazijaweza kurudi kwetu, nakuomba Mheshimiwa Waziri ile taarifa ifanyiwe kazi ili iweze kurudi na tuweze kujua matokeo ya ile taarifa ili tuweze kufanikiwa kwa jinsi ambavyo tunaweza tukaona ina tija na wananchi wetu wakapata mrejesho, wajibu wa wananchi ni nini kwenye ile taarifa au wajibu wa wataalam ni nini na wajibu wa Wizara ni upi, ili kuweza kulinda hizi rasilimali zilizoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza pia Serikali kwa kupeleka pikipiki, tumepeleka pikipiki kwa Maafisa Ugani wa mifugo, ingawa upelekeaji ule haukuwa mzuri kwa sababu mwenye watumishi Watatu alipelekewa pikipiki Tatu, mwenye watumishi Ishirini alipelekewa pikipiki Ishirini. Hii ilitokana na idadi ya watumishi walioko lakini haijaangalia rasilimali mahitaji yalivyo, ukubwa wa eneo na jinsi ambavyo kundi hili la wafugaji linavyohudumiwa na ni kubwa kiasi gani. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kuna mambo mawili kwenye zoezi hili, kwanza ni kuendela kuona namna ya kuweza kupeleka pikipiki zaidi kwenye yale maeneo ambayo bado hayajapata pikipiki, kwa mfano, mimi nimepata tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uwezeshaji wa mafuta, Maafisa wetu tumewapelekea pikipiki Mheshimiwa Waziri hawana uwezo wa kupata hayo mafuta ya kuhudumia

wananchi, kwa hiyo tuangalie utaratibu gani tunaweza tukafanya ili tuweze kuona pikikpiki hizo zinakuwa na tija kwa manufaa ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kuishauri Serikali kuona utaratibu wa namna gani tunapoanzisha mizani kwenye masoko. Mheshimiwa Waziri amebainisha kwenye hotuba yake kwamba sasa mifugo watauzwa kwa kilo minadani. Je, ni kwa kiasi gani mazingira hayo ya minada na masoko kwenye maeneo yetu tayari yana miundombinu ya kilo? Ili kusiwe eneo moja tu tunatoa huduma hiyo kwa kilo ama soko linaendeshwa kwa vipimo lakini eneo jingine halina miundombinu, pengine timu ingepita nchi nzima au wangeomba taarifa wao kama Wizara ili waone basi maeneo gani hawana mizani na nini kifanyike ili eneo hili la miundombinu ya mizani liweze kupatikana na kwa wingi zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine kwa namna ya pekee ninaiomba Serikali itupatie fedha Milioni 130 niliandika barua Halmashauri ya Mji wa Mbulu kujenga masoko Milioni 130, wakati tunapeleka bajeti ile Milioni 130 wakawa wameiondoa. Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe unakumbuka nimekuja ofisini mara kadhaa, nilipokuomba uliniambia nikuandikie barua, nikakuandikia barua ya hali halisi ya Mji wa Mbulu na Halmashauri ya Mji wa Mbulu kwa sababu tayari tuna Kata Kumi ziko Vijijini na hatuna majosho. Kwenye ile barua ulinijibu kwamba itafanyiwa kazi, kwa hiyo naomba Wizara yako itazame upya uataratibu wa ujenzi wa majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule ujenzi uliotumika kipindi kilichopita na ukarabati wa kipindi kilichopita haukuwa na tija sana kwa sababu ilionekana ukarabati wa majosho ulikuwa unasimamiwa na Wizara na fedha nyingi hazikuwa zimetoa

matokeo chanya kwa maana ya thamani ya Shilingi, kwa hiyo ni jukumu letu wote kuona kwamba walau fedha zile zilizotengwa kwa ajili ya miundombinu ya majosho zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa mabwawa. Sababu kubwa ya mifugo kuhama kwanza ni kuwa wengi halafu hawana tija wingi wao kwa mfugaji, pia ukosefu wa malisho na maji. Sababu hiyo inahitaji miundombinu ya mabwawa, kwa hiyo nafikiri kama inawezekana Mheshimiwa Waziri maeneo maalum yaainishwe kwa ajili ya kuchimba mabwawa pia ufugaji uwe wa kupunguza mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye Halmashauri zetu tuna vituo tumejenga nadhani miaka kumi ya huduma za mifugo na kilimo, vituo hivi kwa sasa havitumiki hasa kwenye Jimbo la Mbulu Mji. Utatumiaje vituo sita wakati wewe huna wataalam lakini pia dhana nzima ya kuanzishwa kwake ilikuwa ni namna pekee ya vituo hivyo vitoe elimu kwa wafugaji na semina kwa wafugaji pia na namna ya uzalishaji na uboreshaji wa wafugaji. Kwa hiyo, mimi nadhani kuna haja ya ile miundombinu kutumika, inazidi kuchakaa kama kwenye Jimbo langu inafika karibu sita haitumiki kwa sasa na tulijenga kwa gharama kubwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwenye mpango huu kabambe wa sekta yako ya mifugo basi na eneo hili lifanyiwe kazi ili vituo vile vipate wataalam ambao ni wabobezi lakini pia wamesomea hiyo fani, watatoa elimu kwa wafugaji na wakati fulani semina mbalimbali na huduma za mifugo zinapatikana kwenye yale maeneo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, basi mengine nitandika kwa maandishi naunga hoja mkono kwa asilimia 100.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mheshimiwa Abeid Ramadhan Ighondo na Mheshimiwa Bishop Josephat Gwajima ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mosi, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na *staff* yote kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya, kusema kweli ukiangalia mmejitahidi sana kuboresha mifugo na mmejitahidi sana kuboresha uvuvi. Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwanza kwa namna ulivyoweza katika ile awamu ya kwanza ulivyotoa vizimba mimi kwenye Jimbo langu la Musoma Mjini tuliweza kupata vikundi saba, walipata vizimba kwa hiyo wanasubiri tu mimi na wewe tuende tukawakabidhi ili waanze maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tu kusema kwamba pamoja na shukrani hizo baada ya kuwa wale wamesikia kwamba wenzao wamepata, sasa vikundi vingi zaidi vimehamasika na vinategemea kwamba kwenye awamu itakayofuata basi ni imani yangu kwamba watakuwa wengi watakaoomba ili waweze kufaidika na mpango huo wa vizimba katika Manisapa yetu ya Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nisemee tu kwa ufupi kwamba liko tatizo kidogo ambalo linatusumbua kwenye ufugaji wa samaki, tatizo hilo tunahitaji tuwe *serious* tuone namna ya kulitatua. Unajua watu wengi na hata wale

wanaouza chakula cha samaki pamoja na wale samaki wenyewe wanatupa maelekezo kwamba samaki ndani ya miezo sita ukiwalisha hivi, watakuwa wamefika wastani wa gramu 500 na utapata biashara, lakini huwezi kuamini kwa sababu tuna watu wengi ambao ni watengenezaji wa vyakula vya samaki, wanashindwa kutupa *formular* kamili au kututengenezea chakula kamili kitakachoweza kuwafikisha samaki ndani ya miezi sita wapate uzito ule unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo watu wengi wanaanza kukata tamaa kwa sababu wanafuga mpaka miezi nane lakini samaki wana gramu 200, wana gramu 300. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninakuomba kabisa kwamba hebu hilo ulipe uzito wake kuona kwamba ni kwa namna gani tunaweza kupata watengenezaji wazuri wa chakula cha samaki. Maana leo hii ukiagiza chakula kutoka nje ndani ya miezi sita unaweza kufikisha gramu 500, kwa hiyo nadhani hilo kwetu ni tatizo kubwa kwa sababu ni watu wachache wanaoweza kuagiza chakula cha samaki kutoka nje.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo sasa hilo, ombi kwamba pale Musoma Mjini bahati nzuri wewe unapajua vizuri niko kwenye mwambao wa Ziwa Victoria na katika ule mwambao wa Ziwa Victoria ukienda pale asubuhi kuanzia Saa 12 unawakuta wakina mama wamebeba mabeseni ya dagaa vichwani na hayo mabeseni ya dagaa wakiwa wanatiririkiwa na yale maji ya dagaa, kwa maana ya kwamba wale wavuvi wa dagaa, ile kuanzia alfajiri ya Saa 11 wanafika pale hasa kwenye mwalo wangu wa Makoko, halafu wanawauzia wakina mama zile dagaa, sasa wanaanza kutembea nazo wakati mwingine mpaka kilomita tano kwa mguu. Wakifika sasa ndiyo wanaanza kuanika, tena siku hizi wamekuwa wakianika kwenye zile *net,* hizi *net* kwa maana ya chandarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri tupate hata mashine moja au mtambo mmoja wa kukausha Samaki na dagaa pale ili samaki wakishatoka kule ziwani wanapita pale kwenye mashine wanakaushwa akina mama wetu wa Musoma Mjini waweze kufanya biashara zao kwa raha zaidi, nadhani hiyo itawasaidia kuboresha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana watu tunaowahangaikia ndio hao wenyewe, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri uone namna tutakavyowasaidia. Jambo la pili Mheshimiwa Waziri hili linataka *attention* kubwa sana, ndugu zangu wale wote ambao tunaishi Kanda ya Ziwa kwa maana Mara, Mwanza na Bukoba nadhani mtakubaliana na mimi, samaki wamepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri siku zinavyoenda ni kwamba samaki wanaendelea kupungua, kwetu sisi pale watu wa ziwani kule samaki au lile Ziwa ndiyo madini yetu, kwa hiyo watu wetu wengi wamekuwa wakipata ajira karibu zaidi ya asilimia 50 kutokana na lile Ziwa Victoria. Sasa leo pale kwangu Musoma Mjini tulikuwa na viwanda vinne, tulikuwa na Musoma *Fish Park,* Musoma *Fish Process*, tulikuwa na kiwanda cha Mzee wetu Jamaliwa lakini na *Prime Catch.* Leo huwezi kuamini kimebaki kiwanda kimoja cha Musoma *Fish Process* ambao na wao kwa sababu wanapata samaki kidogo wanalazimika kusafirisha kupeleka Mwanza katika kiwanda chao kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha nini? Kwamba kadri siku zinavyoenda yale maji yatabaki tu labda kwa ajili ya kuoga na kunywa lakini hayatakuwa maji yanayoweza kuwasaidia watu wetu kiuchumi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa

naomba kabisa tuangalie namna tunavyoweza kulisimamia hili Ziwa hasa kuondoa uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo najiuliza hivi kama tunaweza ile Ngorongoro ndogo tukaweka Mamlaka ya Ngorongoro kwa ajili ya kuangalia Hifadhi ya Ngorongoro, tukaweka watu kama *TAWA* kwa ajili ya kusaidia kuangalia wanyama, hivi tunashindwa nini kuweka mamlaka ambazo zinasimsmia haya Maziwa zinasimamia mpaka na kule baharini ili suala la vile viumbe kwa maana ya samaki waweze kufugwa vizuri. Hivyo, nadhani hilo Mheshimiwa Waziri alipe uzito ili liweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja karibu na la mwisho ni suala la hereni. Miongoni mwa wafugaji hapa na mimi naweza nikajinafasi kwamba na mimi ni mfugaji na ninafuga vizuri. Binafsi nitofautiane tu na wenzangu kidogo pale walipoanza kukataa herein, mimi binafsi naliunga mkono sana suala la hereni kuwepo katika mifugo yetu. Kwanza litatuondolea kabisa kitu kinaitwa wizi, nadhani Mheshimiwa Waziri ni kwa sababu haujaeleza vizuri ule umuhimu wa herein. Binafsi mifugo yangu yote inazo hereni lakini ni zile hereni za plastiki, wakati nikiwa kwenye mchakato wa kuweka hizo hereni za elektroniki tayari Serikali mkasema mnaleta, kwa hiyo mpaka leo mimi nazisubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza tu nikatumia nafasi moja ndogo tu ambayo itawa-*convince* watu wote wale ambao ni wafugaji wakubali zile hereni. Leo wako Wajumbe humu wamesema kwamba wafugaji hawakopesheki. Hawakopesheki kwa sababu namna ya ku-*control* ile mifugo yetu inakuwa shida kidogo. Leo Mheshimiwa Waziri tunao watu wa TEHAMA humu katika Wizara yako wamo, hebu waunganishe wale watu wa TEHAMA waunganishe na benki, wafanye tu kitu kimoja, mimi nina ng'ombe wangu 500 zote

zina hereni maana yake ni kwamba zile ngo'mbe ili ziuzwe lazima tuuze kwa kutumia herein, kwa hiyo benki leo ukiwaambia kwamba mimi nina ng'ombe 500 hereni zake ni hizi wanaziingiza kwenye *system*, siruhusiwi yaani nikiuza huyo ngo'mbe hizo fedha lazima ziende wapi? Lazima ziende benki. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo kwanza itakusaidia kuhakikisha kwamba kila mmoja sasa anaona umuhimu wa zile hereni na ni kwamba maana anajua sasa tayari thamani ya zile mifugo zetu zinakuwa tayari ni dhamana kwetu hasa kwenye eneo la benki ambako ndiko wafugaji wengi wanapata taabu. Kwa hiyo, nadhani kama hilo Mheshimiwa Waziri utalipa uzito ni imani yangu kwamba linawezekana kwa sababu mimi nilishalifanyia *research* ni kitu ambacho kiko wazi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Nilimtaja Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Bishop Josephat Gwajima na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote, nianze pia na mimi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Abdallah Ulega, kijana mwenzetu na uzuri namfahamu, alikuwa *Youth League,* ni *committed person, very humble, understanding;* kwa hiyo, naamnini hapa Wizara imepata mtu sahihi pamoja Naibu wake. Ni kwamba tunakwenda kutekeleza hivi vitu tunavyovizungumza ambavyo tumeviona kwenye hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata Katibu Mkuu wa Wizara hii, Profesa, tunatarajia tuone mambo mazuri ya kisomi, ya kitaalamu na wayashushe mpaka kule chini ambako wanatukuta sisi wafugaji ambao hatujui kusoma wala kuandika. Kwa hiyo, watafute namna sasa, kutumia elimu zao hizi nzuri waweze ku-*match* na sisi wanakijiji ili tuweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu ku-*declare interest,* mimi ni mtoto wa mfugaji, nimesoma kwa kutumia mifugo hii. Kwa hiyo, ni sekta muhimu ambayo kimsingi namwomba sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, waitazame kwa jicho la karibu, watumie nafasi ambazo wamepewa na Mheshimiwa Rais, amewaamini vizuri, nasi tuna imaninao kubwa, kuhakikisha hii Wizara inakuwa na tija kwenye pato la Taifa letu na hasa wananchi walioko kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuzungumzia masuala machache ya jimboni kwangu yanayohusu sekta hii, halafu nitazungumza mambo ya jumla ya kitaifa. Kwenye eneo la malisho pamoja na majosho, hasa majosho; kwa kule jimboni kwangu ninashukuru nilipata miradi katika ule mwaka wa fedha unaoisha, majosho manne katika Kijiji cha Muaghamo, Mangida, Minyenye na Makuro. Kwa masikitiko makubwa, hii miradi haikuweza kutekelezeka kwa sababu ya ule utaratibu wa Wizara, kwamba, wanakuwa na zile fedha, mpaka waone josho limetengenezwa na wakandarasi. Wakandarasi watengeneze kwa kutumia nguvu zao, ndipo waje walipwe. Sasa huu utaratibu umekuwa siyo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri utaratibu huu, ingekuwa wanapeleka Halmashauri kwa sababu Halmashauri tunazo kila eneo na ni *Government entity* inayosimamia mambo haya na tunaiamini. Kwa hiyo, fedha hizi ziende pale

ili wale wakandarasi waweze kupewa wafanye kazi kuliko kuzi-*own* huku juu, utaratibu unakuwa ni mrefu na mgumu, na siyo rahisi kufikika. Naomba huu utaratibu urahisisishwe ili nipate haya majosho manne ambayo ilikuwa niyapate. Pia, nashukuru kwa miradi ya majosho mengine manne ambayo naenda kupata kwa mwaka huu unaokuja wa fedha katika Kijiji cha Mukulu, Unyampanda, Ughandi na Mughunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye zile *center* atamizi. Ofisi ya Waziri Mkuu walikuja wakati ikiwa chini ya Wizara hii ya Mifugo. Ni kwamba, wangetuletea *center* kwa ajili ya kituo atamizi kwenye Kijiji changu kimoja cha Nkwaye, lakini mpaka sasa sijaona kinachoendelea. *Center* hii ingekuwa ni nzuri kwa vijana, kwa ajili ya kurithisha mafunzo mazuri, endelevu ya kisasa kwa wenzao wengine. Sasa sijaona kinachoendelea. Naiomba sasa Wizara walichukue hili, ili nione sasa kile kituo cha ufugaji bora utekelezaji ufanyike ili vijana wetu waweze kupata hii elimu, waweze kuwapa na wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu biashara hii inayofanyika ya ng'ombe. Wafanyabiashara wengi walikuwa wanapata leseni na vibali vile vya kusafirishia mifugo kule kule wilayani na wakati mwingine mkoani, lakini sasa hivi Wizara imelimiliki hili zoezi, wafanyabiashara mpaka waje Wizarani. Sasa inawapa taabu, kwa hiyo, ufanyaji wa biashara ya mifugo umekuwa ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, naomba Wizara ibadilishe huu utaratibu ambao upo hivi sasa, irudi kwenye ule utaratibu uliokuwa wa mwanzo, uliokuwa unawawezesha wafanyabiashara wetu wa mifugo ku-*access* hizi leseni kwenye maeneo yao kuliko kuwapa taabu ya kuwafuata watendaji wetu huku Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la muhimu sasa kwenye sekta hii, katika sekta za muhimu katika nchi yetu huwezi kuiondoa mifugo, huwezi kuondoa uvuvi pamoja na kilimo. Hizi ni *production sectors* ambazo ndiyo zinatakiwa ziwe sekta za msingi za uzalishaji na zitazamwe kwa jicho la karibu kwa ajili ya kumsaidia Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nchi hii nimeitembea kidogo, kuanzia Bukoba, nimeenda mpaka Zanzibar. Katikati hapo ukipita huwezi kuacha kuona mfugo. Ukianzia Mbeya mpaka uende Arusha, huwezi kuacha kuona mfugo. Sikitiko langu kubwa ni kwenye eneo la bidhaa za mifugo, tumezipuuza. Hakuna viwanda. Hakuna kiwanda cha nyama, wala kiwanda cha maziwa. Vipo vichache. Kwanza tulikuwa na viwanda vile vya zamani; kulikuwa na *Tanganyika Packers* ambayo leo inatumika kwenye mahubiri. Hivi kweli tunaweza tukafika kwenye *point* hii ya kuidhalilisha sekta hii ambayo inawasaidia wananchi wa Tanzania zaidi ya milioni 60 leo? Tunaacha mifugo inateseka, ngozi inatupwa. Eti leo sisi tuna-*export* ngozi kwenda kuliwa Nigeria na Ghana. Ndiyo tumefilisika kwa kiwango hiki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, watendaji wa Wizara hii pamoja na Serikali, twende tukamkomboe mwananchi wa Tanzania kwa kutumia hii sekta ya mifugo. Nasikitika eti leo naambiwa ni asilimia saba sijui tano, kwenye pato la Taifa ndiyo inatokana na mifugo. *This is joking!* Hapa tunatania, hatujawa *serious* bado. Naomba sana, turudi kwenye viwanda vile vilivyokuwepo vya kusindika nyama. Nakumbuka tulikula nyama ya kopo wakati huo, lakini leo hakuna. Nyama ikikaa siku mbili buchani, unakuta imeharibika, ndiyo tunaumwa matumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungekuwa tunaweza kuweka viwanda vile vya ku-*process* nyama, iwekwe kwenye

kopo; maziwa, *products* za ng'ombe, za mifugo; leo hii tungeongeza thamani ya mifugo yetu, tungeingiza pato kubwa la Taifa kwa kupitia mifugo hii. Hata Singida tulikuwa tuna kiwanda cha kusindika nyama ya ng'ombe. Leo hii naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kusimama uniambie, kiwanda cha ng'ombe Singida, *status* yake ikoje? Naomba hiki kiwanda kirudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sisi tunafuga; tuna ng'ombe wa kutosha, *central zone* hii kwa ujumla wake tuna mifugo ya kutosha; Shinyanga, na kadhalika, tuweke kiwanda pale Singida cha ng'ombe na mbuzi ili tuweze kuinua kipato cha Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la muhimu sana, ni eneo la malisho ya mifugo. Katika eneo ambalo hatujaitendea haki kabisa sekta hii ya mifugo ni eneo la malisho. Naomba sana, tuache kuwadhalilisha wafugaji wetu. Kwa kuwa, tumeshaona wananchi wetu wengi ni wafugaji, nasi tupo kwenye kutengeneza sera na mifumo, tuwatengenezee utaratibu mzuri wa malisho. Majani haya ambayo tumesema ni ya malisho ya mifugo yetu, tuyapeleke mashamba darasa kwenye kila Kijiji, kwenye kila kata. Kwa nini myaache huko Dar es Salaam au Dodoma? Wafugaji hawako Dar es Salaam. Wafugaji na wakulima wako vijijini, tuwafuate waliko tuwapelekee hii huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi suti tuzipeleke kule vijijini ili tukaishi maisha wanayoishi wenzetu kule chini kwenye *grassroot*. Tutawatendea haki, wakulima wetu wataacha kumangamanga, kutafuta malisho huku na kule. Kila siku tunaona migogoro ya wakulima na wafugaji, haitaisha kama hatujaweza kuwapa wafugaji wetu malisho huko kwenye maeneo yao. Yale maeneo ambayo yalipimwa, Mheshimiwa Waziri mlipima maeneo, mliyarasimisha maeneo vizuri kule…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abeid Ramadhani.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ninayo mambo mengi hapa nitayawasilisha mengine kwa maandishi, lakini naomba sana haya ambayo nimeyazungumza yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abeid Ramadhan. Nilimtaja Mheshimiwa *Bishop* Josephat Gwajima, na baadaye Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atamalizia.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nikushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi kuchangia hii hoja iliyoko mbele yetu, ya Wizara ya Uvuvi na Ufugaji. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa bidii yake anayofanya katika kuhakikisha Taifa la Tanzania linajengwa na linabaki salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ujasiri wake wa kumchagua ndugu yangu Mheshimiwa Ulega pamoja na ndugu yake Mheshimiwa David Silinde kuwa Mawaziri wenye dhamana kwa Wizara hii. Hongereni sana. *We have so many good Ministers, and you are one of them.* Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kitandula kwenye mchango wake

pamoja na Mheshimiwa Kaijage na Mheshimiwa Mathayo, Mbunge wa Musoma Mjini. Nikuhakikishie Waziri mwenye dhamana ya mifugo pamoja na uvuvi, mimi sitakuondolea Shilingi na ninaunga mkono hoja yako kabla sijaendelea. Nafahamu kwamba umeomba Shilingi bilioni 295.9, hizo sina neno nazo, na nitakupa na akili nyingine ya kupata zaidi ya hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichokoze jambo. Kwenye *document* ya mtani wangu, Mheshimiwa Waziri Ulega, kwa niaba ya Serikali, ametuonesha kwamba, sekta ya uvuvi inachangia asilimia moja ya pato la Taifa. Hili jambo ni hatari sana kulisikia au kusemwa mbele ya watu wenye akili timamu. Nichokoze jambo ambalo litamfanya kila mtu afikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ukianzia kwenye maji ya chumvi; tuna mikoa ambayo imezungukwa na maji ya chumvi. Kwanza ni Dar es Salaam, Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Tanga na Zanzibar yote. Hii ni mikoa *almost* mitano pamoja na Zanzibar, yote imezungukwa na maji. Ukiamua kuangalia maziwa tuliyonayo, tunayo mikoa ambayo na yenyewe imezungukwa na maji ya maziwa, siyo kwa maana ya maziwa ya kunywa, ni kwa maana ya *lakes*. Mkoa wa Mwanza umezungukwa na maji, Mkoa wa Mara, Mkoa wa Simiyu, Geita, Kagera, Mbeya, Kigoma, Katavi, Rukwa, Ruvuma, Arusha kuna *Natron,* mpaka kuna Ziwa Jipe Kilimanjaro, kuna Manyara, mpaka kwa Wagogo hapa kuna Mtera, tumezungukwa na maji mpaka Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuunganisha hizi *dots* za hii mikoa 16 niliyoitaja yote iko kando ya maziwa. Unaunganisha na hii mikoa mingine niliyoitaja ambayo iko kando ya maji ya chumvi, unakuta mikoa 22 yote imezungukwa na maji. Sasa kwa akili ya kawaida, *it doesn't*

*hold water* kugundua kwamba liko tatizo tunaloli-*face* ambalo tunahitaji kulitatua kwa pamoja ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijaribu kufanya *troubleshooting* kidogo. Kwanza, haikubaliki kwa namna yoyote ile kwamba uvuvi uchangie asilimia moja peke yake kwenye pato la Taifa, haiwezekani ukilinganisha na *resources* tulizonazo. Sasa ushauri wangu wa kwanza ambao umesemwa na wale niliowashukuru; kwanza, ni muhimu sana kufanya sekta ya uvuvi kuwa mamlaka. Kama ambavyo tumefanya kwenye Wakala wa Misitu, tumefanya *TANAPA,* wote hao wako chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini mamlaka itaongeza chachu ya namna ya kutumia maji yetu ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nashauri, sasa wakati umefika Wizara hii ya Uvuvi pamoja na Mifugo kuwa na *vision* ya muda mrefu ya nchi. Nilipata faraja sana nilipoona ule mchakato wa Uzinduzi wa Mpango wa Taifa. Nilikuwa *disappointed* tu kuona kwamba ni miaka 25 peke yake tunawaza, nilifikiri tungewaza miaka 50 ya Mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotupa shida hapa sisi, kwa mfano, tunasema tuna idadi ya ng'ombe milioni 36.6, tuna idadi ya mbuzi milioni 26.6, tuna idadi ya kondoo milioni 9.1, lakini wakati huo huo tumesema tunazalisha maziwa lita bilioni 3.6, maziwa tunayozalisha kwetu. Wakati huo huo tuna idadi ya mifugo wote hao na maziwa yote haya, lakini tumetoa vibali vya watu kuleta maziwa tena hapa nchini kutoka nchi nyingine. Tumetoa vibali 605 vya kuingiza maziwa na lita tulizoingiza ni lita milioni 11.6 za maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaweza kuwaza, tuna mifugo hapa mingi sana, tuna lita za maziwa nyingi sana, tunatoa vibali vingine tena 605 vya watu wengine nao walete maziwa hapa. Inawezekana labda hayatoshi kwa maana ya ku-*compensate,* lakini thamani ya maziwa yaliyoingizwa ilikuwa ni Shilingi bilioni 22.7 thamani ya maziwa ambayo tumeingiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it doesn't make sense* kama tumetumia fedha ya kigeni kununua maziwa kwa *22.7 billion*. Kwa nini tusi-*reserve* hizi fedha za kigeni, tukaamua kuwa na *vision* kabisa ya muda mrefu inayohusu uvuvi. Tukasema, uvuvi tuupe *vision* ya miaka 50 na mifugo tuipe *vision* ya miaka 50, kuwe na *blue print* kabisa ya uvuvi na *blue print* kabisa ya mifugo, ili kila Waziri anapoingia kwenye Wizara hii aikute hii *blue print* imekaa tayari. Tutajikuta tuna *continuation* kwenye hizi Wizara na pato litaongezeka. Nachelea sana mtani wangu, kama huna *blue print* siyo muda mrefu utaanza na wewe kupima samaki pale kwenye *restaurant* ya Bunge hapo kwa sababu, utakosa cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara ya Fedha na Mipango walipoanza kuzindua ule mpango wao wa kuwa na *vision* ya muda mrefu. Kwa sababu, *it doesn't make sense* kwamba tuna *TANAPA,* ni mamlaka, lakini iko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii; tuna *TFS* ni mamlaka iko chini ya Wizara hiyo hiyo; *why not uvuvi,* tukawa na mamlaka, na hiyo mamlaka ikatengeneza *vision* ya uvuvi ya muda mrefu, ili kila Waziri anayeingia anatembea kwenye hiyo hiyo *vision* tukaongeza fedha katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia watu wengi sana wanamtia moyo mtani wangu kwamba, pesa aliyopewa ni kidogo. Nikupe siri ya kupata *sealing* kubwa kwenye hiyo

pesa yako. *Unless* unapeleka *vision* kubwa kwa mamlaka, mamlaka haiwezi kukupa *sealing* kubwa. Ukiipelekea mamlaka maono makubwa kwamba, mimi bwana kwenye Wizara yangu, katika eneo la uvuvi nataka kuwa na *vision* hii hapa. Hii *vision* italeta asilimia 10 ya pato la Taifa. Hiyo mamlaka itaona hiyo *vision* yako itakuongezea *sealing* yako, itakuwa ni rahisi sana, kuliko ile kusema tu kwamba, uongezewe. Za nini? Hata kama ningekuwa ni mimi, nataka kukuongezea mtani wangu, za nini? *You don't lay your plan; you have to lay your plan. It is a proposal that attracts finances.* Kwa hiyo, lazima uweke mpango wako wa muda mrefu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYWEKITI:** Ahsante sana, nashukuru. Tunamalizia na mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wake na Watumishi wote wa Wizara ya Mifugo. Nami leo nimewiwa kuchangia kwenye bajeti hii ya mifugo na ninataka nimwambie tu Mheshimiwa Waziri kwamba, kwenye Wilaya ya Kahama, Halmashauri ya Msalala, Jimbo la Msalala ni wafugaji wazuri sana wa ng'ombe. Nami nijikite sana kwenye kuzungumzia leo ufugaji

wa ng'ombe kwa sababu ndiyo mifugo ambayo tunaifuga katika Jimbo langu la Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Msalala, utaona kabisa wananchi wangu wanafuga ng'ombe kwa wingi. Changamoto kubwa iliyopo kwenye maeneo yale ni malisho pale ambapo mifugo inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna minada mingi ya ng'ombe kwenye maeneo yale. Tuna wafugaji wengi kwenye maeneo yale. Nampongeza sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kupitia Mheshimiwa Waziri wake kwa kuweza kutupatia ng'ombe madume 50 ya ng'ombe ambayo kimsingi yanaenda kuzalisha ng'ombe wa kutosha kwenye eneo lile la Jimbo langu la Msalala. Hawa ng'ombe 560 hawataweza kusaidia, na kwa sababu ni ng'ombe wa kisasa hawataenda kuwasaidia wananchi wangu kama hatutatenga bajeti nzuri ya kuweza kwenda kujenga miundombinu rafiki kwenye mifugo hii ambayo tayari tumeshaipeleka kwenye maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapokea ng'ombe hawa, maelekezo tuliyopewa ni kwamba, ngombe hawa wanahitaji kuoga mara kwa mara; ng'ombe hawa ni adui wakubwa wa kupe. Sasa kwenye maeneo yetu, hasa kwenye Jimbo la Msalala, utaona miundombinu ya majosho bado iko chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wa fedha 2021/2022 tulipokea ahadi ya kupewa majosho matano, lakini ni majosho mawili tu yaliyokuja yakakarabatiwa na yale majosho matatu mengine bado hatujayapokea. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kama tunataka kuilinda mifugo hii ambayo ninyi wenyewe mmetuambia ni *delicate* sana, inahitaji kuoshwa mara kwa mara, ni adui wa kupe, basi

tuhakikishe kwamba kwenye bajeti hii mtutengee majosho ya kutosha ili mifugo hii iweze kuoga, na iwezeshe sasa wananchi kuitumia vizuri na kuzalisha ng'ombe wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hapo nyuma ilizuia juu ya ugawaji wa *ranch*. Nami nikiri tu kwamba, kwenye maeneo yangu ukiangalia, wafugaji wengi wamekua kwa sasa. Kuna baadhi ya wafugaji wana ng'ombe kuanzia 500 mpaka 600, na hivyo kuwafanya waanze kuhamahama kwenye mapori. Wanapoenda kwenye mapori kule, matokeo yake wale ng'ombe wanakamatwa. Sasa naomwomba sana Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wake, hebu wachukue hili, waende wakaangalie lile zoezi la kupitia zile *ranch* ambalo walilisimamisha kufanya uhakiki halijakamilika? Kama limekamilika, hebu mwagawie sasa wananchi wetu kule ili waweze kufuga mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hili aliandike kwamba wananchi wanahangaika kule, waende wakapitie haraka. Mkurugenzi huyu aende akafanye kazi haraka iwezekanavyo, watangaze *ranch* hizo wawagawie wananchi. Wanapata taabu kwenye maeneo yetu huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hapa kuna Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Ushetu, kuna mwananchi wake alikuwa na ng'ombe zaidi ya 600, ng'ombe wale waliingia kwenye hifadhi na walikamatwa na uzuri alishinda kesi, lakini mpaka sasa bado hajalipwa fedha zake. Hii yote ni kwa sababu hatuna maeneo ya kuchungia mifugo yetu. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri awe mlezi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa, Mheshimiwa Waziri, tunazungumzia habari ya wafugaji; yeye anasimamia wafugaji, lakini inapokuja kwamba mfugaji anapata changamoto, wanajitoa. Sasa naomba, hebu endeleeni kusimama na wafugaji. Mfugaji anapopata changamoto yoyote, mshikeni nendeninaye moja kwa moja kuhakikisha kwamba anatendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri amekuja kutembelea kwenye Jimbo langu la Msalala, wakati anatukabidhi madume 50, sambamba na hilo aliahidi kutujengea bwawa la Mkoloni, Busangi. Ninaamini ahadi ile ilitolewa na Mheshimiwa Waziri ambaye alikuwa ni Mheshimiwa Mashimba Ndaki, yuko hapa; lakini Mheshimiwa Mashimba Ndaki hakutoa ahadi, aliyetoa ni Waziri, nawe umekaa hapo Mheshimiwa Waziri. Nikuombe chukua kalamu na karatasi Mheshimiwa Waziri, ahadi hii itekelezwe. Wananchi hawa tumewaahidi bwawa la kunyweshea mifugo kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi kwenye maeneo yale. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri aone katika bajeti hii, atuletee watumishi wengi kwenye sekta hii ya mifugo ili waende wakawasaidie wananchi kwenye maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la mwisho, naomba nichangie kwenye suala zima la minada. Kwenye Jimbo la Msalala tuna minada takribani zaidi ya 10, na minada hii inafanya kazi vizuri sana. Kwenye Wilaya ya Kahama Halmashauri pekee yenye mifugo mingi na yenye minada mingi ni Halmashauri ya Msalala. Sasa changamoto inakuja, hawa watu wanapoenda kuuza mifugo yao, Halmashauri inawa-*charge* fedha. Kwa mfano, kwenye ng'ombe

wanachajiwa shilingi 7,000 kwa ng'ombe, lakini shilingi 3,500 inakatwa moja kwa moja kwenda kwenye Serikali Kuu na haiingii hata kwenu kwenye Wizara, inaenda moja kwa moja kwenye Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwomba Waziri wa Fedha, yuko hapo, fedha ile inapokatwa muweze kuwa mnarudisha *percent* kwa ajili ya kwenda kufanya ukarabati wa miundombinu. Ukienda kwenye minada hii, unakuta choo hakuna, miundombinu ni mibovu, lakini wananchi wanalipa fedha. Pia Halmashauri zimeanza kuogopa kufanya uwekezaji wa kuendeleza minada hii kwa sababu fedha hawapati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta Halmashauri imewekeza zaidi ya Shilingi milioni 200 kukarabati mnada, lakini hapo hapo ninyi mkiona mnada huu umependeza, mnauchukua tena moja kwa moja na fedha zote Halmashauri haipati, zinaenda Wizarani. Sasa naomba, kama Halmashauri inaenda kuwekeza fedha kwenye minada yake, hebu mtuachie tuweze kuiendesha minada hiyo, nanyi msiingilie, mtuachie wenyewe Halmashauri, ili Halmashauri ziwe na moyo wa kuendelea kuwekeza kwenye maeneo hayo. Pia fedha hii ambayo inakatwa kwenda Serikali Kuu, hasa kwenda kwenye Wizara ya Fedha, fedha ile basi iweze kukatwa asilimia kadhaa, ije irekebishe maeneo ya miundombinu kwenye maeneo yale, hasa vyoo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, nakushukuru sana, lakini ahadi hii ya majosho matano mpaka leo hatujui yako wapi, iandike. Ahadi ya Bwawa la Mkoloni, Busangi ni muhimu sana kwa sababu ni ahadi ya kiongozi ambaye aliitoa, ni Waziri, nawe uko hapo umekalia kiti hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi.

Waheshimiwa Wabunge, huyu ndio mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo, na tumekamilisha kazi yetu ya siku nzima ya leo. Nawapongeza sana kwa kuwajibika ipasavyo na michango yote ambayo mmetoa, nikiamini kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu yake wameyachukua yale yote ambayo yana maslahi kwa Taifa letu na watayazingatia kwa uzito unaostahiki.

Baada ya kusema hayo, nawatakia kila la heri. Naahirisha Shughuli za Bunge, hadi kesho Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 3 Mei, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*